Njia ya Haki

Habari Njema kwa Waislamu

Habari na mafundisho ya manabii wa Mungu ndani ya Tora, Zaburi na Habari Njema (Injil)

Kitabu 1

par P.D. Bramsen

Everyday Publications Inc.
310 Killaly Street W.
Port Colborne, ON
Canada L3K 6A6

Copyright © 2006 Paul Bramsen

NJIA YA HAKI

KITABU CHA KWANZA

Copyright © 1998
P.D. Bramsen
The Way of Righteousness (Le Chemin de la Justice)

Traduit en Swahili par permission
par G.I. Harlow

ISBN 0-88873-144-2
Cette série est aussi disponible dans d'autres langues.

Pour permission de traduire LE CHEMIN DE LA JUSTICE dans
d'autres langues veuillez contracter:
TWOR@iname.com / www.twor.com

Imprimé au Canada

Copyright © 2006 Paul Bramsen

Njia ya Haki

Habari na mafundisho ya manabii wa Mungu
ndani ya Tora, Zaburi na Habari Njema (Injil)

Utangulizi

"Hata logo ikilala mia za miaka ndani ya maji halitageuka mamba kamwe" (mezali ya Wawolof wa Senegal) . . . ***vivyo hivyo kushikamana na dini hakuwezi kugeuza mtu kuwa haki.*** Desturi za dini na matendo mema yanasaidia watu kufikili wao ni *watu wa haki* na kuwafanyiza kuonekana kama wenye *haki mbele ya watu,* lakini hayawafanyizi *haki* ***mbele ya Mungu****.*

Njia ya Haki ni tafsiri kwa Swahili-Congo ya **"Yoonu Njub" —** programmes 100 za radio kwa kiwolof kwa Waislamu wa Senegal ya Afrique de l'Ouest. Kuanza na Tora ya Musa programmes hizi zinapeleka wasikiaji kwa safari ya Maandiko ya manabii kuona kusudi lisilobadiliki kamwe la Mungu kwa watu wa dunia na kusikia jibu la furaha kubwa la Mungu kwa neno ambalo nabii Yobu aliuliza miaka elfu ine mbele, ***"Mtu anaweza kuwa na haki mbele ya Mungu namna gani?"*** (Yobu 9:2)

Sasa programmes hizi zimechapwa kwa Swahili ndani ya vitabu vitatu kusaidia Waislamu na watu wengine vilevile kufahamu habari hizi za *manabii ya Mungu* vizuri zaidi.

Kitabu 1	— Masomo	1-28	*Njia ya Haki ndani ya TORA*
Kitabu 2	— Masomo	29-45	*Njia ya Haki ndani ya TORA*
	Masomo	46-59	*Njia ya Haki ndani ya ZABURI na MANABII*
Kitabu 3	— Masomo	60-88	*Njia ya Haki ndani ya HABARI NJEMA*
	Masomo	89-100	*Njia ya Haki — MUHTASARI*

Waislamu wanaamini ya kwamba Mungu amefunua mapenzi yake kwa njia ya vitabu vitakatifu vine (Tora, Zaburi, Habari Njema, Qur'an). Lakini Waislamu wachache tu wamekuwa na njia

Copyright © 2006 Paul Bramsen

kusoma Habari Njema ya Mungu ndani ya Tora, Zaburi, na Maandiko ya Habari Njema. **Masomo haya 100 yanawapatia njia kufanya hivi.**

Watu wengi wanashangaa wakati wanaposikia ya kwamba Qur'an kinaagiza Waislamu kuamini Tora (Taurat), Zaburi na Habari Njema (Injil), sehemu za Maandiko Matakatifu kwa Kiebrania na Kiyunani yanayoita *Biblia.* (Biblia ni kilatin kwa *Kitabu).*

Waislamu wengi wanasema ya kwamba maandiko ndani ya vitabu vya Tora, Zaburi na Habari Njema yamegeuzwa na haifai kuyaamini. Lakini masemo haya si kweli. Kuna karatasi elfu za maandiko ya vitabu hivi vinavyochungwa kwa pahali mbalimbali pa dunia. Karatasi hizi ziliandikwa mia za miaka mbele ya Qur'an. Kuna mafundisho mengine juu ya neno hili ndani ya Somo 90. Lakini hatuhitaji kusimamia Neno la Mungu kwani linasimama imara, Neno takatifu la Mwenyezi Mungu. Neno ambalo inatupasa kufanya si kulisimamia lakini ***kuisoma***.

> *"Maana Neno la Mungu ni hai, lenye nguvu na ukali kupita ukali wa upanga unaokata ngambo mbili, likitoboa hata kutenga nafsi na roho, na viungo na mafuta ndani ya mifupa; nalo ni jepesi kufahamu mawazo na makusudi ya moyo. Hakuna kiumbe kinachofichwa mbele yake, lakini vitu vyote ni utupu na kufunuliwa mbele ya macho yake yeye aliye na maneno yetu."*
>
> (Wabrania 4:12,13)

Ndiyo, uwezo wa kuchoma roho ya **Kweli ya Mungu** na utamu wa milele wa **njia ya haki ya Mungu** zinastahili kwa watu kuwa tayari kupata mateso na hata mauti kwa sababu yake. Nabii Solomono aliandika, "***Katika njia ya haki*** *ni uzima; na katika mapito yake hakuna mauti"* (Mezali 12:28) Allahu Akbar! Mungu ni mkubwa, na kwa wote wanaonyenyekea njia yake ya haki anatoa ahadi kuwapa bila bei neno ambalo dini na matendo mema hayawezi kutupatia: wokovu toka azabu na uwezo wa zambi, kuhesbiwa haki na kujua ya kwamba zambi zetu zimesamehewa, zamiri safi, salama kubwa moyoni, furaha rohoni ambayo hakuna neno linaweza kuharibu, tabia mpya, upatano wa karibu na Mungu, na kao pamoja naye katika Paradiso kwa milele!

Copyright © 2006 Paul Bramsen

Tunaweka kwa Mungu watu wote wanaosoma masomo haya

mia moja, kwa Mungu yule mwenye huruma na rehema, **mwenye haki**—anayetaka kutolea ahadi hii ya kuleta uzima na kugeuza maisha kwa mtu ye yote anayekubali kuipokea.

> ***"Mutanitafuta, na kuniona wakati mutakaponitafuta kwa moyo wenu wote."*** (Yeremia 29:13)

Copyright © 2006 Paul Bramsen

Fahirisi

Kitabu 1

Habari na Mafundisho ya Manabii wa Mungu kupatana na Tora

		ukurasa
	Utangulizi	3
Somo		
1	Mungu amesema (Mwanzo)	11
2	Mungu ni namna gani? (Mwanzo 1)	17
3	Shetani na Malaika (Mwanzo 1:1; Isaya 14; Ezekieli 28	22
4	Namna Mungu alivyoumba dunia (Mwanzo 1:1-26)	27
5	Kwa sababu gani Mungu aliumba mtu (Mwanzo 1:26,27; 2:7)	32
6	Adamu na Hawa (Mwanzo 2)	37
7	Namna gani zambi ilivyoingia duniani (Mwanzo 3:1-6)	43
8	Tunda la zambi ya Adamu (Mwanzo 3:7-19)	48
9	Ahadi ya ajabu (Mwanzo 3:15,21-24)	53
10	Njia ya sadaka (Mwanzo 4:1-5)	59
11	Kutotubu kwa Kaina (Mwanzo 4:1-16)	65
12	Nabii Enoka (Mwanzo 4, 5)	70
13	Nabii Noa : Saburi na gazabu (Mwanzo 6)	76
14	Noa na garika kubwa (Mwanzo 7)	81
15	Noa na uaminifu wa Mungu (Mwanzo 8, 9)	86
16	Babeli! (Mwanzo 10, 11)	91
17	Ukumbusho #1 (Mwanzo 1-11)	97
18	Abrahamu: Kwa sababu gani Mungu alimwita (Mwanzo 11,12)	102
19	Imani ya Abrahamu: (Mwanzo 13-15)	108
20	Abrahamu na Isimaeli (Mwanzo 16,17)	113
21	Abrahamu: Uharibifu wa Sodomo na kuzaliwa kwa Isaka (Mwanzo 18-21)	119

Somo		*ukurasa*
22	Sadaka ya Abrahamu (Mwanzo 22)	125
23	Esau na Yakobo (Mwanzo 25)	131
24	Yakobo anageuka Israeli (Mwanzo 28-32)	137
25	Aibu ya Yosefu (Mwanzo 37-39)	143
26	Kutukuzwa kwa Yosefu (Mwanzo 40-42)	149
27	Baki la habari za Yosefu (Mwanzo 42-50)	155
28	Ukumbusho wa kitabu cha kwanza cha Tora (Mwanzo 1-50; Kutoka 1)	161

Kitabu 2

Masomo 29 – 59

	Utangulizi	3
29	Musa (Kutoka 1,2)	11
30	Musa anakutana na Mungu (Kutoka 3,4)	17
31	Ulizo la Farao: Bwana ni nani? (Kutoka 4-7)	23
32	Hukumu kumi (Kutoka 7-10)	29
33	Mwana-Kondoo ya Pasaka (Kutoka 11,12)	35
34	Njia katikati ya Bahari (Kutoka 13-15)	41
35	Chakula jangwani (Kutoka 16,17)	47
36	Mlima Sinai (Kutoka 19, 20)	53
37	Amri Kumi (Kutoka 20)	59
38	Kusudi la Amri Kumi (Kutoka 20)	65
39	Amri zinazovunjwa (Kutoka 32)	71
40	Hema ya Kusanyiko (Kutoka 24-40, Walawi 16)	77
41	Kutokuamini kwa Waisraeli (Hesabu 13,14)	83
42	Nyoka ya shaba (Hesabu 20,21)	89
43	Maneno ya mwisho ya Musa (Torati)	95
44	Yosua na inchi ya Kanana (Yosua)	101
45	Waamuzi na Ruta (Waamuzi na Ruta)	107
46	Samweli, Saulo na Daudi (1 Samueli 1-16; Zaburi 8,23)	113
47	Daudi na Goliata (1 Samweli 17; Zaburi 27)	121
48	Mfalme Daudi na ahadi ya Mungu (1 Samweli 18 - 2 Samweli 7)	127
49	Mfalme Daudi na Bati-Seba (2 Samweli 11,12; Zaburi 51,32)	133
50	Nabii Daudi na Masiya (Zaburi 1, 2)	139

Somo		*ukurasa*
51	Mafundisho mengine toka Zaburi (Zaburi 22)	145
52	Nabii Solomono (1 Wafalme 2-10; Zaburi 72)	151
53	Nabii Elia (1 Wafalme 6-18)	157
54	Nabii Yona (Yona)	163
55	Nabii Isaya (Isaya)	169
56	Nabii Yeremia (Yeremia)	175
57	Nabii Danieli (Danieli 1,6)	181
58	Nabii Zekaria (Zekaria)	187
59	Jumlisho la unabii wa manabii (Malaki)	193

Kitabu 3

Masomo 60 –100

	Utangulizi	3
60	Nabii Yoane (Luka 1)	11
61	Tangazo (Luka 1; Matayo 1)	17
62	Masiya anazaliwa (Luka 2; Matayo 2)	23
63	Mwana mtakatifu (Luka 2; Matayo 3,4)	29
64	Mwana-Kondoo wa Mungu (Yoane 1,3)	35
65	Mganga mkubwa (Marko 1,2)	41
66	Mwalimu mkubwa (Matayo 5-7)	47
67	Sharti muzaliwe mara ya pili (Yoane 3)	53
68	Mwokozi wa dunia (Yoane 4; Luka 4)	59
69	Amri ya Yesu (Matayo 12; Yoane 5)	65
70	Uwezo wa Yesu (Matayo 12; Yoane 5)	71
71	Mifano mikubwa miwili (Luka 8; Matayo 13)	77
72	Mkate wa Uzima (Marko 6; Yoane 6)	83
73	Yesu analeta matengo (Matayo 15,16; Yoane 7)	89
74	Nuru ya Ulimwengu (Yoane 8,9)	95
75	Bwana wa utukufu (Matayo 16,17)	101
76	Mchungaji Mwema (Yoane 10)	107
77	Moyo wa Mungu (Luka 18,15)	113
78	Ufufuko na Uzima (Yoane 11,12)	119
79	Yesu anaingia Yerusalema (Luka 18-20)	125
80	Masemo magumu na ya kweli (Matayo 22-25)	131
81	Chakula cha mwisho (Matayo 26)	137
82	Yesu anakamatwa (Yoane 14; Matayo 26)	143
83	Yesu anahukumiwa (Matayo 26,27; Yoane 18,19)	149

Somo		*ukurasa*
84	Yesu anasulibishwa (Matayo 27; Marko 15; Luka 23; Yoane 19)	155
85	Yesu amefufuka! (Matayo 28; Luka 24; Yoane 20	161
86	Yesu anapanda mbinguni (Matayo 28; Luka 24; Matendo 1)	167
87	Roho Mtakatifu amekuja! (Matendo 1,2)	173
88	Yesu atarudi tena! (Ufunuo 19-22)	179
89	Habari Njema	185
90	Maulizo ya watu na majibu ya Mungu (#1)	193
91	Maulizo ya watu na majibu ya Mungu (#2)	199
92	Inapasa mwanafunzi wa Kristo kuishi namna gani?	206
93	Ukumbusho #1 Adamu - Neno gumu la zambi (Mwanzo 1-4)	212
94	Ukumbusho #2 Abrahamu - Haki kwa njia ya imani (Mwanzo 6-22)	218
95	Ukumbusho #3: Musa: Sheria takatifu ya Mungu Kutoka 1-20)	224
96	Ukumbusho #4: Yesu Kristo: "Imekwisha!" (Yoane 19, Waebrania 10)	230
97	Hadeze! (Luka 16)	236
98	Paradiso! (Ufunuo 21,22)	243
99	Unafikili nini juu ya Yesu? (#1)	249
100	Unafikili nini juu ya Yesu? (#2)	255

SOMO 1

MUNGU AMESEMA

MWANZO

Salamu kwako, Rafiki. Tunakusalimu kwa jina la Mungu wa salama, anayetaka kila mtu kufahamu, kuamini na kupokea njia ya haki ambayo alitayarisha, na kuwa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi sana kwa sababu tunaweza kuanza leo na mfulizo unaoitwa ***"Njia ya Haki"***. Tunauita *"Njia ya Haki"* kwa sababu tunakusudi kusoma **habari za manabii ya Mungu,** na kutafuta maana ya maandiko ya manabii wanaopasha habari za njia Mungu aliyotayarisha kwa watu kuweza kuwa haki mbele yake.

Wewe unafuata njia gani? Njia ya haki au njia ya uzalimu? Neno la Mungu linasema, *"**Heri wenye njaa na kiu kwa haki**: maana wao watashibishwa."* (Matayo 5:6)

Labda watu wengine wanafikiri, "Tunakwisha kujua njia ya haki. Hatuhitaji kufikiri juu ya maandiko ya manabii wa kwanza. Maneno ambayo tunajua yanatutosha!" Kama haya ndiyo mawazo yako, fikiri juu ya maneno nabii wa Mungu, Solomono, aliyoandika. Alisema, "*Kuna njia **inayoonekana kuwa sawa** kwa macho ya mtu, lakini **mwisho wake ni njia za mauti!**"* (Mezali 14:12).

Ndani ya Maandiko, ndani ya kitabu kinachoitwa Zaburi, nabii wa Mungu, Daudi, baba wa Solomono, alisema mara nyingi juu ya hitaji letu kujua njia ya haki ambayo Mungu aliamuru. Aliandika, *"Wao ni wapotevu ... **hakuna mmoja** anayetenda mema. Wao wote wamepotea; wao wote pamoja wamekuwa wachafu; hakuna mmoja anayetenda mema, hata mmoja."* (Zaburi 14:1,3; Waroma 3:10,12) Kwa sababu hii Daudi aliandika ombi hili ndani ya Zaburi, akisema, "*Unionyeshe njia zako, Ee Bwana; unifundishe mapito yako; uniongoze katika kweli yako."* (Zaburi 25:4,5)

Kama Mungu wetu asipotuongoza ndani ya njia ya kweli, tusingeweza kujua njia ya haki kamwe. Tungekuwa kama mtoto anayepotea katika mji mkubwa au kama kondoo anayepotea mwituni. Lakini Neno la Mungu linasema ya kwamba *"Mungu hataki mtu mmoja kupotea ... lakini anataka watu wote waokolewe na kupata kujua sana yaliyo kweli."* (2 Petro 3:9; 1 Timoteo 2:4) **Rafiki, neno kubwa kupita yote ni kujua hakika ya kwamba wewe ni ndani ya njia ya kweli ambayo inakufikisha kwa Mungu.**

Ndani ya masomo haya yanayoitwa *"Njia ya Haki"* tutajifunza Maandiko Matakatifu kuanza na mwanzo. Maana yake, tutajifunza juu ya habari za manabii wa Mungu mmoja mmoja kuanza na nabii wa kwanza kufika hata nabii wa mwisho. Neno la Mungu lina mwanzo na mwisho. Hivi tunataka kuwaza juu ya habari ndani ya Maandiko tukianza pahali Mungu alipoanza yeye mwenyewe, ndipo kwa mwanzo kabisa.

Tutajifunza maneno makubwa mengi juu ya Mungu na manabii. Tutaona ya kwamba hata kama kuna **manabii wengi** walioandika Maandiko Matakatifu, **kuna Mmoja tu** ambaye aliwaongoza ndani ya maneno waliyoandika, ndiye **Mungu**. Ndani ya Maandiko ya manabii kuna **maneno mengi**, lakini **kuna habari kubwa moja tu** ndani ya maneno haya yote, **ndiyo Habari Njema juu ya namna gani mtu anaweza kufanyizwa kuwa mwenye haki mbele ya Mungu.**

Hivi, tunaomba uweze kuweka roho sana juu ya masomo haya ya *"Njia ya Haki"*. Mungu anasema ndani ya Neno lake ya kwamba *"anawapa zawabu wale ambao wanamtafuta."* (Waebrania 11:6). Anatoa ahadi hii kwa wale ambao wanamtafuta na **roho moja**: *"Nanyi mutanitafuta, na **kuniona**, wakati mutakaponitafuta kwa **moyo wenu wote"*** (Yeremia 29:13).

Hapa kwa *"Njia ya Haki"*, tutaonyesha maneno tunayojua juu ya Mungu na Neno lake. Unajua kama Mungu ni namna gani? Au kama Shetani alitoka wapi? Unajua kwa nini Mungu aliumba mtu? Au namna gani zambi iliingia dunia nzuri sana ambayo Mungu aliumba? Umesoma habari za ajabu juu ya nabii wa Mungu Noa, na garika? Unajua kweli maneno ambayo manabii waliandika? Unajua kwa sababu gani Abrahamu aliitwa *"Rafiki ya Mungu"*? Unaweza kueleza waziwazi habari za manabii kwa watoto wako au rafiki zako?

Elfu za miaka mbele, nabii Yobu aliuliza, ***"Mtu anaweza kuwa na haki mbele ya Mungu namna gani?"*** (Yobu 9:2). Unajua jibu la Mungu kwa ulizo la Yobu? Unajua namna gani unaweza kuwa na

haki mbele ya Mungu? Unajua kabisa kabisa ya kwamba zambi zako zimeondoshwa? Ukitaka kujua jibu la Mungu kwa ulizo hili na maulizo mengi mengine, tunakuomba kusoma na bidii masomo ya mfulizo huu, ndio *Njia ya Haki*. Kweli, Neno la Mungu ni lenye maana sana; ni la ajabu, hai, na lenye uwezo. Na kumbuka neno lingine ndilo hili: Neno la Mungu halifichi kitu. Linaonyesha hali ya kweli ya mtu wazi kabisa. Maandiko Matakatifu yanasema: "*Hakuna kiumbe kinachofichwa mbele yake, lakini vitu vyote ni utupu na kufunuliwa mbele ya macho yake yeye aliye na maneno yetu.*" (Waebrania 4:13)

Ndani ya saa inayobaki leo tunataka kusema juu ya kweli kubwa moja ambayo inatupasa kufahamu. Ni kweli hii: **Mungu amesema**! Mungu, Mjuu zaidi, amesema! Mungu amesema na watu. Maana, Mungu anataka kusema na **wewe.** Hizi ndizo habari za ajabu! Ukipokea barua toka Président, utalisoma? Utaweka roho juu ya maneno ambayo alikuandikia ndani ya barua? Ungeweka roho juu ya maagizo ya President? Zaidi sana inatupasa kuweka roho wakati Mungu Mjuu Sana anaposema nasi!

Mungu amesema na mtu namna gani? Maandiko Matakatifu yanatupasha, "*Mungu, aliyesema zamani na baba zetu katika **manabii** kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi...*" (Waebrania 1:1). Mungu amesema na watu kwa njia ya manabii. Alichagua watu fulani kutangaza Neno lake na kuliandika.

Mungu angaliweza kuandika Maandiko Matakatifu yeye mwenyewe au angaliweza kutumika na malaika kuyaandika. Lakini hakufanya hivi. Alichagua **watu** kuyaandika kwa yeye. Tunaita watu hawa **manabii.** Manabii wa Mungu walikuwa kama karani. Mungu aliweka ndani ya roho zao maneno ambayo iliwapasa kuandika, nao waliyaandika kwa Mungu. Kwa sababu hii Neno la Mungu linasema, "*Mukijua neno hili kwanza, ya kwamba hakuna unabii katika maandiko unafasiriwa kama mtu fulani tu anavyopenda. Maana unabii wo wote haukuletwa kwa mapenzi ya mtu, lakini watu walisema yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.*" (2 Petro 1:20,21)

Hivi tunaona ya kwamba Mungu amesema na watu kwa njia ya manabii ambao alichagua. Na manabii hawa waliandika maneno ya Mungu ndani ya vitabu ili wazazi wetu na sisi sote tulio hai leo tuweze kujua maneno yote ambayo Mungu anataka sisi kujua.

Rafiki, kumbuka saa zote: Mungu amesema, naye **anataka kusema nawe.** Maneno yote ambayo Mungu alisema nasi kwa njia ya manabii wake yana faida kwasi tulio hai leo.

Labda watu wengine wanafikiri, "Ee, mimi sihitaji kujua maneno manabii wa zamani waliyosema. Maneno yao hayana faida kwami. Kila nabii alikuwa na kazi fulani ambayo ilimpasa kufanya. Nabii fulani alikuja, alitimiza kazi yake na alikufa. Mwingine alikuja, alitimiza kazi aliyopewa, akakufa . . . vivi hivi. Sisi tunaoishi leo hatuhitaji kujua maneno manabii wa kwanza waliyosema!" Wewe unafikiri hivi vilevile? Mungu hakubali mawazo haya! Sikia maneno Mungu anayosema.

> *"Kweli ninawaambia ninyi, Hata mbingu na inchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja [herufi ndogo zaidi za lugha ya wakati ule] haitaondoka, hata yote yatimie. Basi mtu ye yote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kufundisha watu hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni!"* (Matayo 5:18,19) *"Miili yote ni kama majani, na utukufu wao wote kama ua la majani. Majani yanakauka, na ua lake linaanguka; lakini Neno la Bwana linadumu hata milele!"* (1 Petro 1:24,25) *"Kila andiko limepewa kwa maongozi ya Mungu, na linafaa kwa mafundisho, na kwa kuonya watu juu ya makosa, na kwa kuwaongoza, na kwa mafundisho katika haki!"*
>
> (2 Timoteo 3:16)

Kweli, maneno yote manabii waliyoandika yana faida kubwa, kwa sababu yaliandikwa ili watu wa kila muda waweze kujua njia ya wokovu ambayo Mungu alitengeneza. Unajua maneno manabii wa Mungu yaliyoandika? Mungu anataka sisi kujua Neno lake, kuliamini na kulitii! Kwa sababu hii Maandiko yanasema: *"Tuna neno la unabii lililo imara zaidi, na inawafaa ninyi kuliangalia kama taa inayongaa katika pahali pa giza!"* (2 Petro 1:19)

Ndiyo, mara nyingine tunasikia watu wanaoshindana na Kitabu cha Mungu (ndiyo Biblia), wakisema, "Haifai kukitegemea! Kuna makosa mengi ndani yake. Watu wamekigeuza kwa hila ..." **Lakini mtu anayeshindana na Neno la Mungu anashindana na Mungu Mwenyewe.** Watu wa taifa lingine wanavyosema, "Haifai yayi kushindana na mwamba!" Neno la Mungu ni Mwamba, na mtu ni yayi! Neno la Mungu ni kamilifu na hakika, bila makosa ndani yake! Hakuna mtu anayeweza kugeuza Neno la kweli la Mungu! Mungu ni mkubwa, na anaweza kulinda Neno lake la milele! Hili ndilo neno Bwana Mwenyewe alilosema ndani ya vitabu vya Habari Njema: ***"Mbingu na dunia zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kabisa"*** (Matayo 24:35).

Watu wengi wanajaribu kushindana na Neno la Mungu kwa sababu linafunua hali ya kweli ya mioyo yao. Sikiliza maneno Mungu anayosema juu ya Neno lake mwenyewe: *"Neno la Mungu ni* ***hai, lenye nguvu*** *na ukali wa upanga unaokata ngambo mbili, likitoboa hata kutenga nafsi na roho, na viungo na mafuta ndani ya mifupa,* ***nalo ni jepesi kufahamu mawazo na makusudi ya moyo."*** (Waebrania 4:12)

Maandiko Matakatifu yanafaa hata leo kwa kila mtu. Hakuna neno kubwa kupita Neno la Mungu. Lakini Neno la Mungu ni kama ugali pamoja na samaki. Kila mtu atakubali ya kwamba ugali na samaki ni chakula kitamu sana, cha kusaidia mwili. Lakini kama nisipokikula hakina faida kwa mimi. Ni lazima kwangu kula mimi mwenyewe. Vivyi hivyo ni lazima kwangu kuonja Neno la Mungu linalokulisha roho yangu, kama nikitaka kupata faida yake. Kwa sababu hii Mungu anasema ya kwamba *"Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno linalotoka katika kinywa cha Mungu"* (Matayo 4:4). Ni *"wenye* ***njaa na kiu*** *kwa haki"* tu watakaoshibishwa (Matayo 5:6). Una njaa kwa Neno la Mungu? Ni chakula, chakula kitamu. Si chakula kinacholisha mwili, lakini kinalisha roho na nafsi yako.

Mbele ya kuacha kwa leo kuna neno moja lingine tunalotaka kusema wazi. Ndani ya mafundisho haya hatutegemei neno lo lote lingine ila yale yanayoandikwa ndani ya Maandiko ya manabii wa Mungu. Sisi tunaotayarisha masomo haya hatujui neno ila yale ambayo Mungu alitujulisha ndani ya Maandiko Matakatifu. Neno mwandishi Yoane alilosema ndani ya Habari Njema ni kweli: *"Mtu hawezi kupokea kitu isipokuwa amepewa toka mbinguni"* (Yoane 3:27) Kwa sababu hii hatuwezi kutangaza neno lo lote lisilotangazwa na Mungu ndani ya Neno lake kwa njia ya manabii wake. Tunaogopa kabisa kutegemea maneno sisi wenyewe tunayojua au mambo yo yote mengine. **Tunategemea Neno la Mungu peke yake.** Tunataka kutangaza maneno Mungu aliyosema ndani ya Neno lake kwa njia ya manabii wake.

Unajua maneno Mungu aliyosema ndani ya Maandiko ya manabii? Wewe ni katikati yao walio na njaa na kiu kwa Neno la Mungu na kwa haki ya kweli? Mungu amefunua ukubwa wake wote, haki yake, mapendo yake na mapenzi yake ndani ya Neno lake takatifu. Tunakuita kutafuta Maandiko ili uweze kufahamu kabisa maneno Mungu aliyosema. Neno la Mungu linatuambia ya kwamba *"Yote yaliyoandikwa, yameandikwa kwa mafundisho yetu, hata kwa saburi na faraja ya maandiko tuwe na* ***tumaini****."* (Waroma 15:4)

Sisi sote tujue neno hili moja kabisa: **Mungu amesema naye**

anataka watu wote kusikiliza na kuishi! Wazee na vijana, wanaume na wanawake, watajiri na wamasikini, Mungu anasema kwa watu wote mmoja mmoja *"Tegeni masikio yenu, na muje kwangu; sikieni na nafsi zenu zitaishi!"* (Isaya 55:3)

~~~~~~~~~~~~

Asante kwa kusoma, Rafiki. Ndani ya Somo 2, tutajifunza juu ya ulizo hili kubwa:

"Mungu ni namna gani?"

Mungu akubariki, na sisi sote tukumbuke mwito mkubwa wa Mungu kwa sisi sote mmoja mmoja:

> ***"Tegeni masikio yenu, na muje kwangu; sikieni na nafsi zenu zitaishi!"*** (Isaya 55:3)
~~~~~~~~~~~~

SOMO 2

MUNGU NI NAMNA GANI?

MWANZO 1

Salama iwe pamoja nawe, rafiki msomaji. Tunakusalimu kwa jina la Mungu wa salama, anayetaka kila mtu kufahamu, kuamini, na kupokea njia ya haki aliyotayarisha, na kupata salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuendelea na Somo 2 la *Njia ya Haki.*

Ndani ya masomo haya tutaona **habari za manabii wa Mungu,** mmoja mmoja. Na tutatafuta vilevile Maandiko Matakatifu yaliyoandikwa na manabii hawa yanayotangaza njia ya haki ambayo Mungu aliamuru ili watu waweze kuhesabiwa haki mbele yake.

Ndani ya somo la kwanza, tulijifunza juu ya maandiko ya manabii. Tuliona ya kwamba kulikuwa na manabii wengi walioandika sehemu ya Maandiko Matakatifu, lakini kuna Mmoja tu ambaye aliwaongoza ndani ya maneno waliyoandika. Yule Mmoja ni Mungu. Ndani ya somo la kwanza tulikuacha na wazo kubwa moja, ndilo hili: **Mungu amesema!** Amesema na watu kwa njia ya manabii naye anataka sisi sote tumsikilize. Mungu anasema nasi kwa njia ya maandiko ya manabii. Mungu hageuki kamwe, na Neno lake haligeuki kamwe vilevile. Mungu amelinda Neno lake ndani ya kila kizazi. *"Maandiko hayawezi kuvunjika"* (Yoane 10:35). *"Dunia inapita . . . lakini Neno la Bwana linadumu kwa milele!"* (1 Yoane 2:17; 1 Petro 1:25). Maandiko yanasema hivi.

Tutaanza mafundisho yetu na **kitabu cha kwanza ndani ya Maandiko Matakatifu.** Kinaitwa ***Tora*** vilevile. Mungu aliongoza mtu mmoja, jina lake Musa, kuandika fungu la vitabu vitano vya kwanza ndani ya Maandiko Matakatifu. Alijulisha Musa maneno ambayo alitaka aandike na Musa aliyaandika. Karibu miaka 3,500 imepita tangu wakati ule.

Kitabu cha kwanza ndani ya fungu hili kinaitwa **Mwanzo**. Kuna sura 50 ndani ya kitabu cha Mwanzo. Kinaitwa Mwanzo kwa sababu ndani yake tunapata habari za maneno yaliyotokea kwa mwanzo.

Lazima tujuane na mambo yanayoandikwa ndani ya kitabu hiki cha kwanza vizuri sana, kwa sababu ni **msingi ambao Mungu aliweka** kutuwezesha kufahamu maneno anayosema ndani ya vitabu vingine vya manabii vinavyofuata. Kutafuta yanayoandikwa ndani ya kitabu hiki, kutatusaidia kujua maneno mengi kupita juu ya kweli nyingi. Tutajifunza juu ya Mungu na kama yeye ni namna gani. Tutajifunza juu ya malaika na Shetani, mbingu na dunia, nyama na watu. Tutaona kama zambi iliingia duniani na kuleta uharibifu na huzuni kubwa. Lakini tutaangalia vilevile njia ya wokovu ambayo Bwana Yesu alitayarisha ili wenye zambi waweze kurudi karibu na Mungu na kuwa na upatano mzuri sana naye. Ndani ya kitabu hiki cha kwanza, tutaona watu wa kwanza, zambi ya kwanza, na mwuaji wa kwanza. Tutasoma juu ya dini za kwanza za uwongo, manabii wa kwanza, na mataifa ya kwanza. Tutawaza juu ya habari za Adamu na Hawa, Kaina na Abeli, Noa na garika, Abrahamu, nabii wa Mungu na kwa nini aliitwa rafiki ya Mungu. Tutaona Isimaeli na Isaka, Esau na Yakobo na Yosefu na ndugu zake waovu. Habari hizi zote ni ndani ya kitabu cha kwanza cha Maandiko . . . na habari nyingi nyingine.

Ndani ya kitabu cha kwanza cha Tora, sura moja na shairi la kwanza, tunasoma neno hili: ***"Katika mwanzo Mungu aliumba mbingu na dunia."*** (Mwanzo 1:1) Ni hapa inapotupasa kuanza somo letu ndani ya Maandiko ya Manabii, kwa sababu ndipo pahali Mungu Mwenyewe anapoanza kitabu chake: "*Katika mwanzo Mungu aliumba mbingu na dunia.*"

Kuna neno kubwa ndani ya shairi hili ambalo inatupasa kuwaza juu yake. Kulikuwa na nini wakati Mungu asipoumba bado mbingu na dunia? Kulikuwa na nini wakati dunia isipokuwa bado? Maandiko yanatupasha ya kwamba hakuna neno lililokuwa . . . ila Mungu. Kwa sababu hii yanasema, "*Katika mwanzo . . . Mungu.*" Kila kitu tunachoweza kuona au kugusa kilikuwa na mwanzo. Hivi zamani kabisa mbingu au dunia, bahari au miti haikuwa. Katika mwanzo, wakati Mungu asipoumba bado mbingu na dunia, jua halikuwa wala mwezi wala nyota zilizo mbinguni sasa. Katika mwanzo hakuna watu wala malaika. Hivi kulikuwa na saa wakati hata neno moja lisipokuwa, hata moja . . ila **Mungu.**

Kwa sababu hii tunasoma ndani ya shairi la kwanza la Maandiko Matakatifu, "*Katika mwanzo **Mungu** aliumba mbingu na dunia.*" Maandiko ***ha***yasemi, "Katika mwanzo Mungu **na** malaika" au "Katika mwanzo Mungu **na** watu." Sivyo. Maandiko Matakatifu

yanatuambia, "*Katika mwanzo* ***Mungu.***" Katika mwanzo, mbele ya kuwa kwa vitu vyo vyote, mbele ya kuwa kwa malaika au watu . . . kulikuwa na Mmoja tu aliyekuwa hai. Yule Mmoja ni **Mungu**!

Shairi hili la kwanza ndani ya Maandiko Matakatifu linatufundisha neno moja, ndilo hili: **Mungu hana mwanzo**. Mungu hakuumbwa katika mwanzo. Mungu ni Bwana wa Milele. Kila kitu sisi tunachojua na kuona hapa duniani kilikuwa na mwanzo. Lakini Mungu hakuwa na mwanzo. Hana asili. Hakuna mwingine aliye sawa naye. Yeye tu alikuwa katika mwanzo. Hakuzaliwa. Hakuumbwa na hakujiumba mwenyewe. Kwa sababu hii tunasoma ndani ya Maandiko Matakatifu, "*Katika mwanzo* ***Mungu.***" Yeye tu hakuwa na mwanzo. Ni yeye aliye tangu milele na anayeishi kwa milele. Jina lake ni "Mungu wa Milele." Alikuwa jana namna alivyo leo. Atakuwa kwa milele namna alivyokuwa jana. **Mungu hageuki kamwe.**

Tunaweza kujifunza neno lingine shairi hili linalosema, "*Katika mwanzo Mungu aliumba mbingu na dunia.*" Ni neno hili: **Mungu ni mkubwa**. Mungu aliyeumba kila kitu ni mkubwa kupita kila kitu na kila mtu. Yeye ni Bwana wa Muumbo. Kweli, sisi tunaojua Mungu, tunaweza kusema na roho yetu yote, "*Allahu Akbar!*" (*Mungu ni mkubwa kupita* kwa Kiarabe) Mungu ni mkubwa! Hakuna mwingine sawasawa naye. Ana uwezo kupita vitu vyote duniani: bahari, upepo, jua na nyota! Yeye ni mwenye hekima kuliko pepo na watu. Anastahili kupokea utukufu kwa milele! Kama yule anayejenga nyumba ni mkubwa kupita nyumba, vivyo hivyo Mungu ni mkubwa kupita kila kitu kwa sababu Mungu ndiye aliyeumba kila kitu. Mungu ni mkubwa! Anaishi kwa uwezo wake mwenyewe. Hategemei kitu cho chote. Hategemei mtu ye yote. Mungu ni mkubwa kupita vyote. Hahitaji kitu cho chote. Hahitaji mtu ye yote. Yeye ndiye Yule Mkuu!

Sisi watu tunahitaji maneno mengi. Kila siku inatupasa kuvuta pumzi na kulala usingizi, kula na kunywa. Tunahitaji jua na mvua, vyakula na maji, mavazi na nyumba, baba na mama, rafiki na mali na maneno mengi mengine. Kweli tuna mahitaji mengi sana! Lakini, Bwana aliyeumba kila kitu hahitaji kitu. Hasikii njaa. Hasikii kiu. Hachoki kamwe. Hana mwili kama mtu. Hana vizuizo. Hana mwisho. Yeye ni Mungu wa milele. **Yeye ni mwenye uwezo wote.**

Ulizo kubwa sana ndilo hili: Kama Mungu asipokuwa kama mtu na hana mwili kama miili yetu, yeye ni namna gani? Maandiko yana jibu lililo wazi kabisa kwa ulizo hili. Yanasema, "*Mungu ni* ***roho****, nao*

wenye kumwabudu sharti wamwabudu katika roho na kweli." (Yoane 4:24) Mungu ni namna gani? **Mungu ni roho**. Mtu ni mwili na roho, lakini Mungu ni roho tu. Hakuna mpaka kwa Roho ya Mungu. Yeye ni pahali pote, juu kupita kila kitu na kila mtu. Anaona yote. Usiku na mchana ni sawasawa kwa Mungu. Ukijificha chumbani mwako, Mungu ni pale naye anakuona. **Mungu anajua maneno yote**. Anajua mawazo yako na makusudi ya moyo wako. Mungu ni mkubwa!

Hivi Mungu ni namna gani? Labda tunaweza kujumlisha maneno tuliyojifunza kwa njia hii: **Mungu si kama mtu ye yote.** Mungu ni Mungu na hakuna mwingine kama yeye! Ndani ya masomo mengine tutajifunza kupita na kupita juu ya namna Mungu alivyo. Ndani ya Maandiko Matakatifu, Mungu ana mia za majina. Yeye ni BWANA. Mjuu sana. Mwenyezi. Mwumba. Mwumba wa uzima. Nuru. Mwenye Haki. Mtakatifu. Mwenye Rehema. Mungu wa Mapendo. Yeye ni Mungu aliye hai na Mungu wa kweli!

Kweli, Mungu, aliyeumba mbingu na dunia kwa mwanzo, ni **Yule mkuu**. Kwa sababu hii Maandiko yanasema,

> *"Tazameni namna ya utajiri wa akili na maarifa ya Mungu! . . . Kwa maana vitu vyote vinatoka kwake, na viko kwa uwezo wake, na viko kwa yeye"* (Waroma 11:33,36). *"Mfalme wa wafalme, na Bwana wa wabwana: ni yeye peke yake asiyekufa, akikaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa; wala hapana mtu ambaye alimwona, wala anayeweza kumwona: ndiye mwenye heshima na uwezo wa milele. Amina."* (1 Timoteo 6:15,16)

Ndani ya sura nyingine ya Maandiko, Musa, nabii wa Mungu, anasifu Mungu ndani ya wimbo mzuri sana akisema, *"Makubwa na ya ajabu ni matendo yako, Bwana Mungu Mwenyezi: njia zako ni za haki na za kweli, mfalme wa mataifa. Ni nani ambaye hakuogopi, Ee Bwana, na kutukuza jina lako? Kwa sababu wewe peke yako ni mtakatifu."* (Ufunuo 15:3,4) Mungu ni mkubwa. Hii ndiyo kweli ambayo shairi la kwanza la Neno la Mungu linatufundisha wakati linaposema, *"Katika mwanzo **Mungu**!"*

Hivi, rafiki, tuchunge ndani ya mafikiri yetu kweli tuliyosikia leo: *"Katika mwanzo Mungu."* Mungu tu alikuwa katika mwanzo na hivi **Mungu tu** anaweza kutufunulia kweli juu ya maneno yaliyotokea katika mwanzo. **Mungu tu** anaweza kutufunulia kweli juu ya maneno yatakayotokea kwa wakati wa kuja. Na ni **Mungu tu** anayeweza kutufunulia kweli juu yake mwenyewe.

Ndiyo, tunajua ya kwamba kuna watu wanaosema, "Hakuna mtu anayeweza kujua Mungu au nini itatokea kwa wakati wa kuja! Lakini Maandiko ya manabii yanatuambia ya kwamba **tunaweza kujua Mungu,** na ya kwamba **tunaweza kujua pahali gani tutakaposhinda kwa milele.** Maana Neno la Mungu linasema,

> *"Ninawaandikia ninyi . . . ili **mujue** ya kwamba muna uzima wa milele! na ili "tu**jue** yeye aliye ya kweli . . . Mungu wa kweli, na uzima wa milele"* (1 Yoane 5:13,20). *"Jicho halikuona, wala sikio halikusikia, wala hayakuingia katika moyo wa mtu, maneno Mungu aliyotengenezea wenye kumpenda. **Lakini Mungu aliyafunua kwetu kwa Roho yake**, kwani Roho anatafuta maneno yote, hata mafumbo ya Mungu."* (1 Wakorinto 2:9,10)

Wewe unayesoma maneno haya leo, **unajua Mungu wewe mwenyewe?** Au kwa mafikiri yako yeye ni Mwumba tu aliye mbali sana nasi hata hatuwezi kumjua? Rafiki mpenzi, Mungu anataka umjue na kuishi kwa milele! Maandiko ya Manabii yanatufundisha namna gani tunaweza kuwa na upatano wa ajabu, wa karibu sana na Mungu, lakini lazima tufungue masikio yetu, na nia zetu, na mioyo yetu kwa maneno ambayo Mungu anasema nasi ndani ya Neno lake. Sikiliza maneno Mungu anayosema ndani ya Maandiko Matakatifu: *"Muniangalie, na mwokolewe, miisho yote ya dunia; kwani mimi ni Mungu, na hapana mwingine!"* (Isaya 45:22)

~~~~~~~~~~~~~~

Ndani ya Somo 3, Mungu akitaka, tutasoma juu ya neno la kushangaza, ndilo: Malaika na Shetani. Unajua habari za Mwanzo wao na kama walitoka wapi?

Mungu akubariki na tunaomba uweze kukaa kuwaza juu ya shairi lile ndani ya Maandiko Matakatifu linalosema,

> ***"Mungu ni Roho, nao wenye kumwabudu sharti wamwabudu katika roho na kweli."*** (Yoane 4:24)
~~~~~~~~~~~~~~

SOMO 3

SHETANI NA MALAIKA

ISAYA 14; EZEKIELI 28

Salama iwe pamoja nawe, rafiki. Tunakusalimu leo kwa jina la Mungu wa salama. Asante kwa kufika kusoma Somo 3 la mfulizo *Njia ya Haki*.

Ndani ya Somo 2, tulisoma shairi la kwanza la Maandiko Matakatifu, linalosema: "*Katika mwanzo Mungu aliumba mbingu na dunia.*" (Mwanzo 1:1) Tuliona ya kwamba kila kitu kina mwanzo ila Mungu. Katika mwanzo, wakati hakuna kitu, kulikuwa na mmoja tu aliyekuwa hai, ndiye **Mungu**. Yeye tu alikuwa katika mwanzo. Mungu ni Bwana wa milele. Mungu ni mkubwa na hakuna mwingine kama yeye!

Mungu hana mwanzo na hana mwisho. Hahitaji kitu. Hana kizuizo. Mungu ni roho na anaweza kuwa pahali pote pamoja. Yeye ni juu ya kila kitu na kila mtu. Anajaza mambo yote. Anaona maneno yote. Anajua kila kitu. Hakuna mwingine kama yeye. Mungu ni mkubwa! Kwa sababu hii Maandiko Matakatifu yanasema, "*Ni yeye peke yake asiyekufa, akikaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa; wala hapana mtu ambaye alimwona wala anayeweza kumwona: ndiye mwenye heshima na uwezo wa milele. Amina.*" (1 Timoteo 6:16).

Leo tunaanza somo letu la tatu ndani ya Maandiko ya Manabii. Tunataka kuwaza juu ya mafundisho ya Neno la Mungu juu ya **malaika na Shetani**. Unajua kama malaika wanatoka wapi? Au pahali gani Shetani na pepo wabaya wanapotoka? Tusingeweza kujua maneno namna hii kama Mungu asingetujulisha. Lakini Mungu alituambia maneno haya ndani ya Neno lake. Hivi tutafute Maandiko Matakatifu kwa bidii ili tuweze kujua kweli juu ya malaika na Shetani.

Tunakukumbusha ya kwamba ndani ya masomo haya *Njia ya Haki* tunajifunza Maandiko ya Manabii toka mwanzo hata mwisho. Hivi ndani ya somo la mbele, tulijifunza juu ya Mungu mwenyewe, kwa sababu Mungu ndiye aliyekuwa kwa mwanzo. Na, ikipendeza Mungu, ndani ya somo litakalofuata, tutapasha juu ya namna gani

Mungu alifanya dunia na vyote vilivyo ndani yake. Lakini mbele ya kuumba watu na dunia ambayo tunakaa ndani yake, aliumba kitu kingine kwanza: **malaika**.

Neno la Mungu linatuambia maneno mengi juu ya malaika. Leo tutajaribu kujumlisha kweli kubwa zaidi juu ya viumbe hivi. Neno la Mungu linatujulisha ya kwamba zamani sana Mungu, aliye roho, aliumba **roho wengi wengine** wanaoitwa ***malaika***. Maandiko yanasema ya kwamba *"malaika wote ni roho za kutumikia."* (Waebrania 1:14) Na Mungu anafanya *"malaika zake kuwa pepo, na watumishi wake ndimi za moto."* (Waebrania 1:7) Hivi Maandiko yanatufundisha ya kwamba malaika, kama Mungu, ni roho na zinasawanishwa na pepo na moto. Hatuwezi kuona pepo. Na hakuna mtu anayeweza kugusa moto. Ni vivyo hivyo na malaika za Mungu. Mungu hakuwaumba na miili kama miili yetu. Sisi watu tuko mwili na roho. Lakini malaika ni roho tu. Kwa sababu hii hatuwezi kuwaona.

Mungu aliumba malaika ngapi? Maandiko yanasema nini juu ya neno hili? Yanasema Mungu aliumba roho wengi sana, wengi kupita uwezo wetu kuyahesabu. Kule juu mbele ya Mungu *"kuna malaika wengi, elfu kumi mara elfu kumi."* (Ufunuo 5:11) Mungu, Bwana wetu ni mkubwa! Mungu, asiye na kizuizo, aliumba kwa yeye mwenyewe elfu na elfu za malaika wema na wenye hekima. Maandiko yanatujulisha ya kwamba malaika za Mungu wana **uwezo mkubwa**. Wana uwezo mkubwa kupita sisi. Lakini, kama viumbe vyote, wana vizuizo. **Hawana uwezo wote**. Hawawezi kuwa kila pahali, na hawajui maneno yote. Ni viumbe tu. Kuna Mmoja tu asiye na kizuizo. Ni Mungu.

Lazima tufahamu neno lingine juu ya malaika, ndilo hili: Wakati Mungu alipoumba malaika wao wote walikuwa **viumbe vitakatifu.** Kwa mwanzo malaika waovu hawakuwa. Shetani hakuwa kwa wakati wa mwanzo. Roho wabaya hawakuwa. Mungu hakuumba malaika waovu.

Lazima tukae kukumbuka kweli hii: Mungu anaweza kufanya maneno yote, ila moja. Hawezi kufanya maovu. Tusisahau neno hili. Mungu hawezi kuumba kilicho kibaya kwa sababu yeye ni **mwema**. Mungu hawezi kuanguka kwa sababu yeye ni mkamilifu. Zambi haiwezi kutoka kwake kwa sababu yeye ni **mtakatifu**. Kila neno Mungu analowaza, na kusema, na kufanya ni zuri, kamilifu na takatifu. Kwa sababu hii Maandiko yanasema, *"Mungu hawezi kujaribiwa na maovu, wala yeye mwenyewe hajaribu mtu."* (Yakobo 1:13) Basi, uovu unatoka wapi? Tutaona jibu la Mungu nyuma kidogo. Lakini kwanza tujifunze neno lingine juu ya malaika.

Neno tunalotaka kujua ndilo hili: Kwa nini Mungu aliumba malaika? Maandiko yanatujulisha ya kwamba Mungu aliwaumba ili waweze kuwa pamoja na Mungu **kumpenda, kumsifu na kumtumikia** katika furaha ya mbingu kwa milele. Wao wote walikuwa mali ya Mungu kwa sababu Mungu aliwaumba. Wao wote walikaa "nyumbani" mwa Mungu, maana yake, juu mbinguni, mbali kupita mwezi, jua na nyota. Unajua ya kwamba kuna **pahali fulani Mungu anapokaa?** Ndiyo, ndani ya somo la mbele tulijifunza ya kwamba Mungu ni pahali pote. Lakini Maandiko yanafundisha vilevile ya kwamba kuna pahali pamoja pa ajabu ndani ya ulimwengu palipo patakatifu, na kujazwa na nuru na uzuri, pahali Mungu anapokaa na kuonyesha utukufu wake wote. Ni pahali manabii wa Mungu wanapoita "*Pahali Mungu alipo*" au ***"Paradiso***" au "*Mbingu*". Ni pahali Mungu anapokaa pamoja na malaika zake watakatifu.

Kuna neno lingine ambalo inatupasa kujua juu ya malaika. Ni hili: Malaika **wote si sawasawa**. Malaika wengine ni wazuri kupita na wenye mapambo kupita wengine. Malaika wengine wanazunguka kiti cha Mungu mbinguni. Wengine wanasaidia na kulinda watu. Malaika wengine, kama **Gabrieli** na **Mikaeli,** wanasimama mbele ya Mungu na wanatumwa kufanya kazi fulani duniani.

Malaika wengine ni kama waangalizi wa wengine. Umesikia jina la **Lusifero** mbele? Neno la Mungu linatujulisha kwamba kulikuwa na wakati Lusifero alipokuwa mkubwa wa malaika wote. Ukijua habari za Lusifero, unajua pahali **Shetani** anapotoka.

Maandiko yanatupasha ya kwamba wakati Mungu alipoumba malaika, **Lusifero alionekana vizuri kupita wote na alikuwa mwenye hekima na mwenye uwezo kupita wao wote.** Maana ya jina hili Lusifero ni "*Mwenye Kungaa*". Lusifero alipita malaika wote wengine kwa njia ya kuonekana, na kujua na hekima, kwa uwezo na amri. Mungu alimpa maneno haya yote. Ingalipasa Lusifero kuabudu Mungu, kumpenda na kumtii kwa milele, kwa sababu Mungu alimwumba na kumbariki sana.

Lakini Neno la Mungu linasema ya kwamba siku moja Lusifero alikuwa na zarau kwa Mungu, na roho yake ilijazwa **kiburi**. Lusifero alisema maneno kama haya: "*Ninaonekana vizuri sana ... nina akili nyingi ... nitapanda mbinguni; nitanyanyua kiti changu cha ufalme juu kuliko nyota za Mungu; ... nitakaa juu ya kiti chake cha kifalme! Nitajifanyiza kufanana na Mungu Mjuu Sana!*" (ona Isaya 14:13,14)

Neno la kushangaza kabisa! Lusifero, asiyekuwa na neno ila yale

ambayo alipewa na Mungu, alitaka kuiba utukufu wa Mungu, Mjuu Sana! Wala si Lusifero tu aliyeasi Mungu, lakini **sehemu moja ya tatu** ya malaika waliokuwa mbinguni walichagua kugeukia Bwana Mungu, na kufuata Lusifero ndani ya zambi yake. (Ona Ufunuo 12:4)

Lakini Mungu ni Mungu, na Mungu alijua kila neno ambalo Shetani na malaika zake walikusudi kufanya. Kama tulivyojifunza ndani ya somo letu la mbele, hakuna mtu anayeweza kufanya neno kwa siri Mungu asilojua kwa sababu Mungu anajua kila neno hata wakati lisipotokea bado. Mungu alijua zambi iliyokuwa moyoni mwa Lusifero na mioyoni mwa malaika ambao walimfuata.

Halafu nini lilitokea? Mungu alifanya nini? Aliruhusu Lusifero ambaye alimwasi, kumkomboa? Mungu aliweza kukubali zambi? **Mungu aliweza kukaa pamoja na zambi ya kiburi na uasi?** Haiwezekani hata kidogo! Maandiko ya manabii yanatufundisha ya kwamba Mungu, Mungu wetu, ni mtakatifu na hawezi kuangalia zambi. Mungu hawezi kukubali zambi, na hataacha mwingine kupata utukufu wake. Mungu ni mmoja tu; hakuna mwingine kama yeye; hakuna mwingine ambaye anaweza kumkomboa!

Hivi, Maandiko yanasema Mungu **alifukuza Lusifero na malaika zake waovu.** Hawakuweza kuishi mbinguni, nyumbani mwa Mungu tena kwa sababu walikuwa wamefanya zambi wakati walipotaka kukomboa Mungu. Kwa sababu hii **Mungu alifukuza Lusifero na malaika zake waovu.** Ni lazima kwa Mungu, aliye mtakatifu, kuhukumu na kuazibu kila kiumbe ambaye anamwasi.

Wakati Lusifero alipokwisha kufanya zambi, Mungu aligeuza jina lake. Hakuitwa tena Lusifero, "*mwenye kungaa*", lakini ***Shetani.*** Maana ya Shetani ni "*Adui*". Lusifero, au Shetani, aligeuka adui ya Mungu. Na, kama unavyojua, Shetani na malaika zake wanakataa Mungu na yote yaliyo mema hata sasa. Wanakataa Neno la Mungu na kulikana. Shetani anashindana na Mungu na anajaribu kuharibu na kuzuiza kazi za Mungu. Lakini Mungu ni Mwamuzi mkubwa, na hakuna kiumbe anayeweza kumshinda!

Maandiko Matakatifu yanatujulisha ya kwamba Mungu, nyuma ya kufukuza Shetani na malaika zake, aliumba **moto wa milele** usiozimishwa kamwe. Kwa wakati wa kuja Mungu atatupa ndani ya moto huu Shetani na malaika zake, na watu wote ambao wanawafuata. Hivi inaandikwa ndani ya Ufunuo 20:10, *"Watateswa mchana na usiku hata milele na milele."*

Lakini Maandiko yanafundisha ya kwamba Shetani si katika moto kwanza. Neno la Mungu linasema **Shetani ni duniani** na anashindana na Mungu. Yeye ni mharibu. Anataka kuharibu kazi ya Mungu. Anataka watu ambao Mungu aliumba, kupotea na kwenda kwa moto pamoja naye. Neno la Mungu linasema ya kwamba **zaidi ya watu wanatawaliwa na Shetani, lakini hawajui neno hili** kwa sababu Shetani ni **mdanganyi.** Hivi Maandiko yanasema, "*Shetani anajigeuza awe malaika ya nuru.*" (2 Wakorinto 11:14) Anajaribu kudanganya watu ili wasiweke roho juu ya Neno la Mungu. Kwa sababu hii mmoja wa manabii aliandika, "*Muwe na kiasi na kuangalia; adui yenu Shetani, kama simba ya kunguruma anazungukazunguka akitafuta mtu ammeze.*" (1 Petro 5:8). Kaa na ange! Shetani anataka kukuharibu kwa milele!

Lakini Mungu asifiwe kwani ametupa sisi Neno lake ili tuweze kuepuka uwezo wa Shetani. Maandiko yanasema, "*Mutajua kweli, na kweli itawaweka ninyi huru!*" (Yoane 8:32) Unajua kweli ambayo inaweza kukufungua toka mashauri mabaya sana ya Shetani? Usisahau: **Shetani** ni mwenye hekima kupita sisi. **Lakini Mungu** ni mwenye hekima kupita Shetani. **Shetani** ni mwenye nguvu kupita sisi. **Lakini Mungu** ana nguvu kupita Shetani. Unajua Neno la kweli linaloweza kukufungua toka uwezo wa Shetani? Watu wengi hawapendi kusikia kweli ya Mungu. Kwa nini watu wanakataa kusikia kweli? Ni kwa sababu Shetani amewadanganya. Anawasukuma kuamini maneno yasiyo kweli. Ndiyo, mara nyingine kweli si tamu kusikiliza. Lakini ukijua kweli ya Neno la Mungu, na kuiamini, utafunguliwa toka uwezo wa Shetani. **Kweli ya Mungu** inaweza kufungua watu toka **wongo za Shetani**. Lakini lazima ujue kweli na kuiamini!

Sikiliza Neno la Mungu, "*Wapenzi, **musiamini** kila roho, lakini **jaribuni kila roho, kama zimetoka kwa Mungu;** kwa sababu manabii wa uwongo wengi wametokea duniani.*" (1 Yoane 4:1) "*Musibeue unabii; lakini jaribuni mambo yote; shikeni lililo jema; mujitenge na ubaya wa kila namna.*" (1 Watesalonika 5:20-22) **Unajua kweli kweli maneno ambayo manabii waliandika?** Unafahamu Neno la kweli? Unaliamini ndani ya moyo wako?

~~~~~~~~~~~~~~~

Tumekwisha kufika kwa mwisho wa Somo 3. Ndani ya Somo 4 utaona namna gani Mungu aliumba dunia.

Kaa kuwaza juu ya ahadi ya ajabu ndani ya Neno lake linalosema,

"Mutajua kweli, na kweli itawaweka ninyi huru." (Yoane 8:32)
~~~~~~~~~~~~~~~

SOMO 4

NAMNA MUNGU ALIVYOUMBA DUNIA

MWANZO 1

Salama iwe kwako, rafiki msomaji, kwa jina la Mungu wa salama, anayetaka watu wote kufahamu, kuamini na kupokea njia ya haki ambayo ametayarisha na kuwa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuendelea leo na mfulizo wetu *Njia ya Haki*.

Ndani ya somo la mbele tuliona maneno ambayo manabii wanasema juu ya **malaika na Shetani.** Tulijifunza ya kwamba kwa wakati wa mwanzo, Mungu aliumba roho elfu nyingi na kuwaita malaika. Mmoja wa malaika hawa alikuwa na akili kupita wengine na alionekana vizuri kupita malaika wengine. Jina la malaika huyu alikuwa Lusifero. Lakini siku moja Lusifero alijitukuza mwenyewe moyoni mwake na kuzarau Mungu, na alitaka kukomboa Mungu.

Malaika wengi wengine walichagua kufuata Lusifero ndani ya zambi yake. Hivi Mungu, asiyeweza kukubali wenye kumwasi, alifukuza Lusifero na malaika waovu mbele yake. Aligeuza jina la Lusifero kuwa *Shetani,* maana yake *"Adui"*. Wakati Mungu alipokwisha kufukuza Shetani na malaika zake, aliumba kwa viumbe hawa moto wa milele. Siku nyingine Mungu atatupa Shetani na wote ambao wanamfuata ndani ya moto ule. Lakini Shetani hajawekwa bado ndani ya pahali pale pa uharibifu. Yeye ni duniani, akitafuta kudanganya watu ili wao waweze kuharibiwa vilevile.

Sasa tuwaze juu ya somo la ine la Maandiko ya Manabii. Ndani ya kitabu cha kwanza cha Biblia, ambacho tunaita *"Mwanzo"*, ndani ya sura ya kwanza na mashairi mawili ya kwanza, Maandiko yanasema, *"Katika mwanzo Mungu aliumba mbingu na dunia. Na dunia ilikuwa ukiwa na utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa kilindi."* (Mwanzo 1:1,2).

Katika mwanzo wakati Mungu alipoumba mbingu na dunia, hakuna kitu kilichoishi hapa duniani. Yote ilikuwa ukiwa na giza. Shetani tu na malaika zake walikuwa hapa. Lakini Mungu alikusudi

kuumba watu watakaoweza kujua Mungu, kumpenda na kumtii milele. Lakini mbele ya kuumba mtu, Mungu alikusudi kufanya dunia nzuri sana pahali mtu atakapoweza kukaa vizuri na kusitawi. Ndani ya somo hili tutaona **namna Mungu alivyotayarisha dunia** kwa watu ambao alikusudi kuumba.

Maandiko yanasema nini juu ya namna Mungu alivyoumba dunia? Yanasema, "*Kwa siku sita Bwana akafanya mbingu na inchi, bahari na vyote vilivyo ndani yao.*" (Kutoka 20:11) Sasa tuangalie sura ya kwanza ya Maandiko ya manabii kuona kama Mungu aliumba nini ndani ya siku zile sita.

1) Juu ya siku ya kwanza, Maandiko yanasema,

> "*Roho ya Mungu akatulia juu ya uso wa maji. Mungu akasema: Nuru iwe: na nuru ilikuwa. Mungu akaona nuru ya kama ilikuwa vizuri; Mungu akatenga nuru na giza. Mungu akaita nuru Mchana na giza aliita Usiku. Na ilikuwa mangaribi na ilikuwa asubui, siku moja.*" (Mwanzo 1:2-5).

Hivi siku ya kwanza Mungu aliagiza **nuru** kuwa katika giza. Mungu aliagiza dunia, iliyo kama mpira mkubwa, kuzunguka mara moja kila saa 24. Kwa sababu hii tuna saa 12 za mchana na saa 12 za usiku. Mungu aliumba dunia kuzunguka hivi kwa kutenga nuru na giza.

2) Juu ya siku ya pili, Maandiko yanasema,

> "*Na Mungu alisema, Iwe nafasi katikati ya maji, itenge maji na maji. Mungu akafanya nafasi, akatenga maji yaliyo chini ya nafasi na maji yaliyo juu ya nafasi, na ilikuwa hivi. Mungu akaita nafasi 'mbingu'.* (Mwanzo 1:6-8)

Hivi, siku ya pili, Mungu aliumba mbingu au **hewa kuzunguka dunia**. Hewa hii inazunguka dunia na kutupa sisi upepo tunaovuta. "Hewa" hii inalinda kila kitu na kila mtu toka moto wa jua na maneno mabaya mengi. Haiwezekani kwa mtu kuishi hapa duniani bila hewa.

3) Siku ya tatu, Mungu aliumba **bahari, inchi kavu na miti na majani.** Sikia maneno Maandiko yanayosema:

> "*Maji chini ya mbingu yakusanyike kwa pahali pamoja, na inchi kavu ionekane; na ilikuwa hivi. Mungu akaita inchi kavu Inchi, kusanyiko la maji akaita Bahari. Mungu akaona ya kama ilikuwa vema. Mungu akasema: Inchi itoe majani, mboga ikitoa mbegu, na mti wa matunda ukizaa matunda ya namna yake, mbegu yake iliyo ndani yake, ya*

namna yake, ... na ilikuwa hivi ... Mungu akaona ya kama ilikuwa vema. Na ilikuwa mangaribi, na ilikuwa asubui, siku ya tatu." (Mwanzo 1:9-11,13)

Hivi siku ya tatu Mungu mwenye uwezo wote, aliumba bahari na mito, pamoja na miti na mapando mbalimbali elfu elfu, kila moja na matunda na mbegu zake mwenyewe. Ndimu, ndizi, tomate, mchele, makalanga, na namna elfu nyingine za chakula. Na Mungu alisema juu ya kila kitu alichoumba kwamba kilikuwa *kizuri*! Kila kitu Mungu anachofanya ni kizuri, cha ajabu na kikamilifu! Tumeona mbele ya kwamba kuna neno moja ambalo Mungu hawezi kufanya. Mungu hawezi kufanya kitu kibaya, kwa sababu **yeye ni mwema**!

Labda unauliza, "Kama Mungu ni mwema, kwa nini basi dunia hii inajaa uovu na vita? Kwa nini mashamba yangu hayakuzaa vizuri mwaka huu? Kwa sababu gani mtoto wangu ana ugonjwa? Kama Mungu ni mwema, kwa sababu gani uovu unatoka ndani ya mtu?" Kweli haya ni maulizo magumu, na Maandiko Matakatifu yanatupa sisi majibu mazuri ambayo tutajifunza ndani ya masomo yanayofuata. Kwa leo, tukumbuke ndani ya roho zetu kweli hii kubwa: Mungu ni mwema, na kwa sababu hii **kila kitu ambacho aliumba ni chema.** Kama tulivyojifunza ndani ya somo la mbele, Mungu hafanyi kitu kibaya kamwe.

Tufikiri kwa saa ndogo **wema wa Mungu**. Tumesikia sasa tu ya kwamba aliumba miti siku ya tatu. Unajua **kwa sababu gani** Mungu aliumba miti na matunda yao? Aliihitaji? Aliumba miti ikijaa matunda matamu kushibisha njaa yake mwenyewe? Hapana! Mungu Mwumba hana njaa kamwe na hahitaji kitu! Kama ni hivi, kwa nini basi Mungu aliumba miti? Maandiko yanatuonyesha ya kwamba Mungu, kwa sababu ya wema wake, aliumba kila kitu **kwa mtu** ambaye alikusudi kuumba siku ya sita.

Unatambua wema wa Mungu? Unaweza kuonja utamu wa ndizi na kunusa harufu tamu ya maua bila kutambua wema wa Mungu? Au unaweza kuona mti bila kumshukuru Yeye ambaye aliufanya kwa wewe? Bila miti maisha yetu yangalikuwa mabaya. Hakuna kuni kuwasha moto wala mbao kufanya meza na viti. Hakuna kivuli kwa kupumzika toka ukali wa jua, wala majani kufanya chai au dawa. Bila miti tutaishi namna gani? Miti ambayo Mungu aliumba ni baraka moja tu ya baraka nyingi nyingi za Mungu ili tuweze kukaa na furaha. Mungu anataka sisi kutambua wema wake. Kwa sababu hii nabii wa Mungu, Daudi, aliandika ndani ya Zaburi, "*Onjeni*

*mwone ya kuwa Bwana ni **mwema**"* (Zaburi 34:8). Lakini sharti tuendelee na mafundisho yetu.

4) Siku ya ine Mungu alisema, "*Iwe miangaza kwa nafasi ya mbingu ipate kutenga kati ya mchana na usiku; nayo iwe kwa alama na kwa nyakati na kwa siku na kwa miaka*" (Mwanzo 1:14). Mungu alitoa agizo tu, na **jua, mwezi, na nyota** ilionekana mbinguni. Mungu alisema neno moja na dunia ilianza kuzunguka jua. Alisema tena na mwezi ulianza kuzunguka dunia.

Kuna neno moja ambalo inatupasa kuonyesha waziwazi. **Mungu alitumia nini kuumba kila kitu duniani?** Maandiko yanasema nini? Yanasema,

> "*Ulimwengu uliumbwa **kwa Neno la Mungu**, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyoonekana*" (Waebrania 11:3).
> "*Katika mwanzo alikuwa **Neno**, na Neno alikuwa pamoja na Mungu, na Neno alikuwa Mungu. Huyu kwa mwanzo alikuwa pamoja na Mungu. Vitu vyote vilifanyika kwa **huyu**; na pasipo yeye hakikufanyika hata kitu kimoja kilichofanyikana.*" (Yoane 1:1-3)

Tumesoma mbele ya kwamba siku ya kwanza Mungu **alisema tu** "*Nuru iwe:*" na nuru ilikuwa. Siku ya pili Mungu **alisema,** "*Iwe nafasi*" na kulikuwa na nafasi. Siku ya tatu Mungu **alisema** tena, na maneno aliyosema yalifanyikana. Vivi hivi ... Hivi Mungu alitumia nini kuumba kila kitu kilicho duniani? Mungu hakutumia kitu ila **neno lake!** Alisema tu, na neno ambalo alisema lilifanyikana. Mungu ali**umba** kila kitu kwa njia ya kusema tu. Na Mungu **anategemeza** kila kitu kwa njia ya **neno lake la uwezo**. Kwa uwezo wa neno la Mungu mwezi na nyota zinabaki kwa pahali pao katika hewa. Kwa agizo la Mungu jua linapanda na kushuka kila siku kwa saa yake. Ingekuwa matata kama tusingalijua kama jua litapanda kesho au sivyo! Lakini Mungu aliagiza jua kupanda nalo linapanda. Maandiko yanasema ***"Mungu ni mwaminifu"*** (1 Wakorinto 1:9). Anatimiza neno lake kila mara. Hageuki kamwe. "*Neno la Mungu linadumu kwa **milele***" (1 Pet. 1:25).

5) Siku ya tano, Mungu aliumba namna mbalimbali elfu nyingi za **samaki na ndege.** Maandiko yanasema,

> "*Mungu akasema: Maji yajae kwa wingi na viumbe vilivyo hai, na ndege waruke juu ya inchi kwa nafasi ya mbingu. Mungu akaumba nyama wakubwa za bahari, na kila kiumbe kilicho hai na kinachotembea, maji yaliyotoa wingi kwa namna zao, na kila ndege kwa namna*

yake. Mungu akaona ya kama ilikuwa vema. Mungu akawabariki, akisema: Muzidi na kuongezeka, mujaze maji baharini, na ndege wazidi inchini. Na ilikuwa mangaribi na ilikuwa asubui, siku ya tano." (Mwanzo 1:20-23)

6) Juu ya siku ya sita, Maandiko yanatupasha namna Mungu alivyoumba **nyama na mtu**. Hatuna saa leo kueleza zaidi matokeo haya makubwa. Hivi ndani ya somo la nyuma, Mungu akitaka, tutaangalia karibu karibu **namna gani** Mungu aliumba mtu wa kwanza na **kwa sababu gani** alimwumba.

Ndani ya somo la leo tuliwaza juu ya **wema wa Mungu.** Tulisoma maneno Daudi, nabii wa Mungu, aliyoandika akisema, *"**Onjeni** mwone ya kuwa **Bwana ni mwema!**"* Rafiki, **umeonja** wema wa Mungu kweli? Kila siku tunaonja na kula vyakula mbalimbali. Lakini tusisahau ya kwamba yule aliyeumba mtu wa kwanza na kumpa vyote anavyohitaji kwa kuishi, anatangaza vilevile ndani ya Neno lake ya kwamba *"mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno linalotoka katika kinywa cha Mungu."* (Matayo 4:4) Ndani ya somo la nyuma tutaona ya kwamba mtu si mwili tu, lakini mwenye nafsi vilevile. Lazima nafsi zetu zilishwe na maneno ya Mungu. Neno la Mungu ni la ajabu sana, lakini lazima tuwe na njaa kwa kulisoma. Moyo wako una njaa kwa kujua Neno la Mungu namna mwili wako una njaa kwa vyakula? Kama ukiwa na njaa namna hii kwa Neno la Mungu, utatambua Kweli ya Mungu inayoweza kukupa salama ya kutimia na Mungu hapa duniani na uriti usioharibika mbinguni! Tunajua neno hili ni kweli, kwa sababu ni ahadi ya Mungu mwenyewe wakati anaposema: *"Heri wenye njaa na kiu kwa haki: maana wao **watashibishwa!**"* (Matayo 5:6) Amina.

~~~~~~~~~~~~~

Mungu akubariki na usisahau kamwe mwito wa ajabu ndani ya Maandiko Matakatifu:

"Onjeni mwone ya kuwa Bwana ni mwema!" (Zaburi 34:8)
~~~~~~~~~~~~~

Somo 5

Kwa sababu gani Mungu aliumba mutu

Mwanzo 1, 2

Salama kwako, Rafiki. Tunakusalimu kwa jina la Mungu wa salama, anayetaka watu wote kufahamu, kuamini na kupokea njia ya haki aliyotayarisha, na kuwa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kuendelea na Somo 5 la mfulizo *Njia ya Haki*.

Ndani ya somo la mbele tuliona **namna Mungu alivyoumba** mbingu, dunia na bahari na vyote vilivyo ndani yao. Mungu wetu alifanya vyote ndani ya siku sita bila kutumika na kitu. Alisema maneno tu. Tuliona vilevile **kwa sababu gani Mungu aliumba** dunia**.** Alifanya kila kitu kwa mtu ambaye alikusudi kuumba. Kweli Mungu ni mwema sana! Aliumba pahali pazuri na pa ajabu sana kwa mtu kuishi na kusitawi.

Leo tunakusudi kuona ndani ya Maandiko **namna gani** Mungu aliumba mtu wa kwanza. Mungu akitusaidia, tutajaribu kuona **kwa sababu gani** aliumba mtu. Ndani ya kitabu cha Mwanzo, sura ya kwanza na shairi 26, Neno la Mungu linasema,

> *"Mungu akasema: Tufanye mtu kwa mfano wetu, mwenye sura yetu na watawale juu za samaki ya bahari na juu ya ndege za hewa na juu ya ngombe, na juu ya inchi nzima, na juu ya kila mtambazi anayetambaa juu ya inchi.* ***Mungu akaumba mtu kwa mfano wake mwenyewe, kwa mfano wa Mungu akamwumba: mume na mke akamwumba."*** (Mwanzo 1:26,27)

Hapa tunaona kweli kubwa sana ambayo inapasa kila mtu kufahamu, ndiyo hii: **Mungu aliumba mtu wa kwanza kwa mfano wake mwenyewe!** Ni neno la kushangaza kabisa! Mungu alifanya mtu kuwa sawasawa naye! Kweli, mtu ni kiumbe mkubwa zaidi cha viumbe vyote Mungu alivyofanya, kwani mtu tu aliumbwa kwa sura ya **Mungu**!

Maana ya Neno la Mungu ni nini pahali tunaposoma, *"Mungu akaumba mtu kwa mfano wake mwenyewe"?* Tunaona jibu kwa ulizo hili

ndani ya shairi 7 la sura 2 linalosema, *"Mungu akafanya mtu wa mavumbi ya inchi, akapuliza pumzi ya uzima ndani ya pua yake; na mtu alikuwa nafsi ya uhai."* (Mwanzo 2:7) Tunaona ndani ya shairi hili ya kwamba wakati Mungu alipoumba mtu wa kwanza, alimwumba na maneno mawili: **mwili** na **nafsi**. Mtu si kiumbe chenye mwili tu. Ana mwili na nafsi. Hakuumba mtu mzima mara moja. Sikiliza kwanza maneno Maandiko yanayosema: **Kwanza:** *"Mungu akafanya mtu wa mavumbi ya inchi";* **la pili:** *"akapuliza pumzi ya uzima ndani ya pua yake; na mtu alikuwa nafsi ya uhai."*

Kwa njia ya shairi hili tunajifunza ya kwamba wakati Mungu alipoumba mtu, aliumba kwanza mwili. Kwa nini Mungu alifanya mwili kwanza? Kwa sababu utakuwa kao pahali atakapoweka nafsi ya mtu. Unajua ya kwamba mwili wako ni "kao" pahali nafsi yako inapopanga? Kwa sababu hii Maandiko yanasema *mwili tulio nao duniani ni kama* ***hema*** (2 Wakorinto 5:1). Mungu aliumba mwili wa mtu kuwa kao kwa nafsi yake.

Mungu aliumba mwili wa mtu wa kwanza namna gani? Maandiko yanasema kwamba aliufanya toka **mavumbi ya inchi.** Kwa wakati wa sasa tunajua kwamba dunia hii ni vitu mbalimbali karibu 20 na ya kwamba vitu hivi vyote vinapatikana ndani ya mwili wa mtu. Kwa sababu hii Daudi, nabii wa Mungu aliandika ndani ya Zaburi, Bwana *"anajua mwili wetu; anakumbuka ya kuwa sisi ni* ***mavumbi!"*** (Zaburi 103:14) Ndiyo, mwili umefanywa toka mavumbi, lakini si kusema mwili ni kitu bule! Ndani ya mwili wa mtu kuna sehemu ndogo tunazoita chembechembe kupita milioni 70 mara milioni moja. Na sehemu hizi zote zinaungwa kutumika pamoja na upatano mzuri kabisa. Kweli **mwili wa mtu ni ajabu!** Mungu ameweka ndani ya miili yetu akili, moyo, mbavu, tumbu, maini, mifupa, mnofu, ngozi, macho, masikio, pua, kinywa, na sehemu nyingi nyingine za kushangaza kabisa. Kila sehemu inajua kazi yake. Ni Mungu tu aliyeweza kuiumba! Kwa sababu hii nabii wa Mungu, Daudi, aliandika vilevile, *"Bwana, ninakushukuru; kwa kuwa* ***nimeumbwa kwa hofu na ajabu****: kazi zako ni za ajabu; na nafsi yangu inajua hivi sana."* (Zaburi 139:14)

Ndiyo, mwili wa mtu ni ajabu la kushangaza kabisa! Lakini ulikuwa mwili ambao Mungu aliumba kwa sura yake mwenyewe? Sivyo! Kwa sababu Mungu hahitaji mwili. Mungu ni roho. Mungu hakuumba mwili ambao tunaona na macho yetu kwa sura yake mwenyewe. Basi maana yake nini wakati Maandiko yanaposema Mungu alifanya mtu kwa sura yake mwenyewe? Ni kusema

Mungu aliumba **nafsi ya mtu kwa sura yake mwenyewe.**

Tumeona mbele ya kwamba wakati Mungu alipofanya mwili wa mtu toka mavumbi ya inchi, mwili huu haukuwa na uzima. Ulikuwa maiti tu. Kwa nini Mungu aliumba mwili wa mtu, mbele ya kuweka nafsi ndani yake? Kwa nini Mungu aliye mwenye uwezo wote, hakuumba mtu mzima mara moja, kama alivyofanya na viumbe vyote vingine? Labda alifanya hivi kwa kutufundisha ya kwamba mtu yeye mwenyewe hana uwezo juu ya uzima. Mtu hawezi kujiletea uzima yeye mwenyewe na mtu hawezi kuumba kitu cho chote chenye uzima. **Mungu ni BWANA wa Uzima,** na ndani yake tu uzima unapatikana. Uzima hautoki kwa mtu; ni **zawadi toka Mungu**! Hivi Maandiko yanasema ya kwamba Mungu *"alipuliza pumzi ya uzima ndani ya pua yake, na mtu alikuwa nafsi ya uhai."* Mwili ambao Mungu aliumba ulianza kuishi. Uliishi kwa sababu gani? Kwa sababu Mungu, Bwana wa Uzima, aliupa nafsi! Mungu alipuliza uzima wake ndani ya pua ya mtu. **Uzima uliokuwa ndani ya Mungu ulikuwa sasa ndani ya mtu.** Hivi, mtu aligeuka kiumbe chenye uzima.

Basi ni kitu gani Mungu alichoumba kwa sura yake mwenyewe? **Nafsi** yake. Mungu aliumba nafsi ya mtu ndani ya sura yake mwenyewe. Ulijua ya kwamba maneno mengine yaliyo ndani ya Roho ya Mungu ni ndani ya roho ya mtu vilevile? Mbele ya kumaliza somo hili tunataka kuwaza juu ya **maneno matatu** yanayopatikana ndani ya Mungu na yanayopatikana ndani ya mtu vilevile. Wakati tunapowaza juu ya maneno haya matatu tunaoshiriki na Mungu, tutaweza kufahamu maana ya Maandiko kupita ya kwamba *"Mungu aliumba mtu kwa sura yake mwenyewe."* Maneno matatu Mungu aliyoweka ndani ya nafsi ya mtu ndiyo haya:

1. Mungu alimpa mtu **akili**, kusudi aweze ku**jua Mungu**.
2. Mungu alimpa mtu **moyo**, ili aweze ku**penda Mungu**.
3. Mungu alimpa mtu **kutaka** kwake mwenyewe aweze ku**tii** Mungu.

Kama Mungu alivyo na nia, moyo na kutaka, aliweka ndani ya nafsi ya mtu nia, moyo, na kutaka. Tuwaze juu ya maana ya maneno haya.

1) Kwanza, Mungu alimpa mtu **nia** inayoweza kujua Mungu na kufikiri namna yeye anavyofikiri. Mungu aliumba mtu na roho au nia ya uwezo hivi kwa sababu alikusudi kwa mtu kuwa na **ushirika wa karibu** naye. Wakati tunaposoma juu ya maisha ya nabii wa Mungu, ndiye Abrahamu, tutaona ya kwamba aliitwa ***"rafiki ya Mungu"***. Abrahamu alijuana na Mungu yeye mwenyewe na alikuwa

na upatano wa karibu naye. Lakini baraka hii si kwa Abrahamu tu. Sisi vilevile tunaweza kuwa "**rafiki za Mungu**". Mungu anataka sisi kuwa na ushirika wa karibu naye. Kwa sababu hii aliweka ndani ya nafsi ya mtu nia inayoweza kupatana na nia ya Mungu.

Labda tunaweza kueleza na ulizo maneno tunayosema. **Mtu na nyama ni mbalimbali kwa njia gani? Kwa njia ya nia.** Nia ya mtu ni namna nyingine na nia ya nyama. Kwa nini nyama hawawezi kusoma maneno haya? Kwa sababu hawana nia kama sisi. Rafiki msomaji, kwa sababu gani unaweza kufahamu maneno yanayoandikwa? Kwa sababu una nia namna ya nia yetu, ndiyo nia ya mtu. Vivyo hivyo roho ya mtu imetungwa kufanana na kuwa na ushirika na Roho ya Mungu.

Lakini si kusema ya kwamba nia zetu ni sawasawa na nia ya Mungu kwa maneno ya hekima na kujua. Sivyo! Hekima ya Mungu ni kubwa sana na kujua kwake kunapita mbali maneno mtu anayojua. Neno ambalo inatupasa kufahamu ndilo hili: Mungu alimpa mtu roho inayoweza kuwa na **upatano na Mungu aliye hai**. Mungu hataki sisi kuwa sawasawa na nyama wasioweza kumjua! Nyama ana akili, lakini hawezi **kufikiri juu ya Mungu**. Nyama ana kinywa, lakini hawezi **kushukuru Mungu** kwa vyakula ambavyo anampatia kila siku. Ana macho, lakini hawezi **kusoma Maandiko Matakatifu**. Ana masikio, lakini hawezi **kusikia Neno la Mungu.** Lakini mtu, ambaye Mungu aliumba kwa sura yake, anaweza kuwaza juu ya Maandiko Matakatifu, na **kujuana na Bwana Mungu!** Unaweza kuwa na upatano mtamu sana naye, kama ukiamini na kupokea njia ya wokovu ambayo Mungu alitayarisha. Tutaeleza njia ya wokovu ya Mungu wazi ndani ya masomo ya nyuma, lakini neno kubwa ambalo inatupasa kufahamu kabisa kabisa leo ni ya kwamba Mungu amempa mtu akili na roho ambazo zinamwezesha kujuana naye.

2) Kuna neno lingine Mungu aliloweka ndani ya nafsi ya mtu, wakati alipomwumba kwa sura yake **moyo**. Mungu alimpa mtu moyo ili aweze **kupenda** Mungu. Hatusemi juu ya moyo unaotembeza damu ndani ya mwili, lakini juu ya maneno **unayosikia ndani ya nafsi yako,** kama furaha, huzuni, na **mawazo yako.** Tunasema juu ya makusudi ya moyo wako. Mungu aliwezesha mtu wa kwanza kusikia maneno yale yale ambayo Mungu mwenyewe anasikia. Mungu anaweza kupenda, kufurahi, kuchukia, kuwa na huzuni, na huruma, vivi hivi. Hivi Mungu aliweka ndani ya nafsi ya mtu moyo unaoweza kusikia maneno kama mapendo na kuchukia. Mungu anataka mtu kupenda maneno ambayo Mungu anapenda na

kuchukia yale ambayo Mungu anachukia. **Mungu anataka umpende na moyo wako wote.** Kwa sababu hii aliumba mtu kwa sura yake mwenyewe na kumpa moyo.

3) Kuna neno lingine ambalo Mungu alimpa mtu wakati alipomwumba kwa sura yake mwenyewe. Aliweka uwezo wa kuchagua ndani ya nafsi ya mtu. Kila mtu ana ruhusa **kuchagua njia yake mwenyewe.** Mungu yeye mwenyewe ana amri kuchagua kama atafanya neno fulani au sivyo. Hivi, Mungu aliumba mtu na ruhusa na kazi ya kuchagua maneno makubwa kwa maisha yake mwenyewe. Mungu angaliweza kuumba mtu atakayefanya mapenzi yake kila mara bila kuweza kuchagua kufanya neno lingine. Lakini Mungu alimpa mtu uwezo na kazi ya kuchagua yeye mwenyewe kama atatii Mungu! Mungu hakutaka kuumba mtu aliye kama machine tu. Hakuumba mtu kwa sura ya jua linalopanda kila siku, lakini lisiloweza kuchagua kama litafanya hivi au sivyo. Jua linafanya mapenzi ya Mungu kila siku kama machine. Mtu ni namna nyingine. Mungu alimwumba kwa Yeye mwenyewe. Mungu anataka sisi **kuchagua** kumpenda na kumwabudu.

Mungu amempa mtu daraka kubwa! Inapasa mtu kuchagua yeye mwenyewe kama atafuata Mungu au Shetani, kama ataheshimu Neno la Mungu au kulizarau. Mungu hatalazimisha mtu ye yote kuamini Neno lake. Hatatulazimisha kamwe kumpenda na kumtii. Mapendo ya kweli ni neno la kutaka, si neno la lazima. Mungu anatuacha sisi sote kuchagua kama tutafuata njia gani. Lakini, mwishoni, Mungu atahukumu kila mtu anayekataa ufalme wake, kwa sababu Mungu alimwumba **kwa yeye mwenyewe.**

Haya ndiyo mafundisho ya Maandiko Matakatifu. Tuko hapa duniani **kwa Mungu**. Hatuko hapa kwa faida yetu wenyewe, au kwa kupata mali au kitu cho chote kwa sisi wenyewe. **Mungu alituumba kwa yeye mwenyewe**. Alituumba na **uwezo kumjua, kumpenda na kumtii kwa milele**. Ndiyo, **kwa milele!** Mungu Mwenyezi ametupa sisi sote nafsi ya milele. Ni mapenzi ya Mungu kwa sisi kuwa na **upatano wa karibu, wa ajabu** naye leo, kesho na kwa milele. Kwa sababu hii Mungu aliumba mtu kwa sura yake mwenyewe.

Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya maneno anayotaka kwako wakati anaposema,

> ***"Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja. Upende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote!"*** (Marko 12:29,30)

SOMO 6

ADAMU NA HAWA

MWANZO 2

Tuendelee na mafundisho yetu ndani ya Mfulizo *Njia ya Haki* juu ya maneno yaliyotokea kwa mwanzo. Leo tutakutana na Adamu na Hawa, na kujifunza juu ya siku yao ya kwanza duniani.

Tulisoma ndani ya kitabu cha pili ndani ya Biblia, "*Kwa siku sita Bwana akafanya mbingu na inchi, bahari na vyote vilivyo ndani yao.*" (Kutoka 20:11) Tumeona vilevile namna Mungu alivyoumba mtu siku ya sita. Mungu aliumba mtu na **mwili na nafsi**. Alifanya mwili wa mtu toka mavumbi ya udongo, kisha aliweka ndani yake nafsi iliyo hai milele. Mungu aliumba nafsi ya mtu kwa sura yake mwenyewe. Ni kusema Mungu aliweka ndani ya nafsi ya mtu nia (roho) kumwezesha **kujua Mungu**. Mungu alimpa mtu moyo vilevile ili aweze kupenda Mungu. Na alimpa **kutaka kwake mwenyewe** aweze **kuwa na amri** kuchagua kwa yeye mwenyewe kama **atatii Mungu** au kumwasi.

Wakati Mungu alipomaliza kuumba mtu, kulikuwa na maneno mengine ambayo ilimpasa kufanya mbele ya kuweza kupumzika toka kazi yake ya kuumba. Tunataka kufikiri juu ya kazi hizi leo. Tuendelee kusoma ndani ya sura ya pili ya Mwanzo, kuanza na shairi 7. Maandiko yanasema,

> "*Bwana Mungu akafanya mtu wa mavumbi ya inchi, akapuliza pumzi ya uzima ndani ya pua yake; na mtu alikuwa nafsi ya uhai.* ***Bwana Mungu akapanda shamba kwa upande wa mashariki kwa Edeni, akatia pale mtu ambaye alimfanya.***" (Mwanzo 2:7,8)

Maandiko yanatujulisha ya kwamba Mungu alitayarisha shamba zuri sana kwa mtu ambaye alimwumba. Shamba liliitwa ***Edeni*** (maana yake mapendezi), au ***Shamba la Paradiso***. Watu wengine wanafikiri ya kwamba shamba hili pahali Mungu alipoweka mtu wa kwanza lilikuwa mbinguni. Lakini Maandiko yanatuonyesha ya

kwamba **lilikuwa hapa duniani**, kwa mashariki, katika Edeni, labda kwa pahali inchi ya Iraq ilipo kwa wakati wa sasa. Maandiko ya manabii wa Mungu yanaonyesha **tofauti kila mara kati ya shamba la Paradiso (Edeni)** hapa duniani, na **Paradiso palipo juu,** mbele ya Mungu.

Ndani ya mashairi yanayofuata, Maandiko yanasema,

> *"Toka udongo Bwana akaotesha kila mti wa kupendeza macho, na mzuri kwa chakula; mti wa uzima vilevile ulikuwa katikati ya shamba, na mti wa kujua uzuri na ubaya. Mto ukatoka katika Edeni kunyesha maji shambani; na toka kule ukatengwa na ulikuwa vichwa vine . . . Bwana Mungu akatwaa mtu [ndiye Adamu], akamtia shambani mwa **Edeni** kulilima na kulichunga."* (Mwanzo 2:9,10,15)

Hivi tunaona ya kwamba Mungu alitayarisha kwa mtu wa kwanza, Adamu, pahali pazuri sana alipoweza kuishi na kusitawi. Mungu alimweka ndani ya shamba zuri sana lililojaa miti iliyozaa matunda mazuri kwa kutazama na macho na matamu kwa kula. Ndani ya pahali hapa pazuri sana **kila kitu kilikuwa kikamilifu na cha ajabu.** Adamu aliweza kuona maneno haya mazuri yote na macho yake na kusikia utamu wa nyimbo za ndege walioimba ndani ya miti, na kunusa harufu tamu ya maua iliyoenea shambani. Mungu alimpa Adamu maneno haya yote aweze kuyafurahia. Tunasoma vilevile namna Mungu, katika uzuri wake, alimpa Adamu **kazi ya furaha** kabisa, ndiyo kutunza shamba, ili aweze kuwa na kazi ya kupendeza.

Neno zuri zaidi lililotokea katika shamba la Edeni lilikuwa **kufika kwa Mungu mwenyewe shambani kila siku** wakati wa mangaribi ili aweze kusemezana na mtu ambaye alikuwa amemwumba kwa sura yake mwenyewe. Ona Mwanzo 3:8. Kwa nini Mungu alikuja kuona Adamu? Alifika kuonana na Adamu kwa sababu, kama tulivyoona mbele, **Mungu aliumba mtu ili waweze kuwa na ushirika pamoja,** kusemezana pamoja, kufurahi pamoja, na kuwa pamoja kwa milele wenye nia na roho moja. Ndiyo, Mungu alitaka mtu kuendelea kuwa na upatano mzuri na wa ajabu naye kwa milele.

Kuna neno lingine ambalo inatupasa kujua juu ya shamba pahali Mungu alipoweka mtu wa kwanza. Katikati ya shamba, Mungu aliweka miti miwili yenye kazi kubwa. Mti mmoja uliitwa *mti wa uzima*, na wa pili *mti wa kujua uzuri na ubaya*. Mungu aliweka **mti wa uzima** ndani ya shamba kukumbusha Adamu ya kwamba alitaka mtu kushiriki naye uzima wake wa milele. Lakini aliweka **mti wa kujua**

uzuri na ubaya katikati ya shamba kuona kama Adamu atamtii. Ona maneno Maandiko yanayosema: "*Bwana Mungu akaagiza mtu akisema: Wa kila mti wa shamba unaweza kula; lakini wa mti wa kujua uzuri na ubaya usile kwa maana siku unapokula, hakika utakufa.*" (Mwanzo 2:16,17)

Kwa sababu gani Mungu alikataza Adamu kula matunda ya mti wa kujua uzuri na ubaya? Mungu ni mwenye choyo? Sivyo, hata kidogo! Yeye ni mwenye ukarimu (Yakobo 1:5). Mungu alisema na Adamu, "Unaweza kula matunda ya kila mti ... ila mmoja." Hii ilikuwa amri ngumu? Sivyo. Mungu, kwa neema yake, alimpa Adamu kila kitu alichohitaji kwa kukaa na furaha. Hakumnyimia kitu kizuri cho chote. Lakini kwa shauri lake kamilifu Mungu alimpa **jaribu dogo** kumpa Adamu njia kuonyesha Mungu ya kwamba alimpenda ya kutosha kutii agizo lake. Bwana Mungu anasema ndani ya Neno lake: "*Kama mtu akinipenda, atatii neno langu . . . Mtu ambaye hanipendi, hatii maneno yangu.*" (Yoane 14:23,24) Mungu alitaka kuona kama Adamu alimpenda kweli, kama nini ilikuwa ndani ya royo yake. Kwa sababu hii alimpa agizo hili dogo. Mungu hakuumba mtu aliye kama machine, lakini mtu mwenye nia, moyo na kutaka ili aweze kuchagua yeye mwenyewe kupenda na kutii Mungu.

Mungu alimwambia Adamu nini itampata kama akikula tunda la mti uliokatazwa? Tusome Maandiko tena. Mungu alisema, "*Usile wa mti wa kujua uzuri na ubaya kwa maana siku unapokula,* ***hakika utakufa!***" Hivi, Mungu alijulisha Adamu ya kama tunda la kuasi agizo lake kutakuwa mauti. Mungu alipenda mtu ambaye alimwumba; hivi alimwonya waziwazi kusema, Adamu, kama ukiniasi, utakufa, kwa sababu sheria yangu takatifu inasema kwamba "nafsi inayofanya zambi itakufa" (Ezekieli 18:20).

Labda unauliza: **Zambi ni nini?** Maandiko yanasema, "*Zambi ni* ***uasi.***" (1 Yoane 3:4) "***Yote yasiyo ya haki*** *ni zambi*" (1 Yoane 5:17). "*Kwa yeye anayejua* ***kutenda mema wala hayatendi,*** *kwake huyu ni zambi*" (Yakobo 4:17). Zambi ni kufuata "*njia yako mwenyewe*" (Isaya 53:6). Zambi ni neno lo lote lisilopatana na Mungu. **Nini itapata watu wanaokosea Mungu?** Neno la Mungu linasema, "*nafsi inayofanya zambi itakufa*" (Ezekieli 18:20). Na shairi lingine linasema, "*mishahara ya zambi ni mauti*" (Waroma 6:23).

Mauti ni nini? Watu wengine wanafikiri ya kwamba kufa ni kutokuwa tena; maneno yako yote yanakwisha na hujui tena kitu. Lakini kama tukitegemea Maandiko ya manabii, tutaona ya kwamba

mauti si hivi. Ndani ya Maandiko Matakatifu, yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiebrania, maana ya mauti ni ***kutengwa***. Mauti ni kutengwa na uzima.

Wakati Mungu aliposema na Adamu: "Siku unapokula ya mti wa kujua uzuri na ubaya, hakika utakufa", maana ya maneno aliyosema ndiyo hii: Adamu, kama ukikula ya mti ambao nilikataza, siku ile utakufa, maana: **utatengwa nami**. Ukiniasi, huwezi kuwa na upatano wa karibu na mzuri nami. Mimi ni mtakatifu na siwezi kukubali zambi au wale wanaokataa kutembea katika njia yangu. Nilifukuza Lusifero na malaika zake wakati walipofanya zambi, na nitakufukuza wewe vilevile kama ukifanya zambi. Vilevile ukikula ya matunda ya mti uliokatazwa, **mwili wako** utageuka mzee na, mwishoni, utakufa, maana yake: nafsi yako itaondokea mwili wako. Na haya si mwisho wa maneno. Ukiniasi, si mwili wako tu ambao utakufa, lakini **nafsi** yako itakwenda kwa pahali palipoumbwa kwa Shetani na malaika zake. Hivi utatengwa nami kwa milele na milele!

Hivi, tunaona ya kwamba **zambi inaleta matengano matatu ya kuogopesha sana.**

Kwanza, nafsi yako **inatengwa na Mungu hapa duniani.** Maana yake, huna upatano na Mungu Mtakatifu kwa sababu ya zambi moyoni mwako.

Neno la pili, nafsi yako **itatengwa na mwili** wako siku utakapokufa. Maana yake, mwili wako utakufa na nafsi yako itakutana na Mungu kwa kuhukumiwa.

Neno la tatu, **nafsi na mwili wako itatengwa na Mungu kwa milele** ndani ya ziwa la moto.

Hivi Neno la Mungu linafundisha nini juu ya mauti? Kwa ufupi, **mauti ni kutengwa na Mungu wa Uzima**. Zambi inatenga mtu na Mungu, asili ya uzima wa kweli. Mungu ni mtakatifu na hawezi kukaa pamoja na zambi. Nafsi inayofanya zambi ni **kama tawi** la mti linalokauka na kutupwa kando. Nini linatokea wakati tawi lisipo sehemu ya mti tena? Tawi linalokatwa, lina uzima? Sivyo! Majani hayakauki mara moja, lakini yameanza kufa. Vivyo hivyo, kama usipopokea njia ya usamehe wa zambi ambayo Mungu alitayarisha, labda unafikiri wewe ni hai, lakini Maandiko ya manabii yanasema ya kwamba, kwa macho ya Mungu, wewe ni ***"mfu*** *kwa sababu ya makosa na zambi "* (Waefeso 2:1). ***"Maovu yenu yamewatenga ninyi na Mungu wenu, na zambi zenu zimeficha uso wake kwenu."*** (Isaya

59:2) Wewe ni kama "***tawi linalotupwa inje na kukauka;*** *matawi namna hii yanakutanishwa na kutupwa ndani ya moto na kuteketezwa.*" (Yoane 15:6)

Tawi lisilo ndani ya mti tena halina faida, kwa sababu halizai matunda. Mwenye zambi ni hivi mbele ya Mungu. Hawezi kufanya kitu cho chote kinachopendeza Mungu **kwa sababu hana upatano na Mungu**, aliye "Mti wa kweli" **asili ya uzima wa kweli**. Hukumu ya haki ya Mungu tu inangojea wenye zambi. Lakini, tunashukuru Mungu kwa sababu ndani ya Maandiko ya manabii, Mungu ametangaza wazi namna gani tunaweza kufanyizwa haki mbele yake na kujua ya kwamba zambi zetu zimeondoshwa. Tutawaza juu ya habari hizi njema ndani ya masomo ya kuja.

Mbele ya kumaliza somo hili, tunataka kusoma maneno yaliyo ndani ya baki la sura hii. Maandiko yanatupasha namna Mungu alivyoumba **mwanamke wa kwanza.**

> *"Bwana Mungu akasema: Si vema mtu awe peke yake; nitamfanyia msaidia anayefaa kwake. ... Na Bwana Mungu alileta usingizi mzito kuangukia mtu, akalala; akatwaa mmoja wa mifupa ya mbavu zake, akafunga nyama kwa pahali penyewe; na mfupa wa mbavu Bwana alioondosha kwa mtu, akafanya mwanamke, akampeleka karibu na mtu. Adamu akasema: Huyu ni mfupa wa mifupa yangu, na nyama ya nyama yangu; ataitwa Mwanamke kwa maana ameondoshwa katika mume. Kwa sababu hii mume ataacha baba yake na mama yake na atafungana na mke wake; na watakuwa mwili mmoja. Nao wawili walikuwa watupu, mume na mke wake, wala hawakuona haya."* (Mwanzo 2:18,21-25)

Hivi tunaona ya kwamba **ndoa** ilitungwa na Mungu. Mungu aliumba mtu mmoja na mwanamke mmoja ili waweze kupendana, kuishi pamoja na kuwa na jamaa ya furaha inayotukuza Mungu. Mungu alipenda Adamu na alitaka Adamu kukaa na furaha kabisa, hivi alimpa zawadi nzuri sana, ndiyo **mke**! Mungu alitaka Adamu kuheshimu mke wake, kumpatia mahitaji yake, na kumpenda kwa kipimo alichojipenda mwenyewe. Na neno kubwa zaidi, Mungu alitaka mwanamume na mwanamke kuwa na upatano mzuri sana na yeye mwenyewe—kumjua, kumpenda, na kumtii kwa milele. (Ona Waefeso 5:21-33; 6:1-4)

Hivi Mungu alimaliza kazi yake ya kuumba. Sikiliza Maandiko:

> *"Na Mungu aliona kila kitu alichofanya, na tazama, kilikuwa* ***kizuri***

> ***sana***. *Na ilikuwa mangaribi, na ilikuwa asubui, siku ya sita. Mbingu na dunia zikamalizwa, na jeshi lao lote.* ***Siku ya saba Mungu akamaliza kazi yake aliyofanya, akastarehe siku ya saba katika kazi yote aliyofanya.*** *Mungu akabariki siku ya saba, akaitakasa; kwa sababu ndani yake alistarehe ndani ya kazi yake yote Mungu aliyoumba na kuifanya."* (Mwanzo 1:31–2:3)

Kwa nini Mungu alistarehe siku ya saba? Alikuwa amechoka? Sivyo, Mungu hachoki kamwe! Maandiko yanasema ya kwamba alistarehe kwa sababu ***"akamaliza kazi yake!"*** Kila kitu kilikuwa kikamilifu. Kwa sababu hii Mungu alistarehe ndani ya kazi yake siku ya saba. Na kwa sababu hii kuna siku saba ndani ya juma moja.

~~~~~~~~~~~~

Ndani ya Somo 7 tutajifunza namna zambi ilivyoingia duniani. Na maneno mengine vilevile...

Mungu akubariki. Waza sana juu ya kweli Neno la Mungu linayotangaza, ndiyo,

> ***"Mshahara wa zambi ni mauti, lakini zawadi ya Mungu ni uzima wa milele ... !"*** (Waroma 6:23a)
~~~~~~~~~~~~

SOMO 7

NAMNA ZAMBI ILIVYOINGIA DUNIANI

MWANZO 3

Salama kwako, rafiki msomaji. Tunaomba uweze kubarikiwa wakati unapojifunza Somo 7 la mfulizo *Njia ya Haki*.

Ndani ya masomo mawili ya mbele, tulijifunza namna Mungu alivyoumba watu wawili wa kwanza. Juu ya neno hili, Maandiko yanasema, *"Mungu akaumba mtu kwa mfano wake mwenyewe,* ***kwa mfano wa Mungu*** *akamwumba; mume na mke akawaumba."* (Mwanzo 1:27) Ndani ya nafsi ya mwanamume na mwanamke, Mungu aliweka roho inayoweza kujua Mungu, na moyo unaoweza kumpenda. Mungu aliwapa vilevile kutaka kwao wenyewe, ili waweze kuchagua kama watamtii au sivyo. Tuliona vilevile ya kwamba Mungu aliweka mtu ndani ya Shamba la Paradiso, shamba zuri ambalo alitayarisha hapa duniani, kwa pahali panapoitwa Edeni. Mungu kwa wema wake alimpa mwanamume wa kwanza, ndiye **Adamu**, na mke wa kwanza, **Hawa**, kila kitu walichohitaji kwa kukaa na salama na usitawi wa kweli. **Mungu alitaka watu kumjua, kumpenda, na kumwabudu kwa milele.**

Hivi tuliona namna Mungu, kupatana na shauri lake, alitayarisha njia moja itakayoonyesha kama mtu atamtii. Katikati ya shamba, Mungu alipanda **mti wa kujua uzuri na ubaya,** kisha aliagiza mtu, akisema, *"Wa kila mti wa shamba unaweza kula; lakini wa mti wa kujua uzuri na ubaya* ***usile****, kwa maana siku unapokula, hakika utakufa."* (Mwanzo 2:16,17)

Kwa nini Mungu alijaribu Adamu kwa njia hii? Mungu alitaka kuonyesha hali ya moyo wa Adamu. Mungu hakufanya hivi kusukuma Adamu kufanya zambi, lakini kumbariki na kumpatisha nguvu. Mtu aliyeumbwa na Mungu hakuwa na kosa wala zambi, lakini neno hili si kusema ya kwamba alikuwa na mapendo makamilifu na tabia ya kukomea. Ni lazima kwa mapendo kujaribiwa. Hivi Mungu aliweka jaribu hili mbele yake, **kujaribu mapendo yake.** Kama Adamu

akishinda jaribu hili na kutii Mungu, neno hili litahakikisha ya kwamba alipenda Mungu kweli. Na vilevile, kama Adamu akishinda jaribu na kukataa kufanya zambi, jaribu hili litampatisha nguvu, kwa sababu Maandiko yanasema ya kwamba *"saburi inafanya uvumilivu."* (Waroma 5:4)

Basi leo tumefika kwa sura ya tatu ya kitabu cha Mwanzo. Sura hii ndiyo sura inayoonyesha **namna zambi ilivyoingia duniani**. Kama tukijuana na mafundisho ya sura hii, halafu tunajua kwa sababu gani moyo wa mtu ni mwovu, na kwa sababu gani dunia inajaa taabu na maumivu.

Tumeona mbele ya kwamba, kwa mwanzo, Adamu na Hawa walikuwa ndani ya Shamba la Paradiso pahali maneno yote yalipowafurahisha na roho zao ziliposhibishwa kabisa. Neno lililokuwa zuri zaidi ndilo hili: **Bwana Mungu alifika shambani kila mangaribi,** ili aweze kusemezana na Adamu na Hawa. Mungu alifika kuwaona kwa sababu alitaka kuwa na upatano mtamu na wa maana pamoja nao.

Lakini Maandiko yanatujulisha ya kwamba **kulikuwa na mwingine shambani vilevile.** Unajua kama alikuwa nani? Alikuwa adui ya Mungu, **Shetani**. Wakati Mungu alipoumba dunia na vitu vyote ndani yake, Shetani alikuwa akiangalia. Wakati Mungu alipoagiza Adamu juu ya mti wa kujua uzuri na ubaya, Shetani alikuwa akisikiliza. Wala hakutazama na kusikiliza tu, lakini **alitunga shauri na njia** kuharibu kazi za ajabu za Mungu. Shetani alifanya shauri kujaribu mtu ambaye Mungu aliumba ili mtu huyu aweze kuasi Mungu, kufanya zambi, kutengwa na Mungu na kupotea! Mungu alijua mashauri yote ya Shetani, lakini Adamu na Hawa hawakujua hata neno moja.

Siku moja, wakati Adamu na Hawa waliposimama karibu na mti ambao walikatazwa kula matunda yake, Shetani alifika kwa sura ya **nyoka** na alianza kusemezana nao. Maandiko yanasema, *"Basi nyoka alikuwa na hila kuliko nyama zote za mwitu Bwana Mungu aliofanya. Akamwambia mwanamke: Ndiyo, Mungu amesema: Musile ya miti yote ya shamba?"* (Mwanzo 3:1)

Basi, tuulize kwanza: Kwa nini Shetani alionekana kama nyoka? Maandiko yanaleta jibu kwa ulizo hili wakati yanaposema, *"Nyoka alikuwa na **hila kuliko** nyama zote za mwitu Bwana Mungu aliofanya."* Shetani ni mjaribu, na hivi alijionyesha kama mwenye akili nyingi. Shetani hakufika karibu na Adamu na Hawa kwa mfano wa joka

mkubwa mwekundu na kusema, "Salamu kwenu, Adamu na Hawa. Mimi ni Shetani, adui ya Mungu! Nimefika leo kuwajaribu ninyi kukataa Mungu, Bwana wa uzima, ili muweze kupotea kwa milele!" Sivyo, Shetani hakufanya hivi! Basi alijionyesha kwao namna gani? Kama kiumbe cha mapambo na akili nyingi. Alichagua kusema nao kwa njia ya nyoka, kwa sababu kwa wakati ule, mbele ya kuingia kwa zambi duniani, nyoka alikuwa na akili kupita nyama wote wengine.

Shetani ni hivi leo vilevile. Yeye ni mwenye hila. Ni desturi yake kuonyesha neno analotaka kututolea kuwa neno jema. Maandiko yanasema: "*Shetani mwenyewe anajigeuza awe* ***malaika ya nuru.***" (2 Wakorinto 11:14) Hivi, Mungu anatuonya ndani ya Neno lake, akisema, "*Angalieni kwa manabii wa uwongo wanaokuja kwenu wakivaa mavazi ya kondoo, lakini kwa ndani wao ni imbwa wakali za mwitu.*" (Matayo 7:15) ***Shetani ni mdanganyi.*** Kwa sababu hii alitokea kwa Adamu na Hawa kama nyoka mwenye akili. Na kwa sababu hii alichagua kusema na Hawa, si Adamu, kwa sababu alitaraji kwamba kujaribu Hawa kutakuwa nyepesi kupita kujaribu Adamu. Shetani alijua ya kwamba Mungu alitolea Adamu agizo juu ya mti huu, mbele ya kuumba Hawa. Lakini Hawa alijua agizo la Mungu vilevile, kwa sababu Adamu alimjulisha habari hizi. Shetani ana akili nyingi naye alijua kabisa neno alilotaka kufanyikana. Alijua kama ataweza kusukuma mwanamke kula tunda la mti wa kujua uzuri na ubaya, labda Adamu atamfuata na kuasi Mungu vilevile.

Hivi, Maandiko yanasema, "*Nyoka akamwambia mwanamke: Ndiyo, Mungu amesema, Musile ya miti yote shambani?*" (Mwanzo 3:1) Ulisikia neno ambalo Shetani alisema na Hawa? Alisema, "*Mungu amesema: Musile ya miti yote ya shamba?*"

Unafahamu neno Shetani alilojaribu kufanya? Alijaribu kuweka shaka ndani ya nia ya Hawa juu ya kweli ya Neno la Mungu. Kwa sababu hii alisema, "Mungu alisema? Mungu alisema hivi kweli?" Shetani anafanya hivi hata sasa. **Anashindana na Neno la kweli**, kwa sababu anajua Neno la Mungu lina uwezo kumshinda na kufunua wongo zake. Shetani anajua ya kwamba kweli inatawanya wongo, kama nuru inavyotawanya giza.

Tusikilize sasa baki la mazungumzo katikati ya mwanamke na Shetani. Maandiko yanasema,

> "*Mwanamke akamwambia nyoka: Matunda ya miti ya shamba tunaweza kula; lakini matunda ya mti ulio katikati ya shamba Mungu*

amesema: Musile yake wala musiyaguse, musife." "*Nyoka akamwambia mwanamke:* ***Hakika hamutakufa,*** *kwani Mungu anajua ya kama siku mutakapokula matunda yake, macho yenu yatafunguliwa, na mutakuwa kama Mungu mukijua uzuri na ubaya."* (Mwanzo 3:2-5)

Maneno haya ni shangao! Mungu alisema neno gani litapata Adamu na Hawa kama wakikula matunda ya mti uliokatazwa? Alisema, ***"Mutakufa!"*** Na Shetani alisema nini? Alisema, ***"Hamutakufa!"*** Hivi Shetani hakuamsha shaka tu juu ya Neno la Mungu, lakini **alilikana** waziwazi! Unafikiri nini juu ya neno hili? Nani alisema kweli, Mungu au Shetani? Maandiko yanasema ya kwamba Mungu ni kweli na hawezi kusema uwongo. Lakini Shetani hashikamani na kweli, *"hakuna kweli ndani yake. Wakati anaposema uwongo anasema* ***yaliyo yake mwenyewe****, kwa sababu yeye ni* ***mwongo*** *na* ***baba ya wongo****."* (Yoane 8:44)

Lakini sharti tukumbuke ya kwamba Shetani hakuwa **mwongo** tu, lakini **mdanganyi** vilevile. Yeye ni mwenye hila. Anakamata maneno **yasiyo kweli** na **kuyachanganya** na maneno ya **kweli.** Tunaweza kuona neno hili ndani ya masemo yake kwa Hawa na Adamu. Alisema, "*Siku mutakapokula matunda yake, macho yenu yatafunguliwa, na mutakuwa kama Mungu, mukijua uzuri na ubaya."* Wakati Shetani aliposema, "*Mutakuwa kama Mungu,"* neno hili lilikuwa **uwongo**, kwa sababu yule anayetenda uwongo si kama Mungu, lakini kama Shetani. Lakini wakati Shetani aliposema, "*mukijua uzuri na ubaya*," alisema **kweli**, kwani nyuma ya kutenda zambi, Adamu na Hawa walijua uzuri na ubaya. lakini Shetani hakuwajulisha mbele uchungu watakaopata kwa sababu ya kujua neno hili. Mungu alisema, "*wa mti wa kujua uzuri na ubaya usile kwa maana siku unapokula, hakika* ***utakufa***" (Mwanzo 2:17)! *Lakini Shetani alisema, "Mukikula ya mti* ***hamutakufa!***" Shetani ni mwongo. Kwa sababu hii, wakati Mungu aliposema, "*Mutakufa*", Shetani alibisha neno la Mungu, wakati aliposema, "***Ha****mutakufa."*

Sasa **ilikuwa saa kwa Adamu na Hawa kuchagua** kama nani alisema kweli, Mungu au Shetani. Watachagua kweli? au uwongo? Watafuata Bwana wa nuru? au bwana wa giza? Wataamini masemo ya Mungu? au masemo ya Shetani?

Tuone kama walichagua nini. Maandiko yanasema: *"Wakati mwanamke alipoona ya kama mti ulikuwa mzuri kwa chakula, na ya kama ulipendeza macho, na ya kama ulikuwa mti wa kutamaaniwa,* ***akatwaa ya***

matunda yake, akakula*; akampa mume wake vilevile pamoja naye, naye alikula"* (Mwanzo 3:6).

Neno la kushangaza kabisa! Mwanamume ambaye Mungu alimwumba kwa sura yake mwenyewe ili aweze kumjua, kumpenda na kumtii milele, mwanamume huyu alifanya nini? Alipenda Mungu ya kutosha hata alitii agizo lake? Sivyo! **Alichagua kuasi Mungu wa mapendo na kufuata Shetani, adui ya Mungu na watu!**

Ilikuwa siku ya huzuni kabisa. Wazazi wetu, Adamu na Hawa waligeuzia Bwana Mungu migongo yao kwa njia ya kula tunda la mti ambalo Mungu aliwakataza kula. Neno la Mungu linasema, *"Kwa mtu mmoja zambi iliingia ulimwenguni, na* ***kufa kwa njia ya zambi,*** *na hivi kufa kulikuja juu ya watu wote, kwa sababu wote wamefanya zambi"* (Waroma 5:12)! Hili ndilo neno lililotokea, hata kama hatufurahi juu yake.

Wewe na mimi, na watu wote tunafanana na Adamu. Tumezaliwa wenye zambi na ni lazima kwetu kufa, **kwa sababu tuko wazao wa Adamu.** Mtu huyu aliyeasi agizo la Mungu ni mzazi wetu **nasi tunafanana naye**. Nani katikati yetu anayeweza kusema kwamba hajaasi maagizo ya Mungu hata mara moja? Zambi **kama ugonjwa mbaya sana uliokuwa ndani ya Adamu imepitishwa kwetu sisi sote.**

Hata hivi, kuna tumaini, kwa sababu Neno la Mungu linasema vilevile, ***"Kama vile kwa kosa moja watu wote walihukumiwa azabu, hivi kwa tendo moja la haki, watu wote walipewa haki yenye uzima"*** (Waroma 5:18). Ndani ya masomo yanayofuata tutajifunza juu ya njia ya haki ya wokovu ambayo Mungu alitayarisha kwa njia yake wenye zambi wanaweza kurudi karibu na Mungu.

~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Ndani ya Somo 8 tunakusudi kuendelea na sura 3 ya Mwanzo na kuona nini ilitokea nyuma wakati Adamu na Hawa walipokwisha kuacha njia ya haki na kufuata njia ya uzalimu.

Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya Maandiko ya manabii, yanayosema,

> ***"Kwa mtu mmoja zambi iliingia ulimwengu, na kufa kwa njia ya zambi; na hivi kufa kulikuja juu ya watu wote, kwa sababu wote wamefanya zambi."*** (Waroma 5:12)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~

SOMO 8

TUNDA LA ZAMBI YA ADAMU

MWANZO 3

Tunakusalimu tena kwa jina la Mungu wa salama, anayetaka watu wote kufahamu, kuamini na kupokea njia ya haki ambayo ameamuru, na kuwa na salama ya kweli naye kwa milele. Tuendelee sasa na Somo 8 la Mfulizo *Njia ya Haki*.

Ndani ya masomo ya mbele tulijifunza ndani ya kitabu cha mwanzo namna Bwana Mungu alivyoumba watu wa kwanza kwa sura yake mwenyewe. Tulijifunza vilevile kama Mungu aliwaumba kwa sababu gani. Mungu alitaka wampende na nia zao zote, na mioyo yao mizima, na vile na nguvu yao yote, na kwa njia hii, waweze kuwa na ushirika wa ajabu naye kwa milele.

Hivi tuliona ya kwamba Mungu alimpa mwanamume **jaribu moja**, kuona kama alipenda Mungu kweli na atamtii. Mbele ya kuumbwa kwa mwanamke wa kwanza, Mungu aliagiza Adamu akisema, *"Wa kila mti wa shamba unaweza kula; lakini wa mti wa kujua uzuri na ubaya usile kwa maana siku unapokula, hakika utakufa"* (Mwanzo 2:16,17). Hivi Mungu alipima Adamu na alimwonya ya kwamba azabu ya kuasi itakuwa kufa na kutengwa naye! Mungu alipenda Adamu na alitaka Adamu kuwa na upatano mzuri naye kwa milele, lakini ndani ya Somo 7 tulisoma ya kwamba **Adamu na Hawa** walisikiliza na kufuata Shetani, na **waliasi Mungu** na kula wa mti ambao Mungu aliwakataza kula matunda yake.

Halafu leo, tutaendelea kujifunza ndani ya sura ya tatu ya kitabu cha Mwanzo, kuona **nini ilitokea wakati Hawa na Adamu walipokosea Mungu.** Ndani ya shairi 7, Maandiko yanasema, "*Nao wawili, macho yao yalifunguliwa; wakajua ya kama walikuwa watupu; wakashona majani ya mtini, wakajifanya nguo"* (Mwanzo 3:7).

Hivi kitu cha kwanza Adamu na Hawa walichofanya wakati walipokwisha kuasi Mungu kilikuwa nini? **Walijaribu kufunika haya na hatia yao!** Tumejifunza mbele ya kwamba wakati Adamu na Hawa wasipokula bado tunda la mti wa kujua uzuri na ubaya, "*walikuwa watupu, mume na mke wake, wala hawakuona haya"* (Mwanzo 2:25). Lakini mawazo yao juu ya miili yao yalikuwa namna nyingine

sasa. Sasa walikuwa na hatia na haya mbele ya Mungu Mtakatifu ambaye atalazimishwa kuwahukumu. Hivi, kwa kuficha haya yao, walishona majani ya mtini pamoja, na kufunika miili yao mitupu. Lakini kifuniko hiki cha miili yao hakikuweza kuondosha hatia mioyoni mwao.

Halafu Maandiko yanasema, *"Kisha wakasikia sauti ya Bwana Mungu akitembea shambani mangaribi; mume na mke wake wakajificha wenyewe mbele ya macho ya Bwana Mungu katikati ya miti ya shamba"* (Mwanzo 3:8). Kweli maneno yalikuwa yamegeuka kwa Adamu na Hawa tangu walipofanya zambi! Mbele ya kukosea Mungu walifurahi wakati Bwana Mungu alipokuja shambani kusemezana nao. Lakini sasa wakati waliposikia Mungu akikaribia, walitetemeka kwa **woga na haya**, **wakajaribu kujificha** katikati ya miti ya shamba! Adamu aliogopa na alifichama kwa sababu gani? Si nguvu kujibu ulizo hili. Kama mtu akiiba chakula toka shamba la mtu mwingine, atafanya nini kama akisikia sauti ya mwenye shamba? Atajaribu kujificha. Vivyo hivyo, Adamu aliyekamata kitu kilichokatazwa na Mungu alijaribu kujificha. Adamu alijua ya kwamba alikuwa amekosea Mungu.

Ilikuwa vizuri kwa Adamu kuogopa nyuma ya kuasi agizo la Mungu? Kabisa! Kwa nini? Kwa sababu Mungu alikuwa amemwambia wazi, *"Usile wa mti wa kujua uzuri na ubaya kwa maana siku unapokula,* ***hakika utakufa****"* (Mwanzo 2:17). Basi Mungu atafanya neno ambalo alisema? Unafikiri nini? Adamu atakufa kweli? **Mungu ataazibu watu ambao aliwaumba? Bwana alitendea Lusifero, ndiye Shetani, nini wakati Lusifero alipokataa kuruhusu Mungu kutawala juu yake?** Aliachilia Shetani na malaika waliofanya zambi? Sivyo, Mungu hakuwaachilia! Aliwafukuza mbali naye. Na zaidi ya ile, aliwatayarishia ziwa la moto! Kama Shetani, Adamu alikuwa amekataa kutawaliwa na Mungu. Basi Mungu aliweza kusema tu, "Ni neno bule!" na kuacha Adamu bila kumhukumu? Sivyo! **Mungu ni mtakatifu na ni lazima kwake kuazibu zambi!** Maandiko Matakatifu yanasema ya kwamba Mungu ana *"macho safi zaidi hata hawezi kutazama mabaya"* (Habakuki 1:12,13). Ndiyo, *"Bwana atahukumu watu wake! Ni neno la kuogopa kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai!"* (Waebrania 10:30,31). Kwa sababu yeye ni mtakatifu, ni lazima kwake kuhukumu na kuazibu kila zambi. Hivi ilikuwa sharti kwaye kuhukumu Adamu na Hawa kwa sababu ya zambi yao. Kwa sababu hii Bwana Mungu *"aliita Adamu, akamwambia: Wewe ni wapi?"* (Mwanzo 3:9).

Mungu alifanya nini wakati Adamu alipokwisha kukosa? Mungu

alikwenda kutafuta Adamu, akimwita na kusema, ***"Wewe ni wapi?"*** Adamu alikwenda kutafuta Mungu? Sivyo! Alikuwa akijaribu kujificha Mungu asimwone! Basi kwa nini Mungu aliita Adamu? Hakujua pahali Adamu alipokuwa? Mungu anayejua mawazo na makusudi yote ya watu alijua pahali Adamu alipokuwa akifichama! Mungu alimwita kwa sababu alitaka Adamu kutambua na kukiri zambi yake mbele yake. Alikaa kumpenda hata wakati Adamu alipokwisha kumwasi.

Adamu alijibu nini wakati Mungu alipouliza, "Wewe ni wapi?" Maandiko yanasema ya kwamba:

> *"[Adamu] alijibu na kusema, Nimesikia sauti yako shambani, na niliogopa kwa sababu nilikuwa mtupu; nikajificha." Bwana Mungu alimwuliza, "Nani alikuambia ya kama ulikuwa mtupu? Umekula wa mti juu yake nilikuagiza: Usile?" Adamu alisema, "Mwanamke ambaye ulinipa awe pamoja nami, yeye alinipa ya mti, na nilikula." Bwana Mungu "akamwambia mwanamke: Nini hii uliyofanya?"Mwanamke akasema, "Nyoka alinidanganya, na nilikula."* (Mwanzo 3:10-13)

Ulisikia namna Adamu na Hawa walivyojibu Mungu? **Kila mtu alijaribu kushitaki mtu mwingine**. Adamu alishitaki Mungu na Hawa vilevile, akisema, "Si kosa langu! Mwanamke yule ambaye ulinipa, ni kosa **lake**!" Basi Hawa alishitaki nyoka akisema, "Usinishitaki mimi! Yule nyoka alinidanganya!" Lakini Mungu anayejua mioyo ya watu alijua **wao wawili** wote walikuwa wenye hatia. Mungu hakuwalazimisha kula matunda ya mti. Na Shetani vilevile hakuwalazimisha kufanya hivi. Shetani anaweza kujaribu na kudanganya watu, lakini hawezi kulazimisha mtu ye yote kufanya zambi. Shetani alidanganya Hawa, lakini Hawa mwenyewe alichagua kula tunda walilokatazwa kula. Na juu ya Adamu Maandiko yanasema ya kwamba hakudanganywa (1 Timoteo 2:14). Yeye mwenyewe alichagua njia ya Shetani. Adamu alijua agizo la Mungu, lakini alichagua kuacha njia ya haki, na kufuata njia ya uzalimu. Wala hakuasi tu Mungu, lakini aliongeza zambi nyingine, ndiyo kujaribu kushitaki watu wengine juu ya kosa lake.

Hata leo watu wanajaribu kushitaki watu wengine juu ya makosa yao, lakini hawawezi kudanganya Mungu. Kwa njia ya Roho Mtakatifu Mungu anasema na watu, **Wewe ni wapi?** Unijibu! Umefanya nini? Kwa nini ulikataa kuamini na kutii Neno langu? Kwa nini unazarau wema wangu? Kwa nini unashitaki watu wengine juu ya zambi yako mwenyewe? *"Sawasawa nilivyo hai, Bwana anasema, kila goti litapigwa mbele yangu, na kila ulimi utakiri Mungu. Basi*

kwa hii kila mmoja wetu atatoa habari zake mwenyewe mbele ya Mungu" (Waroma 14:11,12)

Sasa tuendelee ndani ya sura 3 ya Mwanzo na kuona namna Mungu alivyohukumu nyoka, ndiye Shetani, Hawa na Adamu. Maandiko yanasema,

> *"Bwana Mungu akamwambia **nyoka**: Kwa sababu umefanya maneno haya, umelaaniwa kuliko nyama zote, na kuliko kila nyama ya mwitu; juu ya tumbo lako utakwenda, na mavumbi utakula siku zote za maisha yako; na nitatia uadui katikati yako na mwanamke, na katikati ya uzao wako na uzao wake; ataponda kichwa chako, na wewe utaponda kisigino chake. Akamwambia **mwanamke**: Nitazidisha sana uchungu wako na kuzaa kwako; kwa uchungu utazaa watoto; kutaka kwako kutakuwa kwa mume wako, naye atakutawala. Akamwambia **Adamu**: Kwa sababu umesikia sauti ya mwanamke wako, na umekula wa mti, juu yake nilikuagiza nikisema: Usile matunda yake; udongo umelaaniwa kwa sababu yako; kwa uchungu utakula ya matunda yake siku zote za maisha yako: michongoma na miiba utakuotesha; na utakula majani ya shamba; kwa jasho ya uso wako utakula mkate, hata utakaporudi kwa udongo; kwa maana umetwaliwa katikati yake; kwa sababu mavumbi wewe, na utarudi kwa mavumbi"* (Mwanzo 3:14-19).

Ona matunda ya zambi yao! Ilizaa huzuni na maumivu, michongoma na miiba na jasho, ugonjwa na mauti. Ndiyo *"mishahara ya zambi ni **mauti!**"* (Waroma 6:23) Mungu alisema nini itapata Adamu na Hawa kama wakikula wa mti ambao aliwakataza kula matunda yake? **"siku unapokula,** hakika **utakufa**" (Mwanzo 2:17). Halafu Adamu na Hawa walizikwa siku walipokula? Sivyo. Basi walikufa siku ile? Kabisa! Namna gani? Siku ile ile **Adamu na Hawa walikufa rohoni** kwa sababu hawakuwa na undugu na Mungu wa Uzima tena.

Kama tulivyoona mbele, Maandiko Matakatifu yanafundisha ya kwamba **mauti ni *kutengwa na Mungu***. Wakati Adamu na Hawa walipoasi Mungu, walijitenga na Mungu, **Bwana wa Uzima**. Kwa sababu walichagua kuamini na kufungana na adui ya Mungu, hawakushiriki ndani ya uzima wa Mungu tena. Kwa mfano, ukiwa na adui, na rafiki yako anafungana naye, "rafiki" huyu amegeuka adui yako vilevile. Rafiki ya adui yako ni adui yako vilevile. Vivyo hivyo mtu ye yote anayetii Shetani ni adui ya Mungu. Zambi inatenga mtu na Mungu.

Mbele ya kumaliza somo hili, sharti tufahamu na kukumbuka neno lingine vilevile. Ni hili: Sisi sote tulizaliwa duniani kama wafu kwa sababu ya *makosa na zambi* (Waefeso 2:1), watu *"**waliotengwa***

mbali na uzima wa Mungu" (Waefeso 4:18). Haya ndiyo maneno ya Mungu. Adamu aliyekataa utawala wa Mungu, ni baba ya watu wote walio hai. Siku Adamu alipoasi Mungu, aligeuka *mwenye zambi*. Kwa sababu hii **wazao wake wote ni wenye zambi** vilevile. Na neno lingine ndilo hili: Zambi ya Adamu iliharibu ushirika wake na Mungu. Neno la Mungu linasema, *"Kama kwa mtu mmoja zambi iliingia ulimwenguni, na kufa kwa njia ya zambi; na hivi* ***kufa kulikuja juu ya watu wote, kwa sababu wote wamefanya zambi!"*** (Waroma 5:12)

Adamu, babu yetu, ambaye alijitenga na Mungu, ni **kama tawi linalokatwa toka mti.** Nini ilitokea wakati tawi lisipofungana na mti tena? Linakauka na kufa. Na nini inapata matawi yaliyofungana na tawi hili lililokatwa? Matawi haya yana uzima? Sivyo, yanakufa vilevile kwa sababu ni sehemu ya tawi linalokauka. Vivyo hivyo **watoto wote wa Adamu ni kama matawi madogo** ya tawi lililokatwa. Kwa sababu ya zambi yake, Adamu ni kama tawi linalokauka, nasi ni mmoja naye. Zambi ya babu yetu Adamu inatugusa sisi sote. Sisi sote tunashiriki ndani ya hukumu yake. Hivi Daudi, nabii la Mungu, aliandika ndani ya Zaburi 51:5, *"Tazama, niliumbwa katika hali ya uovu na* ***katika makosa*** *mama yangu alinichukua mimba."*

Zambi inafanana na ugonjwa mbaya wa wakati wa sasa unaoitwa AIDS. Ni mateso makubwa yanayoenea katika dunia nzima. Wakati AIDS unapoingia mwili wa mtu, hautauacha kamwe. Mtu mwenye AIDS anaweza kupitisha ugonjwa huu kwa watoto wake. AIDS unaua watu na kufika sasa waganga hawajui namna gani kuuponyesha. Zambi ni vivyo hivyo. Ni taabu kubwa inayoenea katika dunia nzima. Zambi **ni mwuaji** wa watu wanaokufa kwa milele, na **sisi watu hatuna dawa kwa kujiponyesha.**

Lakini tunasifu Mungu leo na furaha mioyoni, kwa sababu Mungu yeye mwenyewe alitayarisha njia kutuokoa toka azabu na uwezo wa zambi kwa milele! Lakini lazima tuiamini. Mungu akitaka, tutaonyesha ndani ya Somo 9 namna gani Mungu alitolea Adamu na Hawa na wazao wao wote, ahadi ya ajabu juu ya Mwokozi wa uwezo atakayekuja duniani kuokoa wenye zambi toka zambi, Shetani na Hadeze.

Asante kwa kusoma. Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya kweli hii kubwa anayotaka kutufundisha leo. Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya masemo haya ya nabii Daudi:

> ***"Tazama, niliumbwa katika hali ya uovu; na katika makosa mama yangu alinichukua mimba."*** (Zaburi 51:5)

SOMO 9

AHADI YA AJABU

MWANZO 3

Salamu kwako, rafiki msomaji kwa jina la Mungu wa salama. Tunafurahi kuendelea leo na Somo 9 la mfulizo *Njia ya Haki*.

Ndani ya somo la mbele tuliona ya kwamba Adamu na Hawa waliacha njia ya Mungu wakati walipokula matunda ya mti ambao Mungu alikataza. Hivi mtu, aliyeumbwa kwa sura ya Mungu, alichagua kufuata Shetani, adui ya Mungu. Mbele, wakati Adamu na Hawa wasipofanya zambi bado, walifurahi wakati Mungu alipofika shambani kusemezana nao, lakini sasa, wakati waliposikia sauti ya Mungu, **waliogopa na kuwa na haya na walijaribu kujificha** katikati ya miti ya shamba! Lakini Mungu alifuata Adamu na Hawa, akasema nao, na kuwajulisha matunda ya zambi yao: taabu na mateso, miiba na michongoma, ugonjwa na **mauti**.

Hivi, tangu siku ile hata leo, kivuli cha mauti ni juu ya wazao wa Adamu. Wazao wote wa Adamu wanazaliwa na tabia ya zambi. **Sisi sote tunashiriki hali ya zambi ya mzazi wetu** Adamu. Kwa sababu ya zambi ya Adamu sisi sote tunazaliwa wenye zambi. Kama zambi ya Adamu ilimtenga na Mungu, vivyo hivyo zambi yetu imetutenga naye. Kwa sababu hii Maandiko yanasema,

> *"Kama kwa mtu mmoja zambi iliingia ulimwenguni, na kufa kwa njia ya zambi; na hivi kufa kulikuja juu ya watu wote, kwa sababu wote wamefanya zambi"* (Waroma 5:12). *"Kwa sababu wote wamefanya zambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu"* (Waroma 3:23). *"Maovu yenu yamewatenga ninyi na Mungu wenu, na zambi zenu zimeficha uso wake kwenu"* (Isaya 59:2).

Hatufurahi kusikia habari hizi, lakini ni habari za kweli. Kweli hii inachoma roho kama pilipili.

Hivi tunaona ya kwamba **zambi ile moja ilitenga watu wote wa dunia na Mungu.** Siku Adamu alipoasi Mungu, Adamu na wazao

wake wote walitoka ufalme wa nuru na kuingia ufalme wa giza. Hawana ushirika ndani ya Ufalme wa Mungu tena. Kwa sababu ya zambi yao **walifungana na Shetani,** ambaye aliwafunga na kuwafanyiza watumwa. Hawakuwa na tumaini tena ndani ya maisha ya sasa ila utumwa kwa zambi na woga wa mauti; na kwa wakati wa kuja, azabu bila mwisho na moto wa milele zinawangojea!

Kama hizi zingalikuwa habari za mwisho wa Maandiko Matakatifu, kama tungalifunga tu kitabu na kutoa machozi na uchungu kama mtu anayepotea baharini bila tumaini ya kwamba ataponyeshwa. Kama Mungu asingalitayarisha njia ya wokovu kuokoa wana wa Adamu kama tungalipotea kwa milele! Lakini BWANA Mungu wetu abarikiwe, habari za zambi ya Adamu si habari za mwisho za maandiko ya manabii. **Mungu ni mwenye rehema kubwa naye amefungulia wana wa Adamu mlango wa wokovu!** Hivi, Neno la Mungu linasema,

> *"Pahali zambi zilipozidi, neema ilizidi zaidi sana"* (Waroma 5:20). *"Musiogope, kwani tazama, nimewaletea ninyi Habari Njema ya furaha kubwa itakayokuwa kwa watu wote"* (Luka 2:10). *"Kwa sababu neema ya Mungu inayoleta wokovu kwa watu wote, ime-onekana"* (Tito 2:11).

Kama tulivyojifunza mbele, Mungu ni mtakatifu na kwa sababu hii inampasa kuhukumu wenye zambi wote. Mungu ni mwenye haki na hawezi kuona zambi bule. Ni lazima kwake kuazibu kila zambi. Azabu kwa zambi ni mauti na kutengwa na Mungu kwa milele. Mungu habadiliki kamwe na azabu kwa zambi haibadiliki kamwe. Lakini leo tutaanza kusoma **ndani ya Maandiko** ya kwamba **Mungu, yule Mtakatifu, alitayarisha njia kuponyesha wenye zambi toka azabu ya zambi.** Hivi, tutajifunza ya kwamba Mungu si Mtakatifu tu, lakini Mwenye Rehema vilevile! **Mungu, Mwamuzi wetu, anataka kugeuka Mwokozi wetu!**

Leo tutaona namna gani siku Adamu na Hawa walipofanya zambi, Mungu alianza kufunua shauri lake la ajabu kuokoa wenye zambi. Tuendelee sasa kusoma ndani ya kitabu cha Mwanzo, ili tuweze kujifunza juu ya Habari Njema hizi. Tunasoma ndani ya sura 3, shairi 15 Mungu alisema na Shetani aliyekuwa ndani ya nyoka, ***"Nitatia uadui katikati yako na mwanamke, na katikati ya uzao wako na uzao wake; ataponda kichwa chako, na wewe utaponda kisigino chake."***

Kuna kweli kubwa nyingi ndani ya shairi hili. Kwa ufupi,

tunaweza kujumlisha habari za shairi hili hivi: **Mungu alikuwa akianza kujulisha shauri lake kuleta Mwokozi duniani** atakayekomboa wana wa Adamu toka utawala wa Shetani. **Hili ni shairi la kwanza linalotangaza habari za kuja kwa Mkombozi mtakatifu** (Mpatanishi). Ndani ya shairi hili tuwaze juu ya kweli ine juu ya Mkombozi ambaye Mungu aliahidi kutuma.

1) Kweli la kwanza ndiyo hii: Mungu alikuwa akitangaza namna gani Mkombozi huyu **atazaliwa na mwanamke tu**, maana yake, na bikira. Sisi sote tumezaliwa na wazazi mume na mke, lakini Mwokozi huyu atakayekuja atazaliwa na mwanamke peke yake, kwa uwezo wa Mungu. Hatakuwa na baba ya dunia. Haikuwezekana kwa Mwokozi wa dunia kuwa mzao wa Adamu, kwa sababu kila kitu kinachotoka kwa Adamu kinachafuwa na zambi. Sharti Mwokozi wa ulimwengu awe bila zambi. Lazima atoke kwa Mungu, toka mbinguni. Hivi neno la kwanza ambalo shairi hili linatufundisha ndilo hili: Mungu aliahidi kutuma Mkombozi mtakatifu atakayezaliwa na bikira.

2) Kuna neno lingine Mungu alilotangaza siku Adamu na Hawa walipofanya zambi. Juu ya Mkombozi atakayekuja Mungu alisema na Shetani: "Utaponda kisigino chake." Hivi Mungu alianza kutangaza namna **Shetani atakavyotesa Mwokozi** ambaye Mungu atatuma toka mbinguni. Ndani ya masomo ya nyuma, tutaona ya kwamba manabii walitangaza namna Shetani atasukuma watu kutesa, kutaabisha na kuua Mkombozi. Lilikuwa sehemu ya shauri la Mungu kwa Mkombozi kupigwa. Kwa kuturudisha kwa Mungu itapasa Mwokozi wa dunia kufa kama sadaka kwa zambi; Mwenye haki atakufa kwa sisi wazalimu. Ni lazima kwake kubeba azabu ya zambi, ndiyo mauti.

3) Kweli ya tatu juu ya Mkombozi ni ya kwamba Mungu alimwambia Shetani, aliyekuwa ndani ya nyoka ya kuwa Mkombozi *"ataponda kichwa chake [cha Shetani]."* Hizi zilikuwa habari mbaya kwa Shetani, lakini ni habari njema kwa mtu ye yote ambaye anataka kufunguliwa toka uwezo wa Shetani, zambi na Hadeze! Hivi, Mungu alianza kutangaza ya kwamba **mwishoni Mkombozi atashinda Shetani** na kufungua wana wa Adamu toka utumwa wa zambi.

4) Mwishoni, Mungu alianza kutangaza ya kwamba kutakuwa na **mafungu mawili** ya watu duniani: Watu wa Shetani na watu wa Mungu. Watu wa Shetani ndio wale wanaokataa kuamini Neno la Mungu. Watu wa Mungu ndio wale wanaoamini Neno la Mungu na kuamini Mkombozi ambaye Mungu aliahidi kutuma. (Ona Yoane 1:9-13.)

Hivi, siku Adamu na Hawa walipofanya zambi, Mungu alianza kutangaza shauri lake la ajabu kuokoa wenye zambi. Ndani ya masomo ya nyuma tutaona ya kwamba manabii wote wa Mungu walitangaza habari za kuja kwa Mwokozi mtakatifu atakayefungua wenye zambi toka utawala wa Shetani. Kama habari hizi tulizofundisha sasa tu si wazi kwanza kwa ufahamu wako, usifazaike, kwani wakati tutakapoendelea na mafundisho yetu habari hizi zitafahamikana vizuri kupita. Mezali ya kabila moja inasema, "Mtu anaweza kukamata makako polepole tu mwituni." Na mezali nyingine inasema, "Yule anayengoja na saburi kwa kisima mwishoni atapewa ndoo." Wewe unangoja kwa "kisima" cha Neno la Mungu? Vema! Mungu anasema: *"Kama ukiutafuta (ndio ufahamu) kama feza, na kuutafutatafuta kama hazina zilizofichwa; halafu ... utapata maarifa kwa Mungu!"* (Mezali 2:4,5).

Tumalize kusoma sura ya tatu ya Mwanzo. Maandiko yanasema,

> *"Bwana Mungu akafanyia Adamu na mke wake mavazi ya ngozi, akawavalisha. Bwana Mungu akasema: Tazama, mtu amekuwa kama mmoja wetu, kwa kujua uzuri na ubaya; na sasa, isiwe anyoshe mkono wake na kutwaa vile wa mti wa uzima, na kula na kuishi milele; kwa hivi Bwana Mungu akamtoa toka shamba la Edeni, alime udongo pale alipotwaliwa. Hivi akafukuza mtu, akaweka Makerubi kwa mashariki ya shamba la Edeni na upanga wa ulimi wa moto uliogeuka pande zote kuchunga njia ya mti wa uzima."* (Mwanzo 3:21-24)

Huu ndio mwisho wa sura 3. Kuna habari nyingine ambazo inatupasa kueleza kupita, mbele ya kumaliza somo hili.

Maandiko yanasema, "*Bwana Mungu akafanyia Adamu na mke wake mavazi ya ngozi, akawavalisha."* Unakumbuka neno Adamu na Hawa walilofanya nyuma ya kula tunda la mti wa kujua uzuri na ubaya? **Wakashona majani ya mtini** na kufunika miili yao kwa kuficha haya yao mbele ya Mungu. Mungu alikubali mavazi ambayo walijifanyia? Sivyo! Kwa nini Mungu hakukubali mavazi haya? Kwa sababu alitaka kufundisha Adamu na Hawa ya kwamba Yeye ni **mkamilifu** na hawezi kukubali kazi za watu **zisizo kamilifu.** Juu ya neno hili, Maandiko yanasema, *"Lakini sisi sote tumekuwa kama kitu kichafu, na* ***haki zetu zote ni kama vitambaa vya kupasukapasuka vya taka"*** (Isaya 64:6). Hakuna neno mtu analoweza kufanya kufunika zambi zake mbele ya Mungu.

Lakini Mungu alifanya neno moja kwa Adamu na Hawa. **Aliua nyama**, akaondosha ngozi zao na kufanya **mavazi** kwa Adamu na

Hawa. Ndiyo, ni Mungu aliyetoa sadaka ya kwanza ya nyama. Bila shaka Adamu na Hawa walishituka sana wakati damu inayoleta uzima ilipovuya toka nyama ambazo Mungu aliua! Kwa njia ya damu iliyomwangika toka nyama Mungu alifundisha Adamu na Hawa ya kwamba *"mshahara wa zambi ni **mauti**"* (Waroma 6:23), na ya kwamba ***"pasipo kumwanga damu hakuna ondoleo"*** (Waebrania 9:22).

Hatuwezi kueleza maneno yote juu ya habari hizi leo, ila kusema sheria ya Mungu juu ya usamehe ndiyo ya kwamba, ***"pasipo kumwanga damu hakuna ondoleo."*** Ni lazima kwa azabu ya zambi kulipwa. Azabu ya zambi ni mauti. Mungu anaweza kusamehe zambi zile tu ambazo zililipwa. Ni lazima kwa zabihu isiyofanya zambi kufa kwa pahali pa mwenye hatia ya zambi. Kwa njia hii moja tu Mungu anaweza kusamehe zambi za watu bila kuacha kuwa mwenye haki. Tutajifunza zaidi juu ya neno hili nyuma. Leo tukumbuke ya kwamba Mungu alimwanga damu ya nyama kufunika haya ya Adamu na Hawa.

Kisha, **Mungu alifukuza Adamu na Hawa** toka shamba la Paradiso (Edene). Aliweka malaika aliyeshika upanga wa ulimi wa moto kuzuiza mtu asifikie mti wa uzima. Adamu na Hawa walikuwa wamechagua njia ya mauti wakati walipokula tunda lililokatazwa na Mungu. Hivi, hawakuweza kufurahi tena ndani ya baraka za shamba zuri la Paradiso. Tuliona mbele ya kwamba Mungu alifukuza Lusifero, ndiye Shetani, toka kwake kwa sababu ya zambi yake. Na sasa tunaona ya kwamba alifukuza Adamu na Hawa kwa sababu ya zambi yao. Mungu ni mtakatifu, na **ni sharti kwake kuazibu maneno yote yasiyo matakatifu.**

Hivi, rafiki, tukumbuke maneno haya mawili:

1) **Mungu ni mtakatifu**. Hawezi kukubali au kuvumilia zambi. Kwa sababu hii alihukumu Adamu na Hawa na kuwafukuza toka shamba.

2) **Mungu ni mwenye rehema**. Adamu na Hawa hawakustahili rehema ya Mungu. Walistahili hukumu yake tu. Lakini Mungu hataki watu kupotea. Kwa sababu hii aliahidi kutuma Mwokozi atakayeweza kuokoa wenye zambi toka giza la ufalme wa Shetani, na kuwahamisha kwa nuru na utukufu wa ufalme wa Mungu.

Usidanganywe: **haiwezekani kwa rehema ya Mungu kukana haki ya Mungu kamwe.** Sharti maneno haya mawili yafungane

pamoja ndani ya namna Mungu anavyotenda. Ndani ya masomo ya nyuma tutaonyesha namna gani Mungu anaweza kuwa na rehema kwa wenye zambi pamoja na kuwa mwenye haki vilevile.

~~~~~~~~~~~~~~~

Rafiki, hii ndiyo *Njia ya Haki.* Tulisemezana juu ya ahadi ya ajabu Mungu aliyotoa siku Adamu na Hawa walipoacha njia ya Mungu. Tunataraji utaendelea na masomo haya kufika wakati utakapofahamu kabisa ahadi ya ajabu ya Mungu juu ya **Mkombozi** na **Mwokozi** wa dunia.

Mungu akubariki na kukusaidia kuwaza sana juu ya Maandiko yanayosema,

> ***"Pahali zambi zilipozidi, neema [ya Mungu] ilizidi zaidi sana."*** (Waroma 5:20)
~~~~~~~~~~~~~~~

SOMO 10

NJIA YA SADAKA

MWANZO 4

Salama kwako, msomaji, kwa jina la Mungu wa salama, anayetaka watu wote kufahamu, kuamini na kupokea njia ya haki ambayo ameamuru, na kukaa na salama naye kwa milele. Tunafurahi kuendelea leo na Somo 10 la mfulizo unaoitwa *Njia ya Haki*.

Ndani ya somo la mbele tuliona ndani ya kitabu cha Mwanzo ya kwamba wakati Adamu na Hawa walipokwisha kufanya zambi, Mungu alianza kutangaza **shauri lake** kufikisha duniani Mmoja atakayefungua wana wa Adamu toka uwezo wa Shetani. Tulisoma vilevile ya kwamba Mungu hakukubali mavazi ya majani ambayo Adamu na Hawa walijifanyia. Alitaka kuwafundisha ya kwamba hakuna njia kwa wenye zambi kufunika haya yao mbele ya Mungu Mtakatifu ambaye analazimishwa kuwahukumu. Mungu tu anaweza kuokoa wenye zambi toka hatia yao. Hivi, tuliona ya kwamba Mungu mwenyewe alitoa sadaka za nyama na kutwaa ngozi zao kufanya mavazi kwa kuvalisha Adamu na Hawa **Mungu alitoa sadaka ya kwanza ya damu.** Tulisoma vilevile ya kwamba Mungu alisema kuna namna mbili za watu duniani: wale wanaokataa kuamini Neno la Mungu, na wale ambao wanaliamini.

Leo tutasoma juu ya wana wawili wa kwanza wa Adamu na Hawa, ndio **Kaina**, aliyekataa kuamini Mungu, na **Abeli**, aliyeamini Mungu. Kama tulivyoona, saa hii Adamu na Hawa walikaa inje ya shamba la Edeni. Mungu alikuwa amewafukuza kwa sababu ya zambi yao. Kwa sababu ya kuanguka kwao hawakufurahi tena ndani ya baraka za shamba la Edeni. Zambi yao ilikuwa imeharibu upatano wao na Mungu. Lakini Mungu aliwapenda hata hivi na aliwalinda, hata kama hawakufahamu neno hili.

Halafu sasa tuendelee kusoma pamoja toka kitabu cha Mwanzo, sura 4. Pale imeandikwa, "*Mwanamume alijua Hawa, mke wake; akachukua mimba, akazaa **Kaina**, akasema: Nimepata mume kwa Bwana.*

Akazaa tena ndugu yake ***Abeli****. Na Abeli alikuwa mchungaji kondoo, lakini Kaina alikuwa mlimaji udongo"* (Mwanzo 4:1,2).

Adamu na Hawa walizaa wana wawili, Kaina na Abeli. Walikuwa wenye zambi, kama wazazi wao. Zambi ya Adamu ilienea kwa watoto wake, kama ugonjwa. Hawa alikuwa mwenye zambi wakati alipopata mimba ya Kaina na Abeli. Hivi, Maandiko yanasema, *"Adamu alizaa wana kwa sura yake"* (Mwanzo 5:3). Wana walifanana na baba. **Kaina na Abeli walizaliwa na tabia ya zambi.** Walipata nguvu kwa mwili na kuongezeka katika maarifa.

Kaina alishika kazi ya mlimaji. Alitumika nguvu sana. Abeli aligeuka mchungaji kondoo. **Wao wawili walijua habari za Mungu.** Walijua Mungu yuko na ya kwamba yeye ni mtakatifu na anachukia zambi. Na bila shaka **wao wawili walijua ya kwamba wakitaka kukaribia Mungu, iliwapasa kuja na sadaka ya damu, kama Mungu alivyoagiza.**

Basi siku moja Kaina na Abeli walifikiri walitaka kuabudu Mungu na kumtolea zabihu. Hivi, Maandiko yanasema,

> *"Siku zilipopita, Kaina akapeleka ya matunda ya udongo kwa Bwana. Na Abeli, yeye vilevile alipeleka wa wazao wa kwanza wa kundi lake na ya mafuta yake.* ***Bwana akaheshimu Abeli na zabihu yake, lakini hakuheshimu Kaina na zabihu yake.*** *Hivi Kaina akakasirika sana, uso wake ukakunjamana"* (Mwanzo 4:3-5).

Tuwaze juu ya neno hili. Watu wawili walitaka kuabudu Mungu. Wao wawili walitolea Mungu zabihu. Lakini Maandiko yanasema, *"Bwana akaheshimu Abeli na zabihu yake, lakini hakuheshimu Kaina na zabihu yake."* Kwa nini Mungu alipokea zabihu ya Abeli, na alikataa ile ya Kaina?

Zabihu ya Kaina ilikuwa namna nyingine kabisa na ile ya Abeli. Kaina aliletea Mungu **mboga nzuri sana na matunda**. Ndugu yake Abeli alileta **mwana-kondoo bila kipako.** Basi Mungu hapendi mboga na matunda? Mungu hakukataa zabihu ya Kaina kwa sababu ile. Halafu kwa sababu gani Mungu alihesabia Abeli haki lakini aliacha Kaina katika zambi zake? Hii ndiyo sababu yenyewe: **Abeli alileta zabihu namna Mungu alivyoagiza, lakini Kaina alileta neno lingine.** Mungu alihitaji nini ili aweze kusamehe zambi zao pamoja na kukaa mwenye haki? Alihitaji damu, ndio **uzima** wa nyama aliye bila kipako. Abeli aliamini Mungu na alileta sadaka ya damu, kama Mungu alivyoagiza. Lakini Kaina, mtu huyu hakuamini neno

Mungu alilosema. Sikiliza Maandiko, "***Kwa imani*** *Abeli alitolea Mungu zabihu nzuri zaidi kupita Kaina: kwa hii alishuhudiwa menye haki, Mungu akishuhudia sadaka yake"* (Waebrania 11:4) Abeli aliamini Mungu, lakini Kaina hakumwamini.

Maana ya kuamini Mungu ni nini? Kuamini Mungu ni kutumainia Mungu na kutii Neno lake. Kuamini Mungu ni **kuamini maneno Mungu anayosema ni kweli**. Kama ukisema "Ninaamini Mungu", lakini huamini maneno Mungu anayosema ndani ya Maandiko Matakatifu, huamini Mungu kweli. **Mungu na Neno lake ni moja.** Ukiamini Mungu, utaamini na kutii Neno lake. Kama usipoamini maneno Mungu anayosema, unakataa Mungu mwenyewe.

Mungu alikubali Abeli kwa sababu Abeli aliamini Neno lake na alikuja na damu ya mwana-kondoo, kama Mungu alivyoagiza. Mungu hakukubali Kaina kwa sababu Kaina hakuamini Neno la Mungu kabisa kabisa. Kaina alisema aliamini Mungu, lakini matendo yake yalikana masemo yake, kwani hakuleta sadaka ya damu, kama Mungu alivyoagiza.

Labda mtu mwingine anauliza, "Kwa sababu gani Mungu aliagiza wamtolee sadaka ya nyama? Kwa nini Mungu alisema, *"Bila kumwangika kwa damu, hakuna usamehe"?* Alisema hivi kwa sababu ya sheria takatifu ya Mungu inayosema **malipo (mishahara, azabu) ya zambi ni mauti!** Kwa sababu ya neno hili ilikuwa lazima kwa damu kumwangika. Mungu hakusema, "Matunda na mboga zinaweza kulipa kwa zambi." Na vilevile Mungu hakusema ya kwamba watu wanaweza kulipa kwa zambi zao kwa njia ya kutenda mema na kufunga chakula na kutoa mali. Sivyo! Neno Mungu mtakatifu alilosema ni ya kwamba malipo kwa zambi ni **mauti**!

Ndani ya Maandiko ya manabii Mungu anaonyesha ya kwamba kila mtu, kila mtoto wa Adamu amefanya zambi na ya kwamba kila mwenye zambi ana **deni kubwa** karibu na Mungu Mtakatifu. Ni lazima kwa mwenye zambi kufa na kufuta deni ile ya zambi katika Hadeze kwa milele. Deni yako ya zambi ni kubwa sana na huwezi kamwe kufanya matendo mema ya kutosha kuilipa mbele ya Mungu. **Azabu ya zambi ni mauti na Hadeze,** na kwa sababu hii matendo mema hayawezi kutosha kamwe.

Tujaribu kueleza neno hili kwa njia ya mfano. Waza ya kwamba nina deni kubwa ya mali karibu na mtu mmoja, na ninasema naye, "Ninajua nina deni kubwa karibu nawe lakini sina mali hata kidogo

kwa kuilipa. Lakini nina shauri kwa kumaliza deni hii. Hili ndilo shauri langu: Nitakutumikia kwa njia ya kufagia kiwanja cha nyumba yako kila siku kufika siku deni yangu itakapokwisha." Mtu yule mwingine atasema nini juu ya shauri hili? Labda atakasirika, au labda atanicheka, lakini ninajua ya kwamba hatakubali shauri langu! Kwa nini? Kwa sababu haiwezekani hata kidogo kulipa deni ile kubwa kwa njia ya "matendo mema" haya madogo!

Vivyo hivyo hakuna mtu anayeweza kulipa deni yake ya zambi na matendo mema. Kuna kitu kimoja tu kinacholipa kwa zambi —si mali wala kazi njema lakini **mauti**. Azabu ya zambi ni mauti na hukumu. Hivi, Mungu hakuweza kufutia mbali deni za zambi za Kaina na Abeli kwa njia ya kazi za mikono yao wenyewe. Shauri la Mungu kufutia mbali deni yao ya zambi ilikuwa kwa njia ya damu ya zabihu. Ilikuwa lazima kwa yule asiyekuwa na zambi kufa kwa pahali pa mwenye hatia.

Msingi wa usamehe wa zambi si shauri la mtu, lakini shauri la Mungu. Kwa njia ya sadaka (ya mwingine) Mungu alifungua mlango wa usamehe na wokovu kwa wana wa Adamu. Katika miaka ya zamani Mungu alitoa amri kusema sharti kila mwenye zambi alete nyama asiye na kipako, na kumchinja. Nyama yule asiyefanya neno baya alikufa kwa mwenye zambi. Kwa sababu ya damu ya sadaka namna hii, Mungu aliweza kuwa na uvumilivu kwa wazao wa Adamu na kufunika zambi zao kwa wakati. Lakini damu ya nyama ***haikuweza kutangua zambi*** ya mtu, kwa sababu bei ya mtu inapita ile ya nyama. Kwa sababu hii Maandiko yanasema kwamba "*torati ni **kivuli** cha yale mema yatakayokuwa, wala si sura yao wenyewe ... maana **haiwezekani kwa damu ya ngombe na mbuzi kuondoa zambi***" (Waebrania 10:1,4)

Hivi lazima tukumbuke ya kwamba sadaka za nyama zilikuwa **mifano tu ya Mwokozi** atakayefika duniani kulipa deni ya zambi kwa wazao wa Adamu. Mwokozi huyu, ambaye Mungu aliahidi kutuma atakufa "*mara moja kwa ajili ya zambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki ili atulete kwa Mungu*" (1 Petro 3:18) Kama ilivyoandikwa ndani ya Habari Njema [Injil], "*Huyu manabii yote wanamshuhudia ya kwamba kwa jina lake **kila mtu ambaye anamwamini atapewa usamehe wa zambi***" (Matendo 10:43).

Hivi tunaona ya kwamba kwa miaka inayopita lilikuwa shauri la Mungu kwa watu kutoa sadaka za nyama. Lakini Kaina aliona shauri la Mungu bule. Alifanya shauri lingine, dini nyingine, **dini ya**

kwanza ya uwongo. Aliletea Mungu kazi za mikono yake mwenyewe. Alitolea Mungu mazao ya shamba alilolima, mboga ya inchi iliyolaaniwa, isiyokuwa na damu. Mungu alipokea sadaka hii iliyokosa damu? Sivyo. Hakuipokea.

Lakini Abeli aliletea Mungu mwana-kondoo asiyekuwa na kipako na alimwua hata damu ilimwangika. Nyuma yake alimchoma kwa moto. Kwa sababu ya sadaka hii Abeli alikuwa na damiri safi mbele ya Mungu. Alijua ya kwamba alistahili kufa kwa sababu ya zambi zake, lakini **mwana-kondoo asiyekuwa na zambi alikufa kwa pahali pake.** Kwa njia hii Abeli alionyesha imani yake ndani ya Mkombozi atakayefika duniani, na kufa kwa ajili ya wenye zambi, kubeba azabu ya zambi yao.

Tunataka kujumlisha habari za leo kwa njia ya kuuliza neno kubwa sana. Kwa sababu gani Mungu hakupokea sadaka ya Kaina? Kaina alikuwa na zambi kupita Abeli? Sivyo. Wao wawili walikuwa wenye zambi. Wao wawili walitolea Mungu sadaka. Kaina alikuwa mtu wa dini. Tungeweza kusema ya kwamba sadaka ya Kaina ilikuwa nzuri kupita ile ya Abeli. Mboga na matunda yanaonekana vizuri sana, lakini mwana-kondoo anayechinjwa na damu yake si ono la kupendeza macho! Lakini zambi ni kitu cha kuchukiza kwa Mungu na njia ya usamehe ambayo aliitayarisha inasema: ***"Pasipo kumwanga damu, hakuna ondoleo!"*** Hivi, Mungu alikataa Kaina na sadaka yake kwa sababu Kaina hakuheshimu njia ambayo Mungu alitayarisha kwa kumtolea sadaka.

Hakuna mtu anayeweza kufika karibu na Mungu isipokuwa anakuja kwa njia ya haki ambayo Mungu alitayarisha! **Njia ya Mungu ni kamilifu na sawasawa!** Ni kama mathématique. Mwalimu akiuliza mwanafunzi katika darasa,"2+2 ni ngapi?" kuna jibu ya haki moja tu, ndilo **2+2=4.** Mwanafunzi akijibu 3 anaanguka. Yule anayejibu 5 anaanguka vilevile. Ni lazima kwa jumla ya 2 na 2 kuwa 4! Ni vivyo hivyo na njia ya haki ambayo Mungu alitayarisha. Mungu ni Mungu mmoja tu na kuna **njia moja** tu kwa wenye zambi kupatanishwa na Mungu yule Mtakatifu! Njia hii ni **Sadaka mkamilifu kabisa.**

Wewe msomaji, unajua maneno Mungu anayosema juu ya Sadaka mtakatifu ambaye Mungu alitayarisha **kuzima kabisa hatia yako ya zambi?** Unajua ya kwamba Mungu mwenyewe alituma hapa duniani Mwokozi mwenye uwezo wote ili uweze **kusamehewa** toka zambi zako na kuwa na **roho safi** mbele ya Mungu? Ndani ya

masomo ya nyuma, tutajifunza maneno mengi juu ya Mwokozi huyu wa ajabu. Maandiko Matakatifu yanasema juu yake, *"Wala hakuna wokovu katika mwingine, kwa maana hakuna jina lingine chini ya mbingu walilopewa watu tupate kuokolewa nalo"* (Matendo 4:12).

~~~~~~~~~~~~

Sharti tuache hapa leo. Ndani ya Somo 11 tutaendelea kujifunza juu ya Kaina na Abeli. Kaa kukumbuka sheria hii ya Mungu iliyo kama msingi, yanayoandikwa ndani ya Maandiko Matakatifu ya manabii,

"... pasipo kumwanga damu hakuna ondoleo." (Waebrania 9:22)
~~~~~~~~~~~~

SOMO 11

KUTOTUBU KWA KAINA

MWANZO 4

Salama iwe kwako, Rafiki. Ndani ya somo la mbele tulijifunza juu ya wana wawili wa kwanza wa Adamu na Hawa, **Kaina na Abeli.** Tuliona ya kwamba wao wawili walitaka kuabudu Mungu na kumtolea zabihu. Kaina alichukua ya matunda aliyootesha shambani na kuyatoa kwa Mungu. Abeli alitolea Mungu mwana-kondoo bila kipunguo na kumchinga kuwa sadaka inayofunika zambi. Na Maandiko yanasema, *"Bwana akaheshimu Abeli na zabihu yake, lakini hakuheshimu Kaina na zabihu yake."* (Mwanzo 4:5)

Kwa nini Mungu alipokea sadaka ya Abeli, lakini si ile ya Kaina? Kwa sababu haki ya Mungu inahitaji sadaka ya damu kwa zambi. Mungu alihesabia Abeli haki kwa sababu aliamini Neno la Mungu na kuleta sadaka ya nyama kulipa kwa zambi zake. Lakini Kaina alijaribu kukaribia Mungu na kazi zake mwenyewe na kwa sababu hii Mungu hakumkubali.

Leo tunakusudi **kumaliza mafundisho yetu juu ya Kaina na Abeli.** Unajua nini ilitokea wakati Mungu alipokataa kupokea sadaka ya Kaina? Ndani ya kitabu cha Mwanzo, sura 4, shairi 5, Maandiko yanasema: *"Kaina akakasirika sana, uso wake ukakunjamana."* Alikasirika kwa sababu gani? Si nguvu kujibu ulizo hili. Kwa mfano, kama nikifanya neno baya na mtu mwingine anasema nami, "Umetenda mabaya! Geuza mwenendo wako na tenda yaliyo haki!", nitajibu maonyo ya mtu huyu namna gani? Labda nitayapokea na roho ya unyenyekevu na **kugeuza mwenendo wangu**, au nitamkasirikia na **kuendelea kutenda mabaya.**

Mungu alikemea Kaina ili aweze kufahamu ya kwamba kazi za mikono yake, ambazo alitoa kama sadaka, hazikuwa na faida mbele ya Mungu. **Mungu alitaka Kaina kutubu** na kumtolea mwana-kondoo bila kipunguo, kama Abeli alivyofanya. Mungu alitaka kuongoza Kaina katika njia ya haki. Lakini Kaina, mwenye kiburi, alikataa kukubali kosa lake mbele ya Mungu, akakasirika sana na kushindwa moyo.

Hivi *"Bwana akamwambia Kaina: Kwa nini unakasirika? Na kwa nini uso wako unakunjama? Kama ukitenda vema, hutakubaliwa? Na kama hutendi vema, zambi inakaa kwa mlango na inakutamani wewe, lakini sharti uishinde."* (Mwanzo 4:6,7) Mungu aliulizana na Kaina hivi kwa sababu gani? Kwa sababu hakutaka Kaina kupotea. Mungu alitaka Kaina kutubu zambi zake na kufuata njia ya haki. Mungu alikuwa akionya Kaina juu ya adui mbaya sana, ambaye alitaka kumharibu yeye na wazao wake. Adui huyu inaitwa ***Zambi***!

Zambi ni nini? Zambi **inasumbusha dunia nzima**. Ni adui wetu mbaya zaidi. Zambi ni kama nyoka, mwenye kujaa sumu inayoweza kuua watu na nyama. Ni kama **kimeta** kinachoweza kuteketeza mwitu mkubwa. Zambi ni mwenge ambayo Shetani anatumia kuteketeza dunia! Neno la Mungu linasema, *"... kwa yeye anayejua kutenda mema wala hayatendi, kwake huyu ni **zambi**."* (Yakobo 4:17) ***"Zambi** ni uasi ... Yeye anayetenda **zambi** ni wa Shetani; kwa kuwa Shetani **anatenda zambi** tangu mwanzo."* (1 Yoane 3:4,8) Zambi inafanya kazi yake ndani ya viungu vya miili yetu na kushindana na maneno yote yaliyo kweli na mazuri. Zambi ni kitu cho chote kisichopatana na mapenzi ya Mungu. Zambi ni kukataa kuamini na kutii Neno la Mungu. **Zambi ndiyo kufuata njia yangu mwenyewe.** (Isaya 53:6)

Nini itakuwa mwisho wa wale wanaokwenda njia yao wenyewe na wanaokataa kuamini na kutii Mungu? Maandiko yanasema, *"Watakao**azibiwa kwa uharibifu wa milele, kutengwa na uso wa Bwana** na utukufu wa nguvu zake"* (2 Watesalonika 1:9). Wale wanaokaribia Mungu kwa njia ya wokovu ambayo yeye aliamuru watapewa uzima wa milele. Lakini wale wanaoendelea ndani ya zambi na kufanyiza mioyo yao migumu wasikubali kweli ya Mungu watapokea gazabu na hukumu ya Mungu. Lakini, Maandiko yanasema ya kwamba Mungu hataki *"mtu mmoja kupotea, lakini wote wafike kutubu"* (2 Petro 3:9). **Mungu hakutaka Kaina kupotea ndani ya zambi zake.** Alitaka Kaina kutubu, kuacha njia ya uzalimu ambayo alichagua, na kuchagua njia ya haki.

Kama tulivyoona ndani ya somo la mbele, Bwana Mungu alifunua njia namna gani wenye zambi wanaweza kufanyizwa kuwa haki mbele yake. **Abeli aliamini njia ya Mungu**, akaua mwana-kondoo bila kipunguo kama sadaka kufunika zambi. Aliamini maneno ya Mungu wakati aliposema, *"Mshahara wa zambi ni mauti"* na ya kwamba *"pasipo kumwanga damu hakuna ondoleo"* (Waroma 6:23; Waebrania 9:22). Kwa sababu ya zabihu ya mwana-kondoo, Abeli alikuwa na damiri safi mbele ya Mungu. Alijua alikuwa mwenye

zambi aliyestahili kuazibiwa na Mungu, lakini mwana-kondoo asiyekuwa na hatia alikufa kwa pahali pake. Mwana-kodoo ambaye alitolewa kama sadaka na Abeli ni mfano wa Mwokozi atakayekuja duniani na kumwanga damu yake kama zabihu kwa kulipa deni ya zambi ya watu, mara moja kwa wote. Lakini Kaina alijionyesha kuwa mwenye kuamini Mungu, lakini matendo yake hayakuhakikisha neno hili. **Kaina aliheshimu Mungu na kinywa chake, lakini roho yake ilikuwa mbali naye.** Mungu aliagiza wamtolee damu ya mwana-kondoo, lakini Kaina alimtolea kazi za mikono yake. Kuabudu kwa Kaina kulikuwa bule kabisa mbele ya Mungu, kwa sababu hakukubali njia ambayo Mungu aliagiza.

Halafu tuone ndani ya shairi linalofuata nini Kaina alilofanya nyuma ya kuhamakiwa na Mungu kwa sadaka isiyokuwa na faida. Maandiko yanasema, *"Kaina akasemezana na Abeli, ndugu yake. Na ilikuwa wakati walipokuwa shambani, Kaina akasimama juu ya ndugu yake Abeli, akamwua."* (Mwanzo 4:8) Kaina alifanya nini? Alitubu? Aliamini Mungu na kumletea sadaka ya damu ya mwana-kondoo kama sadaka ya zambi? Sivyo! **Kaina aliongeza zambi nyingine tena kwa njia ya kuua ndugu yake Abeli.**

Ajabu muno! Sasa Kaina, aliyekataa kumwanga damu ya mwana-kondoo ili Mungu aweze kusamehe zambi zake, alimwanga damu ya ndugu yake mwenye haki! Unafikiri nini juu ya neno hili? Nani alitia ndani ya nia ya Kaina mafikiri haya ya kwamba ilimpasa kuua ndugu yake? Kaina alisikiliza nani? Alisikiliza Shetani. Maandiko yanasema ya kwamba Kaina aliua ndugu yake kwa sababu *alikuwa wa yule mwovu, ndiye Shetani* (1 Yoane 3:12). Tuliona mbele ya kwamba Mungu alisema kutakuwa na mafungu mawili ya watu duniani, watu wa Mungu na watu wa Shetani. **Abeli alikuwa mtu wa Mungu** kwa sababu aliamini neno la Mungu na kulitii. **Kaina alikuwa mtu wa Shetani** kwa sababu hakuamini Neno la Mungu.

Tusikilize sasa maneno Mungu aliyosema na Kaina wakati alipokwisha kuua mdogo wake.

> *"Bwana akamwambia Kaina:* ***Abeli, ndugu yako ni wapi?*** *Akasema: Sijui; mimi ni mchungaji wa ndugu yangu? Bwana akasema: Umefanya nini? Sauti ya damu ya ndugu yako inalia kwangu kutoka katika inchi. Na sasa umelaaniwa katika inchi, iliyofungua kinywa chake kupokea damu ya ndugu yako kwa mkono wako; wakati utakapolima shamba, halitakupa tena nguvu yake; utakuwa mkimbizi na mwenye kutangatanga duniani"* (Mwanzo 4:9-12).

Hivi Mungu aliazibu Kaina akisema, "*Wakati utakapolima shamba, halitakupa tena nguvu yake*" (Mwanzo 4:12). Watu wa kabila moja la Afrique wanasema, "Ngombe anayepiga mtoto wake na mguu ha-mchukii." Vivyo hivyo Mungu hakuazibu Kaina kwa kumhukumu, lakini kwa kumwongoza kutubu zambi yake na kuokolewa. Basi Kaina alifanya nini? Alitubu? Sivyo. Maandiko yanasema, "*Kaina* ***akatoka usoni mwa Bwana****, akakaa inchini mwa Nodi.*" (Mwanzo 4:16) Kaina aliyeona Neno la Mungu bule, **aligeuzia Mungu mgongo** na hakumpa nafasi katika maisha yake tena. **Si Mungu ambaye alikaa mbali na Kaina, lakini Kaina aliyekwenda mbali na Mungu.**

Kwa wakati wa sasa, zaidi ya wazazi wa Adamu wanafanana na Kaina. Wanapotea katika zambi zao kwa sababu wamefunga mioyo yao kwa sauti ya Mungu. Wanasema, *Mungu ni mkubwa!* lakini ndani ya mioyo yao wanafikiri, *Mungu ni mbali! Hakuna mtu anayeweza kumjua!* Lakini Neno la Mungu linatujulisha ya kwamba **yeye *si* mbali nasi hata kidogo**, kwa sababu ni yeye ambaye anampa kila mtu uzima na pumzi na maneno yote mengine. Yeye ni karibu nasi, kupita mkono wetu wa kuume. Mungu anakujua wewe, na anataka wewe kumjua yeye vilevile! (Matendo 17:24-31; Waroma 10:1-13)

Basi kwa sababu gani zaidi ya watu hawajuani na Mungu wao wenyewe? Neno la Mungu linajibu ulizo hili. Mungu anasema, "*Na hii ndiyo hukumu, ya kuwa nuru imekuja ulimwenguni na* ***watu wamependa giza kupita nuru,*** *kwa sababu matendo yao yalikuwa ma-baya. Sababu kila mtu anayefanya mabaya anachukia nuru, wala hafiki kwa nuru, matendo yake yasikemewe.*" (Yoane 3:19,20)

Watu hawajui Mungu kwa sababu, kama Kaina **wamegeuzia Neno lake mgongo**. Nabii wa Mungu Daudi aliandika, "*Neno lako [la Mungu] ni taa kwa miguu yangu, na nuru kwa njia yangu.*" (Zaburi 119:105). Kama ukigeuzia Neno la Mungu mgongo, utakaa katika giza la zambi tu na hutajuana na Mungu kamwe. Ni kama Mungu ni mbali nawe. Ndiyo, Mungu anataka ujue ya kwamba yeye si mbali. Yeye ni nyuma yako. Yeye ni kando yako. Yeye ni mbele yako. Mungu anakupenda na anataka kuwa na upatano wa karibu nawe. Lakini haifai uwe kama Kaina, aliyetia roho yake ngumu na kukataa njia ya haki ya Mungu. **Mungu alitaka Kaina kutubu**. Hata kwa wakati wa sasa, Mungu anaagiza kila mtu, si neno kama wewe ni nani au pahali gani, kugeuka kwake na kuamini Neno lake.

Unajua maana ya **kutubu**? Ni *kugeuza mafikiri na matendo yako.* Kutubu ni **kukiri zambi zako mbele ya Mungu**, na kusema, "Mafikiri yangu juu ya njia ya wokovu ambayo ulitayarisha

yalikuwa mabaya!" na kumpa Mungu njia kugeuza maisha yako. Kutubu ni **kukubali ya kamba hakuna njia nyingine** kwa wewe kujiokoa toka hukumu ya haki ya Mungu. Toba ya kweli ina sehemu mbili: kuachana na zambi na kugeuka kwa Mungu. Kwanza, inakupasa kugeuka na kuachana na zambi yako, sanamu zako, na matendo yako ya dini kujipatia ukubali wa Mungu. Kisha inakupasa kugeuka kwa Mungu na Neno lake ambalo linakufundisha namna gani unaweza kuokolewa. Hii ndiyo toba ya kweli.

Lakini Kaina hakutubu kamwe. Alichagua kufuata **njia yake mwenyewe**. Alikataa kunyenyekea **njia ya wokovu** ambayo Mungu alitayarisha. Kwa sababu hii Maandiko yanasema, "***Kaina aliangamia katika njia ya uzalimu*** *na kwa sababu hii Mungu alimwekea akiba ya weusi wa giza hata milele!"* (Yuda mash. 11,13).

Ee rafiki, **usiwe kama Kaina**! Weka roho juu ya maonyo ya kuogopesha ya Mungu yanayosema, "*Kama musipotubu, mutaangamia wote, sawasawa nao!*" (Luka 13:3) Hukumu ya Mungu ni ya hakika na itaangukia wote wasiosafishwa kamwe toka zambi zao.

Fahamu neno hili vizuri: hutageuka haki mbele ya Mungu kamwe kwa njia ya matendo mema yako mwenyewe. Kama Kaina, watu wengi wanafikiri wataepuka hukumu ya Mungu kwa njia ya kufuata sheria za dini yao. Lakini Neno la Mungu linasema:

> *"Kwa kazi ya sheria hapana mwenye mwili atakayehesabiwa haki mbele yake (Mungu) ... sisi sote tumekuwa kama kitu kichafu, na* ***haki zetu zote ni kama vitambaa vya kupasukapasuka*** *... kwa maana mumeokolewa kwa neema kwa* ***njia ya imani,*** *wala neno hili* ***halikutoka ndani yenu wenyewe, ni zawadi ya Mungu, si kwa sababu ya matendo,*** *asiwe mtu atakayejisifu!"* (Waroma 3:20; Isaya 64:6; Waefeso 2:8,9)

~~~~~~~~~~~

Ndani ya somo linalofuata tutajifunza juu ya wengine wa wazao wa Adamu, hata nabii wa Mungu Enoka na wengine.

Mungu akubariki na kukusaidia kufikiri sana juu ya maneno uliyosoma leo. Maandiko yanasema,

> ***"Bwana ...ni vumilivu kwetu asiyetaka mtu mmoja kupotea, lakini wote wafike kutubu ... Lakini kama musipotubu, mutaangamia wote!"*** (2 Petro 3:9; Luka 13:3).
~~~~~~~~~~~

SOMO 12

NABII ENOKA

MWANZO 4, 5

Tunakusalimu tena leo kwa njia ya Bwana anayetaka kila mtu kufahamu, kuamini na kupokea njia ya haki ambayo ameamuru, na kukaa na salama naye kwa milele.

Ndani ya somo la mbele tulijifunza juu ya wana wawili wa kwanza wa Adamu na Hawa, Kaina na Abeli. Tuliona ya kwamba wao wawili walitolea Mungu sadaka kwa kumwabudu. Abeli aliamini Mungu na kuleta **damu ya mwana-kondoo**, lakini Kaina alijaribu kukaribia Mungu kwa njia ya **kazi zake mwenyewe**. Mungu alipokea zabihu ya Abeli, lakini alikataa zabihu ya Kaina. Mungu alisema na Kaina kutubu, lakini Kaina alikasirika tu na aliua ndugu yake Abeli.

Leo tunataka kuendelea ndani ya kitabu cha Mwanzo na kujifunza juu ya sura 4 na 5. Neno la Mungu linatuambia ya kwamba Adamu na Hawa walizaa wana na binti wengine, Mwanzo 5:4. Lakini, wa wazao wa Adamu, Mungu ametujulisha habari za j**amaa hizi mbili**: jamaa ya Kaina na jamaa ya Seti, mmoja wa ndugu za Kaina aliyezaliwa nyuma yake.

Tutawaza kwanza juu ya **jamaa ya Kaina**. Kaina alichagua mke katikati ya ndugu zake na walizaa watoto, lakini watoto waliiga namna baba yao alivyowaza na kusema na kutenda. Kama baba yao, **hawakuheshimu Neno la Mungu**. Walikuwa na akili nyingi na walijua maneno mengi, lakini hawakujua Mungu. Waliweka roho juu ya maneno ya dunia tu. Walijenga mji, walifanya vitu vya chuma, vinubi na vilimbi na vitu namna hii. Mmoja wa wazao wa Kaina aliitwa Tubali-Kaina. Vitu alivyofanya vilionekana vizuri sana lakini havikusaidia kupamba moyo wake!

Mmoja wa wazao wa Kaina, jina lake **Lameki** alikuwa kizazi cha saba toka Adamu. Lameki alitembea ndani ya njia ya mzazi wake Kaina lakini alikuwa hata mbaya kupita yeye. Lameki alikuwa mtu wa kwanza aliyeoa wake wawili na, kama Kaina, aligeuka mwuaji.

Maandiko yanasema ya kwamba Lameki aliua watu wawili, kisha alijivuna kusema alikuwa mwovu kupita Kaina! Kama Kaina na wazao wake wote, Lameki hakuweka roho juu ya Mungu wa milele. Alijifikiri mwenyewe na alipenda mali. Alikuwa mwenye kiburi. Alipenda furaha za dunia kupita Mungu. Shetani alikuwa bwana wake, lakini hakutambua neno hili. Lameki alikuwa hivi kwa sababu alichagua kufuata njia ya Kaina. Tuchunge jina la Lameki ndani ya nia zetu kwa sababu tutasema juu yake tena mbele ya kumaliza somo hili.

Asante kwa sababu Maandiko hayakwishi na habari za Kaina na wazao wake wazalimu. Neno la Mungu linatuambia juu ya **jamaa ya Seti** vilevile, na kusema Mungu aliwapa Adamu na Hawa mwana mwingine *"pahali pa Abeli; kwa sababu Kaina alimwua"* (Mwanzo 4:25). Jina lake lilikuwa Seti. Maana ya jina hili ni "chaguliwa". Mungu alichagua Seti kukomboa Abeli. Kwa nini ilipasa Seti kukomboa Abeli? Sikia jibu la ulizo hili. Ndani ya Shamba la Edeni Mungu aliahidi kwamba Mmoja atakuja duniani kushinda Shetani na kufungua wazao wa Adamu toka uwezo wake. Mwokozi huyu angaliweza kufika kwa njia ya jamaa ya Abeli aliyeamini Mungu. Lakini Shetani aliongoza Kaina kuua Abeli. Shetani alitaka kuzuiza shauri la Mungu kutuma Mwokozi duniani. Lakini hekima ya Mungu inashinda ile ya Shetani. Mungu alikuwa na shauri la ajabu kufungua watoto wa Adamu toka zambi zao na hakuna kiumbe aliyeweza kuzuiza shauri hili, hata Shetani hakuweza! Hivi, kupatana na shauri lake, Mungu aliwapa Adamu na Hawa mwana mwingine, ndiye Seti, kukomboa Abeli ambaye Kaina aliua. Hivi, **shauri la Mungu** juu ya Mwokozi lilikaa kuendelea mbele.

Seti alikuwa mwamini wa kweli. Kama Abeli, mkubwa wake, Seti alichagua njia ya wokovu ambayo Mungu alitayarisha. Seti, kama wazao wote wa Adamu, alizaliwa mwenye zambi. Lakini aliamini ahadi za Mungu juu ya Mwokozi atakayekuja na alionyesha imani yake kwa njia ya kuletea Mungu damu ya mwana-kondoo ya Mungu, kama zabihu kufunika zambi zake. Tuone vilevile neno lingine juu ya Seti: alifundisha watoto wake kujua Neno la Mungu wakati alipowalea. Hivi Maandiko yanasema, *"Na Seti, kwake vilevile mwana akazaliwa ... halafu watu walianza kuitia jina la Bwana"* (Mwanzo 4:26).

Hivi tunaona jamaa mbili zilizoanza kwa njia ya Adamu: jamaa ya Kaina na jamaa ya Seti. Unajua kama jamaa hizi mbili ni mifano ya nini? Ni **mifano ya watu namna mbili** walio duniani tangu wakati wa Adamu kufika wakati wa sasa. Kwa macho ya Mungu

kuna watu wa namna mbili tu duniani. Hafikiri juu ya rangi ya ngozi ya mtu au kabila lake, au kama ni tajiri au masikini.

Mungu hana tofauti; hata hivi anatenga watu wa dunia kwa mafungu mawili. Watu gani ni ndani ya mafungu haya? Ndani ya fungu moja ni **wale wanaoamini Neno la Mungu**. Ndani ya fungu la pili ni **wale ambao hawaliamini**. Ndani ya fungu la kwanza ni watu **wanaojua** Mungu, wanaotembea katika nuru na waliosamehewa zambi zao. Watu ndani ya fungu la pili hawamjui lakini wanatembea katika giza na zambi zao hawakusamehewa.

Kila mtu anayeamini Mungu na kuchagua njia ya haki ambayo Mungu alitayarisha ataokolewa (na kwenda mbinguni), kama vile Seti na jamaa yake walivyookolewa. Mtu ye yote asiyeshika njia ya haki ya Mungu atapotea (na kwenda Hadeze), kama vile Kaina na jamaa yake walivyopotea.

Maandiko yanasema ya kwamba Adamu aliishi miaka 930, kisha alikufa. Kwa wakati ule wa zamani watu walikuwa na maisha marefu kabisa. Lakini walikufa namna watu wote walivyokufa. **Adamu na Hawa walikufa,** kama Mungu alivyosema mbele. Wakati Mungu alipoumba watu, hakukusudi kwa watu kufa lakini waishi. Basi kwa nini Adamu na Hawa walikufa? Kwa sababu walikosea Mungu na azabu kwa zambi ni mauti.

Mbele ya kumaliza somo hili, tutaangalia habari za mtu wa Mungu aliyezaliwa ndani ya jamaa ya Seti na aliyeamini Mungu. Mtu huyu ni **Enoka** ... nabii wa Mungu. Ndani ya sura ya tano ya Mwanzo, tunaona wazazi wa Enoka. Maandiko yanasema: **Adamu** alikuwa baba ya Seti; **Seti** akazaa **Enosi**; Enosi akazaa **Kenani**; Kenani akazaa **Mahalali;** Mahalali akazaa **Yaredi**; Yaredi alikuwa baba ya Enoka. Hivi Enoka alikuwa kizazi cha saba nyuma ya Adamu kwa jamaa ya Seti.

Kama watu wote, Enoka alizaliwa **mwenye zambi**. Lakini wakati alipokuwa na miaka 65, Enoka alitubu zambi zake, akageuka kwa Mungu na kuamini ahadi yake juu ya Mwokozi atakayekuja duniani kufa kama zabihu mkamilifu itakayoondosha zambi. Enoka alionyesha imani yake kwa njia ya kutolea Mungu damu ya nyama kama sadaka kufunika zambi zake. Halafu Mungu alihesabia Enoka imani yake kama haki, akasamehe zambi zake, na kusafisha moyo wake. Hivi, Maandiko yanasema, *"Enoka alitembea pamoja na Mungu kwa miaka 300"* (Mwanzo 5:22).

Lakini ilikuwa nguvu kutembea pamoja na Mungu kwa wakati wa Enoka, kwa sababu uovu ulizidi, kama kwa wakati wa sasa vilevile. Zaidi ya watu walioishi kwa wakati wa Enoka waliweka roho juu ya furaha za dunia tu na waliishi maisha ya zambi. Lakini Enoka alifahamu ya kwamba Mungu hakuumba watu kuishi katika uzalimu, lakini katika utakatifu. Hivi Enoka hakuacha tamaa kumtawala kama ilivyotawala majirani yake wasiojua Mungu. Kama Mungu mwenywe, Enoka alipenda haki na alichukia uovu. Watu walimzarau na kumtesa kwa sababu ya mwenendo wake wa haki, lakini Enoka hakuacha neno hili kumchokoza, kwani alijua ya kwamba hakuna neno kubwa kupita kuwa na salama na Mungu.

Mungu alichagua Enoka kuwa mtumishi wake na nabii wake kwa muda ule mwovu. **Kama manabii wote, Enoka alitoa ushuhuda juu ya Mkombozi atakayekuja**. Alitangaza vilevile ya kwamba siku moja Mkombozi atarudi kuazibu wote waliokataa kutubu na kumwamini. Sikia mahubiri ya Enoka:

> "*Angalia,* ***Bwana atakuja*** *na watakatifu wake elfu elfu, ili* ***afanye hukumu*** *juu ya watu wote, na kuazibisha wote wasioogopa Mungu, kwa ajili ya matendo yao yote ya upotevu waliyotenda pasipo kuogopa Mungu, na kwa ajili ya maneno magumu yote wakosayi hawa wasioogopa Mungu waliyosema juu yake*" (Yuda mash. 14,15).

Neno moja lingine tunalohitaji kujua juu ya nabii Enoka ni ya kwamba hakufa. Ndiyo, Neno la Mungu linatuambia ya kwamba **Enoka hakufa!** Linasema, "*Enoka akatembea pamoja na Mungu; kisha hakuonekana kwa sababu Mungu alimtwaa*" (Mwanzo 5:24). Mungu, kwa shauri na uwezo wake alipeleka Enoka mara moja mbinguni bila kumlazimisha kufa kwanza.

Kwa nini Mungu alipeleka Enoka mbinguni hivi? Kwa njia ya maisha ya Enoka, Mungu anataka kutufundisha mawazo yake juu ya watu wale ambao wanamwamini mioyoni mwao na kumpendeza ndani ya maneno yote. Maandiko yanasema:

> "***Kwa imani Enoka alihamishwa asije akaona mauti,*** *wala hakuonekana kwa sababu Mungu alimhamisha; maana mbele ya kuhamishwa kwake* ***alikuwa ameshuhudiwa ya kwamba amependeza Mungu****. Lakini* ***pasipo imani haiwezekani kumpendeza****; kwa maana mtu anayekuja kwa Mungu, sharti aamini ya kuwa yeye yuko, naye anawapa zawabu wale ambao wanamtafuta*" (Waebrania 11:5,6).

Kwa miaka mia tatu Enoka alipendeza Mungu, kwa sababu alikuwa amemwamini, kumpenda na kumtii kwa wakati zaidi ya watu hawakuweka roho juu ya Neno la Mungu. Hivi siku moja Mungu aliita jina la Enoka, na mara moja, gafula, Enoka alikuta yeye ni mbinguni, katikati ya utukufu wa nyumba ya Mungu kwa milele! Ndani ya habari hizi Mungu anataka kutufundisha neno kubwa, ndilo hili: Kama usipokuwa na imani kama Enoka, hutapendeza Mungu! Lakini, ukiwa na imani kama Enoka, Mungu atakuhesabu mwenye haki, na hutahitaji kuogopa mauti tena. Unaweza kujua ya kwamba Mungu ameshinda mauti kwa wewe, kwa sababu kama ukisikiliza Neno la Mungu na kuliamini, wakati maisha yako hapa duniani itakapokwisha, utakwenda kuishi pamoja na Mungu kwa milele, kama Enoka! Lakini sharti uamini maneno Mungu aliyosema juu ya njia ya haki ya wokovu aliyotayarisha kwa wenye zambi.

Kwa kujumlisha mafundisho ya leo, tunataka kusawanisha wazao wawili wa Adamu ambao tulisoma juu yao leo: **Lameki** na **Enoka**.

Wao wawili walikuwa kizazi cha saba toka Adamu. Lameki alizaliwa kwa njia ya **jamaa ya Kaina**, na Enoka kwa **jamaa ya Seti.** Wao wawili waliishi kwa wakati mmoja, lakini mafikiri yao yalikuwa mbalimbali kabisa. Maisha yao yalikuwa mbalimbali kabisa, kama usiku ni mbali na mchana.

Lameki hakuamini Neno la Mungu, lakini **Enoka** aliamini Mungu na kupenda Neno lake.

Lameki alitembea pamoja na Shetani katika uzalimu, lakini **Enoka** alitembea pamoja na Mungu katika utakatifu.

Lameki aliona bule njia ya wokovu ambayo Mungu aliagiza, lakini **Enoka** aliipenda na aliletea Mungu damu ya mwana-kondoo kulipa kwa zambi zake.

Lameki alitamani mali, wanawake, vyakula, mavazi na anasa, lakini **Enoka** alitaka sana maisha ya ushirika wa karibu na Yule ambaye alimpa uzima.

Lameki alikufa katika zambi zake, na alikwenda Hadeze, lakini Mungu alipeleka **Enoka** kuwa pamoja naye mbinguni bila kufa.

Sasa tunataka kuuliza neno kubwa: **Unafanana na Lameki au na Enoka?** Wewe ni mmoja wa watu wa Kaina na Lameki au wewe ni kama watu wa Seti na Enoka? Maisha na mwenendo wako zinaonyesha imani ya Enoka, au unafuata njia yako mwenyewe kama

Lameki? Neno la Mungu linatuagiza, *"**Mujitafute wenyewe** kama ninyi ni katika imani" ... kwa sababu pasipo imani **haiwezekani** kupendeza Mungu!"* (2 Wakorinto 13:5; Waebrania 11:6)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Rafiki, sharti tumalize mafundisho yetu hapa kwa leo. Mara ya nyuma, Mungu akitaka, tutaanza kujifunza juu ya mmoja mwingine wa manabii wa Mungu, ndiye Noa.

Mungu akubariki na uwaze sana juu ya shairi hili toka Neno la Mungu:

> ***"Pasipo imani haiwezekani kupendeza Mungu, kwa maana mtu anayekuja kwa Mungu sharti aamini ya kuwa yeye yuko, naye anawapa zawabu wale ambao wanamtafuta"*** (Waebrania 11:6).
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

SOMO 13

NABII NOA:
SABURI NA GAZABU YA MUNGU

MWANZO 6

Salama iwe kwako kwa jina la Mungu wa salama, anayetaka watu wote kufahamu, kuamini na kupokea njia ya haki ambayo ameta-yarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tuendelee leo na Somo 13 la *Njia ya Haki*.

Ndani ya Maandiko tumeona ya kwamba, katika mwanzo, wakati Mungu alipoumba dunia, maneno yote yalikuwa **mazuri**. Lakini wakati mzazi wetu Adamu alipoasi Mungu **uovu** uliingia duniani kwa njia yake na kuenea kwa watu wote. Ndani ya somo la mbele tulijifunza juu ya jamaa mbili zilizotoka kwa Adamu, wazao wa Kaina na wazao wa Seti. Wazao wa Kaina **hawakuamini Mungu**. Katikati ya wazao wa Seti kulikuwa na wengine **walioamini Neno la Mungu**, na kwa sababu hii Mungu alisamehe zambi zao. Enoka alikuwa mtu wa jamaa ya Seti. Hata kama zaidi ya watu walioishi kwa wakati wa Seti waliishi katika zambi, Enoka alitembea pamoja na Mungu katika utakatifu.

Leo tutajifunza juu ya mtu mwingine aliyetembea pamoja na Mungu kwa muda mwingine wakati uovu ulipozidi. Mtu huyu ndiye **Noa, nabii wa Mungu** [*Noh* kwa lugha ya Waarabu]. Alikuwa kizazi cha tatu toka Enoka. Tumejifunza ya kwamba kwa wakati wa zamani, maisha ya watu yalikuwa marefu kupita leo. Unajua nani aliishi miaka mingi kupita wote? Alikuwa Metusela, mwana wa Enoka. Aliishi miaka 969. Metusela alikuwa baba ya Lameki aliyekuwa baba ya Noa. Lameki huyu, baba ya Noa hakuwa mzao wa Kaina ambaye tulisoma habari zake mbele. Noa alikuwa kizazi cha kumi toka Adamu. Wakati Noa alipokuwa na miaka 500, alizaa Semu, Hamu na Yafeti. Wao wote walikuwa walimaji.

Maneno tutakayojifunza juu ya Noa yatakuwa na faida nyingi kwa sisi, kwa sababu wakati wa Noa ulifanana na wakati wa sasa. Kwa wakati wa Noa, dunia ilijaa kabisa na zambi. Maandiko yanase-

ma ya kwamba "*mawazo yote ya mafikiri ya mioyo yao yalikuwa mabaya tu siku zote*" (Mwanzo 6:5). Mioyo ya wazao wa Adamu ilijazwa na mafikiri mabaya, choyo, wivu, udanganyifu, uchafu, tamaa, maovu, hila, jeuri, macho mabaya, matukano, kiburi, na upumbavu (kama tunavyoona katika Marko 7:21,22). Watu walikuwa wakiharibu dunia Mungu aliyoumba ili waweze kukaa ndani yake. Wengi wao walikuwa na dini, lakini ilikuwa kwa kuonekana tu. Mungu wao ulikuwa tamaa ya mwili na hesabu ya zambi zao ilikaa kuongezeka!

Sikia maneno ya Mungu ndani ya kitabu cha Mwanzo, sura 6 na mashairi 3, 5-7:

> "*Bwana alisema, Roho yangu haitashindana na mtu milele, kwa sababu yeye vilevile ni mwili; hata hivi siku zake zitakuwa miaka mia moja na makumi mbili.*" . . . "*Bwana Mungu akaona ya kama uovu wa watu ulikuwa mkubwa duniani, na ya kama mawazo yote ya mafikiri ya mioyo yao yalikuwa mabaya tu siku zote. Na Bwana alijuta ya kwamba amefanya watu duniani, ikamhuzunisha moyoni mwake. Bwana akasema: Nitaharibu mtu ambaye nilimwumba toka uso wa inchi; mtu na nyama vilevile, na kitu kinachotambaa na ndege ya anga; kwani ninajuta ya kwamba nimewafanya.*"

Hivi tunaona namna Mungu alivyokusudi kufuta wazao wa Adamu toka dunia kwa sababu ya uovu wao. Lakini tutaona ya kwamba Mungu, mwenye rehema alikusudi kuwa na saburi kwa miaka 120 wapate **saa kutubu** ili wasiharibiwe. Lakini nyuma ya muda ule Mungu atahukumu kila mtu aliyekataa kutubu na kupokea Neno lake.

Muda huu wa miaka 120 unatufundisha neno kubwa juu ya Mungu, ndilo hili: **Mungu ni mwenye saburi kubwa, lakini saburi hii ina mpaka vilevile**! Atasema na kushindana na mtu kwa siku nyingi kusudi mtu aweze kutubu, lakini hatashindana naye kwa milele. Kwa sababu hii, kwa wakati wa Noa, Mungu alisema, "*Roho yangu haitashindana na mtu milele ... hata hivi siku zake zitakuwa miaka mia moja na makumi mbili*" (Mwanzo 6:3). Hivi tunaona namna Mungu alivyokusudi kuwa na saburi na wenye zambi kwa wakati, mbele ya kuwahukumu kama wakikataa kutubu. Neno hili linatuonyesha maneno mawili juu ya Mungu: **wema wake** na **hasira yake**. Mungu ni mwema na anaweza kuwa na saburi nyingi; lakini yeye ni mwenye haki vilevile na anaweza kukasirika sana!

Watu wengine wanafikiri Mungu ni mkali na mwenye fimbo kubwa, kama mwenye kufurahi kupiga na kuumiza watu. Lakini

Mungu si hivi. Kuna **watu wengine** wanaofikiri kwamba Mungu hatakasirika kamwe na atakaa kusamehe na kusahau tu zambi za watu. Wanasema "Mungu ni mwema." Lakini sivyo. Mungu ni namna nyingine na mawazo ya watu hawa vilevile.

Maandiko Matakatifu yanatupasha kweli juu ya namna ya Mungu. Mungu ni mwema na mwenye haki! Anaweza kuwa na saburi **na** anaweza kukasirika vilevile. Kwa sababu ya wema na rehema yake ana saburi na wenye zambi, lakini kwa sababu ya haki na utakatifu wake anawakasirikia kwa sababu ya zambi zao. Mungu ni Mwokozi na Mwamuzi. Manabii waliandika maneno mengi juu ya **saburi na gazabu ya Mungu**. Tusikilize mengine ya masemo yake. Maandiko yanasema,

> *"Lakini musisahau neno hili moja, kwamba kwa Bwana siku moja ni kama miaka elfu moja, na miaka elfu moja ni kama siku moja. Bwana hakawii kutimiza ahadi yake, kama wengine wanavyozania kukawia; lakini ni **vumilivu** kwetu **asiyetaka mtu mmoja kupotea**, lakini wote wafike kutubu. **Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwizi**"* (2 Petro 3:8-10). *"**Bwana atahukumu watu wake**. Ni neno la kuogopa kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai ... Angalieni musikatae yeye anayesema ... kwa sababu Mungu wetu ni moto wa kuteketeza!"* (Waebrania 10:30,31; 12:25,29).

Ndani ya kitabu cha Zaburi tunasoma ya kwamba Mungu ni **mwamuzi wa haki**, Mungu **mwenye gazabu** (kwa wenye zambi) kila siku, Zaburi 7:11,12. Ndani ya Agano Jipya imeandikwa:

> *"**Kasirani ya Mungu** imefunuliwa kutoka mbingu juu ya uasi wote na uovu wa watu wanaofunga **kweli** kwa uovu ... hukumu ya Mungu ni ya **kweli** juu yao wanaofanya mambo kama haya. Na wewe mtu unazania ... utakimbia hukumu ya Mungu? Au unazarau **utajiri wa wema wake na saburi na uvumilivu wake,** usijue ya kama wema wa Mungu unakupeleka kwa toba? Lakini kwa ugumu wako, na kwa moyo wako usio na toba, unajiwekea akiba hasira kwa **siku ya hasira** na ufunuo wa **hukumu ya haki ya Mungu**, atakayelipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake"* (Waroma 1:18; 2:2-6).

Kasirani ya Mungu si kama kasirani ya watu. Mtu anaweza kukasirika sana, lakini kasirani yake itapunguka kidogo kidogo pole-pole hata mwishoni atasahau ni neno gani ambalo lilimkasirisha. Kasirani ya Mungu ni namna nyingine! Kupita kwa siku na miezi hakupunguzi kasirani yake. Mungu ni Mwamuzi wa haki naye hasa-

hau hata neno moja! **Kasirani yake kwa wale wanaokataa kutubu haipunguki;** sivyo, lakini **inaongezeka**! Hili ndilo neno tulilosoma sasa tu ndani ya Maandiko: *"Kwa ugumu wako, na kwa moyo wako usio na toba,* ***unajiwekea akiba hasira*** *kwa siku ya hasira na ufunuo wa hukumu ya haki ya Mungu."*

Watu wa wakati wa Noa "walijiwekea akiba" hasira ya Mungu! Hata hivi kulikuwa na mtu mmoja kwa wakati ule aliyependa Mungu na roho yake yote, na aliyeamini Neno la Mungu. Mtu yule alikuwa Noa. Hivi Maandiko yanasema: ***"Lakini Noa akapata neema machoni mwa Bwana ...*** *Noa alikuwa mtu wa haki, mkamilifu katika vizazi vyake; Noa akatembea pamoja na Mungu"* (Mwanzo 6:8,9).

Kwa sababu gani Mungu alionyeshea Noa neema yake? Noa alistahili neema ya Mungu? Sivyo! Haiwezekani kustahili neema au neema hii si neema tena! Kwa nini basi Mungu alitendea Noa kwa neema, lakini hakufanya hivi kwa watu wengine? Maandiko yanasema nini juu ya neno hili? Yanatuambia ya kwamba **Noa aliamini Mungu,** lakini watu wengine hawakumwamini. **Noa aliamini Neno la Mungu.** Aliamini ahadi ya Mungu juu ya Mkombozi atakayekuja duniani kuokoa wenye zambi. Noa alikuwa na zambi, lakini Mungu alihesabu Noa kama mwenye haki kwa sababu aliamini Mungu wa kutosha kumtolea damu ya sadaka kwa zambi zake, kama Mungu alivyoagiza. Hivi, Maandiko yanasema, *"Noa alikuwa mtu wa haki, mkamilifu katika vizazi vyake."*

Siku moja Mungu alisema na Noa (Mwanzo 6:13-21),

> *"Nitaharibu watu wote, kwa sababu dunia inajaa na jeuri kwa sababu yao. Nitawaharibu pamoja na dunia. Hivi* ***ujifanyie safina*** *ya mti goferi na kufanya vyumba ndani yake na kuipakaa na lami inje na ndani. Utaifanya hivi: Urefu wa safina utakuwa mètres 150, upana wake 25 mètres na urefu wake juu mètres 15. Fanya dari juu yake ... Weka mlango kwa mbavu yake na fanya dari tatu, ya chini, ya pili na ya tatu. Nitaleta garika ya maji juu ya inchi, kuharibu miili yote iliyo na pumzi ya uzima ndani yao; kila kitu duniani kitakufa. Lakini nitasimamisha agano langu pamoja nawe; na utaingia safina, wewe na wana wako na mke wako na wake wa wana wako. Na ya kila kitu kilicho hai cha miili yote utaleta wawili wa kila namna ndani ya safina kuwachunga hai pamoja nawe; watakuwa mume na mke ... Utajitwalia chakula cho chote kinachokuliwa na kitakwa chakula kwako na kwao."*

Hivi Mungu alijulisha Noa namna alivyokusudi kuleta maji ya garika juu ya dunia kuharibu watu wote waliokataa kutubu na

kuamini kweli. Mungu aliagiza Noa kujenga **safina** (merikebu) asiharibiwe na garika. Ilipasa urefu wa merikebu kuwa mètres 150. Itakuwa kimbilio kwa Noa na jamaa yake na nyama wengi na mtu ye yote aliyetaka kujiponyesha toka garika. Mungu aliagiza Noa kufanya **vyumba vingi** ndani ya safina, lakini **mlango mmoja tu**, kwa upande wa inje wa safina. **Kila mtu aliyetaka kuepuka hukumu ya garika sharti aingie kwa mlango ule mmoja**. Kila mtu aliyeingia kwa mlango ule **ataponyeshwa**. Wale wasioingia kwa mlango **wataharibiwa!**

Hivi Noa alianza kujenga safina. Ilikuwa kazi kubwa sana. Ilipasa Noa na wana wake watatu kukata mia za miti na kuipasua kuwa mbao na kuzipakaa inje na ndani na lami na kuzifunga pamoja na misumari. Bila shaka mke wa Noa na wake wa wana wake walisaidia ndani ya kazi ile ngumu vilevile. Kwa miaka mia moja, kila siku, Noa na jamaa yake walitumika kutayarisha safina. Lakini Noa hakujenga tu. Alihubiri vilevile kwa watu wa wakati ule. Labda alisema nao maneno kama haya: "Sikilizeni! Bwana ameniagiza kuwaonya ninyi juu ya gazabu yake. Gazabu yake ni kubwa sana kwa sababu ya zambi zenu! Amekusudi kuleta garika ya maji juu ya dunia kuharibu kila mtu asiyetubu. Lakini ninawajulisha ninyi habari hizi njema: Mungu, kwa sababu ya rehema yake, ameniagiza kujenga safina kuwa kimbilio kwa mtu ye yote anayetubu zambi zake na kuamini Neno la Mungu!" Hivi Noa alionya watu na maneno mengi, akawasukuma kuachana na zambi zao na njia zao mbovu.

Basi unafikiri watu wa wakati wa Noa waliamini habari ambazo Mungu aliwatangazia kwa njia ya nabii lake? Tutaona jibu la ulizo hili ndani ya Somo 14 wakati tutakapoendelea na habari za nabii Noa na kuona namna Mungu alivyochunga kila mtu aliyeamini neno lake na kuhukumu wale wasioamini neno hili kwa njia ya kuwaacha kuzama ndani ya maji ya garika kubwa.

~~~~~~~~~~~

Mungu akubariki wakati unapokaa kuwaza juu ya maneno tuliyosoma ndani ya Maandiko leo:

> ***"Bwana hakawii kutimiza ahadi yake, kama wengine wanavyozania kukawia: lakini ni vumilivu kwetu asiyetaka mtu mmoja kupotea, lakini wote wafike wokovu. Lakini siku ya [hukumu] ya Bwana itakuja kama mwizi."*** (2 Petro 3:9,10)
~~~~~~~~~~~

SOMO 14

NOA NA GARIKA KUBWA

MWANZO 7

Karibu, rafiki msomaji. Asante kwani wewe ni tayari kuendelea na mfulizo *Njia ya Haki*.

Ndani ya somo 13 tulianza kujifunza juu ya habari za nabii Noa aliyekuwa kizazi cha ine nyuma ya Adamu. Kwa wakati uovu ulipozidi duniani Noa alitembea pamoja na Mungu. Tuliona ya kwamba **Bwana alihuzunishwa** sana kwa sababu ya zambi ya wazao wa Adamu. Maandiko yanasema ya kwamba *"uovu wa watu ulikuwa mkubwa duniani, na ya kama mawazo yote ya mafikiri ya mioyo yao yalikuwa mabaya tu siku zote"* (Mwanzo 6:5). Kwa sababu hii Mungu, na gazabu kubwa alifanya shauri kuondosha wenye zambi wote toka dunia.

Lakini, **neema ya Mungu** ilikuwa pamoja na Noa, kwa sababu Noa alipenda Mungu na **aliamini Neno lake**. Hivi siku moja Mungu alisema na Noa: Ninakusudi kuleta garika kubwa juu ya dunia, kuharibu kila kiumbe kinachoishi chini ya mbingu. Lakini ninataka wewe kujenga safina kubwa (chombo) kusudi wewe na jamaa yako waweze kuingia ndani yake musiharibiwe na garika.

Noa alitumika kwa miaka mia moja kufanya safina ile kubwa. Lakini hakutumia saa yake yote kwa kujenga safina tu. Alihubiri vilevile kwa watu kando kando yake, akisema, "Mutubu zambi zenu na kugeuka kwa Mungu! Mungu, Mwenye Haki, atahukumu dunia!"

Watu wa wakati wa Noa walitubu zambi zao na kuamini habari ambazo Mungu aliwatangazia kwa njia ya nabii wake? Unafikiri nini? Katikati ya elfu elfu za wana wa Adamu waliokuwa duniani, wangapi walitubu na kuamini Mungu ya kutosha hata kuingia safina? Maandiko yanasema: ***"Wachache, watu wanane tu wali-okolewa"*** (1 Petro 3:20).

Watu wangapi waliamini Mungu? Wanane tu: Noa na mke wake, wana wao watatu na wake wao. Wote wengine hawakuamini Neno la Mungu. Waliona bule mahubiri ya Noa, na kumzarau kwa sababu alijenga chombo. Walimcheka wakifikiri ana wazimu kwa sababu chombo alichotengeneza kilikuwa kwa pahali pasipokuwa na maji. Labda walimzihaki hivi: "Muje kwanza kuona mtu anayejenga chombo kikubwa kwa pahali pa jangwa! Bila shaka Noa ana wazimu! Garika hapa kwa jangwa? Wapi! Haitawezekana kamwe! Na vilevile, Mungu ni mwema; hataharibu watu ambao aliwaumba! Una wazimu, Noa!" Lakini Noa aliona kuzarau kwao bule kwa sababu aliamini maneno Mungu aliyosema. Aliendelea na kazi ya kutengeneza safina na kuhubiri, akisema, "Mutubu! Mungu atakuja kuhukumu dunia kwa haki! Kwa nini munakataa kuamini Neno la Mungu? Kwa nini munataka kupotea?"

Halafu siku ilifika wakati Noa na jamaa yake walipomaliza kazi ya kutengeneza safina. Ndani ya shairi la mwisho la sura ya sita ya Mwanzo tunasoma: "*Noa akafanya ... sawasawa na maneno yote ambayo Mungu alimwagiza, akafanya hivi.*" (Mwanzo 6:22) Merikebu ilikuwa tayari. Kila kitu kilitimia. Neno moja tu lilibaki: Noa na jamaa yake walihitaji kuingia safina. Tunafikiri Noa alijaribu mara moja tena kuita watu: "Musikilize Mungu! Mutubu na kuamini neno lake! Kutakuwa na garika nyuma kidogo! Mwingie safina wakati saa ingali. Sasa mlango ni kwanza wazi! Mtu ye yote atakayeingia ataokolewa. Lakini kama mukikataa kuingia, mutaepuka hukumu ya Mungu namna gani?" Aliwaonya sana **lakini walikataa kusikia**.

Hivi ndani ya sura 7:1-5, Maandiko yanasema:

> *"Bwana akamwambia Noa: Ingia safina, wewe na nyumba yako yote; kwa sababu wewe nimekuona mwenye haki mbele yangu katika kizazi hiki. Ya nyama zote walio safi utajitwalia saba saba, mume na mke wake; na ya nyama wasio safi wawili wawili, mume na mke wake; na ndege vilevile za hewa, saba saba, mume na mke; kuchunga hai uzao juu ya uso wa inchi yote. Kwa maana bado siku saba, na nitaleta mvua juu ya dunia siku makumi ine, mchana na usiku; na kila kitu kilicho hai ambacho nilikifanya, nitakiharibu toka uso wa inchi. Na Noa akafanya sawasawa na maneno yote ambayo Bwana alimwagiza."*

Kwa nini Noa na jamaa yake waliingia safina? Kwa sababu waliona mawingu mbinguni? Kwa sababu waliweza kunusa mvua iliyokaribia? Sivyo! Hawakuona mbinguni alama ya mvua ikikaribia wakati walipoingia safina. Basi waliingia kwa sababu gani? Kuna

jibu moja tu kwa ulizo hili. Waliingia kwa sababu **waliamini neno Mungu alilosema.** Labda kulikuwa na watu wengine inje ya safina waliofikiri: Mimi ninaamini Mungu vilevile, lakini sitaingia ndani ya safina ile! Ninaamini Mungu, lakini siwezi kukubali mahubiri ya Noa! Tunaweza kusema nini juu ya watu hawa? Tunaweza kusema ya kwamba **hawaamini Mungu kweli kweli**, kwa sababu hawakuamini ushuhuda wa Mungu kwa njia ya nabii wake. Walikataa kutubu zambi zao, na walikataa njia ya kupona ambayo Mungu aliwapatia kwa njia ya Noa. Waliheshimu Mungu na midomo yao, lakini mioyo yao ilikuwa mbali naye.

Hivi, Maandiko yanasema,

> *"Noa akaingia safina, na wana wake, na mke wake, na wake wa wana wake pamoja naye, kwa sababu ya maji ya garika. Ya nyama walio safi na ya nyama wasio safi na ya ndege na ya kila kitu kinachotambaa juu ya inchi, wakaingia safina kwa Noa wawili wawili, mume na mke, sawasawa Mungu alivyoagiza Noa ...* ***Bwana akamfunga ndani.****"* (Mwanzo 7:7-9,16)

Ulisikia neno Mungu alilofanya wakati Noa na jamaa yake walipokwisha kuingia safina? Maandiko yanasema, ***"BWANA akamfunga ndani!"*** Siku ya gazabu kubwa ya Mungu ilikuwa imefika. Mungu alikuwa amekaa na saburi na watu wa kizazi kile kwa muda mrefu, lakini sasa **saburi yake ilikwisha! Gazabu tu ilibaki**. Mungu alikuwa amefunga mlango; na wakati Mungu anapofunga mlango, hakuna mtu anayeweza kuufungua.

Hivi Mungu alileta maji ya garika juu ya dunia, kama alivyosema mbele. Mbingu ziligeuka meusi na mawingu makubwa na lalo na ngurumo, na upepo ulianza kuvuma. Kulikuwa na matetemeko ya inchi. Sasa wana wa Adamu **walitetemeka kwa woga**. Wakati maneno yote yalipokuwa kimya na salama hawakuogopa kuzarau Mungu na masemo na matendo yao. Lakini sasa wakati hukumu ya Mungu ilipoanza kuwapata hawakuwa na kitu cha kusema. Vinywa vyao vilifungwa! Saa yao kukutana na hukumu ya haki ya Mungu ilikuwa imefika na hawakuwa na nafasi kufichama!

Hivi mvua nyingi ilianguka, vijito ndani ya udongo vilitoa maji mengi na bahari na mito ilifurika na kulikuwa na garika kubwa. Watu wote walikimbia na kupanda vilima. Wale waliozarau Noa mbele na kukataa Neno la Mungu walijua sasa maneno Mungu aliyosema kwa njia ya nabii wake yalikuwa **kweli**. Lakini kufahamu

neno hili sasa **hakukuweza kuwasaidia** kwa sababu hawakuwa na njia tena kutubu. Labda watu walikuwa wakilalamika, "Noa! Noa! Utufungulie mlango na kutuponyesha. Tunaamini sasa! Tunaamini! Tunaamini!" Lakini Mungu alikuwa amefunga mlango na **siku ya wokovu imepita.** Maombi, kutoa machozi, kupiga mlango, hata kujua kweli ya Mungu hakuna neno lililoweza kugeuza mafikiri ya Mungu. **Wakati Mungu anapofunga mlango wa wokovu, hakuna mtu anayeweza kuufungua.**

Maandiko Matakatifu yanatuambia ya kwamba mvua ilikaa kunyesha na nguvu na maji ya garika yalikaa kuongezeka kufika wakati hata milima ilipofunikwa. Lakini safina ilibebwa juu ya maji.

> *"Miili yote iliyotambaa juu ya inchi ikakufa, ndege, na ngombe, na nyama, na kila kitu kilichotambaa juu ya inchi, na kila mtu ...* ***Noa tu akabaki, nao waliokuwa pamoja naye ndani ya safina."*** (Mwanzo 7:21,23)

Mungu alifanya maneno aliyoahidi? Kabisa! Alihukumu wenye zambi wale waliokataa kutubu? Ndiyo! Alihukumu kila mtu asiyekuwa ndani ya safina, kama alivyosema atafanya.

Mungu akitaka, tutamaliza habari za Noa ndani ya Somo 15 na kuona nini ilipata Noa na jamaa yake ndani ya safina. Lakini mbele ya kumaliza Somo 14, kuna neno kubwa ambalo Mungu anataka kutufundisha kwa njia ya garika ile kubwa. Sikiliza vizuri: **Mungu amefanya shauri kuhukumu dunia siku nyingine.** Siku ile ya hukumu kwa wakati wa kuja itakuwa ya kuogopesha hata kupita hukumu hii iliyopata kizazi cha Noa!

Sikia maneno ambayo mmoja wa manabii wa Mungu alitangaza juu ya siku ile ya hukumu ya mwisho. Aliandika:

> *"Nikaona* ***kiti cha ufalme, kikubwa, cheupe****, naye anayeketi juu yake, dunia na mbingu zikakimbia uso wake; na pahali pao hapakuonekana. Nikaona wafu, wakubwa na wadogo, wamesimama mbele ya Mungu, na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, kilicho cha uzima; na wafu wakahukumiwa katika mambo haya yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao. Na ikiwa mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika* ***ziwa la moto****."* (Ufunuo 20:11-12,15)

Rafiki unayesikiliza, una tumaini rohoni wakati unapowaza juu ya siku ile ya kuogofya ya hukumu? Jina lako linaandikwa ndani ya

kitabu cha uzima wa milele? Umepita kwa mlango wa wokovu ambao Mungu alifungua? Neno la Mungu linasema: ***"Tazama sasa ni wakati wa kukubaliwa; tazama sasa ni siku ya wokovu."*** (2 Wakorinto 6:2) Tuliona namna Mungu alivyoita watu wa wakati wa Noa na saburi nyingi waweze kutubu, kuamini na kuokolewa, lakini mwishoni alifunga mlango wa wokovu. Mtu ye yote aliyekataa kuingia kwa mlango alihukumiwa na Mungu.

Juu ya **siku ile wakati Mungu atakapohukumu dunia**, Maandiko yanasema: "*Siku ya Bwana inakuja kama mwizi katika usiku. Sababu wakati wanaposema, Kuna utulivu na salama, wakati ule uharibifu unakuja juu yao kwa gafula, kama uchungu wa kuzaa unavyokuja juu ya mwanamke mwenye mimba; wala hawatakimbia."* (1 Watesalonika 5:2,3) Hakuna mtu atakayeepuka siku ile, ila wale waliopita kwa mlango ambao Mungu alifungua kwa watu kupata wokovu.

Unajua habari za **Mlango** ambao Mungu amefungua kwa watoto wote wa Adamu? Nani aliepuka hukumu ya garika kwa wakati wa Noa? Wale tu walioingia mlango wa safina! Vivyo hivyo kwa maneno ya hukumu itakayokuja, Maandiko yanatuonyeshea wazi ya kwamba Mungu ametayarisha **mlango mmoja tu wa wokovu** kwa wana wa Adamu. Unajua habari za mlango ule wa wokovu? Basi sikiliza vizuri maneno yaliyosemwa na Mpatanishi Mtakatifu ambaye Mungu alituma duniani. Alisema, "***Mimi ni mlango****; kama mtu ataingia kwa mimi, ataokolewa!"* (Yoane 10:9) *"Kweli, kweli ninawaambia ninyi, Yeye anayesikia neno langu na kumwamini yeye ambaye alinituma ana uzima wa milele;* ***hafiki kwa hukumu****."* (Yoane 5:24)

~~~~~~~~~~~~~~

Ndani ya masomo ya nyuma tutajifunza maneno mengi mengine juu ya Mwokozi huyu ambaye Mungu alituma duniani, Yule aliyesema, ***"Mimi ni mlango; kama mtu ataingia kwa mimi ataokolewa!"*** Na ndani ya Somo 15 tutamaliza habari za nabii Noa.

Mungu akubariki na kukupa ufahamu wakati unapowaza juu ya ulizo hili kubwa ndani ya Neno lake:

> ***"Tutapona namna gani tusipochunga wokovu mkubwa namna hii?"*** (Waebrania 2:3)
~~~~~~~~~~~~~~

SOMO 15

NOA NA UAMINIFU WA MUNGU

MWANZO 8,9

Salama kwako, Rafiki. Leo tunakusudi **kumaliza habari za nabii wa Mungu, ndiye Noa.** Lakini kwanza tujikumbushe maneno tuliyojifunza ndani ya masomo 13 na 14 juu ya Noa na garika kubwa. Ndani ya sura 6 ya kitabu cha Mwanzo, tuliona ya kwamba uovu wa watu ulikuwa mkubwa sana kwa wakati wa Noa; mawazo yote ya mioyo yao yalikuwa maovu. Kwa sababu hii Mungu alifanya shauri kuleta garika juu ya inchi kuharibu kila mwenye zambi aliyekataa kuacha zambi zake na kugeuka kwa Mungu wa kweli aliye hai.

Kwa kizazi kile kibaya kulikuwa na mtu mmoja tu aliyependeza Mungu. Mtu yule alikuwa Noa. Noa alitegemea Mungu na kumpenda. Kwa sababu hii, siku moja, Mungu alisema na Noa, akamwagiza kujenga safina kubwa (ndicho chombo), kitakachokuwa kimbilio kwa yeye, jamaa yake na nyama wengi waweze kupona wakati wa garika. Kwa miaka mia moja, Noa, pamoja na jamaa yake walijenga safina na kuonya watu kutubu na kuamini Neno la Mungu. Lakini **hakuna mtu aliyeweka roho juu ya mahubiri ya Noa.** Hakuna mtu aliyeamini maneno ambayo Noa aliwaambia juu ya garika itakayokuja!

Hata hivi, siku moja kazi ya kujenga safina ilikwisha. Saa kwa Mungu kuhukumu dunia hii mbovu ilikuwa imefika. Mungu alikuwa na saburi na watu hawa ambao walimzarau kwa muda mrefu, lakini sasa saburi yake ilikwisha. Hivi Mungu aliagiza Noa kuingia safina pamoja na jamaa yake na kupeleka pamoja naye waume na wake saba wa kila namna ya nyama waliokuwa safi, na wawili wawili, mume na mke, wa namna zote za nyama wasiokuwa safi. Noa na jamaa yake na nyama waliingia safina kama Mungu alivyoagiza. Na Maandiko yanasema, "*Bwana akamfunga ndani.*" Mungu, aliyekuwa amefungua mlango wa wokovu kwa wana wa Adamu ndiye ambaye aliufunga vilevile. **Siku ya rehema ya Mungu ilipita; siku ya gazabu yake ya kuogopesha ilikuwa imefika!**

Kisha kulikuwa na ngurumo, lalo na matetemeko ya inchi. Mvua nyingi ilianguka na kuleta garika kubwa. Watu wote walikimbia,

wakijaribu kupanda milima, lakina hakuna mtu aliyeweza kuepuka gazabu takatifu ya Mungu! Watu wale waliozarau Noa na kukataa Neno la Mungu mbele, walijua kweli sasa. Lakini **saa ya wokovu ilikuwa imepita!** Mungu alikuwa amefunga mlango.

Kwa siku makumi ine mvua ilizidi kunywesha na visima vya maji vilitoa maji kufika siku hata vilima vilivyofunikwa. Lakini safina ilibebwa juu ya maji. Maandiko yanasema,

> "*Miili yote iliyotambaa juu ya inchi ikakufa, mtu na ngombe na kitu cha kutambaa, na ndege za anga; wakaharibiwa toka dunia.* ***Noa tu akabaki, nao waliokuwa pamoja naye ndani ya safina."*** (Mwanzo 7:21,23).

Hivi Maandiko Matakatifu yanatujulisha ya kwamba Mungu alitimiza azabu namna alivyoahidi. Wote waliokuwa **inje** ya safina waliharibiwa. **Mungu ni mwaminifu na anatimiza Neno lake kila mara.**

Basi nini ilipata wale waliokuwa **ndani** ya safina? Mungu alisahau Noa na jamaa yake? Mungu, anayekulisha ndege za anga na haachi hata mmoja yao kuanguka chini yasipokuwa mapenzi yake, hakuwasahau. Tusome maneno yanayoandikwa ndani ya kitabu cha Mwanzo, sura 8. Maandiko yanasema,

> "***Mungu akakumbuka Noa****, na kila kitu kilichokuwa hai, na nyama zote waliokuwa pamoja naye ndani ya safina. Mungu akapitisha upepo juu ya dunia na maji yalipunguzwa. Na mwezi wa saba siku ya kumi na saba ya mwezi, safina ililala juu ya milima ya Ararati."* (Mwanzo 8:1,4)

Hivi tunaona ya kwamba Mungu alikumbuka Noa na wale waliokuwa pamoja naye ndani ya safina. Alituma upepo kuvuma juu ya inchi kusudi ukaushe maji na maji yaanze kupunguka. Mungu aliongoza safina hata ililala juu ya milima ya *Ararati.* Wakati Noa na jamaa yake walipokwisha kushinda ndani ya safina kwa mwaka mmoja na juma moja, mengi ya maji yaliyofunika dunia yalikuwa yamekauka. Hivi Mungu alisema na Noa, "*Toka katika safina, wewe na wana wako na wake wao pamoja nao."* Hivi Noa na jamaa yake walitoka safina, na nyama wote walitoka vilevile. Wakati alipokwisha kutoka, alijenga mazabahu, akachukua nyingine za nyama na ndege safi na kuzitoa kwa Bwana kuwa sadaka ya kuteketezwa.

Ulisikia nini Noa alifanya kwanza nyuma ya kuondokea safina? **Alitoa sadaka za nyama zisizokuwa na kosa** na kuziteketeza juu ya mazabahu ambayo alijenga. Mungu hakuondosha sheria yake

iliyosema, "*Bila kumwanga damu hakuna ondoleo*" (Waebrania 9:22). Ndiyo, garika **iliharibu zaidi ya wenye zambi toka dunia,** lakini **haikuharibu shina ya zambi** iliyobaki ndani ya mioyo ya wazao wa Adamu. Kwa sababu hii ilipasa Noa na wazao wake kukaa kutolea Mungu sadaka kwa zambi. Kama tulivyoona mbele, sadaka za nyama namna hii ni msingi wa njia ya wokovu ambayo Mungu aliamuru. Sadaka wazazi wetu walizochinja zamani ni mfano wa Mwokozi atakayekuja na kumwanga damu yake mwenyewe kulipa deni kwa zambi za wazao wa Adamu. Kwa sababu hii, wakati Noa alipoondokea safina, kitu cha kwanza alichofanya kilikuwa kumwanga damu, na kwa njia hii alionyesha kwa watoto wake na watoto wao ya kwamba sheria za Mungu hazikugeuka, ya kwamba "*mshahara wa zambi ni mauti*" (Waroma 6:23), na ya kwamba "*Bila kumwanga damu hakuna ondoleo*" (Waebrania 9:22).

Hivi, Maandiko yanasema,

> "*Bwana akasikia harufu tamu (ya sadaka); ... Mungu akabariki Noa na wana wake, akawaambia: Muzidi na kuongezeka na kujaza inchi ... Nitasimamisha **agano langu** nanyi, na pamoja na uzao wenu nyuma yenu ... Miili yote haitakatiwa mbali tena na maji ya garika; wala garika haitakuwa tena kuharibu dunia ... Mungu akasema: Hii ni alama ya **agano** ninalofanya katikati yangu nanyi na kila kitu kilicho hai pamoja nanyi, hata vizazi vya milele: Ninaweka **upinde wangu** winguni na utakuwa alama ya **agano** katikati yangu na dunia. Na itakuwa wakati ninapoleta wingu juu ya dunia, upinde utaonekana ndani ya wingu. Na nitakumbuka **agano langu**, lililo katikati yangu na kila kitu kilicho hai cha miili yote; na maji hayatakuwa garika tena kuharibu miili yote.*" (Mwanzo 8:21; 9:1,9,11-15)

Ndani ya mashairi haya tuliyosoma, kuna neno moja Mungu alilosema kwa Noa mara ine. Ulilisikia? Neno lenyewe ni ***"agano"***. Ndani ya Neno la Mungu agano ni ahadi ambayo Mungu anayofanya na mtu. **Mungu ndiye mwenye kulinda maagano**. Yeye ni mwaminifu, na anataka kuonyesha uaminifu wake kwa wana wa Adamu! Kwa sababu hii, kwa sababu ya wema wake, alisimamisha agano na Noa, na wazao wake, akisema, "*maji hayatakuwa garika tena kuharibu miili yote.*" Hii ndiyo ahadi ya Mungu. Na ahadi yake si masemo bule tu, lakini aliihakikisha kwa njia ya upinde wa mvua wake katika mawingu.

Ulijua ya kwamba **upinde ule wa mvua** wa kuonekana vizuri sana ambao tunaona mara nyingine ndani ya mawingu wakati mvua

iliponyesha sasa tu ni alama inayotangaza **uaminifu wa Mungu**? Kila mara tunapoona upinde wa mvua katika mawingu, Mungu anataka kutukumbusha ya kwamba uaminifu wake unaendelea toka kizazi hata kizazi. Mungu aliweka upinde wa mvua ndani ya mawingu kuhakikisha agano lake la kuahidi kwamba maji hayatageuka tena kamwe garika kuharibu uzima wote. Kweli, Mungu ni Mlinzi wa agano! **Yeye ni mwaminifu!**

Tungeweza kusema juu ya maneno mengine ndani ya baki la maisha ya Noa, lakini nafasi hapana. Unaweza kuyasoma ndani ya sura 9 ya kitabu cha Mwanzo. Utaona ya kwamba nyuma ya garika Noa aliishi kwa miaka 350 mingine, na alikufa wakati alipokuwa mzee sana, akakwenda juu kwa Bwana.

Tunaweza kumaliza mafundisho yetu juu ya Noa na maulizo mawili. Kulikuwa na tofauti gani katikati ya Noa na watu wa wakati wake? Noa alifanya nini kupendeza Mungu? Alifanya neno moja tu. **Aliamini Neno la Mungu.** Kwa sababu hii Noa hakufa pamoja na watu wa kizazi chake. Sikia ushuhuda wa Mungu mwenyewe juu ya Noa:

> "***Kwa imani*** *Noa akikwisha kuonywa na Mungu habari za* ***maneno yasiyoonekana bado****, kwa kuogopa Mungu alitengeneza safina, apate kuokoa nyumba yake. Hivyo alihukumu dunia, akakuwa mriti wa haki inayopatikana kwa* ***imani****." Lakini "pasipo imani haiwezekani kumpendeza (Mungu)"* (Waebrania 11:7,6)

Mbele ya kumaliza somo hili, kuna **mawazo mawili** ambayo inatupasa kuchunga ndani ya nia zetu. Tulifikiri juu ya wazo la kwanza sasa tu. Kwa sababu gani Mungu alipendezwa na Noa? Kwa sababu ya **imani yake. Noa aliamini Mungu, aliamini maneno ambayo Mungu alisema**. Alitumaini Mungu na alitii neno lake hata wakati watu walipomkataa. Ni kwa sababu ya imani yake Mungu alimponyesha toka kizazi kiovu kile, maana watu waovu ambao alikaa katikati yao. Msomaji, **unaamini kweli kweli maneno Mungu aliyosema?** Ni mapenzi ya Mungu kwa sisi sote kuamini Neno lake kama Noa alivyofanya.

Habari za Noa zinatukumbusha neno kubwa lingine, ndilo neno lililo hata **kubwa kupita imani ya Noa**. Unajua kama ni nini? Ni **uaminifu wa Mungu.** Kwa nini uaminifu wa Mungu ni neno kubwa kupita imani ya Noa? Kwa sababu kama Mungu asipokuwa mwaminifu kwa maagano yake na ahadi zake, imani ya Noa isingaliweza kuwa na faida kwake. Fikiri juu ya neno hili: Ukiwa na rafiki anayeahidi, "Nitakuletea mfuko wa mchele kesho," unaamini ahadi

yake. Basi unasikia nini rohoni mwako kama asipotimiza ahadi yake? Utakuwa na huzuni (na labda njaa vilevile)! Faida ya imani yako ndani ya rafiki yako ilikuwa bule. Kwa nini? Kwa sababu rafiki yako hakufanya neno aliloahidi kufanya. Ulikuwa umeamini mtu asiyekuwa mwaminifu.

Mungu si hivi. Maandiko yanasema,

> *"Kama sisi hatuamini, **yeye anakaa mwaminifu**; maana hawezi kujikana mwenyewe" (*2 Timoteo 2:13*). "Miili yote ni kama majani, na utukufu wao wote kama ua la majani. Majani yanakauka, na ua lake linaanguka; lakini **Neno la Bwana linadumu kwa milele** ... naye ambaye anamwamini hataona haya" (*1 Petro 1:24,25; 2:6*).* Ndiyo, ***"Mungu ni mwaminifu!"*** (1 Wakorinto 1:9)

Atafanya maneno ambayo anaahidi kufanya!

Ndani ya habari za Noa tunaona wazi namna **Mungu alivyofanya kila kitu alichoahidi.** Tunasoma namna Mungu aliokoa kila mtu aliyekuwa ndani ya safina na kuhukumu kila mtu aliyekuwa inje, namna alivyosema atafanya. Tuliona vilevile namna Mungu alivyosamehe zambi za Noa kwa sababu alitoa damu ya nyama kama sadaka, namna Mungu alivyoagiza. Na tulijifunza namna Mungu alivyoweka upinde wa mvua ndani ya mawingu ili Noa na watu wote wasisahau kamwe ya kwamba ***"Mungu ni mwaminifu!"***

Kama ukisahau maneno yote tuliyofundisha leo ila moja, kumbuka neno hili: **Mungu ni mwaminifu**! Hawezi kuvunja ahadi zake. Anafanya kila neno analoahidi kufanya, hata kama mara nyingine anakawa kwanza. *"Mungu ni mwaminifu ... naye ambaye anamwamini hataona haya"* (1 Wakorinto 1:9; 1 Petro 2:6). Tumwamini basi na kupokea Neno lake na unyenyekevu. Vizuri habari za nabii Noa na garika kubwa ziwe na faida kwetu na kutusukuma kuiga Noa aliyeamini Neno la Mungu wakati watu wote kando kando walipokataa kuamini na waliharibiwa.

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Ndani ya somo la nyuma, Mungu akitaka, tutaona nini ilipata wazao wa Noa na tutajifunza kwa sababu gani tuna lugha mbalimbali nyingi duniani.

Mungu akubariki na kukusaidia kuchunga ndani ya nia na mawazo yako kweli hii inayoweza kugeuza maisha yako kabisa.

> ***"Mungu ni mwaminifu ... naye ambaye anamwamini hataona haya!"*** (1 Wakorinto 1:9; 1 Petro 2:6)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

SOMO 16

BABELI

MWANZO 10, 11

Salama iwe kwako, rafiki msomaji, kwa jina la Mungu wa salama, anayetaka watu wote kufahamu, kuamini na kupokea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele.

Ndani ya Somo 15 tulimaliza mafundisho yetu juu ya nabii wa Mungu, ndiye Noa. Tuliona shauri la Mungu kuangamiza wana wote wa Adamu na garika kwa sababu ya uovu wao. **Aliwapa wenye zambi miaka mia moja waweze kutubu** wakati Noa alipokuwa akijenga safina itakayokuwa kimbilio kwa wale walioamini Neno la Mungu. Lakini hakuna mtu aliyetubu au kuamini habari toka Bwana Mungu, ila Noa na jamaa yake. Basi kwa mwisho Mungu, **aliye mwenye haki na mwaminifu, alifanya neno ambalo alisema atafanya.** Aliharibu watu wote wasioingia mlango wa safina, na aliponyesha wale walioingia.

Leo tutaendelea kusoma ndani ya kitabu cha Mwanzo na kuona nini ilitokea **katika muda nyuma ya Noa**. Tuliona mbele ya kwamba Noa alikuwa na wana watatu, **Semu, Hamu na Yafeti.** Maandiko Matakatifu yanaonyesha ya kwamba **watu hawa watatu ni wazazi wa mataifa yote ya dunia.** Semu alikuwa baba ya Wayuda na Waarabe. Tunafikiri zaidi ya watu wa Afrique na Chine ni wazao wa Hamu. Wenyeji wa inchi za Europe ni wazao wa Yafeti.

Kama ukitaka kujifunza zaidi juu ya mwanzo wa mataifa, soma sura 10 na 11 za Mwanzo. Lakini ndani ya mafundisho yetu ya leo tuna nafasi kueleza neno moja tu juu ya historia ya wana watatu wa Noa, ndio Semu, Hamu na Yafeti. Ni neno hili: Mungu alichagua **Semu kuwa mmoja wa wazazi wa Mkombozi atakayekuja duniani.** Kwa sababu hii Maandiko Matakatifu yanasema zaidi juu ya wazao wa Semu. Manabii wa Mungu na Mwokozi wa dunia walitoka kwa Semu.

Hivi watu wote wa dunia walitoka kwa wana watatu wa Noa. Wewe na mimi, watu wote wa Afrika nzima, na mataifa yote pahali pote—watu wote wanaoishi duniani leo ni wazao wa Noa. Hivi

tunaweza kusema ya kwamba sisi ni hapa leo kwa sababu Noa aliamini Mungu na alifanya safina kuponyesha jamaa yake; kwani wakati alipoponyesha jamaa yake toka garika, alituponyesha wewe na mimi pamoja nao.

Mungu alibariki Noa na wana wake, akasema nao: "*Muzidi na kuongezeka na kujaza dunia*" (Mwanzo 9:1). Hivi, mia za miaka nyuma ya garika, watu wengi walikuwa wakikaa duniani tena. Na mara moja tena, **dunia ilianza kuchafuwa kwa njia ya zambi.** Tuliona mbele ya kwamba Noa na wana wake walizaliwa wenye zambi kwa sababu walikuwa wazao wa Adamu. Wakati walipoingia safina, **tabia yao ya zambi** waliyopokea toka Adamu, iliingia pamoja nao. Na wakati walipotoka safina walitoka pamoja na **mshina wa zambi** ungali ndani ya mioyo yao. Garika haikugeuza tabia ya zambi ya watu. Watu wote waliozaliwa tangu wakati ule walizaliwa wenye zambi, kwa sababu wao wote ni wazao wa Noa aliye mzao wa Adamu.

Ni huzuni lakini ni kweli ya kwamba mia za miaka nyuma ya garika kubwa, zaidi ya wazao wa Noa hawakukumbuka Mungu tena wala mapenzi yake. **Hawakuamini Neno la Mungu** kama wazazi wao Semu, Enoka na Noa. Walisahau Mungu na hawakumshukuru kwa sababu aliwapa uzima, pumzi na jua na mvua na vyakula. Na kwa maneno ya upinde wa mvua ambao Mungu aliweka katika mawingu kuwakumbusha uaminifu wake, zaidi yao hawakujua maana yake. Sikia maneno Mungu anayosema juu yao:

> "*Kwa kuwa, wakati walipojua Mungu, hawakumtukuza kama Mungu, wala kumshukuru; lakini walikuwa bule katika mawazo yao, na mioyo yao iliyokuwa pasipo ufahamu ilitiwa giza. Wakisema ya kuwa walikuwa wenye akili, walikuwa wapumbavu. Walibadilisha kweli ya Mungu kwa uwongo, wakaabudu na kutumikia kiumbe kupita Mwumba, anayebarikiwa kwa milele. Amina.*" (Waroma 1:21, 22,25)

Kama Kaina na wazao wake, zaidi ya wazao wa Noa walichagua kuacha kweli, na kufuata uzalimu. Walikuwa na dini, lakini ilikuwa dini ya uwongo kwa sababu haikupatana na njia ya haki ambayo Mungu alisimamisha. Hawakusikiliza neno la kweli la Mungu. Walikuwa wakisikiliza Shetani.

Kulikuwa na mtu mmoja, jina lake **Nimurodi**, aliyekuwa mzao wa Hamu, mwana wa pili wa Noa. Nimurodi alikuwa mwindaji nyama wa kujulikana aliyeishi karibu miaka mia tano nyuma ya

garika. Maana ya jina lake ni *mhuni*. Nimurodi alikuwa na akili nyingi, lakini hakujua Mungu. Aliona Neno la Mungu bule na alifuata njia ya Shetani na njia ya Kaina na njia ya watu wa kizazi cha Noa. Nimurodi alijenga miji mikubwa mingine, na alifanya shauri kujenga **mji mkubwa** pahali watu wote wa dunia watakapoweza kuishi pamoja na kuwa na umoja.

Tusome sasa ndani ya sura 11 ya kitabu cha Mwanzo kuona maneno Maandiko yanayosema juu ya mji mkubwa ambao Nimurodi na watu wengine pamoja naye walikusudi kujenga. Maandiko yanasema:

> *"**Na dunia nzima ilikuwa na lugha moja na usemi mmoja**. Na ilikuwa wakati watu waliposafiri kwa mashariki, wakakuta inchi sawa katika inchi ya Sinari; wakakaa pale. Wakasemezana: Tufanye matofali na kuyachoma vizuri kwa moto. Wakakuwa na matofali kwa mawe, na lami kwa chokaa. Wakasema: Tujijengee wenyewe mji na **mnara, kichwa chake kifike mbinguni na tujifanyie jina; hata tusisambazwe juu ya uso wa dunia."*** (Mwanzo 11:1-4)

Hivi, tunaona namna wana wa Adamu walivyofanya shauri kujenga mji mkubwa na **mnara mrefu** utakaogusa hata mbingu. Walitaka kujenga mnara ule mrefu kwa sababu gani? Nimurodi na wale waliokuwa pamoja naye walijitafutia ukubwa duniani. Walikusudi kukusanya watu wa dunia pamoja ndani ya pahali pamoja, ili waweze kuwa wenye uwezo na wasisambazwe duniani pote. Lakini neno walilokusudi kufanya halikupendeza Mungu. Mungu alikuwa ameagiza wana wa Noa kusambaa katika dunia nzima. Mungu, aliyeumba mtu, alijua nini ni vizuri zaidi kwa watu wa dunia. Lakini, zaidi ya wazao wa Noa hawakuweka roho juu ya mawazo ya Mungu. Walifikiri walikuwa na akili kupita Mungu. Kama Shetani mwenyewe, **mioyo yao ilijaa kiburi na uasi juu ya Mungu.** Lakini Maandiko yanasema, *"Naye anayejitukuza mwenyewe, atanyenyekezwa; naye anayejinyenyekeza mwenyewe, atatukuzwa."* (Matayo 23:12) Na *"maneno ambayo watu wanazania kuwa bora ni chukizo mbele ya Mungu."* (Luka 16:15)

Ni zambi mbele ya Mungu kutukuza mtu au kujitafutia jina kubwa, kwa sababu kuna jina moja tu linalostahili kupokea sifa na utukufu. Ni jina la **Bwana Mungu** aliyefanya mbingu na dunia! Kama Maandiko yanavyosema: *"**Yeye anayejisifu, ajisifu katika Bwana.** Kwani mtu anayekubaliwa si yeye anayejisifu mwenyewe, lakini yeye anayesifiwa na Bwana."* (2 Wakorinto 10:17,18)

Lakini, kwa wakati wa Nimurodi zaidi ya watoto wa Adamu hawakuheshimu Bwana. Walifikiri hawakuhitaji Mungu na Neno lake; hawakuhitaji mtu ye yote kuwafundisha neno. Walikuwa wenye **tabia ya kujitawala mwenyewe na ya uasi**. Hata kwa wakati wa sasa wana wa Adamu wana tabia namna hii. Tunaona neno hili hata ndani ya watoto wadogo wakati wanaposema, Ninakataa! Na roho ya namna hii ya uasi inapatikana zaidi sana ndani wa wenye kukomea. Kwa sababu gani kuna vita ndani ya jamaa na mataifa ya dunia? Ni kwa sababu ya roho hii ya kujitawala mwenyewe inayosukuma watu kufikiri: "Ninaweza kujichunga mwenyewe". Desturi zangu ni vizuri zaidi. Dini yangu inatosha kwa mimi. Watu wa kabila langu ni wenye akili zaidi. Jina langu ni jina la heshima sana. Vitu vyangu! Mapenzi yangu! Kazi zangu! Mali yangu! Yangu! Yangu! Yangu! Kweli watu wanajikumbuka wenyewe tu. Kila mtu anaweka roho zaidi juu ya maneno yake mwenyewe. Kwa sababu ya roho ya namna hii dunia inajaa na magomvi na vita. Lakini **Mungu anachukia roho ya namna hii,** kwani jina lake tu linastahili kupata utukufu. Kwa sababu hii anasema ndani ya Neno lake: *"Mimi ni Bwana, ndilo jina langu: na utukufu wangu sitampa mwingine!"* (Isaya 42:8)

Lakini wale waliokuwa wameanza kujenga mnara kufika mbinguni hawakuweka roho juu ya utukufu wa Mungu. Walikuwa wakitafuta utukufu wao wenyewe. Hawakuweka roho juu ya jina la Mwumba wao. Ndiyo, watu wengi wa wakati ule walishikamana na dini sana, lakini **waliona Neno la Mungu bule.** Walifikiri waliweza kufuata njia yao wenyewe kufika mbinguni. Ni ajabu kabisa! Miaka 500 tu nyuma ya garika, watu walifuata njia yao wenyewe tena bila kuweka roho juu ya Bwana ambaye aliwapa uzima na pumzi. Walikuwa kama nguruwe anayerudia kugaagaa ndani ya matope nyuma ya kuoshwa kwa maji! (Ona 2 Petro 2:22) Ni upumbavu na uovu mkubwa kwa mtu kutaka kuishi mbali na Mungu na Neno lake!

Basi Mungu alifanya nini? Aliona bule shauri la watu kuishi maisha yao bila Mwumba wao? Alipokea wale ambao walimwasi? Sivyo. Sikiliza neno Mungu alilofanya. Maandiko yanasema ndani ya Mwanzo 11:5-9:

> *"Bwana akashuka kuona mji na mnara, ambao wana wa watu walijenga. Bwana akasema: Tazama, wao ni taifa moja, nao wote wana lugha moja; na maneno haya wanaanza kufanya; basi sasa hakuna kitu ambacho kitawazuiza wanachokusudi kufanya. Tushuke tuwachanganyie usemi wao, wasisikilizane lugha. Hivi Bwana*

akawasambaza toka kule juu ya uso wa dunia nzima; wakaacha kujenga mji. Kwa hivi jina lake liliitwa Babeli kwa sababu ***Bwana akachanganya usemi wa dunia nzima pale; na toka pale Bwana akawasambaza juu ya uso wa dunia nzima."***

Hivi tunaona namna Mungu alivyoharibu mashauri ya Nimurodi na wengine waliokuwa wameanza kujenga mji mkubwa kwa utukufu wao wenyewe. Kufika wakati ule, watu wote duniani walisema lugha moja. Lakini siku ile, **Mungu alichanganya lugha** yao hata hawakuweza kufahamana tena. Unakumbuka ya kwamba Mungu aliagiza wazao wa Noa *"kujaza dunia"*, maana kuenea pahali pote duniani. Lakini Nimurodi na wafuata wake walitaka kufanya neno lingine na kukusanya watu wote wa dunia kwa pahali pamoja. Mungu aliharibu mashauri yao kwa njia ya kuwapa lugha mpya mbalimbali. Kwa njia hii **Mungu aliwasambaza duniani pote.** Ni kwa sababu hii kuna mia za mataifa na elfu za lugha duniani kwa wakati wa sasa.

Kweli Mungu alichanganya lugha za watu wa dunia kabisa kabisa. Waza juu ya lugha nyingi sana ndani ya inchi ya Congo tu. Kweli Mungu wetu ni mkubwa sana. Hakuna mtu anayeweza kukataa mapenzi ya Mungu na kushitawi. Watu walijaribu kushindana na Mungu na walishindwa. Unajua jina la mji huu ambao watu walijaribu kujenga wakati walipoona kutaka kwa Mungu bule? Ndiyo, jina lake ni **Babeli.** Maana ya Babeli ni machafuko. Mtu akijaribu kuishi mbali na Mungu na Neno lake, maisha yake ni machafuko tu!

Hizi ndizo habari za mji wa Babeli na watu waliojaribu kutukuza jina lao wenyewe. Sisi tunafanana na watu wa Babeli mara nyingine? Mungu anatuambia kwamba ni zambi kufanya hivi. **Unajaribu kutukuza jina la nani?** Jina lako mwenyewe? Au jina la mtu, labda mtu mkubwa wa dini? Au unatukuza jina la **Bwana Mungu peke yake?** Unatafuta kusifiwa na nani? Na watu? Au na Mungu? Kuna neno moja tunalojua kabisa: sifa ya watu haitadumu, lakini ukipata sifa toka Mungu, sifa ile itadumu milele. Neno la Mungu linasema: "*Miili yote ni kama majani, na utukufu wao wote kama jua la majani. Majani* ***yanakauka****, na ua lake* ***linaanguka****, lakini Neno la Bwana linadumu kwa* ***milele****."* (1 Petro 1:24)

Sikia neno hili toka Bwana mwenyewe:

"Mwenye akili asijisifu kwa sababu ya akili yake, wala mwenye nguvu asijisifu kwa sababu ya nguvu zake; lakini mwenye kujisifu

> ***ajisifu kwa maneno haya,*** *ya kwamba ananifahamu mimi, na kujua mimi ni Bwana, ninayetenda wema, na hukumu, na haki katika inchi; maana mimi ninapendezwa na mambo haya, anasema Bwana."* (Yeremia 9:23,24)

~~~~~~~~~~~~~~~~

Mungu akitaka, ndani ya somo la nyuma tutafanya ukumbusho wa maneno yote tunayokwisha kujifunza toka mwanzo kufika sasa.

Mungu akubariki wakati unapokaa kuwaza juu ya shairi la Biblia linalosema:

> ***"Mtu anayekubaliwa si yeye anayejisifu mwenyewe, lakini yeye anayesifiwa na Bwana."*** (2 Wakorinto 10:18).
~~~~~~~~~~~~~~~~

SOMO 17

UKUMBUSHO WA "MWANZO"

MWANZO 1-11

Leo tunakusudi kufanya **ukumbusho na kujumlisha** maneno tunayokwisha kujifunza kufika sasa ndani ya Tora au Sheria ya nabii Musa. Tora ni sehemu ya kwanza ya Maandiko ya Manabii. Sehemu hii ya kwanza ni **msingi** ambao Mungu yeye mwenyewe aliweka, na kwa njia yake tunaweza kupima maneno yote tunayosikia kujua kama yakitoka kwa Mungu. Tora hii ina sehemu au vitabu vitano. Tunaita sehemu ya kwanza "Mwanzo". Kitabu cha Mwanzo kina sura 50. Tunakwisha kujifunza kufika sura 11.

Unakumbuka neno lililoandikwa ndani ya shairi la kwanza la Neno la Mungu. Tulisome tena: *"Katika mwanzo Mungu aliumba mbingu na dunia."* Mungu ni Bwana wa milele. Katika mwanzo, wakati dunia isipokuwa bado, Mungu tu alikuwa. Mungu ni Roho ya Milele asiye na mwanzo. Kwa sababu hii shairi la kwanza la Maandiko linasema: *"Katika mwanzo, **Mungu**!"*

Halafu tuliona ya kwamba mbele ya kuumba ulimwengu, Mungu aliumba elfu nyingi za roho watakatifu na wenye uwezo, akawaita **malaika**. Katikati ya malaika hawa kulikuwa mmoja aliyekuwa mwenye hekima na mapambo kupita wote wengine. Malaika huyu aliitwa **Lusifero** na Mungu alimchagua kuwa mkubwa wa malaika. Lakini Maandiko yanaonyesha ya kwamba siku moja Lusifero alijitukuza mwenyewe na kuzarau Mungu moyoni mwake, akitaka kujikamatia pahali pa Mungu. Malaika wengi wengine walichagua kufuata Lusifero ndani ya zambi hii. Kwa sababu hii Mungu, asiyeweza kukubali zambi, alifukuza Shetani na malaika zake, aligeuza jina la Lusifero kuwa **Shetani**, maana yake *Adui*. Nyuma ya kufukuza Shetani na malaika, akaumba kwa ajili yao **moto wa milele** usiozimishwa kamwe. Maandiko yanasema ya kwamba siku ya hukumu ya mwisho, Mungu, Mwenye Haki, atatupa Shetani ndani ya moto huu pamoja na wote ambao wanamfuata.

Kisha tunasoma namna Bwana alivyoumba **mbingu na dunia** na vitu vyote ndani yao katika muda wa siku sita, bila kutumia kitu

kuviumba, akisema neno tu! Mungu aliumba kila kitu kwa mtu (ambaye alikusudi kumwumba kwa furaha na utukufu wake). **Mtu** ni kiumbe cha maana zaidi ambacho Mungu aliumba, kwa sababu mtu aliumbwa kwa sura ya Mungu. Mungu alitaka kuwa na upatano wa karibu na wa faida na mtu. Kwa sababu hii Mungu alitia ndani ya **nafsi** ya mtu **roho** ya akili (nia) ili aweze kujua Mungu, Mungu alimpa **moyo** kusudi aweze kupenda Mungu, na Mungu alimpa **kutaka kwake mwenyewe** ili aweze kuchagua kutii au kuasi Mungu.

Ndani ya sura 2 ya Mwanzo tunasoma ya kwamba Mungu alipanda **shamba la Paradiso** (Edeni) duniani, na kuweka ndani yake mtu ambaye alikuwa amemwumba, maana yake **Adamu**. Mungu, kwa sababu ya mema yake, alimpa Adamu vyote alivyohitaji ili aweze kukaa na salama na usitawi.

Na siku Mungu alipoumba Adamu alisema naye, *"Wa kila mti wa shamba unaweza kula; lakini wa mti wa kujua uzuri na ubaya usile kwa maana siku unapokula, hakika utakufa."* (Mwanzo 2:16,17) Hivi, tuliona ya kwamba Mungu aliweka **jaribu moja** mbele ya Adamu. Mungu alitaka kuwa na upatano wenye maana na mtu ambaye alimwumba. Kwa sababu hii Mungu alimjaribu, akimpa njia kuchagua kumpenda na kumtii au kutomtii.

Tunasoma vilevile ya kwamba siku Mungu alipoumba Adamu, alimpa zawadi nzuri sana, ndiye mke! Mungu aliumba mwanamke toka mfupa wa mbavu alioondosha toka mwili wa Adamu, akamleta kwa Adamu. Adamu aliita jina lake ***Hawa***. Hivi, kwa muda wa siku sita, Mungu alitimiza kazi yake. Maandiko yanasema: *"Mungu aliona kila kitu alichofanya, na tazama kilikuwa kizuri sana."* (Mwanzo 1:31) Siku ya saba Mungu alistarehe na kufurahia kazi yake yote.

Ndani ya sura 3 tuliona namna **zambi** ilivyoingia dunia yetu. Maandiko yanaonyesha ya kwamba siku moja wakati Adamu na Hawa walipokuwa karibu na mti ambao Mungu aliwakataza kula matunda yake, Shetani aliwakaribia kwa mfano wa **nyoka yenye hila** sana, akisema:

> *"Mungu alisema, Musile ya miti yote ya shamba? Mwanamke alisema na nyoka, Matunda ya miti ya shamba tunaweza kula, lakini alisema vilevile, Musile matunda ya mti ulio katikati ya shamba wala musiyaguse, musife. Nyoka alisema na mwanamke, Hakika hamutakufa, kwani Mungu anajua ya kwamba siku mutakapokula matunda yake, macho yenu yatafunguliwa, na mutakuwa kama Mungu mukijua uzuri na ubaya."* (Mwanzo 3:1-5)

Hivi tuliona ya kwamba S**hetani alikana Neno la Mungu!** Mungu alikuwa amewaambia Adamu na Hawa nini itawapata kama wakikula ya mti ambao alikataza. Ilikuwa nini? Alisema: *"Mutakufa!"* Na Shetani alisema nini? Alisema: *"**Ha**mutakufa!"* Adamu na Hawa walichagua kuamini na kufanya Neno la Mungu? au neno la Shetani? Ni huzuni kusoma ndani ya Maandiko ya kwamba Adamu na Hawa walichagua kuamini masemo ya Shetani na kula matunda ya mti ambayo Mungu alikataza! Shetani alidanganya Hawa naye alikosa. **Adamu alichagua na kutaka kwake kuasi agizo la Mungu na kufuata Shetani**. Hivi, Maandiko Matakatifu yanasema: *"Kwa mtu mmoja zambi iliingia ulimwengu, na kufa kwa njia ya zambi; na hivi kufa kulikuja juu ya watu wote."* (Waroma 5:12)

Kwa sababu ya maneno haya, **Mungu alifukuza Adamu na Hawa** toka Shamba la Paradiso, kama alivyosema mbele. Lakini mbele ya kuwafukuza, **Mungu aliahidi kutuma Mwokozi** duniani kukomboa wana wa Adamu toka uwezo wa Shetani, zambi na mauti! Kwa kuhakikisha ahadi hii, Mungu alichinja nyama na kufanya mavazi toka ngozi zao, akavika Adamu na Hawa nayo. Kwa njia ya **sadaka hizi za nyama** Mungu alifundisha Adamu na Hawa ya kwamba *"mishahara ya zambi ni mauti"* (Waroma 6:23), na ya kwamba *"pasipo kumwanga damu hakuna ondoleo."* (Waebrania 9:22)

Ndani ya sura 4 tulisoma habari za wana wawili wa kwanza wa Adamu, **Kaina na Abeli**. Tuliona ya kwamba **Abeli alitolea Mungu mwana-kondoo asiyekuwa na kosa**, akamchinja kuwa sadaka kwa zambi, namna Mungu alivyofanya kwa wazazi wa Abeli. Lakini **Kaina alijaribu kukaribia Mungu kwa njia yeye mwenyewe aliyochagua**, akileta ya mboga aliyootesha ndani ya udongo ambao Mungu alilaani. Hivi Maandiko yanasema: *"Bwana akaheshimu Abeli na zabihu yake, lakini hakuheshimu Kaina na zabihu yake."* (Mwanzo 4:4,5) Mungu aliita Kaina kueleza sababu ya neno alilokwisha kufanya kusudi aweze kutubu na kukubali njia ya haki ya Mungu, lakini Kaina alikasirika tu, akaua Abeli, mdogo wake.

Kisha, Mungu aliwapa Adamu na Hawa mtoto mwingine, jina lake **Seti**. Seti, kama Abeli, aliamini Mungu na alimkaribia na damu ya sadaka. Hivi tuliona jamaa mbili zilizotoka Adamu, jamaa ya Kaina na jamaa ya Seti. Wazao wa Kaina hawakuamini Mungu. Lakini wengine wa wazao wa Seti waliamini Mungu. Mzazi mmoja wa Seti, jina lake **Enoka**, alitembea pamoja na Mungu katikati ya watu waovu sana. Mwana wa mjukuu mmoja wa Enoka aliitwa **Noa**. Kwa siku za Noa Mungu alifanya shauri kuharibu watoto wote wa

Adamu na garika kwa sababu ya uovu wao. Kwa wakati ule mbaya, **Noa tu aliamini Mungu,** na kwa sababu hii Mungu alimwagiza kujenga safina kubwa sana, ndiyo chombo, itakayokuwa **kimbilio** kwa yeye na watu wa jamaa yake na nyama wingi, na watu wo wote wengine watakaoachana na zambi zao na kuamini Neno la Mungu. Kwa miaka mia moja Mungu alivumilia uovu wa wenye zambi na saburi wakati Noa alipojenga safina. Lakini hakuna mtu aliyetubu zambi zake na kuamini habari za Mungu, ila Noa na jamaa yake. Hivi mwishoni, Mungu alifanya maneno yote ambayo alisema atafanya. Alihukumu watu wote wasioamini kweli. Wote ila Noa na jamaa yake walikufa ndani ya **garika kubwa.**

Noa alikuwa na wana watatu: **Semu, Hamu na Yafeti**. Mataifa yote ya dunia yanatoka kwa wanaume hawa watatu. Lakini tuliona ya kwamba zaidi ya wazao wao walisahau Mungu na Neno lake mbio. Ndani ya somo la mbele, tuliona namna Nimurodi na wale waliofungana naye walifanya shauri kuleta watu wote wa dunia kwa pahali pamoja na kujenga mji mkubwa wenye mnara kwenda juu sana, shauri lisilopatana hata kidogo na mapenzi ya Mungu. Lakini Mungu alichanganya lugha yao, na kuwasambaza katika dunia nzima. Mji huu ulijulikana na jina la **Babeli**, maana yake *chafuko.* Haya ndiyo kwa ufupi maneno tunayokwisha kujifunza kufika sasa ndani ya Mwanzo, sura 1-11.

Basi tunaweza kujumlisha namna gani maneno tuliyoona ndani ya habari hizi zote? Mungu anataka kutufundisha nini kwa njia ya maneno haya yaliyotokea kwa wakati wa mwanzo? Kuna maneno mengi ambayo anataka kutufundisha, lakini leo tuna saa kueleza maneno mawili tu. Neno kubwa moja ndilo ya kwamba **mtu ni mzalimu.** Kweli ya pili ni ya kwamba Mungu ni **mwenye haki**!

Ndani ya mafundisho yetu tumeona tena na tena **uzalimu wa mtu**. Tuliona mwanzo wake ndani ya Shamba la Paradiso, wakati Adamu alipokula matunda ya mti ambao Mungu alikataza. Tuliuona tena ndani ya Kaina, mwana mzaliwa wa kwanza wa Adamu, aliyekataa kufuata njia ya sadaka ambayo Mungu alitayarisha. Tuliona uzalimu huu ndani ya wazao wa Kaina, ndani ya watu wa wakati wa Noa, na ndani ya wale waliojaribu kujenga mnara wa Babeli. Kwa ufupi tunaweza kusema, Habari za wana wa Adamu ndizo hizi: Mtu ni mzalimu! Kama ilivyoandikwa ndani ya Maandiko: ***"Wote ni chini ya zambi ... Hakuna mwenye haki, hata mmoja! ... Wote wametoka kwa njia, wote wamekuwa pasipo faida; hakuna mwenye kufanya mema, hata mmoja!"*** (Waroma 3:9,10,12)

Kama tulivyoona uzalimu wa mtu, vivyo hivyo tuliona **haki ya Mungu**. Maandiko yanatuambia ya kwamba *"Mungu ni **nuru**; wala giza si ndani yake kabisa!"* (1 Yoane 1:5) Tuliona haki ya Mungu wakati alipofukuza Lusifero kwa sababu ya kiburi na uasi wake. Tuliiona tena wakati alipofukuza Adamu na Hawa kwa sababu ya kuasi kwao. Kisha, Mungu alifunua haki yake kwa njia ya kuahidi kutuma duniani Mwokozi mtakatifu atakayelipa deni ya zambi za wana wa Adamu. Tuliona vilevile haki ya Mungu ndani ya sheria yake inayosema, *"pasipo kumwanga damu hakuna ondoleo."* (Waebrania 9:22) Mungu alionyesha haki yake wakati alipopokea Abeli kwa sababu ya damu ya mwana-kondoo, na alikataa Kaina, aliyezarau njia ya usamehe ya Mungu. Tuliona haki ya Mungu kwa wakati wa Noa, wakati, nyuma ya kungoja miaka 100 kwa watu kutubu, alituma garika kuharibu watu wote waliokataa njia yake. Na ndani ya somo la mbele, tuliona namna Mungu alivyofunua haki yake kwa njia ya kuchanganya lugha za watu wa mji Babeli waliokuwa wakimwasi.

Ndiyo, Mungu ni **mwenye haki** na kwa sababu hii ni lazima kwake kuhukumu watu! Wenye zambi wanaokosa haki hawawezi kumkaribia kwa njia ya kutegemea *"kazi zao njema"* zisizotimia. Ni lazima kwa Mungu kuhukumu na kuazibu kila kitu kinachochafuwa na zambi. Kama ilivyoandikwa ndani ya Neno la Mungu: *"Mungu wetu ni moto wa kuteketeza! ... Bwana atahukumu watu wake. Ni neno la kuogopa kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai!"* (Waebrania 12:29; 10:30,31)

Hivi, ndani ya sura kumi na moja za kwanza za kitabu cha Mwanzo, Mungu ametujulisha kweli kubwa sana ya haki yake ya kutimia. Hivi mtu mzalimu hana tumaini tena ya kwamba Mungu atamkubali? Sivyo, Mungu asifiwe, kuna **tumaini kwa wenye zambi!** Mungu, kwa neema yake, amefunua namna gani wana wa Adamu, wenye zambi wanaweza kufanyizwa kuwa haki mbele yake! Unajua njia ya wokovu ambayo Mungu ametengeneza kwa wenye zambi? Kama usipofahamu bado **njia ya haki ya Mungu,** vizuri usome vilevile masomo yatakayofuata juu ya nabii Abrahamu aliyeitwa "rafiki ya Mungu". Ndani ya habari za ajabu za Abrahamu tutaona namna gani wazalimu wanaweza kugeuzwa kuwa haki mbele ya Mungu.

Mungu akubariki wakati unapowaza tena juu ya maneno yote tuliyojifunza leo. Neno la Mungu linasema:

> ***"Yote yaliyoandikwa, yameandikwa kwa mafundisho yetu, hata kwa saburi na faraja ya maandiko tuwe na tumaini."***
> (Waroma 15:4)

SOMO 18

ABRAHAMU: KWA SABABU GANI MUNGU ALIMWITA

MWANZO 11,12

Salamu kwako, Rafiki. Tuendelee sasa na somo lingine la mfulizo *Njia ya Haki*.

Ndani ya masomo ya mbele, tulijifunza juu ya Mungu na njia yake ya haki. Tuliona Adamu na Hawa, Kaina na Abeli, Seti na Enoka, Noa na watu walioishi kwa wakati wake, na Nimurodi na mnara wa Babeli. Wachache tu wa wazazi wetu wamefuata **Mungu na njia yake ya haki;** zaidi yao walifuata **Shetani na njia yake ya uzalimu.**

Leo, tumefika kwa habari za mtu mmoja mwenye jina la kujulikana sana ndani ya Neno la Mungu, na aliyekuwa na kazi kubwa ndani ya shauri la Mungu kukomboa wana wa Adamu. Maandiko yanaita mtu yule *"rafiki ya Mungu"* na *"baba ya wote wanaoamini"*. Unajua ni nani? Ni nabii wa Mungu, **Abrahamu** [*Ibrahim* kwa Kiarabu]**.** Maandiko Matakatifu yanasema maneno mengi juu yake. Jina lake linaonekana ndani ya Maandiko ya manabii kupita mara mia tatu. Kwa sababu hii, Mungu akitaka, kuanza leo na ndani ya masomo yanayofuata, tutatafuta ndani ya Maandiko maneno yanayofundisha juu ya mtu huyu aliyeitwa *"rafiki ya Mungu"*. Leo tunakusudi kufikiri juu ya mwanzo wa habari za Abrahamu, Tutaona **namna gani Mungu alimwita** kumfuata na kama **alimwita kwa sababu gani.**

Mbele ya kuanza, inakupasa kujua ya kwamba kwa mwanzo jina la Abrahamu halikuwa *Abrahamu* lakini ***Abramu***. Kwa somo 20 tutaona kwa sababu gani Mungu aligeuza jina la Abramu kuwa Abrahamu. Lakini kwa leo, tukumbuke ya kwamba Abrahamu aliitwa kwanza Abramu.

Ndani ya sura 11 ya kitabu cha Mwanzo, tunajifunza ya kwamba Abramu alikuwa mmoja wa **wazao wa Semu**. Unakumbuka Semu,

Hamu na Yafeti? Walikuwa wana watatu wa Noa. Kutoka Semu kufika Abramu kulikuwa na vizazi kumi, kama vile kulikuwa na vizazi kumi toka Adamu kufika Noa. Baba ya Abramu alikuwa Tera. Maandiko yanasema: "*Tera akazaa Abramu, Nahori na Harani: Harani akazaa Loti.*" (Mwanzo 11:27) Loti alikuwa mwana wa mkubwa wa Abramu. Baba ya Loti alikuwa amekufa. Jina la mke wa Abramu lilikuwa Sarai. "*Na Sarai alikuwa tasa; hakuwa na mtoto.*" (Mwanzo 11:30) Abramu na Sarai walikuwa na baba mmoja, lakini mama mbalimbali.

Abramu alikaa ndani ya mji jina lake Uri, uliokuwa katika inchi ya Kaldea, inayoitwa Iraq kwa wakati wa sasa. Mji huu haukuwa mbali na pahali Nimurodi alipojaribu kujenga mji ulioitwa Babeli na mnara wake juu sana. Watu wa inchi waliabudu sanamu. Kama wazao wote wa Adamu, **Abramu alizaliwa katika giza la zambi.** Baba ya Abramu hakujua Mungu wa kweli na Abramu hakumjua vilevile.

Lakini Maandiko yanatujulisha ya kwamba siku moja **Bwana Mungu alijifunua kwa Abramu** na kusema naye. Kwa wakati ule wa zamani, Mungu alisema na watu na sauti mara nyingine kwa sababu hawakuwa na maandiko ya manabii kwanza. Leo, Mungu anasema na watu kwa njia ya **Maandiko Matakatifu**. Kwa sababu hii hatuhitaji tena masemo toka mbinguni, wala maono, wala malaika kwa kujua njia ya haki. Wakati tunapofikiri juu ya Maandiko Matakatifu tunasikiliza **sauti ya Mungu** ikisema nasi.

Tusikilize sasa maneno Mungu aliyosema na Abramu. Ndani ya sura 12, shairi la kwanza, tunasoma: "*Bwana akamwambia Abramu:* ***Toka katika inchi yako*** *na katika ndugu zako, na nyumba ya baba yako na kwenda hata inchi ambayo nitakuonyesha.*" (Mwanzo 12:1) Ulisikia neno Mungu aliloagiza Abramu? Aliagiza Abramu kutoka nyumba ya baba yake, kulagana na ndugu na jamaa yake, kuondokea inchi yake, na kuhama kwa inchi ambapo Mungu atamwongoza. Sisi watu tunge-fikiri kwamba neno hili ambalo Mungu aliomba Abramu kufanya lilikuwa neno gumu kabisa, lakini Mungu alikusudi kumbariki sana.

Tusome shairi hili tena pamoja na mashairi mawili yanayofuata, ili tuweze kujua kwa sababu gani Mungu aliita Abramu kuondokea inchi yake na kwenda inchi nyingine.

> "*Basi Bwana akamwambia: Toka wewe katika inchi yako na katika ndugu zako, na nyumba ya baba yako hata inchi ambayo nitakuonye-sha; na* ***nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa****, na nitakubariki,*

> *nitatukuza jina lako, nawe uwe baraka; na nitawabariki ambao wanakubariki; naye ambaye anakulaani nitamlaani vilevile, na* ***ndani yako jamaa zote za inchi watabarikiwa.****"* (Mwanzo 12:1-3)

Kwa nini Mungu aliagiza Abramu kuhama kwa inchi nyingine? **Kwa sababu Mungu alikusudi kufanya kwa njia ya Abramu taifa jipya. Manabii wa Mungu na Mwokozi wa dunia watatoka kwa taifa hili.** Kwa sababu hii Mungu aliahidi Abramu akisema, *"Nitakufanya kuwa taifa kubwa ... nawe uwe baraka ... na ndani yako jamaa zote za inchi watabarikiwa."*

Hii ndiyo **kweli kubwa**. Unaifahamu? Mungu alichagua Abramu kuwa baba ya wazazi kwa njia yao Mkombozi ambaye aliahidi atafika duniani. Mkombozi huyu aliwekwa kuwa Mwokozi kwa watu wote wa dunia, ili mtu ye yote ambaye anamwamini aweze kuokolewa toka utawala wa zambi na Shetani na moto wa milele. Hivi, tunaona ya kwamba wakati Mungu alipoita Abramu, aliendelea mbele na shauri lake kutuma Mwokozi kwa wenye zambi duniani. Abramu mwenyewe hakuwa Mwokozi wa dunia, **lakini atakuwa baba wa taifa kwa njia yake Mwokozi aliyeahidiwa atakuja**.

Hii ndiyo ahadi, ndilo agano Mungu alilofanya na Abrahamu—kama akikubali kuondokea inchi yake na kwenda pahali ambapo Mungu atamwonyesha. Abramu alitii Mungu? Unafikiri nini? Neno la Mungu linatuambia:

> *"****Hivi Abramu akakwenda, sawasawa Bwana Mungu alivyomwambia*** *... Abramu alikuwa na miaka makumi saba na mitano wakati alipotoka kwa Harani. Abramu akatwaa Sarai mke wake, na Loti mwana wa ndugu yake, na mali zao zote walizopata, na watu waliopata katika Harani; wakatoka kwenda kwa inchi ya Kanana; wakaingia inchi ya Kanana."* (Mwanzo 12:4,5)

Kwa nini Abramu alitii Mungu, akiachana na nyumba na dini ya baba yake? Kuna sababu moja tu. **Abramu aliamini Mungu**. Hakujua pahali alipokuwa akikwenda, lakini aliamini neno la Bwana lililosema: "Toka hapa! Ukitoka, nitakubariki sana!" Abramu aliamini Mungu, akaondokea inchi yake kama Bwana alivyomwagiza. Na Mungu, mwaminifu, aliongoza Abramu kufikia inchi ya **Kanana**, inayoitwa leo *Palestina*, au *Israeli.*

Halafu tunasoma: "*Abramu akapita katika inchi ... Na Mkanana alikuwa inchini kwa wakati ule. Bwana akaonekana kwa Abramu, akamwambia:* ***Uzao wako nitawapa inchi hii****."* (Mwanzo 12:6,7) Hivi

tunajifunza ya kwamba Mungu, aliyeahidi kufanyiza Abramu kuwa baba wa taifa jipya, aliahidi kumpa inchi mpya vilevile. Hii ndiyo maana ya maneno ya Mungu wakati alipotokea kwa Abramu na kumtolea ahadi: "*Uzao wako nitawapa inchi hii.*"

Halafu tunaona neno lingine linaloshinda akili yetu ya umtu. Watu wengi walikaa ndani ya inchi ya Kanana. Namna gani Abramu na wazao wake wataweza kuikamata? **Abramu alikuwa na miaka 75. Mke wake alikuwa na miaka 65 na hakuzaa watoto.** Namna gani wazee hawa wawili wataweza kuwa na watoto na wazao wa kutosha kujaza inchi? Itawezekana kweli?

Tujaribu kusema maneno haya tena kwa njia ya mfano wa ahadi hii kwa Abramu. Ni kama mzee asiye na watoto akitoka inchi ya mbali kufika kuona inchi ya Congo. Anafika pamoja na mke wake mzee, aliye tasa. Wakati wanapofika, mtu mmoja anasema nao: "Siku nyingine inchi hii ya Congo itakuwa inchi yenu na ya wazao wenu!" Mzee anacheka mtu huyu, anasema, "Wewe ni mtu wa kuchekesha! Inchi hii itakuwa ya wazao wangu? Basi mimi mzee; sina watoto na mke wangu hawezi kupata mimba! Tena unasema hesabu ya wazao wangu itaongezeka nao watakamata Congo? Una wazimu?"

Labda mfano huu ni mpumbavu kidogo; hata hivi ni sawasawa na ahadi Mungu aliyotolea Abramu—mtu aliyekuwa mzee asiyekuwa na watoto, mwenye mke asiyeweza kupata mimba. Sikiliza neno Mungu aliloahidi Abramu katika sura 13. Alisema,

> "*Inchi yote unayoona, nimekupa wewe na uzao wako hata milele. Na nitafanya uzao wako kuwa kama mavumbi ya inchi;* ***hata mtu akiweza kuhesabu mavumbi ya inchi, halafu uzao wako vilevile utahesabiwa.*** *Simama, utembee inchi urefu wake na upana wake; kwa sababu nitakupa wewe.*" (Mwanzo 13:15-17)

Mungu alitimiza ahadi yake? Alifanyiza Abramu kuwa taifa kubwa? Aliwapa wazao wa Abrahamu inchi ya Palestina? Kabisa! Ndani ya masomo ya nyuma tutaona ya kwamba Abramu aligeuka baba wa taifa la Waebrania na Mungu aliwapa taifa hili inchi inayoitwa *Israeli* kwa wakati wa sasa.

Halafu tunasoma: "*Abramu akaondoka kule hata mlima wa mashariki wa Beteli, akapiga hema yake ... akajenga* ***mazabahu*** *kwa Bwana pale, akaitia jina la Bwana.*" (Mwanzo 12:7,8) Neno la kwanza Abramu alilofanya wakati alipofikia inchi mpya ambayo Mungu alikuwa ameahidi kumpa lilikuwa nini? Alichinja nyama na kuiteketeza juu ya ma-

zabahu aliyojenga. Akiiga Abeli, Seti, Enoka, na Noa, alitoa sadaka za nyama kwa Mungu. Abramu alifanya hivi kwa sababu gani? Alifanya hivi kwa sababu Mungu hakuondosha sheria yake inayosema: *"Pasipo kumwanga damu hakuna ondoleo!"* (Waebrania 9:22) **Abramu, kama wazao wote wa Adamu, alikuwa mwenye zambi.** Kwa sababu moja tu Mungu aliweza kuachilia zambi za Abrahamu, ndiyo hii: Abramu aliamini Mungu na alimletea **damu ya sadaka,** ndiyo mfano wa **Mkombozi mtakatifu** atakayekuja duniani kufa kwa pahali pa wenye zambi.

Tulijifunza maneno makubwa ndani ya somo la leo—haifai tuyasahau kamwe. Unafahamu sasa **kwa sababu gani** Mungu aliita Abramu kuondokea nyumba ya baba yake na kwenda kwa inchi nyingine? Ndiyo, lilikuwa kusudi la Mungu kufanyiza Abramu kuwa taifa jipya litakalokuwa *"lango la baraka"* kwa mataifa yote ya dunia. Shauri la Mungu kwa Abramu lilikuwa **sehemu ya shauri la ajabu** alilotangaza ndani ya shamba la Paradiso, siku wazazi wetu, Adamu na Hawa walipofanya zambi. Unakumbuka ya kwamba Mungu aliahidi kwamba mmoja atakuja atakayeokoa wana wa Adamu toka uwezo wa Shetani? Halafu **miaka elfu mbili ilipita kufika wakati wa Abramu, lakini Mungu hakusahau ahadi yake kwa Adamu!**

Leo tumeona ya kwamba Mungu mwaminifu aliita Abramu ili aweze kuwa baba ya taifa kwa njia yake Mwokozi ambaye Mungu aliahidi kutuma atakuja duniani. Kwa sababu hii Mungu aliahidi Abramu akisema: *"Nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na nitakubariki, nitatukuza jina lako, nawe uwe baraka; na nitawabariki ambao wanakubariki: naye ambaye anakulaani nitamlaani vilevile, na* ***ndani yako jamaa zote za inchi watabarikiwa.****"* (Mwanzo 12:2,3)

Umefahamu mafundisho ya leo vizuri? Uturuhusu kukuuliza maneno mawili yanayojumlisha maneno ambayo tunakwisha kujifunza leo.

La kwanza: **Kwa nini Mungu aliita Abramu kuondokea pahali pa wazazi wake na kwendea inchi nyingine?** Kwa sababu Mungu alikusudi kufanyiza Abramu kuwa taifa jipya.

La pili: **Kwa sababu gani Mungu alitaka kufanya taifa jipya kwa njia ya Abramu?** Kwa sababu kwa njia ya taifa hili Mungu alikusudi kutupa sisi manabii, na mwishoni, Mkombozi mtakatifu mwenyewe.

Hivi ndani ya jumlisho hili tunaona ya kwamba wakati Mungu alipoita Abramu kumfuata, **aliendelea na shauri lake kuleta Mwokozi kwa wenye zambi duniani.**

~~~~~~~~~~~~~~~~

Ndani ya somo la nyuma, tutaona kwa nini Abramu aliitwa "rafiki ya Mungu." Mungu akubariki, na ukae kuwaza juu ya ahadi ya Mungu kwa Abramu, ndiyo ya kwamba:

> ***"Nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa ... nawe uwe baraka ... na ndani yako jamaa zote za inchi watabarikiwa."***
>
> (Mwanzo 12:2,3)
~~~~~~~~~~~~~~~~

SOMO 19

ABRAHAMU, RAFIKI YA MUNGU

MWANZO 13-15

Salama kwako, Rafiki. Asante kwa sababu tunaweza kuendelea tena leo na mfulizo *Njia ya Haki.*

Ndani ya somo la mbele, tulianza kuangalia maneno tunayosoma ndani ya Neno la Mungu juu ya nabii Abrahamu. Tuliona ya kwamba Abrahamu aliitwa ***Abramu*** kwanza. Tuliona vile ya kwamba alizaliwa ndani ya inchi ya Kaldea inayoitwa Iraq kwa wakati wa sasa. Watu wa inchi ile walikuwa waabudaji sanamu. Lakini, Maandiko yanasema ya kwamba Bwana Mungu alitokea Abramu siku moja na kumwagiza kuondokea nyumba ya baba yake, kuagana na ndugu zake, na kuhama kwa inchi nyingine ambayo atamwonyesha.

Unakumbuka **kwa sababu gani** Mungu aliita Abramu kuhama kwa inchi nyingine? Kwa sababu Mungu alikusudi kufanya **taifa jipya** kwa njia ya Abramu, na ya kwamba manabii wa Mungu na mwishoni Mwokozi wa dunia mwenyewe watazaliwa kwa taifa hili. Hivi tuliona ya kwamba wakati Mungu alipoita Abramu, aliendelea mbele na **shauri lake** kutuma Mwokozi duniani. Kwa sababu hii Mungu alisema na Abramu, "*nawe uwe baraka ... n**a ndani yako jamaa zote za inchi watabarikiwa.***" (Mwanzo 12:2,3)

Halafu tulisoma ya kwamba Abramu alitii Mungu na aliondokea mji wake, bila kujua pahali gani Mungu atakapomfikisha. Abramu alikuwa na miaka 75 wakati alipoondokea nyumba ya baba yake. Alipeleka Sarai, mke wake, na Loti, mwana wa mkubwa wake pamoja naye, na mali yake yote na watumishi wake, akaanza safari kwenda inchi ya Kanana, inayoitwa Palestina au Israeli wakati wa sasa.

Wakati Abramu alipofikia inchi ya Kanana, Bwana alitokea kwake tena, akasema naye: "*Uzao wako nitawapa inchi hii.*" (Mwanzo 12:7) Hivi tunaona ya kwamba Mungu, aliyeahidi kufanyiza Abramu kuwa baba wa taifa jipya, aliahidi vilevile kumpa inchi mpya kwa wazao wake kukaa ndani yake. Ajabu kabisa iliyo nguvu kuamini! Abramu na mke wake walikuwa wazee na hawakuwa na

watoto. Basi namna gani wataweza kuwa na wazao watakaojaza inchi? Tutaona jibu la ulizo hili nyuma kidogo.

Sasa tuendelee na habari za Abramu. Tunasoma ndani ya kitabu cha Mwanzo, sura 13. Ndani ya sura hii tunaona **habari za Abramu na Loti, mwana wa ndugu yake.** Maandiko yanasema (Mwanzo 13:2-13):

> *"Naye Abramu alikuwa tajiri sana kwa ngombe, kwa feza na kwa zahabu ... Akakwenda akisafiri kutoka kusini hata Beteli, kwa pahali hema yake ilipokuwa toka mwanzo, katikati ya Beteli na Ai; kwa pahali pa mazabahu, aliyofanya pale kwanza; na pale Abramu aliitia jina la Bwana. Loti vilevile aliyekwenda pamoja na Abramu alikuwa na kondoo na ngombe na hema. Wala inchi haikuweza kuwafaa wapate kukaa pamoja; kwa sababu mali zao zilikuwa nyingi, hivi hawakuweza kukaa pamoja. Na kulikuwa ugomvi katikati ya wachungaji wa ngombe za Abramu na wachungaji wa Loti ... Abramu akamwambia Loti: Ugomvi usiwe, ninakuomba, katikati yangu nawe, wala katikati ya wachungaji wangu na wachungaji wako; kwa sababu sisi ni ndugu. Inchi nzima si mbele yako? Ujitenge, ninakuomba, mbali nami;* ***ukikwenda kwa kushoto, nitakwenda kwa kuume; au ukikwenda kwa kuume, nitakwenda kwa kushoto.***
>
> *Na Loti alinyanyua macho yake, akatazama inchi sawa nzima ya Yorodani, ya kama maji yalifaa pahali po pote, na Bwana hajaharibu bado Sodomo na Gomora, kama shamba la Bwana, kama inchi ya Misri, wakati unapokwenda Zoari. Hivi Loti akajichagua inchi sawa nzima ya Yorodani; Loti akasafiri kwa mashariki; wakajitenga wao kwa wao.* ***Abramu*** *akakaa katika inchi ya Kanana, na* ***Loti*** *alikaa katika miji ya inchi sawa, akahamisha hema yake hata Sodomo. Basi watu wa Sodomo walikuwa wabaya, na wenye zambi sana mbele ya Bwana."*

Hivi tunaona kwamba Loti alichagua mashamba mazuri yenye maji, na aliacha mjomba wake na yale ya kukauka. Lakini sehemu ya inchi ambayo Loti alichagua ilikuwa kwa upande wa Sodomo, ndio mji uliojaa uovu!

Loti alichagua kufuata **mapenzi yake mwenyewe**, lakini Abramu alichagua **mapenzi ya Mungu**. Masomo mawili ya nyuma, tutaona nini ilipata Loti aliyechagua kufanya maneno yeye mwenyewe aliyotaka. Mwishoni, Loti alipoteza yote: mali yake, mke wake, jamaa yake, furaha yake, na ushuhuda wake! Lakini Abramu, aliyeacha maneno yake yote mikononi mwa Mungu, alibarikiwa sana naye.

Habari hizi za Loti na Abramu zinaweza kuwa na faida gani kwa sisi? Labda kwa njia ya kujiuliza: Mimi ninafanana na nani zaidi, na

Loti? Au na **Abramu**? Mimi ninatafuta **maneno ya dunia**, kama Loti? Au **maneno ya milele**, kama Abramu? Kama watu wale wawili inatupasa sisi vilevile kuchagua kufanya au mapenzi yetu wenyewe, au mapenzi ya Mungu. Mtu wa akili atachagua mapenzi ya Mungu. Maandiko yanasema: *"Mtu atapata faida gani, kama akipata ulimwengu wote, na kupata hasara ya uzima wake?"* (Marko 8:36) *"Musipende dunia, wala maneno katika dunia. ... Na dunia inapita pamoja na tamaa zake, l**aki-ni yeye anayefanya mapenzi ya Mungu anadumu milele."*** (1 Yoane 2:15,17) Unataka maneno gani zaidi kupita yote? Maneno ya dunia yatakayopita au maneno ya Mungu yatakayodumu milele?

Halafu tuendelee na habari za Abramu. Maandiko yanasema: (Mwanzo 13:14-18)

> *"Bwana akamwambia Abramu, wakati alipokwisha kutengana na Loti: Nyanyua sasa macho yako, na angalia toka pahali unapokuwa, kwa kaskazini na kusini na mashariki, na mangaribi: kwa sababu **inchi yote unayoona, nimekupa wewe na uzao wako hata milele.** Na nitafanya uzao wako kuwa kama mavumbi ya inchi; hata mtu akiweza kuhesabu mavumbi ya inchi, halafu uzao wako vilevile utahesabiwa. Simama, utembee inchi, urefu wake na upana wake; kwa sababu nitakupa wewe. Abrahamu akahamisha hema yake, akakuja, akapanga kwa mielo ya Mamuri, iliyo kwa Heburoni, akajenga pale mazabahu kwa Bwana."*
>
> (Mwanzo 15:1-6) *"Nyuma ya maneno haya neno la Bwana lili-kuja kwa Abramu katika ndoto likisema: Usiogope, Abramu, mimi ni ngabo yako na zawabu yako kubwa sana. Abramu akasema: Ee Bwana Mungu, utanipa nini kwa kuwa mimi sina mtoto, naye atakayekuwa mwenye nyumba yangu ni Eliezeri Mdamasiki? Abramu akasema: Tazama, hukunipa uzao; na tazama, mmoja aliyezaliwa nyumbani mwangu ni mriti wangu. Na tazama, neno la Bwana lilikuja kwake likisema: Mtu huyu hatakuwa mriti wako; lakini yeye atakayetoka viunoni mwako, yeye atakuwa mriti wako. Akamtoa inje, akasema: Tazama sasa mbinguni, na hesabu nyota kama ukiweza kuzihesabu; akamwambia: Ndivyo itakavyokuwa uzao wako. **Akaamini Bwana; akamhesabia kwa haki."***

Ajabu kabisa! Abramu na mke wake walikuwa wazee na hawakuwa na mtoto. Lakini Mungu alikaa kutolea Abramu ahadi ya kwamba atakuwa baba ya taifa kubwa. Itawezekana namna gani? Namna gani Abramu ataweza kuwa baba ya taifa kubwa? Kuna jibu moja tu kwa ulizo hili, ndilo hili: Bwana Mungu ndiye Mungu

anayeweza kufanya maneno yote! Hakuna neno ambalo linaweza kumshinda! Mungu akiahidi neno fulani, neno hili litafanyikana.

Basi Abramu? Aliamini Bwana aliyeahidi neno "lisilowezekana"? Sikia maneno Maandiko yanayosema: ***"Abramu akaamini Bwana; akamhesabia kwa haki!"*** Neno la kushangaza kabisa! Mungu aliahidi neno kwa Abramu lisilowezekana kwa mafikiri ya watu. Lakini Abramu alijibu namna gani kwa ahadi hii? Aliamini neno ambalo Mungu alimwahidi! Na Mungu alifanya nini? **Mungu alihesabia Abramu haki kwa sababu ya imani yake!**

Ingepasa kweli hii kufurahisha sana mioyo ya wale wanaotaka kuhesabiwa haki mbele ya Mungu. Kwa nini Mungu alihesabu Abramu kuwa mwenye haki? Abramu alikuwa na haki yeye mwenyewe? Sivyo! Ndani ya somo la nyuma tutaona ya kwamba Abramu alikuwa na tabia ya mwenye zambi, kama kila mzao wa Adamu. Basi kwa sababu gani Mungu alihesabia Abramu haki? **Mungu alihesabu Abramu kuwa na haki kwa sababu Abramu aliamini maneno Mungu aliyosema!**

Maana ya kuamini Mungu ni nini? Maandiko Matakatifu ya manabii yaliandikwa kwa lugha ya Kiebrania. Kwa Kiebrania neno kwa "**amini**" ni "**AMAN**" na neno letu ***"Amina"*** linatoka kwa neno lile. Wakati unaposema "Amina" unasema, "Ndiyo! Ni kweli!" au "Ndiyo, ninakubali!" Hii ndiyo maana ya kuamini. Wakati Mungu alipotoa ahadi kwa Abramu, Abramu alisema rohoni mwake: "Amina! Ndiyo! Ni kweli! Ninaamini masemo yako!" **Kwa sababu Abramu alikubali Neno la Mungu, Mungu alihesabia Abramu haki.**

Basi wewe? Unataka Mungu kukuhesabia haki kama alivyofanya na Abramu? Kama ni hivi, sharti uamini Mungu kama Abramu alivyofanya. **Lazima uamini maneno Mungu anayosema, hata kama ni nguvu.** Sharti upokee Neno la kweli la Mungu, hata kama ndugu zako na rafiki zako wakilikataa! Mungu anataka kukuvalisha na haki yake na kukupa ruhusa kuishi kwake milele katika utakatifu, lakini **sharti uamini Neno lake!** Maandiko Matakatifu yanasema:

> *"Pasipo imani **haiwezekani** kupendeza Mungu!"* (Waebrania 11:6), *na "Mumeokolewa **kwa neema kwa njia ya imani**, wala neno hili halikutoka ndani yenu wenyewe, ni zawadi ya Mungu, **si kwa matendo,** asiwe mtu atakayejisifu." (Waefeso 2:8,9)*
>
> *"Basi tuseme nini, Abrahamu baba yetu amepata nini kwa njia ya mwili? Kwa maana kama Abrahamu alihesabiwa haki kwa ajili ya*

> *matendo, ana maneno ya kujisifia; lakini si mbele ya Mungu. Kwa maana maandiko yanasema nini?* ***Abrahamu aliamini Mungu, na ilihesabiwa kwake kuwa haki."*** (Waroma 4:1-3)

Ndiyo, Abramu aliamini Neno la Mungu. Ni kwa sababu hii tu Mungu alimhesabia haki kamilifu. Na neno zuri zaidi ndani ya mambo haya yote ni ya kwamba masemo haya *"Abramu aliamini Bwana, na ilihesabiwa haki"* si kwa Abramu tu. Sisi vilevile tunaweza kushiriki ndani ya masemo haya. **Mungu atatugawanyia haki yake kamilifu kama tukiamini Habari Njema ya Mungu** juu ya Mwokozi atakayekuja duniani nyuma kwa njia ya jamaa ya Abramu.

Basi wewe? **Unaamini Mungu kweli kweli?** Hatuulizi kama ukiamini kwamba **Mungu yuko**, au kwamba Mungu **ni mmoja**. Maandiko yanasema juu ya imani ya namna hii: *"Wewe unaamini ya kuwa Mungu ni mmoja tu; ni vizuri,* ***mashatani wanaamini vilevile*** *na kutetemeka!"* (Yakobo 2:19) Shetani yeye mwenyewe anajua kwamba kuna Mungu mmoja tu. Kuamini kwamba kuna Mungu mmoja **hakutoshi** kwa Mungu kusamehe zambi zako na kukuhesabu kama mwenye haki! Neno Mungu analotaka ni kwa wewe **kuamini Neno lake na kulipokea.** Mungu anataka kusema nawe kwa njia ya Maandiko ya manabii. Anataka ujue na kuamini habari njema za wokovu zinazoonyesha ya kwamba unaweza kufanyizwa haki mbele ya Mungu yule Mtakatifu!

Rafiki, Mungu amekuvalisha na **haki yake**? Au unavaa tu mavazi ya dini? Unasikiliza Neno la Mungu ambalo tunaweza kutegemea? Au masemo ya watu wa dunia tu? **Unajua** maneno Maandiko Matakatifu ya Mungu yanayotangaza juu ya njia ya haki ambayo Mungu aliisimamisha? **Umeyaamini?**

Basi Abramu aliamini Neno la Mungu, si neno kama ikimpasa kuachana na ndugu zake na dini ya baba yake. Na kwa sababu hii aliitwa ***"rafiki ya Mungu!"*** Haya ndiyo maneno ya Maandiko: *"Abramu* ***aliamini Mungu****, ikahesabiwa kwake kuwa ni* ***haki****; naye aliitwa* ***rafiki ya Mungu."*** (Yakobo 2:23) **Wewe** ni rafiki ya Mungu?

~~~~~~~~~~~

Ndani ya somo la nyuma tutawaza juu ya habari za Abramu na Isimaeli. Mungu akubariki na tunakusihi kuwaza sana juu ya shairi hili kubwa toka Neno la Mungu:

> ***"Abrahamu aliamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa ni haki; naye aliitwa rafiki ya Mungu."*** (Yakobo 2:23)
~~~~~~~~~~~

SOMO 20

ABRAHAMU NA ISIMAELI

MWANZO 16,17

Salama iwe kwako, rafiki msomaji, kwa jina la Mungu wa salama, anayetaka watu wote kufahamu, kuamini na kupokea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Asante kwa kufika kusoma somo lingine la mfulizo *Njia ya Haki.*

Ndani ya masomo mawili ya mbele, tulianza kuangalia maneno tunayosoma ndani ya Neno la Mungu juu ya nabii Abrahamu. Tuliona ya kwamba Abrahamu aliitwa Abramu kwanza. **Leo tutaona kwa nini Mungu aligeuza jina lake kuwa *Abrahamu*.**

Ndani ya sehemu ya kwanza ya somo letu leo tutaona **habari za huzuni** za neno ambalo Abrahamu alifanya, neno lisilopendeza Mungu. Watu wengine wanafikiri ya kwamba manabii wa Mungu hawakufanya zambi daima. Lakini Neno la Mungu linatangaza ya kwamba: *"hapana tofauti; kwa sababu **wote wamefanya zambi,** na kupungukiwa na utukufu wa Mungu"* (Waroma 3:22,23) na *"Kama tukisema kwamba hatukutenda zambi, tunamfanya yeye mwongo, wala neno lake si ndani yetu."* (1 Yoane 1:10) Tumeona mbele namna zambi ya Adamu ilivyoenea kwa watu wote—vijana na wazee, wanaume na wanawake, wapagano na manabii. Kuna Mmoja tu asiyechafuwa na zambi ya Adamu, ndiye **Mkombozi mtakatifu** ambaye Mungu alituma duniani kuokoa wenye zambi. Hakuweza kufanya zambi, kwa sababu alikuja toka juu, toka Mungu Mtakatifu. Mwokozi wa dunia hakuzaliwa na baba ya dunia kama wana wote wengine wa Adamu. Alizaliwa na bikira, kwa uwezo wa Mungu. Kwa sababu hii alistahili kufa kwa pahali pa wenye zambi, *"mwenye haki kwa ajili yao wasio haki, ili atulete kwa Mungu."* (1 Petro 3:18)

Ndani ya masomo mawili ya mbele, tuliona ya kwamba **Mungu aliahidi kufanyiza Abramu kuwa baba ya taifa kubwa,** na ya kwamba Mwokozi huyu atatokea kwa njia ya taifa hili. Abramu na mke wake vilevile walikuwa wazee na hawakuzaa watoto, lakini neno hili

halikuamsha shaka ndani ya roho ya Abramu juu ya neno la Mungu. Lakini, leo tutaona ya kwamba wakati miaka kumi ilipokuwa imepita tangu Mungu alipotoa ahadi mara ya kwanza kumpa Abramu wazao, **Abramu alijaribu "kusaidia" Mungu kutimiza ahadi yake.** Lakini neno Abramu alilofanya kwa sababu ya kukosa saburi lilizaa magumu na huzuni.

Basi tuendelee kusoma ndani ya kitabu cha Mwanzo kuona namna Abramu na Sarai walivyotengeneza maneno ili waweze kupata mwana yule ambaye Mungu aliahidi. Ndani ya sura 16 ya kitabu cha Mwanzo, kuanza na shairi 1, Maandiko yanasema:

> "*Basi Sarai, mke wa Abramu hakumzalia watoto; naye alikuwa na kijakazi, Mmisri, jina lake lilikuwa* ***Hagari****. Sarai akamwambia Abramu: Tazama sasa Bwana amenifunga nisizae; ingia, ninakuomba, kwa kijakazi wangu; labda nitapata wana kwa njia yake. Abramu akatii sauti ya Sarai. Sarai mke wa Abramu akatwaa Hagari Mmisri, kijakazi wake, nyuma ya miaka kumi Abramu alipokaa katika inchi ya Kanana, akampa Abramu mume wake, awe mke wake.*
>
> *Akaingia kwa Hagari, akachukua mimba; na wakati alipoona ya kama amechukua mimba, bibi yake akazarauliwa kwa macho yake. Sarai akamwambia Abramu: Uovu wangu uwe juu yako; nimekupa kijakazi wangu kifuani mwako; na wakati alipoona ya kama alichukua mimba, nimezarauliwa kwa macho yake; Bwana ahukumu katikati yangu nawe. Lakini Abramu akamwambia Sarai: Tazama, kijakazi wako ni mkononi mwako; umtendee lililo jema kwa macho yako. Sarai akamtesa, akakimbia toka uso wake.*"

Tunaona ya kwamba zambi ya Abrahamu ilizaa uchungu na magomvi nyumbani mwake. Sarai alikuwa na wivu kwa sababu Hagari alipata mimba. Hagari alipata matata kwa sababu ya Sarai ambaye alimtesa. Basi Hagari alikimbia nyumba ya Abrahamu. Maandiko yanasema katika sura 16,

> "*Malaika ya Bwana akamkuta kwa chemchemi ya maji jangwani, kwa chemchemi njiani kwa Suri. Akamwambia: Hagari, kijakazi wa Sarai, umetoka wapi? Na unakwenda wapi? Akasema: Ninakimbia toka uso wa bibi yangu Sarai. Malaika ya Bwana akamwambia: Rudi kwa bibi yako ujinyenyekeze chini ya mikono yake. Malaika ya Bwana akamwambia: Nitazidisha uzao wako sana, wala* ***hautahesabiwa kwa wingi.*** *Malaika ya Bwana akamwambia: Tazama, una mimba, na utazaa mwana; na utaita jina lake* ***Isimaeli****, kwa sababu Bwana*

amesikia teso lako. Naye atakuwa kama punda ya mwitu katikati ya watu; mkono wake utakuwa juu ya kila mtu, na mkono wa kila mtu utakuwa juu yake; ***naye atakaa mbele ya ndugu zake zote.****" (Mwanzo 16:1-12)*

Basi Hagari alirudia Sarai, bibi yake, kama malaika ya Mungu alivyosema. *"Hagari akazalia Abramu mwana; Abramu akaita jina la mwana wake ambaye Hagari alimzaa Isimaeli. Abramu alikuwa na miaka makumi manane na sita, wakati Hagari alipozalia Abramu Isimaeli."* (Mwanzo 16:15,16) Hivi **Isimaeli** alizaliwa, ndiye baba ya Waarabu. Tutaona ya kwamba Mungu alilinda Isimaeli na alikuwa na shauri kwa maisha yake, lakini Isimaeli hakuwa mwana ambaye Mungu aliahidi kumpa Abramu. Shauri la ajabu la Mungu kufanya taifa jipya kwa njia ya Abramu halikubadilika. Lakini Mungu hakuwa na haraka kama Abramu. Mungu anafanya kila mara maneno anayoahidi kufanya, hata kama kwa mawazo yetu ni kama anachelewa mara nyingine. Hivi Maandiko yanatujulisha ya kwamba kwa miaka 13 nyuma ya kuzaliwa kwa Isimaeli Mungu alikaa kimya bila kusema kitu kwa Abramu. Lakini siku moja Mungu alisema na Abramu tena.

Tusome ndani ya Mwanzo, sura 17, kuanza na shairi 1 kuona kama Mungu alisema nini na Abramu nyuma ya kukaa kimya kwa miaka ile mirefu 13. Maneno tutakayosoma ndiyo maneno ya ajabu:

"Wakati Abramu alipokuwa na ***miaka makumi tisa na tisa****, Bwana akaonekana kwa Abramu akamwambia:* ***Mimi ni mwenyezi Mungu;*** *endelea mbele yangu na uwe mkamilifu.* ***Na nitafanya agano langu katikati yangu nawe, na nitakuzidisha sana.***

*Abramu akaanguka kwa uso wake; Mungu akasemezana naye akisema: Nami, tazama, agano langu ni pamoja nawe, na utakuwa baba ya mataifa mengi. Wala jina lako halitaitwa tena Abramu, lakini jina l****ako litaitwa Abrahamu****: kwa sababu nimekufanya kuwa* ***baba ya mataifa mengi.*** *Na nitakuzidisha sana na nitafanya mataifa nawe, na wafalme watatoka ndani yako. Na nitasimamisha agano langu katikati yangu nawe, na uzao wako nyuma yako, kwa vizazi vyao kwa agano la milele, niwe Mungu kwako na kwa uzao wako nyuma yako. Na nitakupa wewe na uzao wako nyuma yako inchi ya kusafiri kwako, inchi yote ya Kanana, kwa uriti wa milele, nami nitakuwa Mungu wao.*

Mungu akamwambia Abrahamu: Nawe, utachunga agano langu, wewe na uzao wako nyuma yako kwa vizazi vyao. Na hili ni agano

langu ambalo mutalichunga, katikati yangu nawe na uzao wako nyuma yako; kila mwanamume katikati yenu atatahiriwa. Nanyi mutatahiriwa kwa ngovi, na itakuwa ***alama*** *ya agano katikati yangu nanyi. Naye aliye na siku nane atatahiriwa katikati yenu, kila mwanamume kwa vizazi vyenu " (Mwanzo 17:1-12)*

"Mungu akamwambia Abrahamu: Naye Sarai mke wako, hutaita jina lake Sarai, lakini jina lake litakuwa ***Sara****. Na nitambariki, na tena nitakupa mwana kwake; ndiyo, nitambariki naye atakuwa* ***mama ya mataifa;*** *wafalme wa watu watatoka kwake. Halafu Abrahamu akaanguka kwa uso wake, akacheka, akasema moyoni mwake: Mtoto atazaliwa kwake aliye na miaka mia moja? Na Sarai aliye na miaka makumi tisa, atazaa? Abrahamu akamwambia Mungu: Laiti Isimaeli aishi mbele yako! Mungu akasema: Hapana, lakini Sara, mke wako atakuzalia mwana; na utaita jina lake* ***Isaka; na nitasimamisha agano langu pamoja naye kwa agano la milele kwa uzao wake nyuma yake.*** *Na* ***juu ya Isimaeli,*** *nimekusikia; tazama, nimembariki, na nitamzidisha, na nitamwongeza sana sana; atazaa wakubwa kumi na wawili na* ***nitamfanya kuwa taifai kubwa. Lakini agano langu nitasimamisha na Isaka,*** *ambaye Sara atakuzalia kwa wakati huu uliowekwa kwa mwaka wa nyuma.."* (Mwanzo 17:15-21)

Inatupasa kuacha kusoma Maandiko pale kwa leo. Tumeona ya kwamba Abramu alisikiliza shauri la mke wake na alilala pamoja na Hagari mtumishi wake. Neno Abramu alilofanya lilikuwa baya. Isimaeli, mwana wa Abramu na Hagari, hakuwa ndani ya shauri la Mungu kufanyiza taifa jipya toka Abramu litakaloleta baraka kwa mataifa yote ya dunia. Lakini **kutoaminifu kwa watu hakuwezi kuzuiza uaminifu wa Mungu.** Hivi, wakati Abramu alipokuwa na miaka 99, Mungu alionekana kwake tena kusibitisha ahadi ambayo alimtolea zamani. Alisema, *"Mimi ni Mungu Mwenyezi ... utakuwa baba ya mataifa mengi. Hutaitwa Abramu tena; jina lako litakuwa Abrahamu, kwa sababu nilikufanyiza baba ya mataifa mengi."* Kupatana na shauri lake kamilifu, Mungu aligeuza jina la Abramu kuwa Abrahamu, maana yake ***baba ya watu wengi***. Mungu aligeuza jina la Sarai vilevile kuwa Sara, maana ***binti mfalme.***

Hapa tunaona neno la ajabu kabisa. Tunawaza juu ya mume na mke wazee wasiokuwa na mtoto kamwe, ndio Abramu na Sarai. Sasa Mungu atawapa majina mapya kuonyesha neno litakalotokea. Abramu atapata jina jipya, ndilo *Abrahamu*, maana yake **baba ya watu wengi,** na Sarai ataitwa *Sara*, maana yake ***binti mfalme***. Mungu

atawapa Abrahamu na Sara mwana, na kwa njia ya mwana huyu, **taifa zima**. Toka taifa hili wafalme na **manabii wengi watatoka**, na mwishoni, **Mwokozi wa dunia**! Kweli, Bwana ni mkubwa na anastahili kupata sifa kwa milele! Hakusahau neno ambalo aliahidi Abrahamu zamani.

Basi Abrahamu alifanya nini wakati aliposikia Mungu akitoa tena ahadi kumpa mtoto kwa uzee wake? Maandiko yanasema, *"Abrahamu akaanguka kwa uso wake, akacheka, akasema moyoni mwake: Mtoto atazaliwa kwake aliye na miaka mia moja? Na Sara aliye na miaka makumi tisa, atazaa?"* **Abrahamu alicheka**! Lakini hakucheka kwa sababu ya kutokuamini, lakini kwa sababu ya furaha.

Hivi Maandiko yanasema:

> *"Yeye, kwa wakati taraja isipokuwa,* ***aliamini kwa taraja****, ili apate kuwa baba ya mataifa mengi, kama ilivyosemwa: Ndivyo utakavyokuwa uzao wako. Yeye asiyekuwa zaifu katika imani, hakufikiri hali ya mwili wake, na kama umekwisha kufa, (akiwa amekwisha kupata karibu na miaka mia), na hali ya kufa ya tumbo lake Sara:* ***wala hakuona shaka kwa ahadi ya Mungu kwa kutokuamini; lakini alipata nguvu kwa imani, akimpa Mungu utukufu, akijua kabisa ya kuwa Mungu anaweza kufanya yale aliyoahidi."*** (Waroma 4:18-21)

Hata hivi, Abrahamu alitaka kujua nini itapata Isimaeli, mtoto wa mtumishi wake, Hagari. Mungu alimjibu,

> *"Na juu ya Isimaeli, nimekusikia; tazama, nimembariki ...* ***nitamfanya kuwa taifa kubwa. Lakini agano langu nitasimamisha na Isaka,*** *ambaye Sara atakuzalia ... Nitasimamisha agano langu naye kuwa agano la milele kwa wazao wake nyuma yake."* (Mwa. 17:20,21,19)

Hivi, Mungu alimwambia Abrahamu ya kwamba manabii na, mwishoni, Mkombozi mwenyewe atakuja kwa njia ya wazao wa Isaka. Ndani ya somo la nyuma, Mungu akitaka, tutaona namna Bwana alivyowapa Abrahamu na Sara mwana, kama alivyoahidi.

Kweli, **Mungu ni mwaminifu**. Anatimizaga ahadi zake! Hakuna neno ambalo linaweza kumshinda! Sikiliza mashairi haya matamu sana toka Habari Njema [*Injil*],

> *"Tazameni namna ya utajiri wa akili na maarifa ya Mungu! Hukumu zake hazivumbulikani, na njia zake hazitafutikani! Maana ni nani*

aliyejua nia ya Bwana? au ni nani aliyekuwa mshauri wake? Au ni nani aliyempa kitu kwanza, naye atalipwa tena? Kwa maana vitu vyote vinatoka kwake, na viko kwa uwezo wake, na viko kwa yeye. ***Utukufu uwe kwake milele. Amina."*** (Waroma 11:33-36)

~~~~~~~~~~~~~~~~~

Mungu akubariki wakati unapokaa kufikiri juu ya shairi hili ndani ya Maandiko Matakatifu:

"Kama sisi hatuamini, yeye anakaa mwaminifu; maana hawezi kujikana mwenyewe." (2 Timoteo 2:13)
~~~~~~~~~~~~~~~~~

SOMO 21

ABRAHAMU: UHARIBIFU WA SODOMO NA KUZALIWA KWA ISAKA

MWANZO 18-21

Salama iwe kwako, Rafiki, kwa jina la Mungu wa salama, anayetaka uweze kufahamu, kuamini na kupokea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele.

Ndani ya masomo katika kitabu cha Mwanzo, tuliona ya kwamba Mungu aliahidi kufanyiza Abrahamu baba ya taifa jipya, kwa njia yake manabii wa Mungu na Mwokozi wa dunia watakuja. Lakini, kufika sasa ndani ya mafundisho yetu, Sara, mke wa Abrahamu alikuwa hajazaa mwana, naye na Abrahamu walikuwa wazee sana.

Leo tutasikia habari nyingine za ajabu. Kwa mwanzo wa habari hizi tunaona wanaume watatu wakifikia Abrahamu. Lakini watu hawa hawakuwa wanadamu tu. Wawili wao walikuwa **malaika** na wa tatu alikuwa **Bwana Mungu mwenyewe!** Labda wengine wangesema haikuwezekana kwa Mungu mwenyewe kutokea kwa Abrahamu kwa sura ya mtu, lakini watu hawa wanasahau ya kwamba hakuna neno lisilowezekana kwa Mungu. Mungu anaweza kufanya kila neno lililo haki. Hawezi kutenda uzalimu.

Leo tutasoma toka sura ine za Tora. Tutaanza na Mwanzo 18:1-15.

> *"Bwana **alionekana kwake** [Abrahamu] kwa mielo ya Mamure, wakati alipokaa mlangoni mwa hema wakati jua lilipokuwa kali; akanyanyua macho yake, akaangalia, na tazama, **watu watatu** walisimama mbele yake; na wakati alipowaona, alikimbia kukutana nao toka mlango wa hema, akajiinama hata inchi, akasema: Bwana wangu, kama sasa nikikubaliwa machoni mwako, usipite mbali na mtumishi*

wako, ninakuomba; yaletwe sasa maji kidogo munawe miguu na kupumzika chini ya mti; nami nitatwaa chakula kidogo muburudishe mioyo yenu; halafu nyuma mutapita; kwa sababu mulikuja kwa mtumishi wenu. Wakasema: Fanya sawasawa ulivyosema.

Abrahamu akakwenda mbio, akatwaa siagi, na maziwa na ndama ambayo alitayarisha, akaviweka mbele yao; akasimama pamoja nao chini ya mti, wakakula. Wakamwambia: Sara, mke wako, ni wapi? Akasema: Tazama, hemani. Halafu ***Bwana*** *akasema:* ***Hakika nitarudi kwako wakati wa mwaka unaporudi; na tazama, Sara mke wako atazaa mwana.*** *Sara akasikia kwa mlango wa hema, iliyo nyuma yake. Basi Abrahamu na Sara walikuwa wazee na wenye siku nyingi; imekwisha kwa Sara kwa desturi ya wanawake, Sara akacheka ndani yake, akisema: Nilipokwisha kuwa mzee, nitafurahishwa, bwana wangu vilevile akiwa mzee? Bwana akamwambia Abrahamu: Kwa nini Sara alicheka akisema: Hakika mimi nitazaa mwana nikiwa mzee? Kuna kitu kinachoweza kushinda Bwana? Kwa wakati uliowekwa mbele nitarudi kwako, kwa kadiri ya wakati wake, na Sara atazaa mwana. Halafu Sara akakana akisema: Sikucheka; kwa sababu aliogopa. Naye alisema: Hapana, lakini ulicheka.*

Bwana akasema: Kwa sababu ***kilio cha [miji ya] Sodomo na Gomora ni kikubwa,*** *na kwa sababu zambi zao ni nzito sana, nitashuka sasa nione kama walivyofanya kwa kipimo cha kilio chake, kilichofika kwangu; na kama sivyo, nitajua. Watu wakageuka toka pale, wakakwenda Sodomo;* ***lakini Abrahamu alikuwa angali akisimama mbele ya Bwana.***

Abrahamu akakaribia, akasema: Utaharibu wenye haki pamoja na waovu? Labda wenye haki makumi tano ni mjini; utaharibu wala hutaacha pahali pale kwa ajili ya wenye makumi tano walio ndani yake? Haiwezekani kwako kufanya namna hii, kuharibu wenye haki pamoja na waovu, wenye haki wawe kama waovu; sivyo, haiwezekani kwako; ***mwamuzi wa dunia nzima hatatenda kwa haki?***

Bwana akasema: Kama nikikuta ndani ya Sodomo wenye haki ***makumi tano*** *mjini, nitaacha pahali pale pote kwa ajili yao. Abrahamu akajibu, akasema: Tazama, sasa nimeshika kusema na Bwana, mimi niliye mavumbi na majivu tu; labda wenye haki makumi tano watakosa watano; utaharibu mji wote kwa sababu ya kukosa watano? Akasema: Sitauharibu, kama nikikuta* ***makumi ine na watano****.*

Akasema naye tena, akisema: Labda makumi ine wataonekana. Akasema: Sitafanya kwa ajili ya ***makumi ine.*** *Akasema: Bwana asikasirike, na nitasema: Labda makumi tatu wataonekana pale. Akasema: Sitafanya nikikuta* ***makumi tatu*** *pale. Akasema: Tazama sasa, nimeshika kusema na Bwana: Labda makumi mbili wataonekana pale. Akasema: Sitauharibu kwa ajili ya* ***makumi mbili.*** *Akasema: Bwana asikasirike, na nitasema mara moja tu: Labda kumi wataonekana pale. Akasema: Sitauharibu kwa ajili ya* ***kumi.***

Bwana akakwenda zake alipokwisha kusemezana na Abrahamu. Abrahamu akarudi kwa pahali pake."

(Mwanzo 19:1-5) *"Malaika wawili walikuja kwa* ***Sodomo*** *mangaribi;* ***Loti*** *akakaa kwa lango la Sodomo; Loti akawaona, akasimama kukutana nao; akajiinama na uso wake kwa udongo, akasema: Tazama sasa, bwana wangu, mugeuke kando, ninawaomba ninyi, hata nyumbani mwa mtumishi wenu, mukawe usiku mzima na munawe miguu yenu, na mutaamka mapema, mwende zenu. Wakasema: Hapana; lakini tutakaa njiani usiku kucha.*

Akawasukuma sana; wakageuka kwake, wakaingia nyumbani mwake; akawafanyia karamu, na kuoka mkate pasipo chachu, wakakula. Lakini mbele ya kulala watu wa mji, watu wa Sodomo, wakazunguka nyumba, vijana na wazee, watu wote toka kila upande; wakaita Loti, wakamwambia: Watu waliokuja kwako usiku ni wapi? Uwatoe kwetu tupate kuwajua."

Wanaume wengi wa Sodomo waliwakiana tamaa na kufanya matendo ya haya, zambi inayochukiwa kabisa na Mungu, kama unavyosoma kwa Waroma 1:26,27.

(Mwanzo 19:6-17) *"Loti akatoka kwao kwa mlango, akafunga mlango nyuma yake. Akasema: Ninawaomba ninyi, ndugu zangu,* ***musifanye vibaya hivi*** *... Musifanyie watu hawa kitu; kwani wamekuja chini ya kivuli cha dari yangu. Wakasema: Simama kando. Wakasema: Mtu huyu mmoja amekuja kusafiri, kumbe kuhukumu atahukumu; sasa tutakufanyia wewe vibaya kuliko wao. Wakasukuma mtu mwenyewe sana, hata Loti, wakakaribia kuvunja mlango. Lakini watu wakanyosha mkono wao, wakaingiza Loti kwao nyumbani, wakafunga mlango. Wakapiga watu waliokuwa kwa mlango kwa upofu, wadogo na wakubwa, hata wakachoka kwa kutafuta mlango."*

"Watu wakamwambia Loti: Una wengine hapa? Mkwe na wana

wako na binti zako na mtu gani uliye naye mjini; uwatoe katika pahali hapa, kwani tutaharibu pahali hapa, kwa sababu ***kilio chake kimezidi mbele ya Bwana, na Bwana alitutuma kupaharibu.*** *Loti akatoka, akasemezana na wakwewe wake, waliooa binti zake, akasema: Simameni, ondokeni pahali hapa; kwa maana Bwana ataharibu mji. Lakini alionekana kwa wakwewe kama mwenye kuzihaki.*

Na wakati ilipokuwa asubui, malaika walisukuma Loti, wakisema: Simama, twaa mke wako na binti zako wawili hapa; usiharibiwe katika uovu wa mji. Lakini alikawia; watu wakashika mkono wake, na mkono wa mke wake, na mkono wa binti zake wawili; Bwana akimwonyeshea rehema; wakamtoa, wakamweka inje ya mji. Na ilikuwa wakati walipowatoa inje, akasema: ***Kimbia kwa uzima wako; usiangalie nyuma wala usisimame kwa inchi sawa yote; kimbia kwa milima usiharibiwe.***

(Mwanzo 19:24-29) ***"Halafu Bwana akanyesha juu ya Sodomo na Gomora kiberiti na moto toka Bwana mbinguni;*** *akaangusha miji ile; na inchi sawa yote, na wenyeji wote wa miji, nayo yaliyoota katika udongo.* ***Lakini mke wake (wa Loti) aliyekuwa nyuma yake akaangalia nyuma, akakuwa nguzo ya chumvi.***

Abrahamu akaondoka asubui mapema hata pahali aliposimama mbele ya Bwana; *akatazama upande wa Sodomo na Gomora, na upande wa inchi sawa yote, akaangalia, na tazama, moshi wa inchi ukapanda kama moshi wa tanuru. Na ilikuwa wakati Mungu alipoharibu miji ya inchi sawa, Mungu akakumbuka Abrahamu; akatoa Loti katikati ya maangamizi wakati alipoangamiza miji pahali Loti alipokaa."*

Hizi ni habari za kuogopesha za namna Mungu alivyohukumu miji ya Sodomo na Gomora na kiberiti na moto toka mbinguni. Kwa wakati wa sasa maangamizi ya Sodomo yanabaki chini ya Bahari ya Chumvi katika Israeli. Si vizuri kamwe kuchagua kufanya zambi. **Mungu anaweka roho sana juu ya kuhukumu zambi!**

Basi, mbele ya kumaliza somo hili, tunataka kuendelea kusoma ndani ya kitabu cha Mwanzo na kuona ya kwamba **Mungu aliwapa Abrahamu na Sara mwana,** na **kutimiza ahadi** aliyotoa zamani sana. Ndani ya Mwanzo 21:1-7 tunasoma,

"Bwana akaangalia Sara sawasawa alivyosema, Bwana akafanyia Sara ***sawasawa alivyosema.*** *Sara akachukua mimba, akazalia*

Abrahamu mwana katika uzee wake, ***kwa wakati uliowekwa ambao Mungu alimwambia.*** *Abrahamu akaita jina la mwana wake aliyezaliwa kwake, ambaye Sara alimzalia, Isaka. Abrahamu akatahiri mwana wake Isaka wakati alipokuwa na siku nane sawasawa Mungu alivyomwagiza.* ***Abrahamu alikuwa na miaka mia moja*** *wakati mwana wake Isaka alipozaliwa kwake. Sara akasema: Mungu amenichekeza; kila mtu anayesikia atacheka pamoja nami. Akasema: Nani aliyeweza kumwambia Abrahamu ya kama Sara atanyonyesha watoto? Kwa maana nimemzalia mwana katika uzee wake."*

Hivi Mungu alitimiza ahadi aliyotolea Abrahamu na Sara miaka mingi mbele. Sara aliyejulikana kama mwanamke asiyeweza kuzaa, alizaa mwana **kama Mungu alivyosema**. Walimwita ***Isaka***, maana yake *anacheka*. Lakini si watu wote waliofurahia kuzaliwa kwa Isaka.

Maandiko yanasema:

(Mwanzo 21:8-14) *"Mtoto akakua, akaachishwa maziwa; Abrahamu akafanya karamu kubwa siku Isaka alipoachishwa maziwa. Sara akaona* ***mwana wa Hagari ambaye Mmisri alizalia Abrahamu akifanya zihaka.*** *Kwa hivi akamwambia Abrahamu: Fukuza kijakazi huyu na mwana wake; kwa maana mwana wa kijakazi huyu hatariti pamoja na mwana wangu, hata Isaka. Neno hili lilikuwa zito sana kwa macho ya Abrahamu kwa sababu ya mwana wake. Mungu akamwambia Abrahamu: Lisiwe zito kwa macho yako kwa sababu ya kijana na kwa sababu ya kijakazi wako, na kwa maneno yote ambayo Sara alikuambia usikilize sauti yake; kwa sababu katika Isaka uzao wako utaitwa. Na mwana wa kijakazi vilevile nitafanya taifa kwa sababu yeye ni uzao wako. Abrahamu akaamka asubui mapema, akatwaa mkate na chupa ya maji, akampa Hagari akimtia begani, na mtoto,* ***akamruhusu, akakwenda.***"

Ilikuwa nguvu sana kwa Abrahamu kutuma Isimaeli mbali naye, lakini ilikuwa neno la lazima, kwa sababu Mungu alikuwa amemfunulia ya kwamba taifa jipya, na Mwokozi wa dunia, watakuja kwa njia ya **Isaka**, si Isimaeli. Isimaeli aliyekuwa na miaka kumi na mitano alicheka Isaka na **aliona bule shauri la Mungu** kufanyiza Isaka kuwa taifa kubwa kwa njia yake watu wa dunia nzima wataweza kupata wokovu. Basi nini ilipata Isimaeli? Mashairi yanayofuata yanaonyesha ya kwamba alikwenda pamoja na mama yake kukaa jangwani karibu na Misri na alioa mwanamke Mmisri.

Isimaeli aligeuka baba ya taifa la Waarabu, waliogeuka adui za taifa lililozaliwa kwa njia ya Isaka, kama Mungu alivyojulisha Abrahamu mbele. (Ona Mwanzo 16:12.) Hata kufika sasa kuna uadui katikati ya Waarabu na Wayuda, kama sisi sote tunavyojua. Mungu anapenda Waarabu na Wayuda na watu wote wa dunia na anataka wageuke kwake.

Rafiki, tumefika kwa mwisho wa sura hii. Tunataraji ya kwamba umeona tena ya kwamba Mungu wa kweli aliye hai ni **Mungu mwaminifu** asiyeweza kukosa kutimiza Neno lake. Kwa sababu hii aliharibu Sodomo na Gomora—**kama alivyosema** atafanya. Na kwa sababu hii aliwapa Abrahamu na Sara mwana kwa uzee wao—kama alivyoahidi miaka mingi mbele. Na kwa sababu hii aliagiza Abrahamu kutuma Isimaeli pahali pengine **ili makusudi yake yasiyoweza kubadilika yaweze kutimizwa.**

~~~~~~~~~~~~~~

Katika Somo 22 tutasoma juu ya habari kubwa zaidi ndani ya maisha ya Abrahamu, namna alivyotoa mwana wake kuwa sadaka kwa Mungu.

Tunakuomba kukaa kuwaza sana juu ya shairi hili toka Maandiko Matakatifu:

> ***"Tazama namna ya utajiri wa akili na maarifa ya Mungu! Hukumu zake hazivumbulikani, na nia zake hazitafutikani!"***
>
> (Waroma 11:33)
~~~~~~~~~~~~~~

SOMO 22

SADAKA YA ABRAHAMU

MWANZO 22

Salama iwe kwako, Rafiki. Ndani ya masomo katika kitabu cha Mwanzo, tumeona maneno mengi ya maana sana juu ya nabii wa Mungu Abrahamu. Leo tutasoma mafundisho makubwa zaidi ya maisha ya Abrahamu, habari za **sadaka ya Abrahamu** na maana yake.

Katika somo la mbele tulijifunza ya kwamba Mungu aliwapa Abrahamu na Sara mtoto wakati walipokuwa wazee na kutimiza ahadi aliyotoa miaka mingi mbele. Jina la mwana wao lilikuwa Isaka. Mungu alikuwa ameahidi Abrahamu ya kwamba, kwa njia ya Isaka, ataanza taifa jipya na kwa njia ya taifa hili mataifa yote ya dunia watabarikiwa. Tuliona vilevile ya kwamba Isimaeli na mama yake, Hagari, waliondokea nyumba ya Abrahamu, wakakwenda kukaa katika inchi ya Misri. Hivi Isaka tu alibaki nyumbani mwa Abrahamu, yule aliyezaliwa kama Mungu alivyoahidi.

Siku moja Mungu aliagiza Abrahamu kufanya neno la kushangaza, neno gumu sana. Ndani ya sura 22 ya kitabu cha Mwanzo, kuanza na shairi 1 tunasoma,

> *"Na ilikuwa nyuma ya maneno haya Mungu akajaribu Abrahamu, akamwambia: Abrahamu; naye alisema: Mimi ni hapa. Akasema: Twaa sasa mwana wako, mwana wako wa pekee ambaye unampenda, hata Isaka, uende zako hata inchi ya Moria:* ***umtoe pale kwa sadaka ya kuteketezwa juu ya mmoja wa milima ambao nitakuambia****."* (mash.1,2).

Mungu aliomba Abrahamu kufanya nini? Aliagiza Abrahamu kupeleka mwana wake mpendwa kwa mlima wa mbali, na kumtoa pale kuwa sadaka ya kuteketezwa! Namna gani aliweza kutolea Abrahamu agizo namna hii? Abrahamu alikuwa amengoja miaka

mirefu 25 kupata mwana ambaye Mungu alikuwa ameahidi kumpa, na sasa Mungu alimwagiza kutoa mwana huyu kuwa sadaka! Abrahamu alijibu Mungu namna gani? Alibishana na masemo ya Mungu kwa sababu ilikuwa nguvu kwaye kukubali neno hili? Maandiko yanasema kwa Mwanzo 22:3:

> *"**Abrahamu akaondoka asubui mapema**, akatandika punda yake, akatwaa wawili wa vijana wake pamoja naye na Isaka mwana wake; akapasua kuni kwa sadaka ya kuteketezwa, **akaondoka, akakwenda kwa pahali Mungu alipomwambia."***

Kwa siku tatu, Abrahamu na mwana wake na watumishi wawili walitembea na miguu na walitembea na walitembea, kwendea mlima Mungu aliotaja. Roho ya Abrahamu ilikuwa karibu na kuvunjika wakati alipokuwa akikaribia pahali pale ambapo itampasa kuua mwana wake mpendwa na kumteketeza kuwa sadaka! Ndiyo, sisi tunaosoma habari hizi leo tunajua ya kwamba Mungu alikuwa akijaribu tu imani ya Abrahamu, lakini Abrahamu hakujua! Neno Mungu aliloomba kwake lilikuwa jaribu la kuogopesha na kuumiza roho sana!

Halafu Maandiko yanaendelea kusema kuanza na Mwanzo 22:4,

> "*Siku ya tatu Abrahamu akanyanyua macho yake, akaona pahali penyewe mbali. Abrahamu akamwambia vijana wake: Mukae hapa pamoja na punda, nami na kijana tutakwenda kule; na tutaabudu na kurudi tena kwenu. Abrahamu akatwaa kuni kwa sadaka ya kuteketezwa, akabebesha Isaka mwana wake; akashika moto na kisu mkononi mwake, wakakwenda pamoja wao wawili. Isaka akamwambia Abrahamu baba yake, akasema: Baba yangu; akasema: Mimi ni hapa, mwana wangu. Akasema: Tazama moto na kuni; lakini **wapi mwana-kondoo** kwa sadaka ya kuteketezwa? Abrahamu akasema: **Mungu atajipatia mwenyewe mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa**; basi wakakwenda pamoja, wao wawili.*
>
> *Wakafika kwa pahali Mungu alipomwambia. Abrahamu akajenga mazabahu pale, akatengeneza kuni, akafunga Isaka, mwana wake, akamweka juu ya mazabahu, juu ya kuni, Abrahamu akanyosha mkono wake, akatwaa kisu achinje mwana wake. Na malaika ya Bwana alimwita toka mbingu, akasema: Abrahamu, Abrahamu; naye alisema, Mimi ni hapa. Akasema: Usitie mkono juu ya kijana, wala usimfanyie kitu, kwa sababu sasa ninajua ya kwamba unaogopa*

Mungu, kwa sababu hukukataa kunipa mwana wako, mwana wako aliye wa pekee. Abrahamu akanyanyua macho yake, akaangalia na tazama, nyuma yake ***kondoo ndume amefungwa na pembe zake katika kichaka.*** *Abrahamu akakwenda, akatwaa kondoo ndume, akamtoa kwa sadaka ya kuteketezwa kwa pahali pa mwana wake.* ***Abrahamu akaita jina la pahali pale Yehova-Yire, kama inavyosemwa hata leo: Katika mlima wa Bwana itapatikana.***" (Mwanzo 22:4-14)

Haya ni mashairi makubwa sana na lazima tuyaeleze. Kwa kufahamu habari za sadaka ya Abrahamu, inatupasa kufahamu

1) neno lililotokea,
2) kama sadaka hii ilikuwa mfano wa nini, na
3) kama Abrahamu alitabiri nini juu ya neno litakalotokea kwa wakati wa kuja.

1) Tumesoma leo namna Mungu **alivyojaribu imani ya Abrahamu** na **kuponyesha mwana wake** toka mauti kwa njia ya sadaka ya kondoo ndume. Miaka karibu elfu ine imepita tangu wakati neno hili lilipotokea kwa pahali Yerusalema unaposimama sasa.

2) Habari hizi ni **mfano** kutuonyesha kweli tunayosoma ndani ya Neno la Mungu, ya kwamba **sisi sote ni kama mwana wa Abrahamu.** Tumesoma ya kwamba **Mungu mwenye haki, alihukumu mwana wa Abrahamu kufa.** Sisi sote tumehukumiwa kufa na tunastahili kupokea hukumu ya Mungu. Lakini tulisoma vilevile namna Mungu, kwa neema, alivyo**okoa mwana wa Abrahamu toka mauti.** Vivyo hivyo Mungu, kwa neema yake, amekuja kutuokoa sisi kwa njia ya kutayarisha njia kwa wokovu wetu. Njia ile ya wokovu ni nini? Habari za sadaka ya Abrahamu zinatufundisha ya kwamba **njia ya wokovu** inayosimamishwa na Mungu ni njia ya **Sadaka Kamilifu.**

Mungu alitayarisha kondoo ndume kufa kwa pahali pa mwana wa Abrahamu. Pembe zake tu zilifungwa katika kichaka; ngozi ya kondoo haikupasuliwa. Kama kondoo angalikuwa na kipunguo hata kimoja asingaliweza kukomboa mwana wa Abrahamu juu ya mazabahu. Lakini sadaka Mungu aliyotayarisha ilikuwa kondoo mkamilifu, bila kipunguo. Ndani ya mafundisho yetu kwa sura za kwanza za Mwanzo, tulijifunza juu ya njia ya wokovu ambayo Mungu alitayarisha. Unakumbuka kama ilikuwa nini? Wakati Adamu na Hawa walipokwisha kufanya zambi, Mungu aliamuru

kwamba malipo kwa zambi ni mauti, na ya kwamba hakuna usamehe kwa zambi bila kumwanga damu. Hivi, ilipasa watu wote waliotaka zambi zao kusamehewa **kukamata nyama asiyekuwa na kipunguo**, kumwua, na kumtolea Mungu kuwa sadaka ya kuteketezwa. Ile nyama isiyokuwa na kosa ilipaswa kufa kwa mwenye zambi. Kwa njia ile moja tu Mungu aliweza kusamehe zambi za wana wa Adamu, pamoja na kutimiza haki yake mwenyewe vilevile.

Kuna neno lingine ambalo inatupasa kukumbuka, ndilo hili: Maandiko yanasema ya kwamba nyama hizi zilikuwa **mfano** tu wa maneno yatakayotokea; "kivuli cha yale mema yatakayokuwa, **wala si sura yao yenyewe** ... maana haiwezekani kwa damu ya ngombe na mbuzi kuondoa zambi" (Waebrania 10:1,4) Haiwezekani kamwe kwa damu ya nyama kulipa kwa zambi kwa sababu thamani ya nyama si sawasawa na thamani ya mtu. Hivi tunajifunza ya kwamba ile kondoo ndume iliyokomboa mwana wa Abrahamu juu ya mazabahu **ilikuwa mfano wa sadaka kubwa kupita, na kamilifu kupita.** Neno la Mungu linaonyesha kwamba kondoo aliyekufa kwa pahali pa mwana wa Abrahamu ilikuwa **mfano wa Mkombozi mtakatifu** atakayekuja duniani na kufia **wenye zambi wote**, ili Mungu aweze kusamehe kila mtu ambaye anamwamini. Hii ndiyo maana ya mfano wa sadaka ya Abrahamu. Ni mfano wa Mwokozi ambaye Mungu aliahidi kutuma duniani kuokoa wenye zambi toka hukumu yake ya haki.

Kwa **maneno ya unabii**, unakumbuka neno Abrahamu alilosema na mwana wake wakati walipokuwa wakipanda mlima? Alisema naye: "***Mungu atajipatia mwenyewe mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa***." Na unakumbuka neno Abrahamu alilosema nyuma ya kuua kondoo ndume na kumteketeza kwa pahali pa mwana wake? Aliita pahali pale pa sadaka: "Yehova-Yire", maana yake "*Bwana **ata**patia...*" Kwa nini hakusema, "Mungu asifiwe! Bwana a**me**weka sadaka tayari!"? Rafiki, hili ni **ulizo kubwa sana**, kwa sababu jibu lake linatufunulia Habari Njema ya Neno la Mungu ambayo inatupasa sisi sote kufahamu na kuamini!

Kwa nini Abrahamu aliita pahali pale, "*Bwana **ata**patia...*"? Kwa sababu **Abrahamu alikuwa akitangaza habari za neno lingine litakalotokea juu ya milima ile ile** pahali kondoo alipokomboa mwana wake juu ya mazabahu. Kwa ufupi, Abrahamu alikuwa akitangaza: "Ninasifu Mungu kwa sababu alitupatia kondoo kukomboa

mwana wangu juu ya mazabahu. Lakini ninawaambia ninyi ya kwamba juu ya mlima huu tu **Mungu ataweka tayari sadaka nyingine** itakayokuwa sadaka kubwa zaidi kupita yule kondoo aliyeponyesha mwana wangu leo toka kisu na moto. Ndiyo, Sadaka ambaye Mungu ataweka tayari atakuwa na uwezo kuokoa wana wa Adamu toka mauti ya milele ndani ya moto usiozimika kamwe! Mungu atatuma Mkombozi mtakatifu atakayekufa kama sadaka, Yule asiyefanya zambi kwa ajili ya wenye hatia, ili mtu ye yote anayeamini asipote!" Hizi ndizo Habari Njema kwa watu wote ambazo Abrahamu alitangaza wakati aliposema, "*Mungu a**ta**jipatia mwenyewe **mwana-kondoo** kwa sadaka!*"

Mbele ya kumaliza habari za "Sadaka ya Abrahamu" leo, inatupasa sisi sote kujua ya kwamba **Mungu alitimiza unabii wa Abrahamu** karibu miaka elfu mbili nyuma ya wakati Abrahamu alipotabiri. Hatuwezi kusema maneno mengi juu yake leo, lakini wale katikati yenu munaojua *Injil*, ndiyo Habari Njema, mumejua habari za Mkombozi huyu. Munajua kwamba alizaliwa na bikira (msichana asiyelala na mwanamume) na alikuwa mzao wa Abrahamu na Isaka, kama Mungu alivyoahidi. Mkombozi atakayekufa kwa ajili ya wenye zambi hakuwa na baba ya dunia. Alitoka mbinguni na hivi hakuriti tabia ya zambi ya Adamu. Hakuwa na zambi; hakuwa na kipunguo. Kwa sababu hii alistahili kufa kama **Sadaka Kamilifu**, kama mkombozi wa wana wa Adamu wenye hatia! Wakati tutakapofundisha juu ya Habari Njema nyuma, tutajifunza kwamba jina la Mwokozi huyu alikuwa ***Yesu***. Maana ya jina hili Yesu ni ***Mungu anaokoa*.** Watu wengine wanaita Yesu "*Isa*." (Utaona zaidi juu ya neno hili ndani ya Kitabu 3, Somo 61.)

Wakati tutakapofikia vitabu vya Habari Njema (*Injil*) tutasoma juu ya nabii mmoja, jina lake Yoane (jina hili kwa Qur'an ni *Yahya*) aliyetumwa na Mungu kutayarisha njia mbele ya Yesu Mkombozi. Siku moja Yoane aliona Yesu akikaribia, akasema, *"Tazama **Mwana-kondoo** wa Mungu anayechukua zambi ya ulimwengu!"* (Yoane 1:29). Kwa nini nabii Yoane aliita Yesu *"Mwana-kondoo wa Mungu"*? Kwa sababu Yesu alizaliwa kumwanga damu yake kuwa sadaka inayoondoa zambi. **Kama kondoo aliyekufa kwa pahali pa mwana wa Abrahamu, vivyo hivyo Mkombozi alikuja kufa kwa ajili ya wazao wote wa Adamu**. Yesu ndiye Sadaka kamilifu na ya mwisho juu yake Abrahamu alitabiri wakati aliposema: "***Mungu atajipatia mwenyewe mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa.***"

Ndani ya Habari Njema tutasoma ya kwamba Yesu alijitoa na kutaka kwake mwenyewe kwa adui zake, na namna walivyomfunga kwa msalaba. **Yesu Mkombozi, ambaye Mungu alitoa, alitimiza unabii wa mfano huu wa kondoo ya sadaka ya Abrahamu.** Kwa sababu hii, mbele ya kufa kwake, Yesu alilalamika, ***"Imekwisha!"*** (Yoane 19:30). Na nyuma ya siku tatu Mungu alihakikisha ukamilifu na uwezo wa sadaka ya Mkombozi kwa njia ya kumfufua toka wafu! **Yesu tu alitimiza kabisa maana ya sadaka ya Abrahamu**. Ulijua ya kwamba pahali Yesu alipokufa kwa ajili ya wenye zambi ndipo kwa milima Abrahamu alipoua kondoo kwa pahali pa mwana wake? Unajua pahali penyewe? Ni kwa Yerusalema.

Rafiki, pahali po pote ulipo, Mungu anakuagiza kuachana na mawazo yako yasiyo sawa na kazi zako zisizo na faida, na kutumainia kabisa Sadaka kamilifu na ya mwisho aliyotayarisha. Maandiko yanasema: "*[Yesu Mkombozi] alichukua zambi zetu katika mwili wake juu ya mti, hata sisi, tukiwa wafu kwa maneno ya zambi, tuwe hai kwa maneno ya haki; na kwa kupigwa kwake muliponyeshwa,"* (1 Petro 2:24) Leo tuliona ya kwamba mwana wa Abrahamu alikubali sadaka Mungu aliyotayarisha kwa yeye. Basi wewe? **Umepokea Sadaka ambayo Mungu alitayarisha kwa wewe?**

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Mungu akubariki wakati unapowaza sana juu ya maana ya maneno Abrahamu aliyosema juu ya Mlima Moria,

> ***"Mungu atajipatia mwenyewe mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa ... Katika mlima wa Bwana itapatikana."***
>
> (Mwanzo 22:8,14)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

SOMO 23

ESAU NA YAKOBO

MWANZO 25

Salama iwe kwako. Mbele ya kuanza Somo 23 tunakusalimu tena kwa jina la Mungu wa salama, anayetaka watu wote kufahamu, kuamini na kupokea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele.

Ndani ya somo la mbele, tuliwaza juu ya **sadaka ya Abrahamu** {"Id al-Adha"}. Habari Njema {Injil} inajumlisha habari hizi hivi:

> *"Kwa imani Abrahamu, wakati alipojaribiwa, akatoa Isaka awe zabihu; na yeye aliyepokea ahadi, alikuwa akitoa mwana wake, mzaliwa wake wa pekee; ndiye yeye aliyeambiwa: Katika Isaka uzao wako utaitwa, akihesabu ya kuwa Mungu anaweza kumfufua toka wafu, akampata tena kama kwa mfano wa ufufuko."* (Waebrania 11:17-19)

Masomo matano yanayopita yalikuwa juu ya habari za maisha ya nabii Abrahamu. Kuna habari nyingi nyingine ndani ya Tora juu ya Abrahamu tusizoangalia kwa sababu hatuna saa kuzisoma zote. Lakini, mbele ya kuacha habari za Abrahamu na kuendelea na habari za wazao wake, sharti tujue juu ya neno moja lingine. Siku moja, Mungu alimwambia Abrahamu nini itapata wazao wake. Alisema naye:

> *"Jua kabisa ya kwamba uzao wako utakuwa* ***mgeni kwa inchi isiyo yake****, na watatumikia watu wale,* ***nao watawatesa kwa miaka mia ine; na vilevile nitahukumu taifa ambao watawatumikia; na nyuma watatoka na mali nyingi****."* (Mwanzo 15:13,14)

Na maneno haya Mungu alitangaza ya kwamba wazao wa Abrahamu watageuka watumwa katika inchi ya Misri. Mungu aliahidi vilevile ya kwamba nyuma ya miaka mia ine atawaokoa toka utawala wa watu wa Misri. Nyuma ya masomo mane mengine,

Mungu akitaka, tutaanza kuona kutimizwa kwa unabii huu, namna Mungu alivyomwambia Abrahamu.

Halafu ndani ya sura 25, Maandiko yanasema:

> *"**Abrahamu akampa Isaka vyote alivyokuwa navyo.** Na hizi ni siku za miaka ya maisha ya Abrahamu alizoishi, miaka mia moja makumi saba na mitano, Abrahamu akakata roho, mwenye uzee wema, mzee wa miaka mingi; akakusanyika kwa watu wake. Isaka na Isimaeli wana wake walimzika kwa pango la Makipela, shambani mwa Efuroni mwana wa Zohari Mhiti lililo mbele ya Mamure; shamba Abrahamu alilonunua kwa wana wa Heti; Abrahamu alizikwa pale na Sara mke wake."* (Mwanzo 25:5, 7-10).

Hivi, kwa mwisho wa maisha yake, Abrahamu, rafiki ya Mungu, alifika kwake Bwana ambaye alijua na kupenda.

Namna gani tunaweza kumaliza na kujumlisha somo letu juu ya Abrahamu, nabii wa Mungu? Labda na maulizo na majibu mawili. 1. **Kwa nini Mungu aliomba Abrahamu kuhama na kwendea inchi nyingine?** Jibu: Kwa sababu lilikuwa kusudi la Mungu kuanza taifa jipya toka Abrahamu, kwa njia yake Mwokozi atafika duniani. 2. Basi **kwa nini Mungu alihesabu Abrahamu kuwa mwenye haki na alimpokea kwake kwa milele?** Jibu: Kwa sababu Abrahamu aliamini maneno Mungu aliyosema hata kama ilikuwa nguvu kuyaamini. Abrahamu aliokolewa kwa njia ya imani ndani ya ahadi za Mungu, si kwa njia ya kazi zake mwenyewe. Hii ndiyo maana ya maneno ya Maandiko: *"Abrahamu **aliamini Mungu**, ikahesabiwa kwake kuwa ni haki; naye aliitwa rafiki ya Mungu."* (Yakobo 2:23)

Ndani ya sura 25 ya kitabu cha Mwanzo, Maandiko yanaendelea na habari za historia ya wazao wa Abrahamu. Tuendelee sasa ndani ya Tora na kujifunza habari za **Isaka na wana wake wawili waliokuwa mapacha**. Maandiko yanasema, kuanza na shairi 19:

> *"Na hivi ni vizazi vya Isaka, mwana wa Abrahamu: **Abrahamu** akazaa Isaka; na **Isaka** alikuwa na miaka makumi ine wakati alipooa **Rebeka**, binti ya Betueli, Msuria wa Padani-Aramu, ndugu ya Labani, Msuria. Isaka akaomba Bwana kwa sababu ya mke wake, kwa sababu alikuwa tasa; Bwana akamkubali, na Rebeka mke wake alichukua mimba. Watoto wakashindana pamoja ndani yake; naye alisema: Kama ni hivi, kwa nini ninaishi? Akakwenda kuuliza kwa Bwana. Bwana akamwambia: **Mataifa mawili** ni tumboni mwako,*

na watu namna mbili watatengwa tumboni mwako; kabila moja watakuwa hodari kuliko la pili; naye mkubwa atatumikia mdogo." (Mwanzo 25:19-23)

"Na wakati siku zake za kuzaa zilipotimia, tazama, ***mapacha*** *walikuwa tumboni mwake. Wa kwanza alitoka, mwekundu pia kama vazi la nyole; wakaita jina lake* ***Esau.*** *Na nyuma yake ndugu yake akatoka; na mkono wake ulikuwa umeshika kisigino cha Esau; jina lake likaitwa* ***Yakobo****; Isaka akakuwa na miaka makumi sita wakati alipowazaa. Vijana wakakua, Esau akakuwa fundi la kuwinda, mtu wa poli. Yakobo akakuwa mtu kimya akikaa hemani."* (Mwanzo 25:24-27)

Hivi tunaona ya kwamba Isaka na Rebeka walikuwa na wana mapacha, wakawaita **Esau** na **Yakobo**. Hata vijana walikuwa mapacha, walikuwa mbalimbali kwa desturi zao. Wakati Esau alipopata nguvu aliweka roho juu ya **vitu vya dunia** vilivyokuwa kwa wakati tu, lakini Yakobo aliweka roho juu ya **maneno ya Mungu** yaliyo kwa milele. Esau aliona bule ahadi ambazo Mungu alitolea Abrahamu, tata yake, na Isaka, baba yake, juu ya taifa litakalotoka kwao. Lakini Yakobo aliweka roho juu ya ahadi za Mungu.

Esau alikuwa mzaliwa wa kwanza. Hivi, kwa desturi ya watu, ingalimpasa yeye kupokea uriti wa mzaliwa wa kwanza na kugeuka baba ya taifa kubwa ambalo Mungu aliahidi kwa tata yake Abrahamu, na baba yake Isaka. Lakini hata mbele ya kuzaliwa kwa mapacha wale, Mungu alimwambia Rebeka, mama yao ya kwamba *"mkubwa atatumikia mdogo."* (Mwanzo 25:23) Mungu, anayejua mbele yote yatakayotokea kwa wakati wa kuja, alitangaza ya kwamba uriti wa mzaliwa wa kwanza na wazao wa taifa jipya watakuja **kwa njia ya Yakobo,** si kwa njia ya Esau. Basi ingalipasa Yakobo kungojea Mungu na kuacha mikononi mwake mwenye uwezo kumpa uriti ule kwa wakati wa kukubaliwa. Lakini, **Yakobo hakungojea Mungu.** Tusome sasa namna Yakobo alivyotenda kunyanganya uriti wa mkubwa wake Esau.

Maandiko Matakatifu yanasema ndani ya Mwanzo 25:29-34:

"Yakobo akapiga mchuzi wa nyama na mboga; Esau akarudi toka poli-ni, naye amechoka; Esau akamwambia Yakobo: Unilishe, ninakuomba, na mchuzi huu wekundu wa nyama na mboga; kwa sababu nimecho-ka; kwa hivi jina lake liliitwa Edomu. Yakobo akasema: Uniuzishe leo

haki ya mzaliwa wa kwanza. Esau akasema: Tazama, mimi ni karibu kufa; na ***haki ya mzaliwa wa kwanza itakuwa na faida gani kwangu?*** *Yakobo akasema: Uniapie leo; naye alimwapia; akauza haki yake ya mzaliwa wa kwanza kwa Yakobo. Yakobo akampa Esau mkate na mchuzi wa ndengu; akakula na kunywa, akasimama, akakwenda zake; ndivyo Esau alivyozarau haki yake ya mzaliwa wa kwanza."*

Unafahamu neno Esau alilofanya? Aliuza uriti wake wa mzaliwa wa kwanza kwa chakula kidogo! Zania mwenye mali mingi sana aliye na wana wawili. Mtu yule ana mashamba na nyumba, na vitu na mali nyingi. Ingepasa mzaliwa wake wa kwanza kuriti zaidi ya utajiri wake. Lakini siku moja, yule mzaliwa wa kwanza anarudi toka poli, anakuta mdogo wake akipika nyama na wali. Mzaliwa wa kwanza anasema na mdogo wake: "Ninakufa kwa njaa, unipe wali na nyama kidogo nipate kula!" Lakini mdogo anajibu, "Sitakupa bule, lakini unaweza kukinunua." Mkubwa anauliza, "Unaomba bei ngapi?" Mdogo anajibu, "Haki yako ya uriti wa mzaliwa wa kwanza." Mkubwa anajibu, "Ninakubali. Nina njaa zaidi hata kufa. Haki yangu ya mzaliwa wa kwanza ina faida gani kwangu?" Hivi mkubwa anatoa kiapo ya kwamba atampa mdogo wake uriti wake wote! Kisha mzaliwa wa kwanza anaketi, anakula na kunywa, anasimama na kwenda zake.

Tutasema nini juu ya mzaliwa huyu wa kwanza aliyebadilisha mashamba na nyumba, utajiri na amri kwa sahani ya nyama na wali? Tunaweza kusema neno moja tu: "**Mpumbavu.**" Kama mzaliwa huyu wa kwanza alivyozarau baraka za baba yake na utajiri wa dunia, vivyo hivyo **Esau alizarau baraka za Mungu na utajiri wa Milele.** Faida ya vitu ambavyo Esau alizarau zinapita mbali faida ya mali ya dunia, kwa sababu neno ambalo Esau alizarau lilikuwa haki ya kuwa ndani ya taifa lile jipya kwa njia yake Mwokozi wa dunia atakuja.

Mungu anataka kutufundisha nini leo kwa njia ya habari za Esau na Yakobo? Mungu anataka kutuonya tusitende kama Esau aliyebadilisha utajiri wa Milele kwa furaha za dunia zilizo kwa wakati tu. Sikiliza neno Bwana analosema juu ya neno hili:

"*Ni faida gani kama mtu akipata dunia nzima, na kupata hasara ya* ***uzima wake****? au mtu atatoa nini badala ya* ***uzima wake****?"* (Matayo 16:26) *". . . mukiangalia sana mtu asipungukie neema ya*

Mungu ... asiwe mwasherati au asiyeogopa Mungu, kama ***Esau aliyeuza uriti wake wa mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya chakula kimoja.*****"** (Waebrania 12:15,16)

Esau alikosa kupata neema ya Mungu kwa sababu alifikili maneno ya Mungu hayana faida. Hivi, Mungu anatuonya, akisema: Usitembee katika njia ya Esau! Usione bule baraka ambazo ninataka kupa.

Basi wewe unafikili nini? Unataka baraka za Mungu? Mungu anakupenda na anataka kukubariki sana, lakini sharti umpe pahali pa kwanza ndani ya maisha yako. Sharti Neno la Mungu liwe na faida kwako kupita chakula na mali. Halafu utaanza kufahamu maana ya shairi la Maandiko linalosema: ***"Jicho halikuona wala sikio halikusikia, wala hayakuingia katika moyo wa mtu maneno Mungu aliyotengenezea wenye kumpenda."*** (1 Wakorinto 2:9) Mungu anataka kutubariki sana. Anataka kusamehe zambi zetu zote, kugeuza mioyo yetu miovu, kutusafisha na kutujaza na mapendo, furaha, salama na matumaini yake. Na baraka hizi ni sehemu tu ya uriti ambao Mungu anataka kumpa kila mzao wa Adamu! Lakini sharti utafute kwanza mambo ya Milele **na moyo wako wote**. Mtu asiyetaka na roho yake yote kupokea baraka za milele za Mungu hatazipokea kamwe.

Unataka kupokea baraka za Mungu? Halafu inakupasa kufahamu maneno Mungu aliyoahidi ndani ya Neno lake. Unajua ahadi zake za ajabu, zilizo kubwa sana hata zinashinda ufahamu wa watu? Unazitunza? Au unatafuta maneno ya dunia tu? Neno la Mungu linatuonyeshea ya kwamba kuna watu namna mbili tu duniani: Wale **wanaothamini dunia** na kutafuta maneno ya dunia, na wale **wanaotaka sana mambo ya milele** na wanaoweka roho juu ya maneno ya juu. Wewe ni mtu wa namna gani?

Sikiliza maneno yanayoandikwa ndani ya Zaburi 1:

*"**Heri mtu yule** asiyekwenda katika shauri la waovu, wala haketi barazani mwa wenye kuzarau. Lakini furaha yake ni katika sheria ya Bwana; na katika sheria yake anawaza mchana na usiku. Atakuwa kama mti uliopandwa kando ya vijito vya maji, unaozaa matunda yake kwa wakati wake, wala majani yake hayakauki; na yote anayofanya yatabarikiwa. **Waovu si hivi;** lakini wao ni kama makanda yanayopeperushwa na upepo. Kwa hivi waovu hawatasimama katika*

hukumu, wala wenye zambi katika makutano ya wenye haki. Kwa kuwa Bwana anajua njia ya wenye haki; lakini njia ya waovu itapotea." (Zaburi 1:1-6).

Basi wewe? Unatembea ndani ya njia gani? Unakwenda katika njia ya wale **wanaotaka sana ahadi za Mungu**? Au wewe ni kama Esau **aliyebadilisha ahadi za Mungu** kwa vitu vya dunia vilivyo kwa muda mfupi tu? Neno la Mungu linatuonya, na kusema:

*"Ni faida gani kama mtu akipata **dunia nzima**, na **kupata hasara ya uzima wake**? au mtu atatoa nini badala ya uzima wake?"* (Matayo 16:26) *"Musifanye kazi kwa **chakula chenye kuharibika,** lakini **kwa chakula kinachodumu hata uzima wa milele**, ambacho Mwana wa watu atawapa ninyi, kwani huyu ndiye aliyetiwa mhuri na Baba."* (Yoane 6:27) *"... mukiangalia sana mtu asipungukie neema ya Mungu ... Asiwe ... asiyeogopa, kama Esau aliyeuza uriti wake wa mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya **chakula kimoja.**"* (Waebrania 12:15,16)

~~~~~~~~~~~~~~~

Tumefikia mwisho wa Somo 23. Ndani ya Somo 24, Mungu akitaka, tutaendelea ndani ya Tora na habari za Yakobo ...

Mungu akubariki wakati unapowaza sana juu ya maonyo haya toka Neno lake:

"... mukiangalia sana mtu asipungukie neema ya Mungu ... kama Esau aliyeuza uriti wake wa mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya chakula kimoja." (Waebrania 12:15,16)
~~~~~~~~~~~~~~~

SOMO 24

YAKOBO ANAGEUKA ISRAELI

MWANZO 28–32

Salama kwako, Rafiki. Leo tutasoma juu ya namna gani Yakobo alipata jina jipya.

Ndani ya somo la mbele, tulisoma juu ya mapacha ambao Isaka alizaa, **Esau na Yakobo.** Esau alizarau ahadi Mungu alizotoa kwa tata yake, Abrahamu, akabadilisha uriti wake wa mzaliwa wa kwanza kwa chakula! Lakini Yakobo aliheshimu ahadi za Mungu. Hata hivi Yakobo alianguka kwa njia nyingine vilevile! Maana ya jina lake ni mdanganyi. Halafu leo, tunakusudi kuendelea kusoma ndani ya Tora na kuona **namna Mungu alivyogeuza Yakobo—mdanganyi kuwa Yakobo—mtu wa Mungu.**

Basi Yakobo alikuwa mdanganyi kweli.. Maandiko hayafichi upungufu wa manabii na yanatujulisha namna Yakobo alivyodanganya mkubwa wake Esau mara mbili kwa kumnyanganyia haki yake ya mzaliwa wa kwanza. Kwa sababu hii Esau, akikasirika sana, alikusudi kuua mdogo wake. Hivi Rebeka, mama yao, aliita Yakobo kwa siri na kusema naye vizuri akimbie kwa mjomba wake Labani (ndugu ya Rebeka) aliyeishi kwa Harani, na kukaa pamoja naye kufika wakati gazabu ya ndugu yake Esau ilipokwisha kupoa.

Halafu sasa tusome ndani ya kitabu cha Mwanzo, sura 28, kuona nini ilipata Yakobo nyuma ya kuondokea nyumba ya baba yake Isaka na kuanza safari kwenda kwa nyumba ya mjomba wake Labani. Maandiko yanasema, kuanza na shairi 10 kufika shairi 19:

> "*Na Yakobo alitoka Beri-Seba, akakwenda Harani.* (Harani ndiyo inchi pahali Abrahamu alipokaa mbele ya kuitwa na Mungu.) *Akafika pahali pamoja, akalala pale usiku kwa sababu jua limeshuka; akatwaa moja la mawe ya pahali pale, akaliweka chini ya kichwa chake, akalala usingizi pale.*

Akaota, na tazama, ***kipandio kimesimamishwa juu ya inchi, na kichwa chake kilifika mbinguni;*** *na tazama malaika za Mungu wakipanda na wakishuka juu yake. Na tazama, Bwana akasimama juu yake, akasema:* ***"Mimi ni Bwana, Mungu wa Abrahamu baba yako, na Mungu wa Isaka. Inchi unayolala juu yake nitakupa wewe, na uzao wako****, na uzao wako utakuwa kama mavumbi ya inchi, na utaenezwa kwa mangaribi na kwa mashariki, na kwa kaskazini na kwa kusini; na ndani yako na ndani ya uzao wako jamaa zote za inchi watabarikiwa. Na tazama, mimi ni pamoja nawe na nitakulinda pahali gani unapokwenda, na nitakurudisha tena kwa inchi hii; kwa sababu* ***sitakuacha, hata nitakapokwisha kufanya yale ambayo nilikuambia."***

Yakobo akaamka toka usingizi wake, akasema: Hakika Bwana ni pahali hapa; wala sikujua. Akaogopa, akasema: Pahali hapa ni ma-ogopesho kabisa! hii si nyingine ila nyumba ya Mungu, na hili ni lango la mbingu. Yakobo akasimama asubui mapema, akatwaa jiwe alilloweka chini ya kichwa chake, akalisimamisha kama nguzo, akamwanga mafuta juu yake. Akaita jina la pahali pale Beteli [maana yake, "nyumba ya Mungu"]."

Hivi **Mungu** alionekana kwa **Yakobo** ndani ya ndoto na **kuahidi neno lile ambalo aliahidi** kwa tata yake **Abrahamu** na baba yake **Isaka**—ya kwamba atafanyiza wazao wake kuwa taifa kubwa. Hivi tunaona ya kwamba mwishoni Mungu alimpa uriti wa mzaliwa wa kwanza ambao Yakobo aliiba toka mkubwa wake. Yakobo hakustahili kuwa baba wa taifa jipya kwa njia yake Mkombozi atafikia dunia. Lakini, Mungu ni Mungu wa rehema na neema, ambaye anawapa wale wasiostahili mambo mema.

Yakobo aliona nini ndani ya ndoto yake? Maandiko yanasema aliona **kipandio** kilichosimamishwa juu ya inchi, na kichwa chake kilifika mbinguni na malaika za Mungu walikuwa wakipanda na wakishuka juu yake. Yakobo aliona **kipandio.** Kipandio Yakobo alichoona kilikuwa kipandio namna nyingine kabisa, kirefu sana, kilichofika hata **mbinguni toka inchi** na kuingia mbele ya Mungu!

Kwa njia ya ndoto hii ya kipandio kirefu, Mungu alionyesha Yakobo ya kwamba alitaka kuwa na ushirika wa karibu na mtamu sana naye. Mungu alitaka kumwonyesha vilevile ya kwamba **Mkombozi** atakayekuja duniani atakuwa kama **kipandio kile** kili-

chopita toka dunia hata mbinguni—**Mpatanishi katikati ya watu na Mungu.**

Hata kufika sasa, watu wengi wanafikili wanaweza kupanda na kuingia Paradiso kwa njia ya matendo mema yao wenyewe. Lakini, Neno la Mungu linatuambia ya kwamba kuna **"kipandio" kimoja tu katikati ya Mungu na mtu** na ya kwamba "kipandio" hiki hakitoki kwa watu lakini kwa Mungu. Sisi, wana wa Adamu, hatuwezi kwa nguvu yetu wenyewe kupanda na kutokea mbele ya Mungu. Kwa nini? Kwa sababu ya zambi zetu na kwa sababu tunakosa kabisa nguvu kupendeza Mungu Mtakatifu. Lakini Mungu, aliye mwenye rehema, kwa sababu ya mapendo yake makubwa kwa watu, ame-fungua njia ya wokovu kwa wazao wa Adamu.

Hivi kipandio Yakobo alichoona ndani ya ndoto zake ni mfano wa Mpatanishi ambaye Mungu aliahidi kutuma duniani kuokoa wenye zambi. Mpatanishi ni kama kipandio ambacho Yakobo aliona katika mbingu na dunia. Hii ndiyo maana ya mashairi haya ya Maandiko: *"Kwa sababu **Mungu ni mmoja tu, na mpatanishi katikati ya Mungu na watu ni mmoja**, yule mtu Kristo Yesu, ambaye alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote . . . ili kila mtu akimwamini asipotee, lakini apate uzima wa milele."* (1 Timoteo 2:5,6; Yoane 3:16) Neno la Mungu ni wazi kabisa. Hakuna mtu anayefika karibu na Mungu, ila kwa njia ya Mpatanishi mtakatifu aliyetumwa na Mungu toka mbinguni.

Sasa tuone nini ilitokea wakati Yakobo alipofika kwa nyumba ya mjomba wake. Neno la Mungu linasema ya kwamba *"yo yote mtu anayopanda, ndiyo atakayovuna."* (Wagalatia 6:7). Tumesikia mbele namna Yakobo alivyodanganya mkubwa wake. Sasa tutaona namna alivyodanyganywa na mjomba wake. Jina la mjomba wake lilikuwa Labani naye alikuwa mtu wa hila.

Tunasoma ndani ya sura 29 ya Mwanzo, kuanza na shairi 14:

> *"Labani [ndugu ya mama ya Yakobo] akamwambia [Yakobo]: Hakika wewe ni mfupa wangu na mwili wangu. Akakaa pamoja naye muda wa mwezi mmoja. Kisha Labani alimwambia Yakobo: Kwa sababu wewe ni ndugu yangu utanitumikia bule? Uniambie, mshahara wako utakuwa nini? Na Labani alikuwa na binti wawili: jina lake mkubwa lilikuwa Lea, na jina lake mdogo **Rakeli.** Na macho ya Lea yalikuwa zaifu; lakini Rakeli alikuwa mzuri sana na wa uso mzuri. Yakobo akapenda **Rakeli**; akasema: Nitakutumikia miaka saba kwa Rakeli,*

binti yako mdogo. Labani akasema: Afazali nikupe wewe kuliko mtu mwingine; kaa pamoja nami. Yakobo akatumika miaka saba kwa Rakeli; na ilikuwa kwake kama siku chache kwa mapendo ambayo alimpenda nayo.

*Yakobo akamwambia Labani: Unipe mke wangu, kwa maana siku zangu zimetimia, niingie kwake. Labani akakusanya watu wote wa pale, akafanya karamu. Na ilikuwa mangaribi akatwaa **Lea** binti yake, akamleta kwake; na aliingia kwake . . . Na ilikuwa asubui, tazama, alikuwa Lea; akamwambia Labani: Umenifanyia nini? Sikukutumikia kwa sababu ya Rakeli? Kwa nini basi umenidanganya? Labani akasema: Si desturi hapa kwetu kuleta mdogo aoane mbele ya mkubwa. Timiza juma la huyu vilevile na tutakupa mwingine vilevile kwa utumishi ambao utanitumikia miaka saba mingine. Yakobo akafanya hivi, akatimiza juma lake; akampa Rakeli binti yake kuwa mke wake. . . . Akaingia kwa Rakeli, akapenda Rakeli kuliko Lea, akatumika kwake [Labani] tena miaka saba mingine." (Mwanzo 29:14-30)*

Hivi tunaona namna Labani alivyodanganya mwana wa ndugu yake, ndiye Yakobo. Neno hili lililotukia halikuwa neno jema, lakini tunajua kabisa ya kwamba Mungu aliongoza maneno yote yaliyopata Yakobo na atatumika nayo kwa baraka ya Yakobo. Nyuma ya wakati Yakobo aligeuka baba ya **wana kumi na wawili**. Yakobo alikaa nyumbani mwa mjomba wake kwa miaka makumi mbili. Katika miaka ile yote, Mungu, mwenye mapendo, aliacha Yakobo kupatwa na mambo magumu sana, ili aweze kumfundisha na kusafisha imani yake, namna moto unavyosafisha zahabu.

Halafu siku ilifika wakati Mungu alipotokea Yakobo, akasema: *"Rudi kwa inchi ya baba zako na kwa jamaa zako; na nitakuwa pamoja nawe."* (Mwanzo 31:3) Hivi Yakobo alifunga vitu vyake, akakwenda zake pamoja na jamaa yake. Walikwenda kwa upande wa inchi ya **Kanana**—ndiyo inchi ambayo Mungu aliahidi kuwapa Abrahamu, Isaka, Yakobo na wazao wao.

Wakati Yakobo na jamaa yake walipokuwa wakikwenda Kanana, Mungu alitokea Yakobo tena, akageuza jina lake. Sikiliza maneno Maandiko yanayosema ndani ya sura 32, kuanza na shairi 24:

"Naye Yakobo aliachwa pekee; mtu akashindana naye hata mapambazuko. Na wakati alipoona ya kwamba hakumshinda, akagusa mvungu wa paja lake; mvungu wa paja la Yakobo ulishutushwa

> *wakati aliposhindana naye. Naye alisema: "Uniache kwenda, ni mapambazuko." [Yakobo] akasema: "Sitakuacha kwenda, ila utanibariki." Akamwambia: "Jina lako nani?" Naye alisema: "Yakobo." Akasema: "Jina lako halitaitwa tena Yakobo, lakini* ***Israeli****; kwa sababu umeshindana na Mungu, na watu, nawe umeshinda." Yakobo akamwuliza, akasema: "Uniambie, ninakuomba, jina lako." Akasema: "Kwa nini unauliza jina langu?" Akambariki pale. Yakobo akaita jina la pahali pale Penueli [maana yake "uso wa Mungu"]; kwa maana alisema, Nimeona Mungu uso kwa uso, na uzima wangu umeponyeshwa."* (Mwanzo 32:24-30)

Hizi ni habari za ajabu ambazo zinatufundisha maneno mengi. Tunaona Mungu akitokea kwa Yakobo kama mtu na kushindana naye. Alishindana na Yakobo kwa sababu gani? Kwa sababu alitaka Yakobo kufahamu uzaifu wake mbele ya Mungu. Bwana alitaka Yakobo kujua ya kwamba nguvu na akili yote ya kweli zinatoka kwa Mungu peke yake! Mungu alikuwa na mashauri mazuri sana kwa Yakobo, lakini **baraka nzuri zaidi toka Mungu ni kwa wale tu wanaofahamu ya kwamba hawawezi kupendeza Mungu kwa nguvu yao wenyewe**. Yakobo alikuwa akianza kufahamu uzaifu wake mwenyewe mbele ya Mungu. Usiku ule Mungu alimpa Yakobo jina jipya, ndilo **Israeli**. Maana ya Yakobo ni *mwenye kudanganya*. Lakini maana ya Israeli ni ***mwenye kutawala pamoja na Mungu***. Taifa jipya Mungu aliloahidi kusimamisha toka wazao wa Abrahamu, Isaka na Yakobo litaitwa Israeli. Unajua ya kwamba taifa la Israeli lilitoka kwa wana kumi na wawili wa Yakobo. Na Mkombozi alifika duniani kwa njia ya taifa la Israeli.

Labda wengine wanataka kuuliza: Kwa nini Mungu alichagua mdanganyi kama Yakobo na kumfanyiza baba ya taifa litakalozaa Mkombozi duniani? Sikia jibu la Maandiko Matakatifu:

> *"Mungu alichagua vitu vipumbavu vya dunia kupatiza wenye akili haya; na Mungu alichagua vitu zaifu vya dunia kupatiza vitu vya nguvu haya; na vitu vinyonge vya dunia, na vitu vinavyozarauliwa Mungu alichagua, na vitu visivyo kufanya vitu vilivyo viwe bule: kusudi* ***hata mwili mmoja usijisifu mbele ya Mungu.****"* (1 Wakorinto 1:27-29)

Yakobo alikuwa mdanganyi. Hakuweza kupendeza Mungu kwa nguvu yake mwenyewe. Hakuna kitu kizuri ndani yake, ila neno

moja: **Yakobo aliamini Neno la Mungu**. Yakobo aliweka roho sana juu ya ahadi za Mungu. Aliweka roho juu ya kupokea baraka ya Mungu kupita maneno yote mengine duniani. Kwa sababu hii Mungu alijifunua kwa Yakobo na kumbariki. Kwa sababu hii vilevile Mungu aligeuza moyo wa **Yakobo mdanganyi**, kuwa **Israeli, mtu wa Mungu**.

Basi wewe? Kama Yakobo, umefahamu ya kwamba huwezi kupendeza Mungu kwa nguvu yako mwenyewe? Sikiliza maneno Maandiko Matakatifu yanayosema juu ya neno hili:

> *"Heri walio **masikini wa roho**: maana ufalme wa mbinguni ni wao."* (Matayo 5:3). *"Mungu anashindana na wenye kiburi, lakini anawapa wanyenyekevu neema. **Mujinyenyekeze basi chini ya mkono wa uwezo wa Mungu, ili awatukuze ninyi kwa wakati wake."*** (1 Petro 5:5,6)

~~~~~~~~~~~~~~~

Ndani ya somo la nyuma tutaanza kusoma habari za ajabu za Yosefu, mmoja wa wana wa Yakobo ...

Mungu akubariki. Tunakuacha na shairi hili toka Neno la Mungu:

> ***"Na hivi basi Bwana atangoja, ili apate kuwahurumia ninyi, na hivi atatukuzwa apate kuwarehemu ninyi; kwa maana Bwana ni Mungu wa hukumu; heri wote ambao wanamngojea."***
>
> (Isaya 30:18)
~~~~~~~~~~~~~~~

SOMO 25

AIBU YA YOSEFU

MWANZO 37–39

Salama iwe kwako, Rafiki. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuendelea na somo lingine leo ndani ya mfulizo *Njia ya Haki* ndani yake tunapasha habari za Manabii wa Mungu, mmoja mmoja. Tutakaa kusoma ndani ya sehemu ya kwanza ya Neno la Mungu linaloitwa ***Tora*** vilevile.

Ndani ya somo la mbele, tulijifunza juu ya nabii wa Mungu Yakobo, mwana wa mwana wa Abrahamu. Tuliona ya kwamba Mungu alimpa Yakobo jina jipya: **Israeli**. Maana ya Yakobo ni *mdanganyi*, lakini maana ya Israeli ni *mmoja anayetawala pamoja na Mungu*. Sasa Mungu alikuwa na majina mawili: Yakobo na Israeli. Israeli ni jina la taifa jipya vilevile ambalo Mungu aliahidi kufanya toka Abrahamu, Isaka na Yakobo. Yakobo alikuwa na wana kumi na wawili. Waisraeli walitoka kwa wana hawa kumi na wawili — ndilo taifa kwa njia yake Mkombozi atakuja.

Unajua majina ya **wana kumi na wawili wa Yakobo**? Walikuwa Rubeni, Simeoni, Lawi, Yuda, Zebuluni, Isakari, Dani, Gadi, Aseri, Nafutali, Yosefu na Benyamina. Leo tutaanza habari za kupendeza mno za wana wa Yakobo — zaidi juu ya mmoja wao, jina lake **Yosefu**, aliyekuwa mwana wa kumi na mmoja. Sasa tuendelee na habari za ajabu za Yosefu!

Tusome toka kitabu cha Mwanzo, sura 37. Maandiko yanasema kuanza na shairi 2:

> *"Hivi ni vizazi vya Yakobo.* ***Yosefu akiwa na miaka kumi na saba****, alikulisha kondoo pamoja na ndugu zake . . . Na Yosefu alileta habari zao mbaya kwa baba yao. Na Israeli alipenda Yosefu kuliko wana wake wote kwa sababu alikuwa mwana wa uzee wake; akamfanyia vazi la rangi mbalimbali.* ***Ndugu zake*** *wakaona ya kama*

*baba yao alimpenda kuliko ndugu zake zote; **wakamchukia**, wala hawakuweza kusemezana naye kwa salama.*

*5 Yosefu akaota **ndoto**, akaipasha kwa ndugu zake, wakazidi kumchukia. Akawaambia: Sikieni, ninawaomba ninyi, ndoto hii niliyoota; tazameni, tulikuwa tukifunga miganda shambani na tazama, mganda wangu ukaondoka, ukasimama, vilevile; na tazameni, miganda yenu ilizunguka iliinama mbele ya mganda wangu. Ndugu zake wakamwambia: Wewe utatutawala sisi? au kweli utakuwa na amri juu yetu? Wakazidi kumchukia kwa sababu ya ndoto zake, na kwa masemo yake.*

*9 Akaota tena ndoto nyingine, akaipasha kwa ndugu zake, akasema: Tazameni, nimeota ndoto nyingine; na tazameni, jua na mwezi na nyota kumi na moja zikainama mbele yangu. Akaipasha kwa baba yake na kwa ndugu zake; baba yake akamhamakia, akamwambia: Nini ndoto hii uliyoota? **Mimi na mama yako na ndugu zako tutakuja kweli kuinama mbele yako kwa udongo?** Ndugu zake wakamwona kwa wivu; lakini baba yake alichunga neno hili moyoni mwake.*

*12 Ndugu zake walikwenda Sekemu kulisha kondoo za baba yao. Israeli alimwambia Yosefu: Ndugu zako hawakulishi kondoo kwa Sekemu? **Kuja, nitakutuma karibu nao**. Akamwambia: Mimi hapa. Akamwambia: Kwenda sasa uone kama ndugu zako ni vizuri na kama kondoo ni vizuri; na uniletee habari.*

*17 ... Yosefu akafuata ndugu zake, akawakuta kwa Dotana. Wakamwona mbali, na mbele ya kufika karibu nao, **wakafanya shauri kumwua**. Wakasemezana wao kwa wao: Tazama, bwana wa ndoto anakuja. Basi kujeni tumwue, na tumtupe ndani ya moja la mabirika na tutasema: Nyama ya mwitu amemkula; na tutaona nini itakayokuwa ya ndoto zake. Rubeni akasikia, akamponyesha toka mikono yao; akasema: Tusiondoshe uzima wake. Rubeni akawaambia: Musimwange damu; mumtupe ndani ya birika lililo jangwani; lakini musimtie mkono; hata amponyeshe katika mikono yao na kumrudisha kwa baba yake.*

*23 Na ilikuwa wakati Yosefu alipokuja kwa ndugu zake, **wakaondolea Yosefu vazi lake**, vazi la rangi mbalimbali alilovaa; **wakamtwaa** na kumtupa ndani ya birika, na birika lilikuwa bule, maji hayakuwa ndani yake. Wakaketi kula chakula; wakanyanyua macho yao, wakaangalia, na tazama, kundi la wafanyaji biashara wa*

Waisimaeli walikuja toka Gileadi pamoja na ngamia zao, wakibeba manukato na zeri na manemane, wakisafiri kushuka nazo hata Misri. Yuda akawaambia ndugu zake: Ni faida gani kwa sisi kuua ndugu yetu na kuficha damu yake? Kujeni tumwuze kwa Waisimaeli, wala mkono wetu usiwe juu yake kwa sababu yeye ni ndugu yetu, na mwili wetu. Ndugu zake wakamsikia. Wamidiani wakapita, wafanyaji biashara; wakavuta, wakapandisha Yosefu toka birika, ***wakauza Yosefu*** *kwa Waisimaeli kwa vipande makumi mbili vya feza. Wakaleta Yosefu kwa Misri.*

29 Rubeni akarudi kwa birika, na tazama, Yosefu hakuwa ndani ya birika; akapasua mavazi yake. Akarudi kwa ndugu zake, akasema: mtoto hayuko; nami nitakwenda wapi? Wakatwaa vazi la Yosefu, wakaua mbuzi ndume, wakatia vazi ndani ya damu; wakatuma vazi la rangi mbalimbali, wakalileta kwa baba yao, wakasema: Tumekuta hili; tambua sasa kama ni vazi la mwana wako au sivyo. Akalitambua, akasema: Ni vazi la mwana wangu; nyama mbaya amemkula; hakika Yosefu amepasuliwa vipande vipande. ***Yakobo akapasua mavazi yake, akavaa gunia viunoni, akaombolea mwana wake siku nyingi.*** *Wana wake wote na binti zake zote wakaondoka kumfariji; lakini alikataa kufarijiwa; akasema: Hapana, nitashuka kwa kaburi karibu na mwana wangu nikiomboleza. Baba yake akamlilia."*

(Mwanzo 39:1) *Na Yosefu* ***aliletwa chini kwa Misri****; Potifari, akida la Farao, mkubwa wa walinzi, Mmisri, akamnunua kwa mkono wa Waisimaeli walioshuka naye kule.* ***Bwana akakuwa pamoja na Yosefu****, naye alikendelea vizuri; akakuwa nyumbani mwa bwana wake Mmisri. Bwana wake akaona ya kama Bwana alikuwa pamoja naye, na ya kama Bwana alibariki maneno yote aliyofanya mkononi mwake. Yosefu akapata neema kwa macho yake, naye alimtumikia; akamweka msimamizi juu ya nyumba yake, na vitu vyote alivyokuwa navyo alitia mkononi mwake. Na ilikuwa toka wakati alipomweka msimamizi nyumbani mwake, na juu ya yote aliyokuwa nayo, Bwana akabariki nyumba ya Mmisri kwa ajili ya Yosefu; baraka ya Bwana ilikuwa juu ya vyote alivyokuwa navyo, nyumbani na shambani. Akaacha yote aliyokuwa nayo mkononi mwa Yosefu; wala hakujua kitu alichokuwa nacho ila chakula alichokula. Na Yosefu alikuwa mzuri, mwenye uso mzuri.*

7 Na ilikuwa nyuma ya maneno haya, mke wa bwana wake akaangalia Yosefu; akasema: Lala nami. Lakini yeye alikataa, akamwa-

mbia mke wa bwana wake: Tazama, bwana wangu hajui iliyo pamoja nami nyumbani, naye ameweka yote aliyo nayo mkononi mwangu. Hakuna mtu aliye mkubwa kuliko mimi nyumbani hii; wala hakunikataza kitu ila wewe, kwa sababu wewe ni mke wake; basi ***nitafanya uovu mkubwa huu namna gani, na kukosea Mungu?*** *Na ilikuwa wakati aliposemezana na Yosefu kila siku, hakumsikia alale naye wala kuwa pamoja naye.*

11 Na ilikuwa kwa wakati huu, akaingia nyumbani kufanya kazi yake, wala hakuna mtu wa watu wa nyumba aliyekuwa nyumbani. Akamshika kwa nguo yake, akasema: Lala nami: akaacha nguo yake mkononi mwake, akakimbia inje, akaita watu wa nyumba yake, akasema nao akisema: Tazameni, ameleta Mwebrania kwetu kutuzihaki; ameingia kwangu kulala pamoja name, na nililia kwa sauti nguvu; na ilikuwa wakati aliposikia ya kama nilipaza sauti yangu na kulia, akaacha nguo yake kwangu, akakimbia, akatoka inje.

16 Akaweka nguo yake karibu naye hata mume wake alipokuja nyumbani. Akamwambia sawasawa na maneno haya akisema: Mtumishi Mwebrania ambaye ulimleta kwetu, aliingia kwangu kunizihaki; na ilikuwa wakati niliipopaza sauti yangu na kulia, akaacha nguo yake kwangu, akakimbia inje. Na ilikuwa wakati mume wake aliposikia maneno ambayo mke wake alimwambia akisema: Mtumishi wako amenifanyia kwa namna hii, kasirani yake iliwaka. Bwana wa Yosefu akamtwaa, akamweka kwa mnyororo, pahali wafungwa wa mfalme walipofungwa; akakuwa pale katika mnyororo. Lakini Bwana alikuwa pamoja na Yosefu, akamwonyeshea wema, akampa ukubali kwa macho ya mlinzi wa mnyororo. Mlinzi wa mnyororo akaweka wafungwa wote waliokuwa katika mnyororo mkononi mwa Yosefu; na yote waliyofanya pale, ndiye aliyafanya. Wala mlinzi wa mnyororo hakuangalia neno lililokuwa mkononi mwake, kwa maana ***Bwana alikuwa pamoja naye; na yote aliyofanya, Bwana aliyabariki.”***

Huu ndio mwanzo wa habari za Yosefu, mwana wa Yakobo. Tunaweza kujumlisha maneno tuliyoona leo hivi: **Yosefu alipenda haki na kuchukia uovu.** Alitaka kuteswa gerezani kupita kujifurahisha na zambi zilizo kwa wakati tu. Kwa sababu hii, wakati mke wa bwana wake alipomwomba kulala naye na kufanya uzini, Yosefu alikataa, akijibu: “Nitafanya uovu mkubwa huu namna gani na kukosea Mungu?”

Yosefu alijua ya kwamba mtu hawezi **kutumikia Mungu na zambi pamoja**! Alikuwa amejitoa mzima kwa Mungu. Kwa sababu hii alipenda haki na kuchukia uovu. Kama tata yake Abrahamu, **Yosefu aliamini vilevile ahadi za Mungu juu ya Mwokozi** atakayekuja duniani kufa kwa zambi za wazao wa Adamu. Mungu alihesabu Yosefu kuwa haki kwa sababu Yosefu **aliamini** neno la Mungu. Kwa sababu ya imani yake, Mungu alisamehe zambi za Yosefu na alijaza moyo wake na uwezo kushinda zambi na kuishi maisha ya haki katika dunia yenye kujaa uovu.

Mungu "alitembea" pamoja na Yosefu kwa sababu Yosefu "alitembea" pamoja na Mungu. Yosefu hakuweza kufurahia zambi kwa sababu alipenda Mungu na roho yake yote. Mtu yule anayeamini na kuabudu Mungu na roho ya kweli **anapenda maneno Mungu anayopenda na kuchukia maneno Mungu anayochukia.** Hii ndiyo maana ya Maandiko Matakatifu ndani ya Matayo 6:24:

> ***"Hakuna mtu anayeweza kutumikia bwana wawili:*** *kwa maana atachukia mmoja, na kupenda mwingine; au atashikamana na mmoja, na kuzarau mwingine."* Na kwa 2 Wakorinto 6:14 tunasoma: *"Kwa maana shirika gani ni katikati ya* ***haki*** *na* ***uovu****? Au upatano gani ni katikati ya* ***nuru*** *na* ***giza****?"* Na 1 Yoane 1:5,6 yanasema: *"Mungu ni* ***nuru****, wala* ***giza si ndani yake*** *kabisa. Kama tukisema ya kwamba tunashirikiana naye, tena tukitembea katika giza, tunasema uwongo, wala hatufanyi yaliyo kweli."*

Wale walio watu wa Mungu kweli wanaamini Neno la Mungu na wanajaribu kumtii. Lakini wale wasio watu wa Mungu wanatawaliwa na zambi. Labda **wana*onekana* kama watu wa dini**, lakini **zambi inatawala** mawazo yao, na makusudi ya mioyo yao, masemo na matendo yao. Labda wanakusudi kushinda zambi, lakini hawawezi kufanya hivi, kwa sababu **zambi ina nguvu zaidi**. Wanakosa **uwezo wa Roho Mtakatifu wa Mungu** ndani ya mioyo yao, ambaye Mungu anawapa wote wanaoamini Neno lake na kupokea njia ya wokovu aliyotayarisha.

Wewe msomaji, Mungu amefanyiza moyo wako mpya kwa uwezo wake? Umepokea **Habari Njema** juu ya Mwokozi aliye na uwezo kusafisha moyo wako toka zambi? Au unatawaliwa na zambi hata sasa? Maandiko yanasema: *"****Karibieni Mungu, naye atawakaribia ninyi.*** *Takaseni mikono yenu, ninyi wenye zambi, na*

safisheni mioyo yenu, ninyi wenye mioyo miwili . . . Mujinyenyekeze mbele ya Bwana, naye atawanyanyua ninyi." (Yakobo 4:8,10)

~~~~~~~~~~~~~~

Kwa somo la nyuma, Mungu akitaka, tutaendelea na habari za Yosefu na kuona namna alivyotoka gerezani na kugeuka mtawala wa inchi nzima ya Misri...

Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya shairi hili ndani ya Maandiko Matakatifu:

> ***"Mungu ni nuru, wala giza si ndani yake kabisa. Kama tukisema ya kwamba tunashirikiana naye, tena tukitembea katika giza, tunasema uwongo wala hatufanyi yaliyo kweli."***
>
> (1 Yoane 1:5,6)
~~~~~~~~~~~~~~

SOMO 26

YOSEFU ANATUKUZWA

MWANZO 40–42

Salama iwe kwako, Rafiki, salama ya kweli toka Mungu, Bwana wa salama, anayetaka ufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo amekutayarishia.

Ndani ya somo letu la mbele, tulianza kujifunza juu ya Yosefu, aliye mwana wa kumi na mmoja wa wana kumi na wawili wa Yakobo. Tulisoma namna Yosefu alivyoota ya kuwa ndugu zake watainama mbele yake siku nyingine. Ndugu za Yosefu hawakumwamini. Lakini leo tutaona namna **Mungu alivyotimiza ndoto ya Yosefu** na kufanyiza wana wa Yosefu kuja na kupiga magoti mbele yake.

Kama tulivyojifunza, ndugu za Yosefu, wakubwa wao, walimchukia na kumtesa kwa sababu ya ndoto zake. Kwa sababu ya kasirani na wivu wao, walimwuza kuwa mtumwa kwa wafanya biashara waliokuwa wazao wa Isimaeli. Waisimaeli walipeleka Yosefu hata Misri na kumwuza kwa mtumishi wa Farao, mfalme wa Misri. Lakini Yosefu alikuwa mtumishi mwaminifu na mwenye kutenda kwa haki ndani ya kazi yake, kwa sababu **alitembea pamoja na Mungu**. Yosefu alionekana mzuri sana vilevile, na neno hili liliamsha tamaa ndani ya mke wa bwana wake, alitaka kulala naye. Lakini Yosefu alikataa, akajibu mwanamke, "*Nitafanya uovu mkubwa huu namna gani, na kukosea Mungu?*" Wakati Yosefu alipokataa kuzini naye, mwanamke alimshitaki kwa mume wake naye alimfunga gerezani. Lakini kwa macho ya Yosefu kwenda gerezani ilikuwa vizuri kupita kujifurahisha na furaha za zambi kwa muda mfupi. Yosefu aliweka Mungu kwanza ndani ya maisha yake. Alibaki gerezani kwa miaka miwili, lakini Mungu hakumsahau.

Halafu sasa, tuendelee kusoma ndani ya Tora na kuona namna Mungu alivyogeuza hali ya Yosefu. Tutasoma ndani ya Mwanzo sura 41, kuanza na shairi la kwanza:

> *"Na ilikuwa kwa mwisho wa miaka miwili mizima,* ***Farao*** [mfalme wa Misri] ***akaota****; na tazama, alisimama kando ya mto. Na tazama, wakatoka katika mto ngombe saba wazuri na wanono, wakajikulisha katika manyasi. Na tazama, ngombe wengine saba wakapanda nyuma yao toka mto, wabaya nao wamekonda, wakasimama kando ya ngombe wengine kwa ukingo wa mto. Ngombe wabaya na wa kukonda wakakula ngombe saba wazuri na wanono. Basi Farao akaamka.*
>
> *5 Akalala usingizi, akaota mara ya pili. Na tazama, masuke saba ya nafaka yakakomea kwa ubua mmoja, makubwa na mazuri. Na tazama, masuke saba, membamba yaliyopigwa kwa upepo wa mashariki yakakomea nyuma yao. Masuke membamba yakameza masuke saba makubwa yaliyojaa. Farao akaamka, na tazama, ilikuwa ndoto. Na ilikuwa asubui roho yake ikafazaika; wakatuma kuita wachawi wote wa Misri, na wote wenye akili wake; Farao akawaambia ndoto yake, lakini hakuna aliyeweza kutafsiria Farao.*
>
> *9 Kisha mkubwa wa wanyweshaji akasema na Farao akisema: Ninakumbuka makosa yangu leo. Farao akakasirikia watumishi wake sana, akanitia kulindwa nyumbani mwa jemadari wa walinzi, mimi na mkubwa wa waokaji; na usiku mmoja tuliota ndoto, mimi naye. Tukaota kila mtu kwa tafsiri ya ndoto yake. Na kijana mmoja alikuwa pamoja nasi, Mwebrania, mtumishi wa jemadari wa walinzi; tukamwambia, akatutafsiria ndoto zetu; akatafsiria kila mtu sawasawa na ndoto yake. Na ilikuwa sawasawa alivyotafsiria, ndivyo ilivyotokea; mimi nilirudishwa kwa kazi yangu, naye alitundikwa.*
>
> *14 Halafu* ***Farao akatuma, akaita Yosefu****, wakamleta upesi toka mnyororo; akajinyoa, akabadilisha vazi lake, akaingia kwa Farao. Farao akamwambia Yosefu: Nimeota ndoto, wala hakuna mtu kuitafsiri; na nimesikia juu yako ya kama wewe ukisikia ndoto unaweza kuitafsiri. Yosefu akajibu Farao, akisema:* ***"Si mimi; Mungu atampa Farao jibu la salama****."*

Halafu Farao alimwambia Yosefu ndoto yake. Kisha alisema na Yosefu,

> *24 "... na niliipasha kwa wachawi; lakini hakuna aliyeweza kunielezea. Yosefu akamwambia Farao: Ndoto ya Farao ni moja; Mungu*

ameelezea Farao atakayofanya nyuma kidogo. Ngombe saba wazuri ni miaka saba, na masuke saba mazuri ni miaka saba; ndoto ni moja. Na ngombe saba za kukonda na wabaya waliopanda nyuma yao ni miaka saba, na masuke saba matupu yaliyopigwa na upepo wa mashariki; haya ni miaka saba ya njaa. Hili ni neno ambalo nilimwambia Farao; Mungu amemwonyeshea Farao atakayofanya bado kidogo. Tazama, ***miaka saba ya kushiba sana*** *inakuja katika inchi nzima ya Misri; na nyuma yao* ***miaka saba ya njaa*** *itatokea; na kushiba kwote kutasahauliwa katika inchi ya Misri; na njaa itaharibu inchi; wala kushiba hakutatambuliwa inchini kwa sababu ya njaa inayofuata, kwa sababu itakuwa nzito sana. Na kwa ndoto ya Farao kurudi mara mbili, ni kwa sababu neno hili linasimamishwa na Mungu, na Mungu atalifanya bado kidogo. Kwa hivi Farao ajitazamie mtu wa akili na hekima amweke juu ya inchi ya Misri. Farao afanye hivi na kuongeza wasimamizi juu ya inchi, na sehemu tano ya mavuno ya inchi ya Misri itwaliwe miaka saba ya kushiba. Wakusanye chakula chote cha miaka mizuri hii inayokuja, na kuweka nafaka chini ya mkono wa Farao kwa chakula mijini, na kuichunga. Na chakula kitakuwa akiba inchini kwa mwaka saba ya njaa itakayokuwa katika inchi ya Misri; inchi isiharibiwe kwa njaa.*

37 Na neno hili lilikuwa jema kwa macho ya Faao na kwa macho ya watumishi wake wote. Farao akawaambia watumishi wake: ***Tunaweza kupata mwingine kama huyu, mtu mwenye roho ya Mungu?*** *Farao akamwambia Yosefu: Ikiwa Mungu amekufahamisha maneno haya yote, hakuna mwingine mwenye akili na hekima kama wewe; utakuwa juu ya nyumba yangu, na kwa kinywa chako watu wangu wote watatawaliwa. Kwa kiti cha enzi tu nitakuwa mkubwa kupita wewe.*

41 ***Farao akamwambia Yosefu: Tazama, nimekuweka juu ya inchi nzima ya Misri****. Farao akaondosha pete yake mkononi mwake, akaitia mkononi mwa Yosefu, akamvalisha na mavazi ya kitani nzuri, akamtia mkufu wa zahabu shingoni, akampandisha kwa gari la pili alilo nalo, wakalia mbele yake: Pigeni magoti; akamweka juu ya inchi nzima ya Misri. Farao akamwambia Yosefu: Mimi ni Farao, na pasipo wewe mtu hatanyanyua wala mkono wala mguu katika inchi yote ya Misri.*

45 Farao akaita jina la Yosefu ***Zafenati-Panea****; {maana yake* ***Mlinzi wa Uzima****] . . . Yosefu alikuwa na miaka makumi tatu*

wakati aliposimama mbele ya Farao, mfalme wa Misri. Yosefu akatoka mbele ya uso wa Farao, akapita katika inchi yote ya Misri. Na katika miaka ile saba inchi ikazaa kwa wingi. Akakusanya chakula chote cha miaka saba iliyo kwa inchi ya Misri, akaweka chakula katika miji, chakula cha mashamba yaliyozunguka kila mji, akaweka kwa mji ule. Yosefu akaweka nafaka kama mchanga wa bahari, nyingi sana, hata aliacha kuihesabu . . .

53 Na miaka saba ya kushiba iliyokuwa katika inchi ya Misri ilikwisha. Miaka saba ya njaa ilianza kuja sawasawa Yosefu alivyosema, na njaa ilikuwa katika inchi yote; lakini chakula kilikuwa katika inchi yote ya Misri. Na wakati inchi yote ya Misri ilipoona njaa, watu wakalia mbele ya Farao kwa vyakula. Farao akawaambia Wamisri wote: Kwendeni kwa Yosefu; neno ambalo anawaambia ninyi, fanyeni. Na njaa ilikuwa katika dunia yote; Yosefu akafungua nyumba zote alipoweka nafaka, akauza kwa Wamisri; na njaa ilikuwa nzito katika inchi ya Misri. Na ***inchi zote zilikuja kwa Yosefu kununua nafaka****, kwa sababu njaa ilikuwa nzito duniani pia.*

(Mwanzo 42:1) Yakobo (baba ya Yosefu na ndugu zake) akaona ya kama nafaka ilikuwa kwa Misri, akawaambia wana wake: Kwa nini munatazamana? Akasema: Tazameni, nimesikia ya kama nafaka ni kwa Misri; shukeni mutununulie toka kule; tuishi wala tusife. ***Ndugu kumi za Yosefu wakashuka kununua nafaka toka Misri****. Lakini Yakobo hakutuma Benyamina ndugu ya Yosefu pamoja na ndugu zake; kwa sababu alisema: hasara isimpate. Wana wa Israeli wakakuja kununua katikati yao waliokuja; kwa maana njaa ilikuwa katika inchi ya Kanana.*

6 Yosefu alikuwa mtawala juu ya inchi; alikuwa yeye aliyeuza kwa watu wote wa inchi; ndugu za Yosefu wakakuja, ***wakainama mbele yake*** *na nyuso zao hata udongo. Yosefu akaona ndugu zake, akawatambua, lakini akajifanya mgeni kwao. Akasemezana nao kwa maneno makali; akawaambia: Mumetoka wapi? Wakasema: Toka inchi ya Kanana kununua chakula.* ***Yosefu alitambua ndugu zake, lakini wao hawakumtambua. Yosefu akakumbuka ndoto alizoota juu yao****.* (Mwanzo 42:1-8)

Unafahamu maneno yaliyotokea? Tunaona ndugu wakubwa wa Yosefu wakiinama mbele ya mdogo wao Yosefu, namna alivyoota zamani! Yosefu huyu ambaye walimchukia, na kutaka kumwua—

ndiyo, waliinama mbele yake! Yosefu alitambua ndugu zake mara moja, lakini wao hawakumtambua yeye kwa sababu miaka 20 ilikuwa imepita tangu walipomwona! Ndani ya somo ya nyuma Mungu akitaka, tutamaliza habari za Yosefu na namna alivyojifunua kwa ndugu zake.

Lakini somo la leo linatufundisha nini? Mungu anataka kutufundisha nini kwa njia ya habari za Yosefu na ndugu zake? Mungu anataka kutujulisha ya kwamba maneno yaliyotukia katikati ya Yosefu na ndugu zake ni **mfano** wa maneno yatakayotukia katikati ya Mwokozi wa dunia na wazao wa Adamu. Rafiki, ukikumbuka neno moja tu la somo la leo, liwe hili: **Yosefu ni kivuli** (mfano) **wa Mwokozi** ambaye Mungu aliahidi kutuma duniani. Kuna maneno mia moja au zaidi ndani ya habari za Yosefu yaliyo mfano wa habari za Mkombozi aliyekuja duniani nyuma ya karibu miaka 1800. Hatuwezi tuyataja yote ndani ya somo hili, lakini hata hivi tutasema juu ya maneno matatu.

1) Tuliona ya kwamba ndugu wakubwa wa Yosefu **walimkataa** na walikataa kuamini ndoto zake. Walimchukia, walimzarau na hata kumwuza. Maneno haya yalipata Mwokozi ambaye Mungu alituma duniani. Watu wa dunia walikataa Mkombozi na habari alizoleta. Walimzarau, walimtesa, walimwuza, na mwishoni walimfunga juu ya msalaba na misumari.

2) Mfano wa pili ndio huu: Kwanza, watu walizarau, waliona bule, walitesa na kufunga Yosefu. Lakini kwa wakati uliochaguliwa na Mungu mfalme wa Misri **aliweka** Yosefu kuwa mtawala juu ya inchi nzima, akitangaza kwa watu wote waliotaka kuokolewa toka njaa na mauti: "Kwendeni kwa Yosefu, Mlinzi wa Uzima!" Vivyo hivyo, juu ya Mwokozi wa dunia ambaye Mungu alituma duniani, Bwana Mungu anasema: Kwendeni kwa Mwokozi ambaye niliweka! Yeye ni Mlinzi wa Uzima; Uzima unatoka kwake! Ukimnyenyekea yeye, hutakuwa na njaa moyoni mwako tena kamwe na nafsi yako itaishi kwa milele.

3) Mlingano wa tatu katikati ya Yosefu na Mkombozi linatuleta kufikili sana. Mwishoni ndugu za Yosefu **walijiweka** chini ya amri yake. Waliweza kufanya neno moja tu, ndilo kuinama na nyuso zao hata udongo mbele ya mtu yule ambaye walimkana na kumzarau! Vivyo hivyo, Neno la Mungu linatangaza ya kwamba Mkombozi, anayekataliwa na kuaibishwa na watu kufika hata leo, atarudi

siku nyingine kuhukumu dunia na haki. Siku ile watu wote wa dunia watainama mbele yake; wote watajua ni yeye aliyewekwa na Mungu kuwa Mwokozi na Mwamuzi wa dunia!

Rafiki unayesoma mafundisho haya, **Umejiweka chini ya Mwokozi** aliyewekwa na Mungu kukuponyesha toka hukumu ya milele? Au utangoja kufika wakati saa inapopita, kufika Siku ya Hukumu—wakati utakapolazimishwa kuinama mbele yake?

~~~~~~~~~~~~

Kaa kuwaza juu ya somo la leo! Mungu akubariki na kukupa ufahamu wa maneno haya yote. Neno la Mungu linasema:

> ***"Tuna neno la unabii lililo imara zaidi, na inawafaa ninyi kuliangalia, kama taa inayongaa katika pahali pa giza."***
>
> (2 Petro 1:19)
~~~~~~~~~~~~

SOMO 27

BAKI LA HABARI ZA YOSEFU

MWANZO 42-50

Salama iwe kwako, rafiki. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuendelea na somo lingine ndani ya kitabu hiki *Njia ya Haki*.

Ndani ya masomo mawili yanayopita tulisoma juu ya Yosefu, mwana wa Yakobo. Somo ya leo ni juu ya **baki la habari za Yosefu**, na linatufikisha kwa **mwisho wa kitabu cha Mwanzo.** Tumeona mbele ya kwamba Yakobo, mwana wa mwana wa Abrahamu, alikuwa na wana kumi na wawili. Yosefu alikuwa mwana wa kumi na mmoja. Wao wote waliishi katika inchi ya Kanana, ndiyo inchi Mungu aliyoahidi mbele kuwapa wazao wa Abrahamu, Isaka na Yakobo. Wakati Yosefu alipokuwa kijana, aliota ya kwamba siku nyingine wakubwa wake watainama mbele yake. Lakini wakubwa wake walimzarau na ndoto zake, wakamwuza kuwa mtumwa inchini mwa Misri. Lakini Mungu aliponyesha Yosefu toka taabu yake yote, na kumpa akili kutafsiri ndoto ya Farao, mfalme wa Misri. Mungu akimsaidia, Yosefu alionyesha Farao ya kwamba kutakuwa na njaa kwa miaka saba inchini. Hivi, Farao aliweka Yosefu kuwa mtawala mkubwa wa inchi nzima ya Misri.

Nyuma ya miaka saba ya usitawi, tuliona ya kwamba kulikuwa na wakati wa njaa inchini mwa Misri, kama Yosefu alivyotabiri, na katika inchi ya Kanana. Lakini kwa inchi ya Misri nafaka nyingi ziliwekwa akiba kwa sababu ya neema na akili ambazo Mungu alimpa Yosefu.

Wakati Yakobo aliposikia ya kwamba kuna nafaka katika Misri, alituma wakubwa kumi za Yosefu kwenda kununua kwa mahitaji yao. Lakini hakutuma Benyamina, mdogo wa Yosefu, pamoja na ndugu wengine kwa sababu aliogopa atapata matata. Nyuma yake tuliona wakubwa kumi wa Yosefu wakifikia Misri na kuinama mbele

ya ndugu yao Yosefu, wakitimiza ndoto ambayo Yosefu aliota miaka mingi mbele. Yosefu alitambua wakubwa wake, lakini ndugu zake hawakumtambua kwa sababu miaka zaidi ya makumi mbili ilipita tangu walipomwona, nao walifikili Yosefu alikuwa amekufa.

Leo tutamaliza habari za Yosefu na kuona **namna Yosefu alivyojifunua kwa ndugu zake**. Hakujifunua kwa ndugu zake mara moja, kwa sababu alitaka kuwajaribu, kuona kama mioyo yao miovu na ya udanganyifu ilikuwa imegeuka. Hivi, Maandiko yanasema: *"Yosefu akaona ndugu zake, akawatambua, lakini akajifanya mgeni kwao. Akasemezana nao kwa maneno makali; akawaambia: Mumetoka wapi? Wakasema: Toka inchi ya Kanana kununua chakula."* (Mwanzo 42:7)

Yosefu aliwauliza maneno mengi, akawashitaki kusema walikuwa wapelelezi na aliwafunga gerezani. **Alitaka wawaze kwanza juu ya maisha yao na hali ya roho zao mbele ya Mungu.** Nyuma ya siku tatu aliwaruhusu kwenda, wote ila mmoja ambaye alibaki gerezani. Alisema na ndugu wengine kurudia Misri pamoja na mdogo wao Benyamina, mtoto wa mwisho wa baba yao.

Nyuma ya miezi mingi, wakubwa wa Yosefu walirudi kwa Misri kununua nafaka nyingine, na walipeleka Benyamina pamoja nao. Wakati walipofika, walikutana tena na Yosefu, mtawala wa inchi—lakini hata saa ile hawakumtambua. Waliogopa sana kwa sababu Yosefu aliwaleta nyumbani mwake mwenyewe. Halafu aliwatayarishia karamu, akawaketisha kuzunguka meza kwa utaratibu, kuanza na mkubwa wao kufika mdogo wao, akawapa vyakula toka meza yake mwenyewe. Benyamina alipokea vyakula mara tano kupita wengine. Labda Yosefu alikuwa akijaribu ndugu zake kuona kama wataonea Benyamina wivu namna walivyomtendea yeye mbele. Lakini hata mmoja wao hakuonyesha wivu juu ya mdogo wao Benyamina.

Nyuma ya karamu, Yosefu aliagiza mtumishi kujaza mifuko yao na nafaka na kuficha kopo yake ya feza ndani ya mfuko wa Benyamina. Wakati ndugu za Yosefu walipokwisha kuanza safari, Yosefu aliagiza msimamizi wa nyumba yake kukimbia nyuma yao na kuwashitaki kusema wameiba. Wakati msimamizi alipowafikia, alisema, "Kwa nini mumerudisha mabaya kwa mema? Hamukukamata kopo ya kunywa ya bwana wangu?" Walijibu, "Hatukuikamata. Yule ambaye unakuta kopo ndani ya mfuko wake afe na sisi wenyewe tutageuka watumwa wako!" Msimamizi alijibu, "Yule

ambaye kwake kopo itaonekana atakuwa mtumwa wangu, lakini ninyi wengine munaweza kwenda zao."

Msimamizi alitafuta ndani ya mifuko yote, kuanza na mkubwa wa ndugu kufika mfuko wa mdogo wao — akapata mfuko ndani ya mfuko wa Benyamina! Wakati walipoona neno hili, ndugu za Yosefu walipasua mavazi yao, wakarudia mji, wakajitupa chini mbele ya Yosefu. Yosefu alisema nao, "Mumefanya nini? Hamukujua ya kwamba hamutaweza kunidanganya?" Yuda, mwana wa ine wa Yakobo alimjibu, "Basi tutasema nini? Namna gani tutaweza kuonyesha kwamba hatuna kosa? Mungu amefunua matendo yetu mabaya na uzalimu wetu! Sisi ni watumwa wako, sisi pamoja na yule kwake ulipata kopo!"

Yosefu alijibu, "Mwanamume yule tu kwake kopo ilipatikana atakuwa mtumwa wangu. Ninyi wengine munaweza kurudi na salama karibu na baba yenu." Halafu Yuda alikaribia Yosefu na kumwambia tena juu ya maumivu makubwa ya roho ya baba yake wakati aliporuhusu Benyamina kwenda Misri pamoja nao. Halafu Yuda alisihi Yosefu kuwarehemu na kuruhusu Benyamina kurudi karibu na baba yake. Yuda aliomba vilevile yeye aweze kuwa mtumwa wa Yosefu kwa pahali pa Benyamina. Wakati Yosefu alipoona maumivu rohoni mwa ndugu zake kwa sababu ya zambi walizofanya miaka mingi mbele, na namna walivyohurumia baba na mdogo wao, Yosefu alijua ya kwamba **wakubwa wake walikuwa wametubu kwelikweli.** Alijua kwamba **saa ilikuwa imefika kwa yeye kujifunua** kwa ndugu zake!

Maandiko yanasema, kuanza na Mwanzo 45:1,

> *"Halafu Yosefu hakuweza kujifunua tena mbele yao wote waliosimama karibu naye; akalia: Toeni kila mtu mbele yangu. Wala hakusimama mtu pamoja naye wakati Yosefu alipojitambulisha kwa ndugu zake. Akapaza sauti kwa kulia: Wamisri wakasikia, nyumba ya Farao wakasikia. Yosefu akawaambia ndugu zake:* ***Mimi ni Yosefu****; baba yangu anaishi hata leo? Wala ndugu zake hawakuweza kumjibu, kwa sababu wakaogopa mbele yake.*
>
> *Yosefu akawaambia ndugu zake: Karibieni kwangu, ninawaomba ninyi. Wakakaribia. Akasema:* ***Mimi ni Yosefu ndugu yenu ambaye mulimwuza kwenda kwa Misri.*** *Basi sasa musihuzunishwe, wala isiwe hasira kwa macho yenu ya kwamba muliniuza hapa; kwa sababu* ***Mungu alinituma mbele yenu kwa kuponyesha maisha za***

watu. *Kwa sababu miaka hii miwili njaa imekuwa inchini; na miaka mitano mingine njaa itakuwa isiyo na kulima wala kuvuna. Mungu amenituma mbele yenu kuponyesha baki duniani na kuwaponyesha ninyi* ***kwa wokovu mkubwa***. ***Basi sasa hakuwa ninyi ambao mulinituma hapa, lakini Mungu;*** *naye amenifanya kuwa baba kwa Farao, na bwana wa nyumba yake yote, na mtawala juu ya inchi nzima ya Misri. Fanyeni mbio, pandeni kwa baba yangu mumwambie: Mwana wako Yosefu amesema hivi: Mungu ameniweka bwana juu ya Misri yote; shuka kwangu, usikawie; nawe utakuwa katika inchi ya Goseni, na utakuwa karibu nami, wewe na wana wako; na wana wa wana wako na kondoo zako na ngombe zako na yote uliyo nayo; na nitakukulisha pale; kwa sababu miaka mitano mingine ya njaa itakuwa; usiwe masikini, wewe na nyumba yako, na yote uliyo nayo. Na tazama, macho yenu yanaona, na macho ya ndugu yangu Benyamina ya kama ni kinywa changu ambacho kinasema nanyi. Na mutamwambia baba yangu utukufu wangu wote katika Misri na juu ya vyote mulivyoona; na mutafanya mbio na kushusha baba yangu hapa. Akaangukia Benyamina kwa shingo yake, akalia, Benyamina akalia juu ya shingo yake. Akabusu ndugu zake zote, akalia juu yao; nyuma ya yale ndugu zake wakasemezana naye.*" (Mwanzo 45:1-15)

Nyuma yake ndugu zake walijitayarisha kurudi kwa nyumba ya baba yao. Yosefu aliwapa magari kama Farao alivyoagiza na aliwapa vyakula kwa safari vilevile.

"Wakapanda toka Misri, wakakuja kwa inchi ya Kanana kwa Yosefu baba yao. Wakamwambia wakisema: ***Yosefu anaishi hata leo****, naye ni mtawala juu ya inchi ya Misri. Moyo wake ukazimia, kwa sababu hakuwaamini. Wakamwambia maneno yote ya Yosefu, ambaye aliwaambia; na wakati alipoona magari Yosefu aliyotuma kumbeba, roho ya Yakobo baba yao ikarudi; Israeli akasema: Inafaa; Yosefu mwana wangu angali hai; nitakwenda kumwona mbele ya kufa kwangu."* (Mwanzo 45:25-28)

Halafu Maandiko yanapasha namna Yakobo na jamaa yake walivyotoka inchi ya Kanana na kwenda Misri. Yakobo alitoa sadaka njiani, na pale Mungu alisema naye:

"Mimi ni Mungu wa baba yako; usiogope kushuka kwa Misri; maana ***nitakufanya taifa kubwa pale****; nitashuka pamoja nawe kwa Misri,*

*na hakika **nitakupandisha tena**; na Yosefu ataweka mkono wake juu ya macho yako."* (Mwanzo 46:3,4)

Nyuma ya safari ndefu, Yakobo na jamaa yake walifikia inchi ya Misri. Yakobo alikuwa na furaha tele kuona mwana wake mpendwa tena nyuma ya miaka ile mingi! Hivi Yakobo, anayeitwa vilevile ***Israeli***, na jamaa yake walipanga katika Misri kwa inchi ya Goseni. Hesabu yao iliongezeka sana nao waligeuka kabila kubwa sana. Yakobo alikaa katika Misri kwa miaka kumi na saba. Urefu wa maisha yake mazima ulikuwa miaka 147. Halafu Yakobo, baba ya makabila ya Israeli, alikufa, akakwenda juu kukaa pamoja na Mungu. Yosefu na ndugu zake na watu wote wa Misri walimwombolea kwa siku makumi saba. Wana wa Yakobo walizika baba yao inchini mwa Kanana, kwa pahali pa maziko pa Abrahamu tata yake.

Ndani ya sura ya mwisho ya kitabu cha Mwanzo, sura 50, Maandiko yanasema kuanza na shairi 15:

*"Wakati ndugu za Yosefu walipoona ya kama baba yao amekufa, wakasema: Labda Yosefu atatuchukia naye atatulipia mabaya yote ambayo tulimtendea. . . . 19 Lakini [wakati Yosefu aliposikia neno hili] akawaambia: Musiogope; mimi ni pahali pa Mungu? **Nanyi, mulikusudi mabaya juu yangu, lakini Mungu alikusudi mema yafanywe, kama ni leo, kuponyesha uzima wa watu wengi**. Kwa hivi sasa musiogope, nitawakulisha ninyi, na watoto wenu. Akawafariji, akasema vema kwao.*

22 Yosefu alikaa kwa Misri, yeye na nyumba ya baba yake; Yosefu akaishi miaka mia moja na kumi. . . 24 Yosefu akawaambia ndugu zake: Ninakufa, lakini hakika Mungu atawaangalia ninyi, na kuwapandisha ninyi toka inchi hii hata inchi ambayo aliapia Abrahamu, Isaka na Yakobo. Yosefu akaapiza wana wa Israeli, akisema: Hakika Mungu atawaangalia ninyi, na mutabeba mifupa yangu toka hapa. Hivi Yosefu akakufa, mwenye miaka mia moja na kumi, wakapakaa maiti yake isioze, akatiwa ndani ya sanduku katika Misri." (Mwanzo 50:15-26)

Hizi ni habari za mwisho wa kitabu cha Mwanzo: *"Hivi Yosefu **akakufa** . . . na . . . akatiwa ndani ya **sanduku** katika Misri."* Hivi kitabu hiki kilichoanza na habari za namna Mungu alivyoumba **uzima**, kinakwisha na habari za **mauti**. Kwa sababu ya zambi ya Adamu, mauti ilipata watu wote. Kwa nini? Kwa sababu *"mishahara ya zambi*

ni mauti!" (Waroma 6:23) Ilipasa hata mtu mzuri kama Yosefu, aliyeitwa *Mwenye Kulinda Uzima* kufa kwa sababu yeye vilevile alikuwa mzao wa Adamu na alikuwa na mashina ya zambi ndani ya moyo wake. Yosefu, akisaidiwa na Mungu, aliweza kulinda watu wa Misri, na jamaa yake mwenyewe wasife kwa njaa, lakini **hakuweza kuwalinda wasipatwe na mauti yenyewe**. Hata hivi tunaweza kusifu Mungu na mioyo yenye furaha kwa sababu ndani ya kitabu cha Mwanzo, tunasoma vilevile juu ya **ahadi ya ajabu ya Mungu** kutuma kwetu Mwokozi anayetosha kabisa na **atakayeshinda mauti yenyewe**. Mauti ni tunda la **zambi**. Mwokozi ambaye Mungu aliahidi kutuma ataokoa wazao wa Adamu toka **shina la zambi** na **azabu ya zambi**. Shina la zambi ni Shetani na moyo mwovu wa mtu. Azabu ya zambi ni mauti na Hadeze. Mwokozi ambaye Mungu aliahidi kutuma ameshinda maneno haya na anaweza kugeuza maisha ya wale ambao wanamwamini.

Wewe unayesikiliza leo, unajuana na Mwokozi huyu wa kutosha kabisa, aliyeshinfa Shetani na zambi, mauti, na Hadeze na anayetaka kuwapa uzima wa milele wote ambao wanamwamini jina lake? Habari Njema {injil} inasema juu ya Mwokozi huyu kusema: *"Atukuzwe Bwana, Mungu wa Israeli; kwani amekuja kwa watu wake, na kuwakomboa.* ***Ametunyanyanyulia pembe ya wokovu . . . kama alivyosema kwa vinywa vya manabii yake watakatifu, waliokuwa tangu mwanzo!"*** (Luka 1:68-70) Amina!

~~~~~~~~~~~~

Ndani ya somo la nyuma, Mungu akitaka, tutaanza kusoma kitabu cha pili ndani ya Tora, kinachoitwa *Kutoka* . . .

Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya shairi hili la Maandiko linalojumlisha maneno makubwa ya kitabu cha Mwanzo:

> ***"Pahali zambi zilipozidi, neema [ya Mungu] ilizidi zaidi sana!"*** (Waroma 5:20)
~~~~~~~~~~~~

SOMO 28

UKUMBUSHO WA KITABU CHA KWANZA CHA TORA

MWANZO 1 – KUTOKA 1

Salama iwe kwako, Rafiki, kwa jina la Mungu wa salama, anayeta-ka watu wote kufahamu, kuamini na kupokea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tuendelee sasa na somo la mwisho la kitabu cha kwanza cha la *Njia ya Haki*.

Kama unavyojua, Tora ni kitabu cha kwanza cha Maandiko ya Manabii na ina sehemu au vitabu vitano. Sehemu ya kwanza inaitwa *Mwanzo*. Ndani ya somo la mbele, tulimaliza masomo yetu ndani ya Mwanzo. Basi leo tunaanza na sehemu ya pili ya Tora, inayoitwa ***Kutoka***. Ndani ya kitabu hiki tunapata habari za kushangaza za namna Mungu alivyofungua watoto wa Israeli toka utumwa ndani ya inchi ya Misri.

Mbele ya kuanza kusoma kitabu cha Kutoka, tufanye **ukumbusho** wa maneno tuliyojifunza ndani ya kitabu cha kwanza cha Maandiko. Ni neno la sharti kwa sisi kujua kabisa habari za kitabu cha Mwanzo, kwa sababu ni msingi ambao Mungu aliweka ili tuweze kufahamu na kuamini maneno yote yanayoandikwa ndani ya vitabu vingine vya manabii vinavyofuata.

Unakumbuka shairi la kwanza la kitabu cha Mwanzo? Linasema: "*Katika mwanzo Mungu aliumba mbingu na dunia.*" Neno hili ni neno kubwa. "Katika mwanzo **Mungu**! Wakati vitu vyote visipokuwa bado kulikuwa na Mmoja tu, ndiye Mungu. Nyuma yake tulijifunza ya kwamba Mungu aliumba milioni za **malaika** watakatifu, kwa uwezo wa neno lake la uwezo na Roho Mtakatifu wake. Mungu aliumba malaika ili waweze kumtumikia na kumsifu kwa milele. Katikati ya malaika kulikuwa na mmoja aliyeshinda

wengine kwa akili na uzuri wa kuonekana. Alikuwa **Lusifero**, mkubwa wa malaika. Lakini Maandiko yanatujulisha ya kwamba siku moja Lusifero aligeuka mwenye kiburi na alizarau Mungu moyoni mwake. Lusifero na malaika wengi wengine walianza kufanya shauri kuangusha Mungu. Lakini haiwezekani kuangusha Mungu. Mungu hawezi kukubali kukaa karibu naye wale wanaokataa kutawaliwa naye. Hivi Mungu alifukuza Lusifero na malaika zake waovu na aligeuza jina la Lusifero kuwa **Shetani**, maana yake *Adui.* Na nyuma ya kufukuza Shetani na malaika zake, Mungu aliumba kwa ajili yao moto wa **hadeze**. Maandiko yanasema ya kwamba Siku ya Hukumu Mungu, Mwenye Haki, atatupa Shetani ndani ya moto ule pamoja na wote ambao wanamfuata.

Halafu tulisoma namna Bwana alivyoumba **dunia** kwa watu ambao alikusudi kuumba. **Mtu** ndiye kiumbe cha maana zaidi ambacho Mungu aliumba kwa sababu mtu aliumbwa kwa sura ya Mungu! Mungu alitaka kuwa na ushirika na upatano wa karibu zaidi na mtu. Kwa sababu hii aliweka ndani ya nafsi ya mtu **nia** inayoweza kujuana na Mungu, alimpa **moyo** unaoweza kupenda Mungu, na alimpa uwezo wa kuchagua kutii Mungu.

Kisha Mungu aliweka **jaribu** (mtihani) mbele ya mwanamume na mwanamke ambao aliwaumba. Mungu alionya Adamu akisema: "*Una ruhusa kula matunda ya kila mti shambani; lakini haifai ule wa mti wa kujua uzuri na ubaya, kwa sababu hakika ukikula ya matunda yake utakufa!*" maana yake: utatengwa nami milele!

Lakini, tuliona ya kwamba wazazi wetu, Adamu na Hawa, walichagua kutii Shetani kwa njia ya kula matunda ya mti ambayo Mungu alikuwa amekataza. Hivi, Neno la Mungu linasema: "*Kwa mtu mmoja **zambi** iliingia ulimwenguni, na **kufa** kwa njia ya zambi; na hivi **kufa kulikuja juu ya watu wote**.*" (Waroma 5:12) Kwa sababu ya zambi ya Adamu, sisi sote ni wenyewe zambi. Kwa sababu ya zambi ya Adamu, sisi sote tunastahili kufa na kuhukumiwa na Mungu.

Halafu tuliona ya kwamba Mungu alifukuza Adamu na Hawa toka Shamba la Paradiso kwa sababu ya zambi yao. Lakini mbele ya kuwafukuza, Mungu alitangaza ya kwamba alikusudi kutuma **Mkombozi** duniani kuokoa wana wa Adamu toka uwezo wa Shetani na toka azabu ya zambi. Mungu alikuwa na shauri tayari kukomboa wenye zambi. Shauri lake lilikuwa kutuma duniani Mtu mkamilifu asiyechafuwa na zambi ya Adamu. Mtu huyu wa haki atakubali

kumwanga damu yake kulipa deni ya zambi kwa wana wa Adamu. Kwa njia hii, Mungu ataweza kusamehe zambi za watu bila kuharibu haki yake mwenyewe. Ndiyo, ahadi ya Mungu juu ya kuja kwa Mkombozi ni ahadi ya ajabu kabisa!

Halafu Mungu alihakikisha ahadi yake ya ajabu kwa njia ya kutoa nyama wengine kama sadaka, na kufanyia Adamu na Hawa mavazi. Mungu alikuwa amefundisha Adamu na Hawa ya kwamba "*mshahara wa zambi ni mauti*" na ya kwamba "*bila kumwanga damu hakuna usamehe.*"

Nyuma ya maneno haya tulijifunza juu ya wana wawili wa Adamu. Tuliona ya kwamba Abeli alitolea Mungu **mwana-kondoo** bila kilema na kumchinja, akionyesha mfano wa **Mkombozi** atakayekuja duniani na kufa kwa wenye zambi. Basi Kaina alijaribu kukubaliwa na Mungu kwa njia ya kazi zake mwenyewe, akamtolea zabihu ya vyakula vya shamba lake. Maandiko yanatujulisha ya kwamba Bwana "*akaheshimu Abeli na zabihu yake, lakini hakuheshimu Kaina na zabihu yake.*" Kwa sababu gani Mungu alikataa zabihu ya Kaina? Kwa sababu sheria **haikusema**, "malipo kwa zambi ni **mate-ndo mema**!" Sivyo, yanasema kwamba "*mshahara wa zambi ni **mauti!***" na "*bila **kumwanga damu** hakuna usamehe wa zambi.*" Mungu alisihi Kaina kutubu na kukubali njia ya haki ambayo alitayarisha, lakini Kaina alikasirika sana, akaua mdogo wake Abeli.

Zaidi ya wazao wa Adamu walifuata Kaina, hivi kwa wakati wa Noa, Maandiko yanasema Bwana "*akaona ya kama uovu wa watu wa dunia ulikuwa umekuwa mkubwa sana, na ya kama mawazo yote ya mafi-kili ya mioyo ya watu **yalikuwa mabaya tu siku zote**.*" Kwa sababu ya uovu wa mioyo ya watu Mungu alikusudi kutuma garika kufuta waasi. Kwa wakati ule mbaya, Noa tu aliamini Mungu, na kwa sababu hii Mungu alimwagiza kujenga merikebu kubwa, itakayokuwa kimbilio kwa wote walioingia ndani yake. Mungu alikuwa na saburi na wenye zambi kwa muda mrefu wakati Noa alipokuwa akijenga safina. Lakini hata mtu mmoja hakutubu na kuingia chombo, ila Noa na jamaa yake.

Noa alikuwa na wana watatu, Semu, Hamu na Yafeti. Nabii Abrahamu alikuwa mzao wa Semu. Tulisoma ya kwamba Mungu aliagiza Abrahamu kuondokea nyumba ya baba yake na kwenda kwa inchi ya Kanana. Mungu alikusudi kufanya **taifa jipya** kwa njia ya Abrahamu na ya kwamba manabii wote wa Mungu na **Mwokozi**

wa dunia watatoka kwake. Kwa sababu hii Mungu alisema na Abrahamu, "*Nitatukuza jina lako, nawe uwe baraka . . . na ndani yako jamaa zote za inchi watabarikiwa.*" (Mwanzo 12:2,3)

Hivi Abrahamu aligeuka baba ya Isaka wakati alipokuwa mzee, kama Mungu alivyoahidi. Halafu Isaka alikuwa baba ya Yakobo, na Yakobo, aliyepewa jina lingine na Mungu, ndilo Israeli, aligeuka baba ya wana kumi na wawili. Na taifa jipya ambalo Mungu aliahidi Abrahamu lilitoka wana kumi na wawili wa Yakobo. Taifa hili liliitwa Israeli.

Ndani ya masomo matatu ya mbele, tulisoma habari za kushangaza sana za wana wa Yakobo, zaidi habari za Yosefu, mwana wa kumi na mmoja. Wakubwa wa Yosefu walimchukia, lakini Mungu alimbariki na kumfanyiza mtawala wa inchi nzima ya Misri. Nyuma yake Misri na inchi nzima ya Kanana ziliteswa na njaa, iliyokuwa taabu kubwa. Kwa sababu hii Yakobo na wana wake walikosa vyakula. Wakati Yakobo aliposikia kwamba kulikuwa na nafaka katika Misri, alituma wana wake kule. Halafu tuliona namna Yosefu alivyojifunua kwa ndugu zake, aliwasamehe, na aliita baba yake na jamaa yake nzima kuhama na kupanga katika Misri. Hivi, kwa **mwisho wa kitabu cha Mwanzo** tunaona **wana wa Israeli** hawakuwa inchini mwa Kanana tena, inchi ambayo Mungu aliahidi kumpa Abrahamu, lakini walikuwa **katika Misri**. Hata hivi maneno haya yalitokea kutimiza ahadi ya Mungu kwa Abrahamu miaka mingi mbele wakati aliposema naye:

> "*Jua ya kwamba **uzao wako utakuwa mgeni kwa inchi isiyo yake**, na watatumikia watu wale, nao watawatesa miaka mia ine; na vilevile nitahukumu taifa ambao watawatumikia; na nyuma watatoka na mali nyingi.*" (Mwanzo 15:13,14)

Mungu yeye mwenyewe alikuwa juu ya maneno yote yaliyopata wana wa Israeli. Kwa nini Mungu aliacha wazao wa Abrahamu, ndio Waisraeli kukaa katika Misri wakati alipoahidi kuwapa inchi ya Kanana? Kwa sababu Mungu alikusudi kuonyesha utukufu na uwezo ndani ya maneno yatakayopata Waisraeli katika Misri. Mungu alikusudi kuponyesha wana wa Israeli kwa uwezo wake mkubwa na wa kuogopesha, **ili watu wote waweze kujua ya kwamba Yeye ni Mfalme wa wafalme; Bwana wa wabwana, Mwenyezi!**

Mbele ya kumaliza somo hili, tusome toka sura ya kwanza ya kitabu cha **Kutoka**, kuanza na shairi 6:

"Yosefu akakufa na ndugu zake zote, na kizazi kile chote. Wana wa Israeli wakazaa, wakazidi sana, na kuongezeka, wakakuwa hodari sana sana; inchi ikajaa nao.

8 Akakuwa mfalme mpya juu ya Misri asiyejua Yosefu. Akawaambia watu wake: Tazameni, watu wa wana wa Israeli wamekuwa wengi, nao ni hodari kuliko sisi; basi tuwatendee kwa akili; wasiongezeke na isiwe wakati vita itakapotokea waungane na adui zetu wapigane nasi na kupanda toka inchi. Kwa hivi wakaweka wasimamizi wa utumwa juu yao kuwatesa kwa mizigo. Wakajengea Farao miji ya kuwekea akiba, Pitomu na Ramisesi. Lakini hata kadiri walivyowatesa ndivyo wakazidi kuwa wengi na kuenea. Waka-chukizwa kwa sababu ya wana wa Israeli. Wamisri wakatumikisha wana wa Israeli kwa nguvu; wakawatia maisha yao uchungu kwa utumwa mkali, na chokaa na matofali, kwa utumwa wote wa mashamba, kila utumwa ambao waliwatumikisha kwa nguvu.

15 Mfalme wa Misri akasema na wazalisha wa Waebrania, jina la mmoja lilikuwa Sifura, na jina la mwingine Pua; akasema: Wakati munapozalisha wanawake wa Waebrania, mukiwaona kwa pahali pa kuzaa; mtoto akiwa mwanamume, halafu mutamwua; lakini akiwa mwanamke, halafu ataishi. Lakini wazalisha wakaogopa Mungu, wala hawakufanya kama mfalme wa Misri alivyowaagiza, lakini wakaacha watoto wanaume wazima. Mfalme wa Misri akaita wazalisha, akawaambia: Kwa nini mulifanya neno hili na kuacha watoto wanaume hai? Wazalisha wakamwambia Farao: Kwa maana wanawake wa Waebrania si kama wanawake wa Wamisri: kwa sababu wao ni wenye uzima wingi, nao wanazaa wakati mzalisha hajafika bado karibu nao.

20 Mungu akatendea wazalisha mema; watu wakaongezeka, wakakuwa hodari sana. Na ilikuwa kwa sababu wazalisha waliogopa Mungu, akawafanyia nyumba. Farao akaagiza watu wake wote akise-ma: Kila mototo mwanamume atakayezaliwa mutatupa mtoni, na kila mtoto mwanamke mutaacha hai." (Kutoka 1:6-20)

~~~~~~~~~~~~

Sura ya kwanza ya kitabu cha Kutoka inakwisha hivi. Na tumefi-ka kwa mwisho wa Kitabu 1 ya Mfulizo "*NJIA YA HAKI*". Ndani ya
~~~~~~~~~~~~

Somo 1 la Kitabu 2 tutasoma habari za namna Mungu alivyoita na kutayarisha mtu mmoja kuponyesha wana wa Israeli toka mkono wa Farao, yule mfalme mwovu wa Misri. Unajua jina la mtu huyu? Ndiyo, ni Musa—nabii wa Mungu.

Tunataraji utajipatia **Kitabu 2** cha **Mfulizo** ***"NJIA YA HAKI"*** na kuendelea na masomo haya. Mungu akubariki. Kumbuka vilevile ya kwamba

> ***"Yote yaliyoandikwa, yameandikwa kwa mafundisho yetu, hata kwa saburi na faraja ya maandiko tuwe na tumaini"***
>
> (Waroma 15:4)